Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Thelathini na Nane – Tarehe 2 Agosti, 2011**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na**:-

**WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):** Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 348

**Uchimbaji wa Bwawa Jimboni Mbogwe**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE** aliuliza:-

Serikali imewazuia Wananchi wa Kijiji cha Nsango, Kata ya Iponya, kunywesha maji mifugo yao katika mto ulioko katika Hifadhi ya Msitu wa Kigosi Muyowosi kwa ahadi kwamba kutakuwa na Mradi wa Uchimbaji wa Bwawa ambalo lingetoa huduma mbadala ya maji ya mto:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha uchimbaji wa bwawa hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli taratibu za hifadhi za wanyamapori haziruhusu shughuli zozote za kijamii kufanyika ndani ya hifadhi ikiwemo unyweshaji wa mifugo. Kutokana na sababu hiyo, Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe katika Mwaka wa Fedha wa 2010/2011, iliandaa andiko la Mradi wa Ujenzi wa Bwawa na kuliwasilisha kwenye Mfuko wa Wanyamapori wa Taifa, ikiomba kupatiwa shilingi milioni 78.1 kwa ajili ya kazi hiyo. Mfuko wa Wanyamapori wa Taifa ulikubali kutoa kiasi cha shilingi milioni 25 kwa kazi ya ujenzi wa bwawa hilo. Fedha hizo kiasi cha shilingi milioni 25 zilitolewa tarehe 13 Julai, 2010 na kuingizwa kwenye akaunti ya Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa bwawa katika Kijiji cha Nsango kilichopo katika Kata ya Iponya na siyo ndani ya Hifadhi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kutokana na upungufu huo, Halmashauri imepanga kutumia fedha hizo kwa ajili ya kuanza kujenga bwawa kwa kuanza na tuta, yaani *charco darm embankment construction,* litakalogharimu kiasi cha shilingi milioni 28.2, ambapo shilingi milioni 3.2 ni mchango wa Halmashauri. Kazi ya ujenzi inatarajiwa kuanza tarehe 22 Agosti, 2011. Aidha, Halmashauri inajitahidi kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa bwawa hilo kwa mwaka 2011/2012.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri swali moja la nyongeza. Ningependa kujua ni kiasi gani cha pesa ambacho Serikali imepanga mwaka huu wa fedha ili kuweza kukamilisha ujenzi wa bwawa hili?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Masele, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hela zilizoombwa na Halmashauri kwa ajili ya kusaidia zilikuwa shilingi milioni 78.1; hela zilizotolewa na Idara ya Wanyamapori zilikuwa ni shilingi milioni 25; na hela ambazo Halmashauri imesema kwamba, itaongeza pale ni shilingi milioni 3.1; jumla shilingi milioni 28.1. Hizo ndizo hela zilizotengwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Na. 349

**Utafiti wa Volkano ya Mlima Kilimanjaro**

**MHE. BETTY E. MACHANGU** aliuliza:-

Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro ilianzishwa rasmi mwaka 1973 kwa lengo la kuhifadhi Mlima huo na maeneo yanayouzunguka; Mlima huo una vilele vitatu ambavyo ni Shira, Mawenzi na Kibo; Kilele cha Shira kina *volcano* iliyokufa na vile vya Kibo na Mawenzi vina *volcano* iliyolala:-

Je, Seriklai imefanya utafiti wowote kuhusu *volcano* ya vilele vya Mawenzi na Kibo ili kujua kama kuna uwezekano wa kulipuka wakati wowote katika uhai wa *volcano?*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, ninaomba nitoe maelezo ya awali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Hifadhi ya Mlima Kilimajaro *(KINAPA)*, ilianzishwa mwaka 1973 kwa lengo la kuhifadhi Mlima huo na maeneo yanayozunguka. *KINAPA* ilitambuliwa na *UNESCO* mwaka 1987 kama Hifadhi ya Dunia *(Global Natural Heritage Sites)* na imekuwa na mafanikio makubwa katika kuhifadhi na kusaidia jamii inayozunguka katika Miradi mbalimbali; kwa mfano, kuelimisha Wananchi, ujenzi na ukarabati wa barabara, shule, vituo vya afya na Miradi mingine.

Pamoja na mafanikio hayo, bado kuna changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira unaosababishwa na uvamizi wa hifadhi kwa ajili ya makazi, kilimo na mifugo.

Mheshimiwa Spika, sasa ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Kama alivyoeleza Mheshimiwa Machangu, Mlima Kilimanjaro una vilele vikubwa vitatu: Kibo urefu wa mita (5,895), Mawenzi (mita 5,149) na Shira (mita 3,962), juu ya usawa wa bahari. Vilele hivyo vilitokana na mlipuko mkubwa wa *volcano* miaka milioni moja iliyopita. Taarifa za Wataalam zimethibitisha kwamba, volcano za Mawezi na Shira zimekufa (*Dead Volcano);* maana yake hakuna uwezekano wa kulipuka tena kwenye vilele hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kibo, *volcano* kwenye kilele hicho, inasemekana imelala, lakini kuna dalili halisi za uhai. Kwenye kasoko (*crater*) ya Kibo kuna chemchemi zinazofukuta, zenye majivu ya moto na kutoa gesi aina ya salfa. Tukio la mwisho kulipuka lilitokea miaka 200 iliyopita na kusababisha shimo (*Ash Pit),* ambalo lipo mpaka hivi leo.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hakuna utafiti wa kina uliofanywa kuangalia uwezekano wa kulipuka tena. Hata hivyo, kutokana na matukio ya milipuko

ya hivi karibuni, sehemu mbalimbali duniani, Serikali kupitia Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania *(TANAPA)*, linakusudia kutafuta wataalam wa mlipuko wa *volcano* ili kufanya utafiti na kuangalia uwezekano wa kulipuka tena kwenye kilele hicho. Sasa hivi Wizara yangu ikishirikiana na *TANAPA*, ipo kwenye mchakato wa kutafuta mabingwa hao.

**MHE. BETTY E. MACHANGU**: Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa vile tafiti duniani zinaonesha kwamba mpaka mwaka 2025 barafu ya Mlima Kilimanjaro itakuwa imeyeyuka. Je, Serikali imefanya tafiti zozote au inafanya mkakati gani kuunusuru Mlima huo na tatizo hilo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Betty Machangu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa barafu ya Mlima Kilimanjaro inayeyuka na nilishawahi kujibu swali kama hili hapa Bungeni kwamba, tafiti mbalimbali zimefanyika ikiwemo *University of Dar es Salaam,* Mashirika mbalimbali na pia Shirika la *Climate Change* wamefanya tafiti na tafiti ya mwisho ilitolewa mwaka 2007 kwamba; ni kweli barafu ya Mlima Kilimanjaro itayayuka kutokana na *climate change*. Ninachoweza kusema ni kwamba, Wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro, wajitahidi sana na sisi wote tujitahidi kuutunza Mlima huu, kwa sababu kwanza, nimesema kabisa kuna kilele cha Kibo, *volcano* inaweza ikatokea kwa sababu bado volcano yake iko *high.* Kwa hiyo, tunapoendelea kuharibu zaidi huo Mlima, maana yake tunaleta madhara yaliyoko ndani ya Mlima ule chini kabisa na mengine yanayosababishwa na wanaadamu. Kwa hiyo, sisi wote kwa pamoja tujitahidi kuuhifadhi huo Mlima kwa kupanda miti ya kutosha ili kuunusuru usiendelee kulipuka na pia kusitokee madhara ambayo yanasababishwa na wanaadamu. Ahsante.

Na. 350

**Mgao wa Fedha za Wafadhili**

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Wazanzibari wengi wanakerwa na matatizo ya Muungano kama vile mgao wa fedha zitokanazo na Wafadhili kwa ajili ya maendeleo:-

Je, kwa nini misaada haitolewi kwa uwiano na wakati mwingine haiwafikii Wazanzibari?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, ninaomba kujibu swali namba 779, lililoulizwa na Mheshimiwa Mariam Salum Msabaha, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa zimekuwepo changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya Muungano. Kati ya changamoto zilizojitokeza ni mgawanyo wa misaada na mikopo kutoka nje. Hata hivyo, suala la ugawaji wa misaada ya kibajeti inayotolewa na Wafadhili kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, limepatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchukua nafasi hii kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kuwa, Zanzibar sasa inapata mgao wake wa fedha za misaada ya kibajeti na zimekuwa zikipitia Fungu 31 - Ofisi ya Mkamu wa Rais na kuwasilishwa kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Fedha hizo hutolewa kwa ajili ya nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, mgao wa fedha hizi hufuata *formula* iliyokubaliwa ya muda ya asilimia 4.5.

Mheshimiwa Spika, kwa kutibitisha hayo niliyoyasema, ninaomba nisome takwimu za mgao wa fedha zilizokwenda Zanzibar kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Katika mwaka wa fedha

2005/2006, Zanzibar ilipata mgao wa shilingi bilioni 18.6; 2006/2007 shilingi bilioni 23, 020,000; 2007/2008 shilingi bilioni 27,338,000; 2008/2009 shilingi bilioni 23, 040,000; na 2009/2010 shilingi bilioni 30, 200,000. Aidha, Serikali inaweka utaratibu wa namna bora ya kuhakikisha pande zote mbili za Muungano zinafaidika na fedha za misaada, mikopo na Miradi kutoka nje, kwa kuweka Mwongozo wa Ushirikishwaji wa Zanzibar katika Taasisi za Kimataifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa, hebu soma *figure* ya mwaka 2009/2010.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, *figure* ya 2009/2010 ina marekebisho, siyo shilingi bilioni 50 bali ni shilingi bilioni 30.

**MHE. MARIAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri. Ninaomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:

(i) Kwa kuwa Wazanzibari wanasahaulika kwenye masuala mengi ya Muungano; je, 2010 atanihakikishiaje Wazanzibari hawa wanapata fedha ambazo zinatolewa na Wafadhili nao wafaidike katika Miradi mbalimbali ya Maendeleo?

(ii) Kwa kuwa Wafadhili wamekuwa wakiwafadhili wanafunzi kwenda kusoma nje. Je, ni Wazanzibari wangapi wanafunzi nao wamepata ufadhili wa kwenda kusoma nje?

**SPIKA**: Mheshimiwa Waziri majibu, lakini sina uhakika alimaanisha 2010 au vipi; maana 2010 ilishapita!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Msabaha, kama ifuatavyo:-

Katika majibu ya msingi nilifikia mwaka 2009/2010, lakini katika mwaka 2010/2011, Zanzibar ilipata gawio la shilingi bilioni 36.7 kama nilivyowasilisha kwenye Kitabu cha Bajeti.
Mheshimiwa Spika, kuhusu Wazanzibari wanaofadhiliwa kwenda nje, ninaomba anipe nafasi nifanye kazi na Wizara ya Sayansi, Teknolojia na Elimu ya Juu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili nipate *figure* kamili.

**SPIKA:** Kwa sababu ni swali jipya.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa kuwa *formula* ya mgawanyo wa mapato ya Uvuvi wa Bahari Kuu imepatikana, Zanzibar inapata asilimia 40 na Jamhuri ya Muungano au Tanzania Bara inapata asilimia 60; ni kwa nini *formula* ya mgawanyo wa gesi mpaka leo isipatikane?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, ninaomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, *formula* ya mgawanyo wa mapato wa Uvuvi wa Bahari Kuu imepatikana na kwa kweli katika mijadala yetu, tulifikia kiwango hicho hicho kwa ajili ya mafuta na gesi. Tulishindwa kuafikiana katika mambo mengine na ndiyo maana suala hili bado hatujalipa maamuzi, lakini tulielekea katika mwelekeo huo.

**MHE. CHIKU A. ABWAO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa ni kawaida kwa Watanzania waishio Zanzibar kujiita Wazanzibari; na kwa kuwa kizazi kilichozaliwa kabla ya Muungano na hata wakati wa Muungano kinazidi kwisha; je, Serikali haioni kuna umuhimu sasa Watanzania wanaoishi Tanganyika nao wakajiita Watanganyika ili kuienzi historia?

**SPIKA:** Maswali mapya kabisa, lakini Waziri wa Nchi, hebu jibu kwa sababu na wewe ni *all weather*.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO):** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, ninaomba kujibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mheshimiwa Chiku Abwao, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Watanzania walioko Zanzibar au waliozaliwa Zanzibar, hujiita Wazanzibari kama vile waliozaliwa Shinyanga kujiita Wanyamwezi au Wasukuma, waliozaliwa Iringa wakajiita Wahehe au makabila mengine yoyote na hata kule Zanzibar waliozaliwa Makunduchi, sisi tunajiita Wamakunduchi na wengine waliozaliwa Pemba wanajiita Wapemba. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali Watanzania wajiite Watanzania, lakini pamoja na kujiita Watanzania, kuna *identification* ndogondogo na kwa sababu Zanzibar hakuna makabila, basi wote wanaotoka kule hujiita Wazanzibari. *(Makofi)*

Na. 351

**Mpango wa Kuchimba Visima vya Maji Vijijini**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MOHAMED G. DEWJI)** aliuliza:-

Serikali ina mpango wa kuchimba visima virefu vya maji kupitia Mradi unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ulioanza mwaka 2008: Je, mpango huo utaanza kutekelezwa lini kwenye vijiji kumi kwa kila Wilaya kwenye Jimbo la Singida Mjini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI) (K.n.y. WAZIRI WA MAJI):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mbunge wa Singida Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Singida Mjini ilimwajiri Mtaalam Mshauri, *M/S ENG Consult Ltd.,* mwezi Aprili, 2011 kwa ajili ya kusanifu, kupima, kuandaa zabuni na kusimamia ujenzi wa Miradi katika vijiji kumi vilivyochaguliwa na Halmashauri. Vijiji hivyo ni Mtamaa A, Mtamaa B, Unyianga, Mwankoko A, Mwankoko B, Kisaki, Ititi, Manga, Mtipa na Uhamaka. Mtaalam Mshauri amekamilisha taarifa za awali na kuainisha kazi zitakazofanyika na maeneo yatakayochimbwa visima. Makabrasha ya zabuni kwa ajili ya kumwajiri Mkandarasi yaliandaliwa na kutangazwa na tayari Halmashauri imepokea maombi. Kazi inayoendelea sasa ni tathmini ya zabuni kwa ajili ya kumwajiri Mkandarasi na itakamilika mwezi huu wa Agosti, 2011. Kazi ya kuchimba visima itaanza mara baada ya Mkandarasi kuajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Wananchi wa Vijiji nilivyovitaja, walihamasishwa na kuelimishwa kuhusu uchaguaji wa teknolojia inayowafaa na watakayoweza kulipia gharama za uendeshaji na vijiji vyote kumi vilichagua teknolojia ya visima virefu.

Mhesihmiwa Spika, jumla ya shilingi milioni 597.2 zilitolewa kwa ajili ya Miradi ya Maji katika Halmashauri ya Singida Mjini, kuanzia Juni, 2007 hadi Desemba, 2010. Fedha hizo zilitumika kutekeleza Miradi yenye kuleta matokeo ya haraka *(quick wins)* na kusanifu Mradi wa Vijiji Kumi. Katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, shilingi milioni 310.5 zimetengwa kuendeleza Miradi ya Maji katika Halmashauri hiyo na Wizara ya Maji itaendelea kutenga fedha mwaka hadi mwaka ili kukamilisha utekelezaji wa Miradi ya Maji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuchukua nafasi hii, mbele ya Bunge lako Tukufu, kumpongeza Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Singida Mjin, kwa juhudi zake binafsi anazochukua kuboresha huduma ya maji kwa Wananchi wa jimboni kwake.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ambayo yanawatia moyo Wananchi wa Singida Mjini pamoja na Mbunge wao; ninapenda kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameonesha nia ya dhadi kabisa kwamba Mradi huu sasa unatekekezeka; je, anaweza kuwaambia Wananchi wa Singida Mjini Mradi huu utachukua muda gani?

(ii) Kwa kuwa Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Singida Mjini amejitahidi sana kupeleka maji kwenye baadhi ya Kata pale alipoona kwamba Wananchi wanapata adha sana na Miradi ya Serikali inachelewa; je, Serikali haioni kwamba pesa zinazotengwa ni ndogo kiasi kwamba Mradi huu utachukua muda mrefu, sasa iongeze kiwango cha kutenga?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema hapa, hela na shughuli zote ambazo zilikuwa zimekusudiwa kufanyika kwa maana ya *feasibility study* na mambo mengine yote, mpaka ile *no objection* yote imekwishapatikana kutoka kwenye *World Bank.* Kwa hiyo, mimi nina hakika kwamba, sasa tumefikia hatua nzuri, ambayo itabidi kukisia kwamba, watachukua muda gani, itategemeana na usimamizi wao kule kwenye Halmashauri ya Singida Mjini watakavyofanya.

Hili la pili ambalo anazungumzia kwamba, hela zinazotengwa ni ndogo; hela zinazotengwa ni hizi ambazo zinakuja hapa tunazipitisha sisi wote. Kitu kimoja ambacho ninataka nikiri hapa, ambacho Mheshimiwa Diana Chilolo, anakizungumza hapa ni suala la *contribution* ya Mbunge wa eneo hili, Mheshimiwa Dewji kwamba, amefanya kazi kubwa sana. Mimi mwenyewe nimekwenda katika Halmashauri ile, nimeona Mheshimiwa Dewji amefanya kazi kubwa katika hili. Lazima tutamke hapa kwamba, tuna *value contribution* yake kwa sababu hela tunazopeleka kule ni kidogo. Kwa hiyo, ninapenda kusema kwamba, sisi hapa Halmashauri ndiyo tunaopanga kiasi cha pesa kinachohitajika. Kazi yetu sisi ni kusema, kama tunafikiri *priority* kubwa ni maji na kwa kweli kwa maana ya Singida, *priority* ni maji na tatizo lililo Singida na Dodoma hapa tunafahamu sisi sote kwamba ni maji.

Kwa hiyo, ninachoweza kusema hapa ni kwamba, waweke sasa katika bajeti zao na Mheshimiwa Diana Chilolo, amekuwa anafanya kazi hiyo kutusaidia; waweke katika bajeti zao na kama hiyo ni *priority* sisi hatutaacha kusaidia katika mpango huo. *(Makofi)*

**MHE. SAIDI M. MTANDA:** Ninakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Miradi hii ya *World Bank* maeneo mbalimbali ikiwemo katika Jimbo la Mchinga kwa takriban miaka miwili sasa imeshindwa kutekelezeka hasa katika Vijiji vya Kilolambwani, Likwaya na Namkongo. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha Miradi hiyo ili Wananchi wa maeneo hayo waweze kunufaika na maji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Spika, hili linalosemwa na Mheshimiwa Mbunge ni kweli kumekuwepo na hali ya kusuasua na kumekuwepo na ucheleweshaji. Tumeeleza hapa na Mheshimiwa Waziri wa Maji amekuwa anaeleza hapa, tatizo kubwa ambalo tumekuwa nalo ni hili la urasimu kwamba; ni lazima mfanye usanifu, mkimaliza ni lazima apeleke mpaka Dar es Salaam na iende ikapate *no objection* na mzunguko ule umekuwa mrefu mno mpaka wamalize, wawasiliane tena na Wizara halafu baadaye irudishwe tena kwenye Halmashauri; ni kweli anachosema Mheshimiwa Saidi Mtanda.

Kitu ambacho kimefanywa na Wizara ni kwamba, kwa hivi sasa wameanzisha Kitengo Maalum pale kwenye Wizara kwa ajili ya kuratibu haya yote yanayozungumzwa na huo mzuko anaousema. Matumaini yangu ni kwamba, baada ya kuanzisha sasa hicho Kitengo ambacho kitakuwa kinaratibu, huenda tatizo hili ambalo Mheshimiwa Mtanda analisema, likawa halipo tena kama ilivyokuwa huko nyuma.

Na. 352

**Upatikanaji wa Dawa/Vifaa, Madaktari na Watumishi Wengine Katika Vituo vya Afya Kwenye Kata**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Serikali imesisitiza kila Kata iwe na Kituo cha Afya na katika Jimbo la Lulindi tayari ujenzi umeanza kwenye Kata ya Mnavira na maandalizi yanaendelea katika Kata nyingine zote:-

Je, Serikali inatuhakikishiaje juu ya upatikanaji wa Madaktari na Watumishi wengine, dawa na vifaa mbalimbali kwenye Vituo hivyo ili huduma zinazotolewa ziwe na ubora unaotakiwa?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mbunge wa Lulindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Serikali imesisitiza kila Kata iwe na Kituo cha Afya na ninampongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa jitihada za kuendeleza ujenzi kwenye Kata ya Mnavira.

Pia ninapenda nimwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, utaratibu wa kujua mahitaji ya watumishi, dawa, vifaa na vifaa tiba vinavyohitajika ili kuviwezesha vituo kutoa huduma zenye ubora unaotakiwa ni jukumu la Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kupata madaktari na wataalam wengine, Halmashauri husika ni lazima iombe kibali cha kuajiri watumishi wanaohitajika kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, wakati wa maandalizi ya Bajeti ya Mishahara ya Watumishi *(Personal Emolument).* Kibali kitakachotolewa kitawasilishwa katika mamlaka husika ili iwatafute wataalam hao na kuwapeleka katika Halmashauri wakaajiriwe. Ni vyema kama Halmashauri ya Wilaya ya Masasi itaweka maombi ya watumishi wanaohitajika katika bajeti yao na kuomba kibali cha kuajiri kutoka Utumishi ili pindi ujenzi utakapokamilika, Kituo kianze kutoa huduma mara moja.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, itatenga fedha na kufungua Akaunti Bohari ya Dawa *(MSD),* kwa ajili ya Kituo cha Afya kinachojengwa Mnavira na vingine vitakapoanza kufanya kazi. Fedha zitakazowekezwa katika Akaunti, zitaviwezesha Vituo hivyo kuagiza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi, kufuatana na mahitaji na fedha zilizopo.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri, kwa kunipongeza kwa juhudi zinazofanywa na Wananchi katika Kata ya Mnavira za kujenga Kituo cha Taifa. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Je, Mheshimiwa Waziri na Serikali inaweza kulithibitishia Bunge hili kwamba kila Halmashauri inapoomba kibali inapewa kulingana na mahitaji yanayohitajika kwa sababu katika Jimbo la Masasi Halmashauri yangu ilishawahi kuomba watumishi mwaka jana lakini katika kibali ikaonekana kwamba watumishi 15 hawakuweza kupata kibali?

(ii) Je, Mheshimiwa Waziri atalithibitishia Bunge hili juu ya kuhakikisha Wananchi wa Jimbo langu na katika maeneo mengine wanaweza kupata kweli madawa kutokana na hali ya *MSD* kuwa hoi na Serikali kutokuwalipa madeni?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kila Halmashauri wanapopeleka mahitaji ya kupata watumishi je vibali hivyo vinaweza kukamilishwa. Jibu lake ni kwamba, hivi vibali vinatolewa kutokana na masuala mawili; upatikanaji wa watumishi hao kwa kada mbalimbali ikiwemo madaktari, manesi na upatikanaji wa fungu la fedha. Serikali kwa kujali na kuona umuhimu wa sekta hiyo, katika bajeti hii na katika kipindi cha miaka mitano, kipaumbele kimojawapo kilichopewa umuhimu ni Wizara ya Afya kwamba, tunaajiri moja kwa moja na nimepewa nafasi ya kutosha kuajiri hawa watumishi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, taarifa kwamba vibali vitaombwa Halmashauri, changamoto ni kwamba, Halmashauri waombe vibali vya watumishi wa kutosha katika Halmashauri zao na pindi watakapopatikana katika soko, wote tutawaajiri.

Swali la pili kuhusu *MSD;* Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge ni kwamba, lengo letu Serikali ni kuhakikisha zahanati, vituo vya afya na hospitali zote, dawa zinapatikana kadiri ya

mahitaji yanavyohitajika. Pale ambapo tunashindwa kutimiza haya na ndiyo maana vipo vipengele vingine ambavyo vinaviwezesha kujazia pale.

Ninaomba nimhakikishie ndugu yangu Bwanausi kwamba, suala la *MSD* siyo kwamba lipo hoi na lile deni ambalo MSD wanaidai Serikali, Wizara ya Afya tumesema deni hili tunalihamishia Hazina na litalipwa na siyo kwamba deni lile linaweza kuwafanya hawa *MSD* wawe wanashindwa kutimiza wajibu wao. Katika hotuba yangu, nilizungumzia kwamba, mojawapo ya suala ambalo *MSD* inalifanyia kazi ni mfumo mzima wa usambazaji wa dawa, ambao tumesema tunaufanyia kazi. Tayari tumeanza kwa majaribio Mkoa wa Tanga, ambao badala ya *MSD* kuishia kwenye Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya, sasa hivi wanapeleka moja kwa moja mpaka kwenye vituo husika, zahanati au kituo cha afya na kwa mwaka huu wa fedha, tumeanza kwa mikoa sita.

Kwa maelezo hayo ...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, hayo makofi siyo kwamba, wanakushangilia; wamechoka na majibu wala hujaulizwa. Kwa hiyo, umekula maswali ya nyongeza ya wengine. Basi tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 353

**Shirika la Ndege la Tanzania**

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED** aliuliza:-

Shirika la Ndege la Nchi ni utambulisho na fahari ya Taifa ndani na nje ya nchi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kusafisha Menejimenti pamoja na Bodi ya Shirika hili?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kulifufua Shirika la Ndege la Tanzania?

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na Shirika la Ndege lililo imara, ambalo litakuwa utambulisho wa Taifa ndani na nje ya nchi. Serikali pia inatambua umuhimu wa kuwa na Menejimenti nzuri na Bodi mahiri, ambayo itasimamia Shirika na kuhakikisha kwamba, linafikia malengo yake. Kwa sasa Menejimenti iliyopo inashikilia tu kwa muda, kwani Serikali iko katika mchakato wa kuteua Menejimenti na Bodi mpya ambayo itakuwa na uwezo wa kusimamia Kampuni ya Ndege ya Tanzania ili iweze kufikia malengo.

(b)Mheshimiwa Spika, Serikali itaipatia kampuni vitendea kazi na mtaji wa kujiendesha *(Working Capital)* ili iweze kuendeshwa kibiashara bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini. Vilevile kupitia Sera ya Ushirikishwaji wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi *(Public-Private Partnership Policy),* Serikali inaendelea na majadiliano na makampuni mbalimbali ili kumpata mbia mahiri na mwenye uwezo wa kuibadilisha *ATCL* iweze kutoa huduma za hali ya juu kwa ufanisi mkubwa, sambamba na makampuni ya ndege mengine nchini ili kukuza usafiri wa anga nchini.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nina maswali mawili ya nyongeza.

(i) Je, Serikali ina mpango gani wa kulipa madeni wanayodaiwa *ATCL* na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Zanzibar?

(ii) Katika kuchukua hatua ya kuboresha Shirika la Ndege la *ATCL;* je, Serikali imejipanga vipi katika kuhakikisha kwamba Shirika hili linaendeshwa na Viongozi Wazalendo wenye taaluma ya usafiri wa anga?

**SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Rukia, kwa kuuliza maswali vizuri. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Rukia, kama ifuatavyo:-

(a) Kuhusu suala la madeni ya Zanzibar, kama nilivyoeleza katika jibu la msingi, Serikali baada ya kuipatia Kampuni vitendea kazi na mtaji kujiendesha, yaani *working capital,* nina imani kuwa itaweza kufanya biashara na hivyo kupata fedha za kuwalipa wadeni wake wote ikiwemo Mamlaka ya Viwanja vya Ndege vya Zanzibar.

(b) Kuhusu kuhakikisha Kampuni inaendeshwa na Viongozi Wazalendo; kwa kuwa Serikali ilikutana na changamoto nyingi za kiutendaji katika Kampuni yetu ya *ATCL* kutokana na kuongozwa na baadhi ya Viongozi wasiokuwa na taaluma ya usafiri wa anga; Serikali inajipanga kuunda Menejimenti pamoja na Bodi mpya zitakazoongozwa na wataalam waliobobea katika masuala ya usafiri wa anga. Aidha, msisitizo mkubwa utaelekezwa kwenye kuwa na utaratibu wa kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara wataalam wa kampuni ili kuendesha kufuatana na mabadiliko ya teknolojia.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, *ATCL* ina ndege ngapi zinazoruka hivi sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Swali hilo lichukue nusu dakika tu. Jibu liwe nusu tu, hakuna maelezo zaidi. Umeuliza ngapi? Ziko wapi siyo *point. (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, *ATCL* sasa hivi haina ndege inayoruka, lakini nina barua hapa, *Dash Eight/Q Dash Eight* inakuja hapa Tanzania tarehe 8, imetoka kwenye matengenezo. Ndege nyingine inakwenda na tunafanya utaratibu mwingine wa ile *Boing* iliyoko matengenezo nayo ije kuboresha usafiri wetu wa anga. *(Makofi)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nchi ndogo kama ya Rwanda ambayo ukubwa wake na rasilimali zake ni ndogo kuliko hata Mkoa wa Kagera wana ndege tano mpaka sasa; *Being 2; ...*

**SPIKA:** Swali, swali.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Taifa kubwa kama la Tanzania tunapokosa ndege tunabaki na mipango; hivi Serikali haioni aibu kukosa ndege hata moja kila siku mipango?

**WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):** Mheshimiwa Spika, Serikali ilianzisha Shirika la Ndege mwaka 1977, ikalipatia Shirika hili ndege mpya takribani 11; *Boeing* 373 mbili, *Fokker Friendship* tatu na *Twin Otter* nne. Kudorora kwa utendaji wa Shirika la Ndege la Tanzania siyo kwa sababu Serikali haikuipatia Shirika hilo vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, Shirika hili lipo katika hali mbaya sasa hivi na tunajipanga kulirudisha kama lilivyokuwa hapo mwanzo.

**SPIKA:** Anayeongoza kikao ni mtu mmoja tu, wengine wanasema nini? Waziri jibu kwa kifupi, maana umeulizwa hii inaendelea mpaka lini.

**WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):** Tunajipanga kuliboresha na kulirudisha kama mwanzo. Ninaomba Waheshimiwa Wabunge wote, wasubiri waone tutafanya nini. Ahsante sana Mheshimiwa Spika. *(Makofi)*

Na. 354

**Masoko ya Mipakani**

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA** aliuliza:-

Wananchi wa Manyovu hufanya biashara na nchi jirani za Burundi na Rwanda, lakini kumekuwa hakuna masoko ya mipakani yanayotambuliwa na hivyo kufanya Wananchi kuonekana kana kwamba biashara hizo ni za magendo:-

(a) Je, ni lini Serilai itaweza kutambua umuhimu wa masoko ya mipakani na kwa upande wa Tanzania ni lini masoko hayo yataanzishwa na kutambuliwa?

(b) Kwa nini Wananchi wanasumbuliwa mipakani kwa kukamatwa na mizigo yao huku tukijua kwamba hatujaweka utaratibu wa njia za kupita na Serikali itawasaidiaje Wananchi hao ili wafanye biashara zao kwa amani?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Albert Obama Ntibaliba, Mbunge wa Manyovu, lenye sehemu (a) na (b), kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuanzisha masoko ya mipakani ili kukuza na kuendeleza biashara iliyo rasmi kati ya Tanzania na nchi jirani, hususan katika kipindi hiki ambacho tumeingia katika Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kufanikisha azma hii, Wizara ilitembelea maeneo ya mipakani kufanya tathmini ya biashara kati yetu na nchi jirani. Tathmini hiyo ambayo ilihusisha pia mpaka kati ya Tanzania na Burundi, eneo la Mnanila (Manyovu) katika Wilaya ya Kasulu, ilionesha umuhimu wa kujenga soko la mpakani katika eneo hilo. Soko hilo ni moja kati ya masoko saba yanayojengwa katika maeneo ya mipakani katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa soko la mpakani kati ya Tanzania na Burundi na eneo la Manyovu, utatekelezwa kupitia Mradi wa Uwekezaji wa Sekta ya Kilimo *(District Agricultural Sector Investment Project – DASIP),* unaoratibiwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika. Taratibu za kuanza kwa ujenzi huo zinaendelea na ujenzi unatarajiwa kuanza katika kipindi cha mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika pamoja na TAMISEMI, kuhakikisha soko hilo linajengwa mpakani kutokana na kutambua umuhimu wa kuwepo soko katika mpaka wa Manyovu. Hii itasaidia kuwarahisishia wafanyabiashara walioko mpakani, kufanya biashara rasmi, kuongeza mapato kwa Serikali na kupunguza usumbufu kwa wafanyabiashara wanapovuka na mizigo mpakani.

Mheshimiwa Spika, Wizara hutoa elimu kuhusu Sheria na taratibu za biashara kati ya nchi na nchi kwa wafanyabiashara wadogo mipakani ili waweze kuzizingatia na kuondokana na bughudha za kukamatwa. Aidha, jitihada zinafanyika ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za mipakani mahali pamoja ili kupunguza bughudha ya huduma za wakaguzi mipakani pamoja na kupunguza gharama na muda wa kupitisha mizigo na magari.

**MHE. ALBERT O. NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninashukuru kwa majibu mazuri. Ninashukuru kwamba, Serikali imetupatia soko zuri na Wananchi wangu wa Manyovu watalitumia.

Kwa kuwa ule mpaka Ukanda wake ni mpana na wote hawawezi kuja sehemu moja; je, Serikali ina uwezo wa kutuongezea soko lingine maeneo ya Kibande au Kilelema?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Obama, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ninapokea pongezi zake na ninataka kumhakikishia kwamba, tutajitahidi soko hili lijengwe kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, mpaka wa Tanzania na nchi jirani ambazo zinatuzunguka ni mpana sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Obama anaposema lile eneo ni pana, ninakubaliana naye kabisa. Kwa hivi sasa kutokana na mahitaji ya masoko kuwa mengi sana, jambo linalofanyika sasa hivi na

mipango iliyopo ni masoko saba kama nilivyosema. Kuna soko hili la Manyovu ambalo linajengwa pale Wilaya ya Kasulu, kuna Soko la Mtukula Wilaya ya Misenyi, kuna Soko la Murongo Wilaya ya Karagwe, Soko la Mkwenda Wilaya ya Karagwe, Soko la Kabanga Wilaya ya Ngara, Soko la Sirari Wilaya ya Tarime na Soko la Isaka, ambayo ni Bandari Kavu Wilaya ya Kahama. Hayo ndiyo masoko ambayo tumeyatengea fedha, tunajitahidi, lakini uwezo wa Serikali ukiongezeka, ninamhakikishia Mheshimiwa Obama, tutaangalia na eneo lingine kupanua hilo eneo ambalo anasema kwamba ni pana sana.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona na kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo tu la nyongeza, lakini lenye uzito mkubwa. Imenishangaza na kunisikitisha kidogo; Mheshimiwa Waziri anapoyataja haya masoko yaliyopewa kipaumbele, ameacha kutaja mpango wa kujenga soko mpakani mwa Tanzania na Msumbiji katika Kijiji cha Mkenda na ahadi ya kujenga soko hilo kule mpakani ni ya miaka takribani sita sasa na Waziri anafahamu.

Je, Mheshimiwa Waziri anataka kuniambia nini; je, ahadi ile aliyonipa ilikuwa siyo ya ukweli kwa miaka hiyo yote?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jenista Mhagama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninakubaliana na yeye kwamba, alishaleta ombi hilo na Wizara imelipokea inalifanyia kazi. Nilichokua ninatoa hapa ni *list* ya masoko ambayo yanajengwa katika huu utaratibu wa *DADPs* na ambao unasimamiwa na Wizara ya Chakula, Kilimo na Ushirika. Ninataka nimhakikishie kwamba, suala lake lipo Mezani, tunalifanyia kazi na mambo yatakapokuwa mazuri, basi ataona soko lake nalo linaanza kufanyiwa kazi.

Na. 355

**Ujenzi wa Viwanda vya Mawese Kigoma**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI (K.n.y. MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA)** aliuliza:-
Mafuta ya Kula ya *KORIE* yanatokana na Mawese ambayo yanalimwa kwa wingi sana Mkoani Kigoma lakini viwanda vya kusindika mafuta hayo viko Dar es Salaam:-

Je, Serikali kwa busara zake haioni kwamba kuna haja ya kujenga viwanda angalau viwili vya kusindika mafuta ya mawese Mkoani Kigoma?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikifanya juhudi za kujenga uwezo wa usindikaji wa mafuta ya mawese hatua kwa hatua katika Mkoa wa Kigoma. Katika Wilaya ya Kigoma Vijijini, kabla ya mwaka 2009, kulikuwa na viwanda vidogo 59 vya kukamua mafuta ya mawese. Viwanda hivi viliajiri jumla ya watu 693, wakiwemo 218 wenye ajira za kudumu na 475 wa ajira ya muda.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2009/2010 hadi kufikia Desemba 2010, Serikali kupitia *SIDO* ikishirikiana na Mashirika ya Umoja wa Mataifa *(WFP, UNDP* na *UNIDO),* yanayofadhili Miradi mbalimbali Mkoani Kigoma, imewezesha kuanzishwa kwa viwanda vidogo 18 vya kukamua mafuta ya mawese katika Vijiji vya Ilagala, Bitale, Bubango, Mahembe, Kagera na Ruiche vilivyoko katika Wilaya ya Kigoma Vijijini na kiwanda kimoja katika Wilaya ya Kasulu. Viwanda hivi hutumia nishati ya dizeli na kila kiwanda kina uwezo wa kukamua zaidi ya lita 600 za mafuta ya mawese kwa siku. Viwanda hivyo vilivyoanzishwa viliongeza ajira 372, zikiwepo 126 za kudumu na 246 za muda mfupi. Hali kadhalika, kuna viwanda 34 vya kukamua mafuta ya mawese

katika Manispaa ya Kigoma Ujiji, ambapo Serikali kupitia *SIDO,* ilisaidia uanzishwaji wa viwanda 18 ndani ya Mtaa wa Viwanda Vidogo *SIDO* Kigoma.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuimarisha uwezo wa usindikaji mazao kwa Wananchi, Mpango Mkakati wa *SIDO* wa Mwaka 2010/2011 – 2013/2014, umedhamiria kuendelea kutoa huduma za uongezaji thamani ya mazao sambamba na utoaji wa elimu ya ujasiriamali kwa Wananchi. Mkakati huu utawajengea uwezo Wananchi kuanzisha na kupanua viwanda vidogo na kuvifanya viwe endelevu.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(i) Kwa kuwa ujenzi wa viwanda huwa unafuata rasilimali zilipo; sasa Serikali haioni kwamba ni muda mwafaka kujenga kiwanda kikubwa kwa ajili ya kutumia zao hili la mawese ili tukuze Uchumi wa Taifa hili?

(ii) Serikali haioni kwamba kuna haja ya kuwaongezea uwezo hivi viwanda vya *SIDO* ambavyo amekuwa anavitaja hapa Mheshimiwa Waziri ili viweze kuzalisha mafuta kwa wingi zaidi?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mkosamali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, hoja yake ya kuwa na kiwanda kikubwa kabisa ni hoja nzuri, lakini uwezo uliopo sasa ni kuwa na hivi viwanda vidogo ambavyo kama nilivyosema, ninafikiri vinakaribia 100 sasa katika eneo zima la Kigoma. Mtizamo ni kwamba, unaweza ukawa na kiwanda kimoja kikawa cha mtu mmoja akaajiri watu wengine, lakini sisi Serikali kupitia *SIDO,* tunawawezesha watu mmoja mmoja wanakuwa na viwanda vidogo vidogo, kwa hiyo. kunakuwa na Wajasiriamali wengi ambao wana viwanda.

Mheshimiwa Spika, sasa kazi iliyopo kwetu Serikali na hata kwa Mheshimiwa Mbunge na Halmashauri yake ni kujaribu kuwakusanya wale wajasiriamali ambao wana viwanda vidogo vidogo, wakusanye mitaji yao, teknolojia zao na tuangalie mfumo wa masoko ili kwa pamoja, tuweze kuwa na kiwanda kimoja sasa ambacho kitafanya kazi kubwa zaidi. Kwa hiyo, ninaomba ushirikiano katika hilo.

Mheshimiwa Spika, hilo la pili la kuongeza uwezo wa *SIDO,* tukubaliane kwamba, kwanza, *SIDO* ni ya Serikali, maana anauliza kana kwamba, *SIDO* ni kitu tofauti na Serikali. Hiyo, kazi imefanyika kwa kupitia *SIDO,* Serikali imefanya kazi hiyo na kama nilivyosema awali, *SIDO* ingeweza ikafanya kazi kubwa sana kama tungekuwa na rasilimali za kuweza kufanya mambo mengi. Kwa sababu ya keki yetu kuwa ndogo na kadhalika, *SIDO* inajitahidi kwa kadiri ya uwezo wake, kutumia kile ambacho inakipata, kuwafikia Wananchi katika kona mbalimbali ikiwepo na Kigoma na tutaendelea kufanya kazi hiyo kwa kadiri ya uwezo wetu.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana kwa kuniona. Kwa kuwa mafuta ya Mawese au *KORIE* kama ilivyoandikwa kwenye swali la msingi ndiyo leo nimejua kwamba ndiyo *KORIE;* ni kwa nini Watanzania wengi wana mtazamo hasi kuhusu haya mafuta ya *KORIE* na hasa yale yanayoagizwa kutoka nje?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, utashi wa mlaji au mtumiaji ni utashi ambao Serikali haiwezi kuuingilia. Kitu ambacho Serikali inafanya ni kuhakikisha kwamba, mafuta yale yanaboreshwa, kama ni kuchujwa yanachujwa vizuri na yanafika katika soko. Sasa mtu akipenda mafuta kutoka nje, akipenda mafuta kutoka ndani, kwa kweli inakuwa ni chaguo lake. Bunge hili ni mshuhuda, Wizara ya Viwanda na Biashara, imekuwa kila wakati inawaambia Watanzania wanunue bidhaa za Tanzania na kuijenga Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nitumie fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla wafahamu kwamba, mafuta ya mawese yanayotokana na mawese ni mafuta ambayo yanatoka Tanzania; tuyanunue ili tuweze kuijenga Tanzania. Ahsante sana.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Miaka ya 60 Malaysia walichukua mbegu hapa kwetu Tanzania na zao hilo limekuwa kubwa sana na ni zao lao kuu la biashara hivi sasa. Je, kwa nini sasa Serikali haioni haja ya kuliendeleza zao hili kwa sababu Wananchi wanalima kwa kutumia zana duni sana na hasa ukizingatia kwamba imethibitika hayana madhara kwa afya ya binadamu?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mhonga Ruhwanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli analosema kwamba, nchi nyingi zimekuja Tanzania zimechukua mbegu za mazao mbalimbali na pengine zimefanikiwa kulikoa hata Tanzania. Katika jibu langu la msingi, mambo niliyokuwa ninayaelezea hapa kuhusu kazi ambayo *SIDO* imefanya ya kujenga viwanda mbalimbali katika mitaa mbalimbali Kigoma na Tanzania kwa ujumla, ni dhamira ya dhati kwamba, Serikali haijalala, inaendeleza zao hilo. Ninaomba tushirikiane ili wakati wenzetu ambao wamechukua mbegu hapa wananufaika na sisi kama nchi, tuweze kutumia fursa tuliyonayo kunufaika.

Mheshimiwa Spika, tushirikiane kwa pamoja badala ya kulaumu tu wale wenzetu, lakini Serikali iko makini na mambo niliyoyasema hapa ni ushuhuda. Hata kwenye bajeti yangu nitakayoitoa, nitaeleza kwa undani juu ya kuviendeleza viwanda hivyo. Ahsante sana.

Na. 356

**Kiasi cha Misaada na Mikopo Kutoka Nje kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 na 2009/2010**

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA** aliuliza:-

(a) Je, kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita (2009 na 2010) Tanzania ilipata misaada na mikopo kiasi gani kutoka nje?

(b) Je, katika misaada na mikopo hiyo na kwa mgawo wa 4.5% ni kiasi gani kilikwenda Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Khalifa Suleiman Khalifa, Mbunge wa Gando, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilipata misaada na mikopo ya masharti nafuu, yenye thamani ya jumla ya shilingi za Kitanzania trilioni 2.341 kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009 na shilingi za Kitanzania trilioni 2.413 kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa makubaliano yaliyopo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), SMZ hupokea mgao wa misaada ya kibajeti wa 4.5% kwa ajili ya malengo yafuatayo: Kukuza uchumi na kupunguza umaskini; kuboresha hali ya maisha ya Wananchi na ustawi wa jamii; kuimarisha Utawala Bora na uwajibikaji kwa Wananchi; na kuimarisha usimamizi wa uchumi jumla, ikiwa ni pamoja na usimamizi wa matumizi ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kutokana na makubaliano hayo, kiasi cha misaada na mikopo ya Kibajeti na Miradi ya Maendeleo iliyokwenda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni Shilingi za

Kitanzania bilioni 93.54 kwa Mwaka wa Fedha wa 2008/2009 na Shilingi za Kitanzania bilioni 112.56 kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010.

**MHE. KHALIFA SULEIMAN KHALIFA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na pia ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake.

Mheshimiwa Spika, ukiliangalia swali namba 350 na swali namba 356 la kwangu mimi, maudhui yake yanalingana, lakini nimeshtuka kuona majibu ya Serikali hii hii moja yana tofauti kubwa sana! Mfano, Mheshimiwa Waziri wa Muungano amesema kuwa, misaada iliyokwenda Zanzibar mwaka 2008/2009 ilikuwa bilioni 23.04 na mwaka 2009/2010 ilikuwa bilioni 36.7, lakini Naibu Waziri wa Fedha anasema mwaka huo wa 2008/2009 ilikuwa ni bilioni 93.54 na mwaka 2009/2010 ilikuwa bilioni 112.56!

(i) Inakuwaje Serikali hii hii moja ina majibu mawili yanayotofautiana sana? *(Makofi)*

(ii) Kwa hali hii inavyoonesha; je, tukifanya utafiti kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na tukaona kuwa kilichokwenda hakioani na maelezo haya; je, Serikali inachukua ahadi ya kulipa hilo pengo litakalojitokeza kama inavyoonesha hapa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khalifa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, la kwanza; ni kweli kwamba, kuna tofauti ya *figures* ambazo zimetoka lakini pia kuna tofauti ya maudhui. Kwa *figure* ambazo nimetoa mimi, zinajumuisha Miradi ya Maendeleo ambayo orodha yake ninayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake (b); kwa sababu, *figures* zipo na ushahidi upo, sidhani kama kutakuwa na haja ya kuweka ahadi kwamba, tutarudishiana.

**MHE. ZAHARA HAMAD ALI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Kwa idhini yako, ninaomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha, swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, mgawo wa 4.5% uliwekwa na Mshauri Mwelekezi kama mgawo na tutumie kwa muda. Je, ni lini mgawo wa kudumu utakamilika na kuondoa malalamiko yaliyopo katika pande zote mbili za Muungano? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na yeye kwamba, mgawo wa 4.5% uliwekwa mwaka 1994 na Mtaalamu Mwelekezi na ni vigumu kusema lini utabadilika, lakini ni hivi karibuni kwa sababu mchakato upo karibu kukamilika wa kuwezesha kupata mgawo wa aina nyingine kama itawezekana.

Na. 357

**Kero Kubwa Ndani ya Shirika la Bima kwa Wanachama Wake**

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR (K.n.y. MHE. CLARA DIANA MWATUKA)** aliuliza:-

Mashirika ya Umma ikiwemo Shirika la Bima *(NIC)* hutumia lugha ya kuvutia pale wanapotaka Wanachama lakini ifikapo muda wa Wanachama kudai haki zao hutokea mzunguko na kero kubwa kwa mhusika kupata stahili zake:-

(a) Je, Shirika halioni kuwa kwa kupoteza mafaili ya Wanachama kiutatanishi na kuwapa stahili zao pungufu na inavyostahili ni kuwadhulumu Wanachama?

(b) *SACCOS* pia huchukua fedha za Wanachama na kutumia kwa muda mrefu bila kutoa fidia; je, Serikali haioni kuwa Wanachama wanadhulumiwa haki zao?

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu. Nimekunyima swali la nyongeza, nilifikiria wewe ndiyo Mwatuka, *sorry*.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ninapenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, Shirika la Bima la Taifa, halijapoteza mafaili ya Wanachama wake na ndiyo maana hata sasa linapolipa madai, linatumia mafaili ya Mwanachama *physical file* na siyo vinginevyo. Serikali inachukua hatua za makusudi kuhakikisha kwamba, Shirika linalipa wateja wake stahili zao bila upungufu wala dhuluma yoyote.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulijulisha Bunge lako kwamba, mafaili ya Wanachama wote wa bima za maisha na zisizo za maisha, yapo yametunzwa katika stoo maalum. Kwa kutumia mafaili hayo, Shirika linaweza kuchambua na kuhakiki madai kama yanavyowasilishwa na wateja na hivyo kulipa madai kulingana na makubaliano ya Kimkataba baada ya uhakiki.

(b) Mheshimiwa Spika, katika mazingira ya kawaida, *SACCOS* ni miongoni mwa vyama vya hiyari, demokrasia na uwazi. Aidha, kanuni na taratibu zinazoongoza *SACCOS,* huandaliwa na kupitishwa na Mkutano Mkuu wa Wanachama wote.

Wanachama wapya nao watahamasika kujiunga na *SACCOS* husika endapo tu kanuni na taratibu zilizopo wataona zinawafaa. Kwa hiyo, kwa kutumia utashi wa kawaida wa kibinadamu, hatutarajii kuwa wanachama watajiwekea kanuni na taratibu zilizo kandamizi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli huu, mara nyingine panaweza kutokea ukiukaji wa kanuni na taratibu katika uendeshaji wa *SACCOS.* Serikali inawashauri Wanachama kuchagua Viongozi waadilifu na mara zote kufanya shughuli zao kwa kufuata kanuni na taratibu walizojiwekea.

Mheshimiwa Spika, sisi Waheshimiwa Wabunge, tunafahamu umuhimu, faida na namna *SACCOS* zinavyoendeshwa. Rai yangu kwa Waheshimiwa Wabunge ni kuendelea kuuelimisha umma ili Wananchi waendelee kupata faida kutokana na taasisi hizi muhimu.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri na mipango mizuri; je, mbona Wananchi bado wanapata usumbufu mkubwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba, hapo nyuma Shirika la Taifa la Bima lilikuwa na matatizo na hata kushindwa kuwalipa, licha ya kuwapunja hata kuwalipa ilishindikana kabisa, lakini sasa baada ya kufanya marekebisho, restructuring, Shirika linaendelea kulipa na hakuna tatizo tena la namna ile.

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Shirika lina madeni mengi; jambo ambalo limeshindwa kutoa ushindani kibiashara; je, Serikali inasema nini kuhusu hili?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. PEREIRA AME SILIMA):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salim, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba, Shirika lilikuwa na matatizo kama nilivyosema kwenye swali la nyongeza la mwanzo, lakini sasa hivi fedha zipo na madai yanafanyiwa uhakiki na tayari

wameanza kulipa na matarajio ni mazuri sana, kwa sababu hela ipo ya kutosha, mwenye madai aende.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha pia na maswali yenyewe yamekwisha. Katika swali namba 355, ambalo Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera aliuliza, ninaona ofisi yangu mlisema ni Viti Maalum, huyu ni Mbunge wa Kasulu Vijijini, ninaomba rekodi ikae vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wachache ambao tunawatambulisha; kwanza kabisa, tuna Mheshimiwa Mericy Mussa Emmanuel, yeye ni Mbunge Mstaafu kipindi kilichopita, ahsante sana; ni vizuri kuja kututembelea, siyo kwamba, mkishastaafu ndiyo basi hamtakiwi kuja mnatakiwa kuja ili tuwe tunaonana. Ahsante, karibu sana, tumefurahi kukuona. *(Makofi)*

Tuna wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo, hawa Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma, ninafikiri jana walikuwepo; sijui wako wapi, wako upande huu; ahsante, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 50 na walimu wao kutoka Shule ya Sekondari ya Ibra Dodoma; wako wapi na walimu? Ninadhani wamekosa nafasi watapata mchana. Kuna wanafunzi 80 na walimu watano wa Shule ya Msingi ya Alliance, Arusha; wako wapi na walimu? Karibu sana. Tunashukuru walimu kuwaleta watoto waweze kuliona Bunge lao. *(Makofi)*

Kuna wanafunzi 47 na walimu wawili wa Shule ya Sekondari ya Jikole. Wanafunzi wa Jikole na walimu wao; ahsanteni, karibuni sana. Tuna wanafunzi 47 na walimu wao watano kutoka Shule ya Msingi *Rainbow* Dodoma, ninaona leo ni kundi lingine jana walikuja wengine; karibuni sana na endeleeni kusoma vizuri. *(Makofi)*

Tunaye Mheshimiwa Dkt. Said Gharib Bilal, ni Mbunge wa Afrika Mashariki, ahsante sana, tumefurahi kukuona.

Tunaomba tuwakaribishe na wageni wengine wote, Bunge ni la watu wote.

Shughuli za kazi; leo nina tangazo moja tu; Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Prof. David Mwakyusa, anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati yake kwamba, leo saa saba na robo, kutakuwa na Kikao cha Kamati, ambacho kitafanyika katika Ukumbi Namba 227, kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati hiyo wanataarifiwa.

Baada ya maelezo hayo, Waheshimiwa Wabunge, tuna Waziri wa Nchi.

**HOJA YA KUTENGUA KANUNI ZA BUNGE**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, ninaomba radhi, jana nilitoa maelezo kutengua hoja ambayo Waheshimiwa Wabunge, watanivumilia niyatoe tena leo baada ya kufanya marekebisho mengine, kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1) ya Kanuni zetu za Kudumu, Toleo la 2007.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mkutano wa Nne wa Bunge unaoendelea umepangwa kumalizika tarehe 26 Agosti, 2011; na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2), Bunge linakutana hadi saa saba mchana, ambapo Spika ataahirisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa kumi na moja jioni; na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, kifungu cha 28(4), Bunge huendelea kukaa mpaka saa 1.45 usiku ambapo Spika husitisha shughuli na kuliahirisha hadi tarehe na siku nyingine inayofuata; na kwa kuwa kwa mujibu wa Kanuni ya 104(1), wakati wa Kamati ya Matumizi, Mwenyekiti ana mamlaka ya kuongeza dakika zisizozidi thelathini, iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha Kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kupitisha mafungu; na kwa kuwa ndani ya kipindi hiki cha Mkutano wa Nne kilichobakia, waumini wa Dini ya Kiislaamu watakuwa kwenye Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambao umeanza jana tarehe 1 kwa kipindi cha mwezi mmoja; na kwa kuwa Waumini wote wa Kiislamu waliofunga hutakiwa kuswali na kufuturu kila siku ifikapo saa 12.30 jioni; ili

kuliwezesha Bunge kutekeleza shughuli zote zilizopangwa kikamilifu na kwa wakati huo huo kuwawezesha Waheshimiwa Wabunge ambao ni Waumini wa Dini ya Kiislaamu waweze kuswali na kufuturu kwa wakati mwafaka kwa mujibu wa taratibu za Dini yao; inabidi Bunge litengue Kanuni kadhaa za Bunge zinazotumika kwa sasa kwa mujibu wa Kanuni ya 150(1); na kwa kuwa Kikao cha Kamati ya Uongozi kilichofanyika jana kwenye Ukumbi wa Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wote Kamati za Kudumu za Bunge wamekubaliana na umuhimu wa kutengua Kanuni husika; hivyo basi, Bunge linaazimia kwamba, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa shughuli za Bunge katika Mkutano huo wa Nne, Kanuni ya 28(2)(4) na Kanuni ya 104(1)(2) zitenguliwe kama ifuatavyo:-

(i) Kanuni ya 28(2) ambayo kwa ujumla wake inaeleza kwamba, Bunge litakutana saa saba mchana ambapo Spika ataahirisha shughuli yoyote itakayokuwa inafanyika hadi saa 11.00 jioni itenguliwe na badala yake Bunge likutane hadi saa saba na robo mchana ambapo Spika ataahirisha shughuli hadi saa kumi na moja jioni.

**SPIKA:** Saa kumi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)**: Saa kumi jioni samahani.

(ii) Kanuni ya 28(4) ambayo kwa ujumla wake inaelekeza kwamba, Bunge litaendelea kukaa hadi saa moja na dakika arobaini na tano usiku, ambapo Spika atasitisha shughuli na kuliahirisha hadi kesho yake itenguliwe na badala yake Bunge liendelee kukaa hadi saa kumi na mbili na nusu jioni.

(iii) Kanuni ya 104(1) ambayo kwa ujumla wake inampa mamlaka Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Matumizi kuongeza dakika zisizozidi 30 iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia muda wa kuahirisha Kikao cha Bunge na Kamati ya Matumizi bado haijamaliza kupitisha mafungu itenguliwe na badala yake Mwenyekiti asiongeze muda wowote katika hatua hiyo. *(Makofi)*

(iii) Kanuni ya 104(2) ambayo kwa ujumla wake inaidhinisha kupitisha mafungu yote yaliyobakia kwa pamoja baada ya Mwenyekiti kuwa ameongeza nusu saa itenguliwe na badala yake utaratibu ufuatao ufuatwe kwamba, iwapo zimesalia dakika kumi kabla ya kufikia saa kumi na nusu na Kamati bado haijamaliza kufikia mafungu yote yanayohusika, Mwenyekiti atafunga mazungumzo yoyote yanayoendelea na papo hapo atawahoji kuhusu mafungu yaliyosalia kama yapo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UCHUKUZI (RELI, BANDARI NA USAFIRI WA MAJINI):** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Bunge liliafiki Utekelezwaji wa Hoja iliyotolewa)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyosema jana, pale tulipokutana tayari watu walikuwa wameanza kufunga, kwa hiyo, tulikuwa tuna matatizo ikabidi tumalize saa moja kasorobo. Sasa tumeangalia tutakuwa tunaahirisha mchana, saa saba na robo, tutarudi saa kumi, tukirudi saa kumi tunamaliza hapa saa kumi na mbili na nusu. Kwa hiyo, hawa jamaa zetu wanaweza kufanya shughuli zao kwa urahisi zaidi kuliko kukimbizana na muda. *(Makofi)*

Pili, kwa mujibu wa kifungu cha 104, ukiongeza dakika thelathini zile anazoongeza Spika, zikibaki dakika kumi ndiyo tuna *guillotine.* Sasa mkifanya hivyo, basi mtalala humu humu ndani. Kwa hiyo, saa kumi na mbili na nusu ni saa ya kufunga, hakuna kuongeza muda. Hii ni sehemu mojawapo na sisi pia kujitolea na kujitoa kwa ajili ya wenzetu wanaofanya kazi hii ya kufunga kwa niaba yetu wote. *(Makofi)*

Kikubwa sasa, Waheshimiwa Wabunge, wanapojibu Mawaziri maswali mliyouliza au mliyoandika, wengine hamuwi ndani, matokeo yake sasa unauliza swali ambalo lilishajibiwa hapa. Sasa unakuta ni *repetition*, ambayo Bunge inakataa. Halafu ya pili, wametuambia hata Wananchi, hizi habari za kusalimia wake zetu na watoto wetu na nani; wanajua mpo hapa mnapoteza muda; ni vizuri ukaenda kwenye hoja yako uliyojipanga vizuri ukamaliza kabla ya wakati wako na ikawa vizuri.

Halafu kwenye Kamati ya Matumizi, leo tukimaliza saa saba na robo, atafuata Waziri, halafu itafuata Kamati ya Matumizi. Kamati ya Matumizi, Mshahara wa Waziri msiulize kwamba na kijiji changu kile kilifanya nini; ni maswali ya Sera, unauliza kitu kidogo tu, kwa sababu hapa ninajua itakuwa barabara yangu itajengwa lini. Kanuni zinakaa, kama haipo humu ndani haiwezi kujengwa kwa sababu umeuliza hapa. Kwa hiyo, mnatakiwa mjifunze kwa mtindo huo.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru. Tunaendelea na shughuli za leo. Mheshimiwa Lucy Owenya; kitu gani?

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, Kanuni ya 68(7), niisome?

**SPIKA:** Ninajua hebu eleza *issue* yako.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, hoja yangu inahusu mjadala unaoendelea kuhusu Wizara ya Ujenzi; jana baadhi ya Wabunge wamekuwa wakichangia na kusema kwamba, Mkoa wa Kilimanjaro unapendelewa kuhusu barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Barabara Kuu kuelekea Dar es Salaam…

**SPIKA:** Sasa wewe mwongozo unataka kusema nini? Usinieleze tena.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mwongozo ninaotaka kusema ni kwamb, Bunge linaelekea kuleta ubaguzi, sisi ni Watu wa Kilimanjaro, ni Watanzania kama wao, ninaomba ukemee tabia hii kwa sababu hata sisi tunahitaji barabara ya lami, imepita kwenye Barabara Kuu kama ilivyotoka Dar es Salaam mpaka …

**SPIKA:** Haya sasa usichangie, ulichosema ni kwamba, tusilete ubaguzi. Waheshimiwa Wabunge, jana nilikuwa nimemwacha Mwenyekiti anaendesha kikao hapa; kwanza kabisa, mtu anapewa nafasi ya mwongozo kumbe anataka kuhutubia Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, Mwongozo hupaswi kuhutubia, alihutubia Mheshimiwa Ole-Sendeka, alihutubia Mheshimiwa Deo Sanga, sasa sivyo hivyo. Wakati wa kujadiliana, kama tutafanya uvumilivu anayejadili ndiyo amepewa nafasi kujadili, sasa kama hupendi kumsikiliza wewe mwache aseme amalize. Ukitaka na wewe useme kama anavyosema yeye huwezi.

Waheshimiwa Wabunge, mtu akipewa nafasi yake mwache aseme anavyoona yeye, watakuja kujibu kwa nini barabara ziko wapi na nyingine ziko wapi, lakini wewe uliyesema uwe na uhakika na unachokisema; msije mkaigawa nchi hii. Barabara ni *network*, hata ukijenga barabara kutoka nyumbani kwa mtu, barabara ni mtandao.

Kwa hiyo, ninaomba sana muwe na uvumilivu, mtu akipewa nafasi yake mwacheni aseme anavyoona yeye na kwa sababu ni Mbunge wa eneo fulani, atahukumiwa yeye mwenyewe huko huko, mimi wala sina tatizo, kwa sababu wote wanaofanya vurugu hapa wameletwa na hao waliowaleta, kama waliwaleta watu viboko huku watajua wenyewe sasa. Sisi itakuwa kazi yetu ni kumwambia Mheshimiwa na waliomchagua wamshangae kwamba, walimchagua mtu wa namna gani, hamna namna nyingine. *(Makofi)*

Kwa hiyo, huyu anayesema ninaomba mwongozo usitumike mahali pa kuhutubia wengine ni kutaka mwelekeo tu basi. Tunaendelea tusianze kujibishana. Katibu kwa hatua inayofuata.

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi kwa Mwaka 2011/2012

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MHE. ANNA M.J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia katika Wizara ya Ujenzi. Aidha, nichukue nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu......

**SPIKA:** Wanaotoka nje watoke kimyakimya!

**MHE. ANNA M.J. MALLAC:** Aidha, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na nguvu ya kuweza kusimama mbele yako. Vile vile nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru Viongozi wa Chama changu cha Demokrasia na Maendeleo kwa kuniweka mahali hapa nilipo, nasema ahsante sana na Mungu awazidishie afya njema.

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye mchango wangu kwa Wizara ya Ujenzi. Pamoja na kuisikiliza vizuri hotuba ya Waziri wa Ujenzi, napenda nijikite zaidi kwenye barabara za vijijini. Barabara za vijijini zimesahaulika sana kwa sababu vijijini ndiko wanakoishi Watanzania maskini ambao wanategemea kilimo. Barabara za vijijini zimesahaulika sana kiasi kwamba wananchi ambao ni wazalishaji kwa kutumia kilimo hawana barabara za kupitisha mazao yao kuleta mjini kwa ajili ya matumizi ya kawaida au kutafuta masoko. Nitolee mfano kwa Wilaya yangu ya Mpanda, kutokana na miundombinu mibovu ya barabara na ukizingatia Wilaya yetu tunazalisha sana mahindi, mpunga na tuna mazao ya biashara kama tumbaku, miwa ambayo ni laini sana ambayo hata kibogoyo anatafuna na mengine mengi kama madini ya dhahabu, tuna *green Tomalin*, tuna *copper* na mengineyo. Lakini tumekuwa tukiachwa nyuma sana na badala yake tunachanganyikiwa, ndiyo maana tunajikuta kama wananchi wa Sumbawanga tunaamua kunywa pombe kwa hasira zote kwa sababu ya uchungu wa kukosa barabara.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri anapotenga fedha za kutengeneza barabara awajali sana Wakurugenzi wetu kwa kuwapelekea fedha katika Halmashauri ili waweze kuwakumbuka wananchi wa vijijini ili waweze kupita kwa urahisi katika kutafuta huduma za afya, elimu na maji. Kwa kweli wananchi wa vijijini wanahangaika sana jamani, wanapofuata huduma za afya ukizingatia vijiji vyetu bado unatembea zaidi ya kilomita tano kuitafuta afya, Zahanati ipo mbali zaidi ya kilomita tano, lakini mwananchi anatembea kwa kubahatisha kwa kupitia zile barabara walizotujengea watani zetu Wasukuma wanapochunga ng'ombe. Basi ndiyo wanapopita humo katika kutafuta huduma ya afya. Kwa hiyo, wananchi wanahangaika sana, naomba Waziri asikie, ajipange na ikiwezekana tafuta muda uje utembelee vijiji ambavyo nakutajia.

Mheshimiwa Spika, vijiji hivi ni Kambanga hadi Bujombe hawana barabara wanapita kwa kubahatisha, Sikonge hadi Bugwe wanaishi kama vile hawako duniani na kama siyo Watanzania, Mpanda Ndogo hadi Ngoma Lusambo nilikwenda kufanya mkutano huko ilikuwa ni balaa, nilirudi na makovu kwa mieleka ya pikipiki, walikuwa wamenipakia watoto wangu. Kwa kweli inasikitisha sana, sijui wao wenyewe wanafanyaje kiasi kwamba ukitaka kwenda huko kwa usafiri wa gari inabidi kwanza kuwe na mtu ambaye umemwandaa wa kutembea, analaza majani ndipo gari lipite, pia inabidi akupe taarifa kwamba hakuna visiki wala vichuguu ndani ya barabara ile. Naomba muwakumbuke sana watu wa vijijini nao ni watu na ni sehemu ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni Kijiji cha Itenga hadi Kakese, hawa ni wazalishaji wazuri sana wa zao la mpunga, lakini wanapovuna wanajikuta wanakosa kupeleka mazao yao sokoni kwa ukosefu wa barabara. Wanakwenda wanabahatisha tu kwenye mashamba hatimaye kutokeza kwenye barabara kubwa.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti yako vilevile sijasikia barabara zilizotajwa kama vile Mpanda Mwese na Mpanda Kalema na Mpanda Mpimbwe. Barabara hizi kwetu wana Mpanda

ni muhimu sana, kwani hizi ndizo zinazoleta mawasiliano kati ya Tarafa na Makao Makuu ya Wilaya ya Mpanda Mjini. Vile vile barabara hizi zikitengenezwa zitaleta faida hata katika kunasa wakimbizi katika Ziwa Tanganyika kwani hawa wakimbizi wanaorudi kwa njia za panya wamezagaa sana katika Tarafa ya Kalema, wamezagaa huko Mishamo na juzi juzi wamechomana visu sidhani kama hizo taarifa zimewafikia. Kwa hiyo, naomba hizi barabara ziwekwe kwenye bajeti. Mheshimiwa Waziri afanye maarifa yako yote, akija Mpanda itabidi tutembelee mimi na yeye katika hizi barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda tena kuongelea suala la majengo. Majengo ya nyumba za watumishi hasa wao wenyewe wa Idara ya Ujenzi kwa kweli ukiziona ni za miaka nenda rudi. Vyoo vimejaa vimefurika na kutapika, majumba yamechakaa huwezi kufananisha na viongozi wanaoishi ndani yake, zimekuwa kama nyumba za kupigia ramli. Naomba muwakumbuke, hizi nyumba zikarabatiwe, zimechoka kwani zimekuwa ni za muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya kutoka Ipole-Inyonga mpaka Mpanda, barabara hii pamoja na kwamba haina madhara sana lakini naomba vile vichuguu na kalvati zina miinuko mikubwa sana kiasi cha kuhatarisha maisha kwa wasafiri. Pia katika barabara hiyo kuna sehemu ukitoka Urwira kuelekea Mpanda kuna daraja linaloitwa Nzaga, daraja lile limejengwa mwezi Desemba 2006 lakini mpaka leo ninavyoongea lina mipasuko na limetitia. Kwa kweli unapopita pale inabidi ushike roho mkononi upige ishara ya msalaba ndiyo upite. Naomba Mheshimiwa Waziri aliandike, akaliangalie na alidadisi ili lifanyiwe matengezo, ni hatari kwa sababu ile njia inatumiwa na mabasi yanayobeba roho za watu na magari yanayobeba mizigo kama tumbaku, mbao, mahindi na kadhalika. Naomba nalo liwekwe kwenye bajeti yake.

Mheshimiwa Spika, vilevile natoa wazo kwamba miaka ya nyuma nilikuwa naona kuna magenge katika barabara, yale magenge wale wafanyakazi walikuwa wanafanya kazi za dharura barabara zinapoharibika. Sasa ukiangalia Mkoa wetu wa Katavi Wilaya ya Mpanda bado tuna zile barabara zinazotumia changarawe, bado hatuna lami. Kwa hiyo, inapofika masika barabara zile zinaharibika kwa haraka sana lakini kama hayo magenge yangerudishwa ingekuwa ni vizuri sana kuliko inavyotumika sasa barabara zikiharibika inabidi mpaka watangaziwe Wakandarasi ndiyo waanze kutoa maombi, Mkandarasi achaguliwe ndiyo kwenda kutengeneza huku wananchi tayari tumeathirika. Naomba na kupendekeza kwamba yale magenge yangerudishwa. Isitoshe barabara hiyo ya Inyonga ina eneo kubwa sana la mapori kiasi kwamba hata utekaji vilevile kwa kweli tunakwenda na roho mkononi. Naomba Waziri afikirie sana.

Mheshimiwa Spika, naona niishie hapo na huo ndiyo mchango wangu, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante na sasa nimwite Mheshimiwa Mntangi.

**KUHUSU TAARIFA**

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Spika, taarifa !

**SPIKA:** Nani anasema taarifa? Nimeshamwita mtu mwingine anazungumza. Endelea Mheshimiwa Mntangi.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba ya Wizara hii muhimu sana kwa Taifa letu. Lakini vile vile naomba nichukue nafasi hii kuwapongeza viongozi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wamefanya na jinsi hotuba yao ilivyoandikwa. Lakini kubwa zaidi ni jinsi ambavyo kwa kisayansi walivyofanya utaratibu wa kutuwezesha Wabunge wakati hotuba inaendelea kuona vigezo vya kazi ambazo wamefanya katika *screen* ndani ya Bunge. Nawapongeza sana kwa utaalam huo.

Mheshimiwa Spika, mtandao wa barabara sasa hivi umefikia kilomita zaidi ya 85,000, kiasi hiki Kitaifa bado ni kidogo lakini tumepiga hatua ni vema tukafahamu kwamba huko vijijini hatujakugusa sana. Kwa hiyo, japokuwa tuna mtandao wa kilomita 85,000, bado zipo kilomita

nyingi zaidi vijijini ambazo bado hatujazigusa. Waheshimiwa Wabunge wanafahamu huko kwenye Kata na kwenye Vitongoji bado hali siyo nzuri, inawezekana takwimu ambazo mmezipata kama Wizara kutoka katika Halmashauri bado siyo sahihi za kutosha. Tunahitaji kuongeza mtandao na lazima tujiandae.

Mheshimiwa Spika, nianze kuzungumzia hali halisi kwa kadri ninavyoiona, kila mara Waheshimiwa Waabunge wamekuwa wakitamani sana barabara zao zipandishwe daraja kwa sababu moja kubwa ambayo ni ya kweli kwamba fedha zinazopelekwa katika mfuko wa barabara katika Halmashauri zetu ni ndogo kiasi kwamba haziwezi kutengeneza barabara zenye urefu ambao upo ndani ya Halmashauri zetu. Mara kwa mara hili limekuwa likitokea na *TANROADS* wamekuwa wakiomba wakubali barabara hizo kupandishwa daraja.

Mheshimiwa Spika, lakini lipo jambo moja kuhusu uwezo wa *TANROADS*, jukumu tunalotaka kuwapa la kuwaongeza uwezo au *network* yao kwa sababu kwa mtandao uliopo sasa hivi wana kilomita 33,000 ambazo ni Taifa 12 na zile za Mkoa 21,000. Kwa hiyo, tunaposema tunapandisha daraja maana yake tunataka kuwaongezea *network* kubwa zaidi watu wa TANROADS, hilo ni sahihi. Lakini lazima liendane na jambo moja muhimu sana kwamba lazima tuiboreshe *TANROADS* ili tuweze kuijengea uwezo mkubwa zaidi ili waweze kuhudumia *network* kubwa zaidi. Bila kuwapa elimu ya kutosha, bila kuongeza idadi ya Watendaji na bila kuwapa fedha haya majukumu tutakayokuwa tukiwaongeza kila siku tutafika mahali badala ya *TANROADS* kuwa *efficient* itaanza kudidimia na utendaji kazi wake utashuka.  Kwa hiyo, jambo moja kubwa ambalo ni lazima tuchukue hatua ni kuimarisha *TANROADS* sasa.

Mheshimiwa Spika, lakini lazima tuiimarishe *TANROADS* kwa sababu tunataka kuwapa majukumu makubwa zaidi. Hili la kupandisha hadhi barabara za Wilaya tuna kazi moja kubwa sana tunataka kuikabidhi *TANROADS*. Tunataka *TANROADS* isimamie suala zima la kuondoa msongamano wa magari katika Jiji la Dar es  Salaam. Tukisema kazi hii tuziachie Halmashauri za Majiji yaani Temeke, Ilala na Kinondoni itachukua muda mrefu sana kwa sababu tuna dhamira ya kutaka hili lifanyike. Jukumu likabidhiwe *TANROADS*, watazame mfumo wa namna ya kutekeleza mapendekezo  ambayo hata Kamati yangu imeyatoa juu ya barabara zile. Kwa hiyo, chombo ndani ya chombo kiundwe kwa ajili ya kusimamia mpango huo wa kuondoa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam na tunasema si Jiji la Dar es Salaam tu, sasa hivi angalau tuanze kwa Jiji la Dar es Salaam na Mwanza halafu twende hatua kwa hatua kila mwaka kwa sababu na miji mingine inaendelea kukua, miji hiyo ni kama Tanga, Mbeya, Arusha na hata Dodoma, hali hiyo ni lazima itatokea. Kwa hiyo, tufanye maandalizi mapema kabla mambo hayajawa mabaya.

Mheshimiwa Spika, nirudi Muheza. Muheza tuna mpango wa barabara ambao upo katika mpango unaoitwa *PMMR*. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri *PMMR* imeonyeshwa katika ukurasa wa 90, lakini katika ukurasa wa 90 kilichoonyeshwa  ni kilomita tu ambazo zipo chini ya mpango huo lakini hazikuelewa kwamba zipo wapi na utaratibu wake uko wapi na mpango wake wa fedha zitatoka kwenye Mfuko wa Taifa lakini hata ni kiasi gani kimetengwa kwa mpango huo wa *PMMR* hakikuelezwa.

Mheshimiwa Spika, lakini *PMMR* imekuja katika Mkoa wa Tanga na hivyo ipo *PMMR* upande wa *Tanga East* na *Tanga West.* Barabara zilizopo katika mpango wa *PMMR Tanga East* zinagusa Wilaya ya Pangani, Tanga na Wilaya ya Muheza. Katika kipindi cha miaka miwili iliyopita tangu Mkandarasi aliyeteuliwa kufanya kazi hiyo kufanya kazi kwa miaka miwili imepita hakufanya jambo lolote. Katika semina ambayo Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Tanga tulipata Jijini Tanga kuhusu mpango huo, Mtaalam Mwelekezi *Company Consultant* alituhakikishia  kwamba barabara ya kutoka Muheza kwenda Amani *performance* ilikuwa sifuri kwa kipindi cha miaka miwili na Mkandarasi yule amelipwa fedha zaidi ya shilingi 900 milioni. Amelipwa na kazi hakufanya na bado yuko kwenye eneo la *sight* mpaka leo. Yeye anakuja na maneno mengi kwamba nitafanya kazi, lakini nenda kwenye *sight* anapeleka greda hata matairi hakuna. Sasa hali hii inasikitisha sana.

Mheshimiwa Spika, naiomba *TANROADS* ambayo ndiyo wasimamizi wa mpango huo wachukue hatua madhubuti, hatuwezi kuendelea namna hiyo. Barabara kwa miaka miwili haitengenezwi, Mkandarasi bado yupo. Lakini nawaomba pia Wataalam wa *TANROADS*

mtuangalizie hawa, kampuni zipo mbili, nilishazungumza hapa Bungeni kwamba ukienda kwa *Registrar of Companies* kupekua jinsi zilivyoandikishwa majina ya kampuni hiyo ya *Y&N* na Laki ni watu walewale. Kimsingi ni sawa mnasema zipo kampuni mbili lakini zinamilikiwa na mtu mmoja na wakifanya *tender* kwa mfano *tender* iliyofanywa ya barabara ya Raskazoni Tanga walio-*quote* kwenye *tender* ni kampuni hizo hizo mbili yaani *Y&N na Laki* peke yao eti wanashindana mmoja kaweka milioni 200 na mwingine ameweka milioni 150 maana yake anapata wa pili ambaye ni kampuni ya mtu huyo huyo mmoja.

Kwa hiyo, ndugu zangu tuwe makini na tuitendee haki Wilaya ya Muheza na Pangani, hatuwezi kuendelea, tumekaa katika Wilaya tumemkataa Mkandarasi. Katika kikao cha *RCC* Mkoa , tamko limetolewa, tumemkataa ....

**MBUNGE FULANI:** Lakini bado yupo!

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Lakini bado yupo! Sasa Mkoa hawamtaki, Wilaya imemkataa, nani anamng'ang'ania huyo na kwa sababu gani? Si kwamba ameharibu tu barabara za Tanga Mjini, Tanga barabara za Raskazoni na ukienda Kinondoni kaharibu *record* yake siyo nzuri. Kwa hiyo, naomba zichukuliwe hatua zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, la pili, katika barabara ya Muheza kwenda Amani walijitokeza Watanzania wanaoishi Marekani, walikuja Tanzania kwa lengo la kutaka kusaidia Taifa hili katika utengenezaji wa barabara kutumia kemikali ambazo zinaitwa *TerrainZyme* na wakajitolea kutengeneza kilomita nne katika barabara ya Muheza-Amani na wakasema kwamba tunazitengeneza kwa gharama zetu, leteni wataalam wenu tuwafundishe. Wamekwenda wameshuhudia kazi imefanyika kilomita nne na wakasema mwaka mmoja tunataka itumike hii barabara halafu muangalie hali itakavyokuwa. Ndugu zangu napenda niwathibitishie kwamba tangu barababara hii imetengenezwa mwezi Julai mwaka 2010 hadi sasa mwezi Julai 2011 barabara ile ni imara na inapitika, haina matatizo makubwa.

Mheshimiwa Spika, cha msingi ni nini? Shabaha yao ni kusaidia Tanzania kwamba hivi sasa tunatengeneza barabara nyingi sana za udongo na changarawe na kila mwaka zinarudiwa, kwa hiyo, gharama ya kuzitengeneza ni kubwa sana. Kwa kutumia mpango huo ambao wametuonyesha kipande hicho cha barabara kilomita nne zilizotengenezwa barabara hiyo haitatengenezwa tena kwa kipindi cha miaka mitatu inayokuja. Maana yake ni nini? Maana yake fedha zile ambazo tungezitumia kwa kipindi cha miaka mitatu kutengeneza hizo kilomita nne ni dhahiri kwamba fedha hizo sasa tutazitumia kwa dhamira hii niliyosema ya kuongeza mtandao wa barabara hapa nchini. Tunaomba *TANROADS* ambao ndiyo waliosimamia utekelezaji wa mpango huo watuambie sasa, je, mpango ule unatufaa Watanzania?

Mheshimiwa Spika, nikipiga hesabu, kwa mfano, tukitengeneza kilomita 600 katika kila kilomita moja tunaokoa zaidi ya shilingi milioni tano kwa mpango huo. Kwa kilomita 600 kwa miaka mitatu ambayo hamtatengeneza barabara tutaokoa zaidi ya shilingi bilioni tisa. Hivi hatuna kazi za kufanya na shilingi bilioni tisa katika mtandao wa barabara hapa Tanzania kama tunaweza kweli tukaziokoa hizo na nina uhakika hizo zinaweza zikaokolewa. Lakini tuliache jambo hili mikononi mwa wataalam ili wataalamu wafanye hesabu zao kama hizi nilizozitolea mfano. Nimetolea kwa kiwango cha chini sana lakini wafanye wao.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo lingine moja kubwa sana ambalo nashauri ni kwamba, Wizara ya Ujenzi ina kitengo cha ushauri wa barabara. Kitengo hiki kishirikiane na vitengo vingine vya mazingira. Kuna Wizara inayoshughulika na mambo ya mazingira, waende wakasimamie watazame, je, mfumo huo unaweza kweli ukaharibu mazingira ya wale wanaoishi pale jirani? Ili tuwe waangalifu kwa sababu watakaopitiwa na barabara hizo ni Watanzania wenzetu. Kule Zanzibar mpango huu ulijaribiwa na ulishindwa, lakini kwa Tanzania Bara na hususan Muheza umefanikiwa na tunaambiwa vilevile katika eneo la Fami umefanyika na umekwenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, hawa Watanzania walioko Marekani wametupa nafasi wanasema, nyie Watanzania tumewafanyia kazi hiyo kwa mpango huo, tunawataka mtuletee watu wenu wasome. Ma- *engineers* waende Marekani kwa gharama zao hawa wenzetu Wamarekani ili

wakafundishwe namna ya kuitumia hiyo teknolojia. Vile vile wajue hiyo *terrainZyme* yenyewe inatengenezwa vipi. Wamesema mwezi Oktoba wako tayari kuwapokea Watanzania, ni juu yetu sasa kuitumia nafasi hiyo. Tuwatafute ma-*engineers* hawa waende Marekani, watajua enzyme hii maana yake ni nini, watajua namna ya kuitengeneza na watakapokuja watatusaidia katika hali yote ya kusimamia.

Mheshimiwa Spika, lakini ni lazima tuwaambie Watanzania hao wanaokwenda Marekani kwamba, watazame kwa umakini kama kuna madhara ya mazingira, ili watakaporudi watwambie tunaweza kuendelea na mpango huo au hatuwezi.

Mheshimiwa Spika, nilitaka niyaseme hayo kwa dhamira hiyo kwamba, tutazame teknolojia mpya zilizopo zitakazoweza kusaidia Taifa hili kupunguza gharama za kutengeneza barabara. Zipo teknolojia mpya za kisasa, kwa mfano, hiyo anayoizungumza ya Wamarekani, kinachofanyika pale ni kwamba greda inapita katika barabara ile na udongo ule ule wa eneo lile ndiyo unaokusanywa kutengeneza tuta lile la barabara.

**SPIKA:** Haya, asante!

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nishukuru sana kwa kupata fursa hii. Nianze kwa kuipongeza Wizara kwa juhudi kubwa iliyofanya na bajeti nzuri iliyotuletea. Kwa kweli kuna kila sababu ya kumshukuru Rais kwa kutuletea viongozi hawa katika Wizara hii ambayo ni Wizara chachu kwa maendeleo ya sekta zingine.

Mheshimiwa Spika, nasema hili nikiwa nimezingatia sana kazi ambayo imekuwa ikifanywa ya kuunganisha Taifa kutoka maeneo tofauti tofauti kupitia mpango wa kuunganisha mikoa kwa mikoa pamoja na barabara za Kitaifa. Wizara ilivyotoa takwimu kwamba ni kilomita elfu kadhaa kutoka barabara fulani kwenda barabara fulani, inawezekana wananchi wasielewe ni kitu gani hasa kinaongelewa kutokana na zile takwimu.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea barabara bora za kutoka maeneo kadhaa kuunganisha maeneo mengine, tunaongelea maisha ya kila siku ya wananchi wa Tanzania na inatoa majibu ya malalamiko mengi ambayo yamejitokeza kwa sasa ndani ya nchi, likiwepo lile la kupanda kwa gharama za maisha. Nitatolea mfano Mkoa wa Rukwa ambako ndiko, kuna chakula kingi cha akiba. Hadi juzi mmesikia wananchi wakisema wanakosa hata wahifadhi wapi mahindi waliyovuna ya mwaka jana na wanayotarajia kuvuna sasa. Barabara inapokuwa imekosekana hata kama magari yataweza kubeba mazao yale kupeleka sehemu yenye upungufu, lazima gharama ya usafirishaji itakuwa kubwa sana na kutokana na gharama za usafirishaji kuwa kubwa, bei nazo zinakuwa kubwa na hivyo kufanya gharama ya maisha izidi kupanda.

Mheshimiwa Spika, hata kwenye uwekezaji ambao tumeelezewa katika Nyanda za Juu Kusini, uwepo wa barabara ni wa muhimu sana kwa sababu ndiyo utakaosaidia na maeneo mengine ambayo yana upungufu. Kwa hiyo, kwenye hili kwa kweli nina kila sababu ya kuishukuru Serikali na Wizara, kwa kazi nzuri wanayofanya. Niliona kwenye hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani wakitumia neno uhuru, wanasema eti sisi tuna kilomita chache tu, tunazidiwa hata na watu tuliowasaidia kupata uhuru. Huku ni kulinganisha vitu visivyofanana.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea uhuru hatuna maana kwamba ile nchi haikuwepo kabla ya uhuru. *South Africa* imepata uhuru juzi juzi tu, nikiwa na akili zangu timamu hivi hivi na ina *flyovers.* Kwa hiyo, hauwezi ukasema eti *South Africa* tumeipa uhuru juzi na leo ina *flyovers. That is ridiculous*! Hauwezi ukasema eti mbuzi huyu ni mzee anazidiwa na mtoto wa tembo aliyezaliwa jana. *Is nonsensical*! Ni vitu ambavyo havifanani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia hata Zimbabwe, Kenya, wale watu waliokuwa wanakaa kabla ya uhuru walikuwa ni *settlers,* tofauti na Tanzania ambayo ilikuwa *under trustee*. Kwa hiyo,

wale ambao walikuwa wanaishi pale Zimbabwe au Kenya walikuwa wanajua hawaondoki na walikuwa wanaijenga nchi. Sisi tulichofanya ni kurejesha nchi katika wananchi wale, miundombinu ilikuwepo ilikuwa inajengwa. Mnaokumbuka mliosoma historia, wale waliokuwa wameshikilia Tanzania walijenga nini? Kwa hiyo, tunapofananisha hivi vitu, barabara na uhuru, tuone sisi tumeanzia wapi. Sasa hawakutaja *South Africa* kwa sababu wanajua ina *flyovers* na juzi juzi ndiyo tumeisaidia kupata uhuru. Tunapolinganisha hivi vitu, tulinganishe na kwenye nia tunataka kujenga kitu gani na siyo kwa ajili ya kupotosha wananchi.

Mheshimiwa Spika, haya mambo ya kudandia dandia haya, utakuja kudandia hata na mambo ya ajabu. Niliona hata jana Mheshimiwa mmoja anatoa Mwongozo akidhania nina bendera ya Chama, kumbe ni bendera ya Taifa. Unajua hii miongozo ya mchana tunatakiwa tuwe makini sana nayo...

**SPIKA:** Mheshimiwa Nchemba, hilo lilikuwa suala la Mwenyekiti na halikuwa la kwako, kwa hiyo naomba uendelee kuchangia hoja yako.

**MHE. MWIGULU L.N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, nikiishatoka hapo nirejee upande wa barabara zinazopatikana katika Jimbo langu la Iramba.

**SPIKA:** Nasema mwacheni aongee, anayetaka angoje amalize ili aongee.

**MHE. MWIGULU L. M. MADELU:** Mheshimiwa Spika, katika upande wa barabara zinazopatikana na Jimbo la Iramba, niishauri Wizara iendelee na utaratibu wake wa kufuatilia fedha zinazopelekwa katika Halmashauri kwa ajili ya barabara za Wilayani. Hii si tu kwa Iramba, bali hata kwa maeneo mengine ya Wilaya zingine. Inawezekana hata zile fedha wala haziibiwi, lakini utaratibu wa kuwa na barabara nyingi ambazo fedha inayopatikana ndiyo inagawanywa kwenye barabara hizo inaweza ikasababisha tusipate matunda ambayo yanatarajiwa na inasababisha thamani halisi ya ile fedha iliyopelekwa isionekane.

Mheshimiwa Spika, leo hii Waheshimiwa Wabunge tunapigania tupate barabara zilizopandishwa kwenda hadhi ya Wakala wa Barabara (*TANROADS*) kwa sababu wao wanachukua baadhi tu ya barabara na wanazitengeneza kwa kiwango ambacho zinaweza zikapitika muda wote. Kwa hiyo, ningeshauri na kwa ngazi ya Wilaya kuwe na barabara ambazo ni za kipaumbele kwani ufuatiliaji na ujenzi wake utakuwa ni wa uhakika na utawezesha zile barabara kupitika wakati wote.

Mheshimiwa Spika, nitatolea mfano barabara inayotoka Shelui–Mtoa–Mtenkete–Urugu–Kibaya, ambayo inahitaji itengewe fedha za kutosha kwa mwaka huu na unapokuwa umemaliza barabara hiyo unakuwa umekwishajihakikishia kwamba umetatua kero ya wananchi wengi ambao wanategemewa hata kwa ajili ya uchumi wa Jimbo zima la Iramba ya Magharibi. Lakini ukipeleka fedha zikatengeneza barabara hiyo, watengenezaji wakatengeneza kwa koleo, wakasambaza kifusi kwa koleo, ni dhahiri kwamba kila mwaka fedha zitakwenda lakini baada ya mvua kunyesha mara moja fedha zote zitakuwa zimepelekwa na maji. Kwa hiyo, hali itaendelea kuwa hiyo hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia hata tunapolenga barabara tunayoitengeneza ni vema tukawa na malengo kwamba tunataka ile barabara ifike wapi. Kwa mfano; tunayo barabara ya kutoka Shelui–Sekenke–Ntwike, lengo lilikuwa iende mpaka Tulia na Kidalu lakini imeishia njiani. Maeneo ya vijijini hakuna daladala, sasa tunapokuwa tumetengeneza barabara na ikaishia njiani inakuwa haisaidii sana lengo lililotarajiwa. Barabara ingeweza kufika pale Ziwani Dolomoni, tungeweza kusema labda inachochea ile shughuli ya uvuvi inayoendelea pale. Lakini inaishia Nsunsu – Ntwike, kule ambako haitimizi sana kusudi lile la kuunganisha eneo lile ambalo ni la msingi sana kwa biashara pamoja na kilimo.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kama ambavyo nimeona kwenye hotuba ya Waziri kuna barabara ambayo imetokea Kiomboi kushuka Kidalu. Ni vema sana kama barabara hii ilivyokuwa imepandishwa kwa mwaka huu ikafanyiwa kazi ili magari ya abiria yaweze kupita katika maeneo hayo. Hiyo itasaidia sana kwa sababu maeneo yale magari ya abiria huwa hayapiti, hivyo shughuli

za kibiashara haziendi vizuri lakini pia hata gharama za maisha zinapanda na hata watumishi wa Serikali wanapopangiwa kule hawaripoti na wengine wakiripoti wakishuhudia hali iliyopo wanaondoka moja kwa moja. Kwa hiyo, barabara inayotoka Wilayani kwenda Kata ya Kidalu na ile inayokwenda Tulya, Mheshimiwa Waziri naomba aiangalie na aitengee fedha ili ifanyiwe kazi haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, pia kuna barabara ya Misuna. Misuna ni *centre* moja nzuri sana ya biashara lakini imesahaulika. Ilitengewa fedha lakini kwa utaratibu ule ule niliosema wa kutenga fedha kidogo kidogo sana. Naomba kwenye ule ule usimamizi iweze kutengenezwa kwa kiwango ambacho itaweza kupitika muda wote.

Mheshimiwa Spika, sisi tuliochunga mifugo, jirani yako akipata dharura huwa tunaunganisha ile mifugo. Unaichukua na mifugo yake unaichunga na jioni unairudisha kwa uaminifu kabisa. Sasa kwa ruhusa ya Wanairamba naomba nichukue na mifugo ya jirani. Daraja la Mbutu ni kiungo muhimu sana cha Tarafa ya Igulu B na Igunga Mjini. Wananchi wa Kata zaidi ya saba wanaathirika sana kwa kukosekana kwa daraja hilo. Kata za Mbutu, Igulu B, Mwamashimba, Kining'inila, Itunduru pamoja na Kinungu, zinapata shida sana kutokana na kukosekana kwa daraja hilo ambalo linaunganisha Tarafa hiyo na Igunga Mjini ambako ndiko wanakotegemea mahitaji yao ya kila siku. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, kama ambavyo umeonesha kwenye ukurasa wa 29 na 113 pamoja na kwenye majedwali yote yale yanayoongelea madaraja, naomba daraja la Mbutu ulipe kipaumbele na ulitengeneze kabla ya mvua kuanza kunyesha. Hilo ni jambo la muhimu sana na utakuwa umewasaidia sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu wa Usukumani hawajamwomba Mheshimiwa Waziri gari, wameomba daraja tu. Akishawatengenezea daraja watapita na mikokoteni yao, magari, na hata baiskeli, wapite tu pale wakishasema '*yaonage nzela'* wapite kwenye lile daraja bila matatizo. Kwa hiyo, nakuomba sana ulizingatie hili daraja ili liunganishe hizi Kata za Tarafa hii pamoja na Igunga Mjini, ambako wanategemea kwa ajili ya mahitaji yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya Mheshimiwa Waziri kuwa ameliangalia lile daraja, pia aziinue hata zile barabara za Kata zingine. Igunga ina maeneo ambayo ni ya mbali sana na katika maeneo mengine wanatumia barabara kufuata maji. Kwa hiyo, unapokuwa umetengeneza barabara itasaidia hata shughuli zao zile za kupata mahitaji ya kila siku na kujipatia maendeleo. Kwa hiyo, kwenye hili nitamwomba sana kama ambavyo amesema tayari upembuzi ulikwishafanyika, naomba tenda itangazwe haraka sana na aweze kuwafumbulia hilo tatizo ambalo limepigiwa kelele sana kwa muda mwingi na Mbunge aliyepita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, labda tu kwa kumalizia niwatakie kheri ya mfungo wa mwezi Mtukufu wa Ramadhani Waislamu wote katika kipindi hiki walichoanza tangu jana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. Kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kusema 'shika neno, tenda neno'

Mheshimiwa Spika, katika mjadala huu wa Wizara ya Ujenzi, Bunge ndilo linalotunga na kupitisha Sheria. Sasa tumepata Waziri ambaye zile sheria tulizotunga na kupitisha anazifanyia kazi, lakini bado yanakuja malalamiko. Kwa hilo tunaona kwamba hatumtendei haki Waziri mhusika kwa sababu tulipitisha wenyewe kwamba mtu anayejenga nyumba kabla ya mita 25 kutoka kwenye barabara lazima ibomolewe. Hiyo sheria tuliipitisha, leo tunaipigia kelele sana. Je, tunataka Mawaziri wasiotekeleza vitu vyao? Eeh, kwa sababu watu wasiotekeleza mnapiga kelele, hawa hawafai? Wanaofaa mnapiga kelele, sasa mnataka Mawaziri gani? Lazima tuwe wakweli na tupende watu wanaojitolea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa najikita katika Jimbo langu la Kilombero ambalo ni la wakulima wenye kulima vyakula vya kila aina na hivyo miundombinu ni kitu muhimu sana kwao. Tukisemea barabara ya kutoka Kidatu – Ifakara, ni barabara ya miaka mingi na inajengwa kama kidonge cha *tetracycline***,** hapa lami kidogo, inaachwa maili thelathini (30) lami kidogo, wanaacha maili

moja lami kidogo, sasa hiyo inatuvunja nguvu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hilo, ile barabara ni muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwamba Mheshimiwa Waziri ametupatia fedha kidogo za daraja la Kilombero. Asiyeshukuru kidogo hata kikubwa hawezi kushukuru. Lakini hata mtu ukishukuru kwa kile kidogo unaweza kumwambia aliyekupa kwamba hapa bwana sijashiba niongezee kidogo. Sasa fedha iliyotengwa ni ndogo mno kiasi kwamba daraja linalotakiwa shilingi bilioni hamsini (50) leo hii tumepata shilingi bilioni moja na pointi. Sasa labda Mheshimiwa Waziri anataka atwambie anakwenda kujenga nguzo moja tu mwaka huu, halafu nguzo zingine miaka ijayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, daraja lile ni muungano mkubwa wa Jimbo la Ulanga na Kilombero. Kabla ya hapo Wilaya ile ilikuwa moja na wananchi wa Kilombero walikuwa wanakwenda kulima ng'ambo ya mto, lakini sasa hivi wanapata matatizo makubwa, pantoni kila wakati inaharibika. Mimi mwenyewe binafsi nakumbuka Mheshimiwa Mwakyembe nilikuwa namwamsha hata usiku na kumwambia Mheshimiwa, pantoni limechukuliwa na maji. Nashukuru alikuwa ananisaidia sana na mpaka siku ya mwisho akaniambia eeh, ndugu yangu Mteketa, hapa sasa inabidi tujenge daraja, hii pantoni inatusumbua. Kwa hiyo, hata yeye anaafiki kwamba lile daraja ni la maana sana. Kama Serikali inashindwa basi watafute mwekezaji ajenge lile daraja halafu atoze pesa. Mbona pantoni watu wanalipa pesa? Tafuteni mwekezaji ambaye atajenga, watu watalipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pili ni barabara ya kutoka Ifakara kwenda Mlimba. Nimeona kwamba Waziri ameipa fedha za kufanyia upembuzi yakinifu, lakini pamoja na hayo, barabara hiyo naomba aifanyie juhudi sana kwa sababu inabeba mazao ya kila aina, mpunga, mahindi, matunda, ndizi, zote zinatoka barabara hiyo. Ni barabara ambayo ni uti wa mgongo katika Jimbo la Kilombero.

Mheshimiwa Spika, barabara hii kila wakati inakumbwa na mafuriko na Serikali inapoteza fedha nyingi za kuikarabati kila wakati. Tungeomba kabisa barabara hiyo itengenezwe kwa lami kwa sababu nayo vilevile kuna vivutio. Kuna Kihansi ambako kuna vyura kule ambao wanapatikana Tanzania peke yake na watalii wanataka kwenda kuwaona. Barabara hii ina matatizo na tunaomba muitengeneze.

Mheshimiwa Spika, kuna Kata yangu moja ya Uchindile ambapo huko hakuna barabara yoyote inayoiunganisha na makao makuu ya Wilaya. Ukitaka kwenda Uchindile mpaka upitie Mikumi kama nilivyosema mwanzo. Tunaomba Serikali itufanyie mpango tupate barabara ya kuunganisha Uchindile na makao makuu ya Wilaya yake.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara nyingine ya kwenda Tanganyika Masagati. Huko ndizi ziko kubwa kama vile ulivyoona kwenye Maonyesho ya Nane Nane, mkungu kama mimi, lakini unauzwa shilingi 500/= au 1,000/= kwa sababu hakuna usafiri, ukiununua utaubebaje? Kuna matunda, machungwa mengi sana yanaoza, mapapai yanaoza, Tanganyika Masagati kuna zao la mpira liko msituni tu watu wanashindwa kwenda kuwekeza hakuna miundombinu au hakuna barabara. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Waziri aliangalie suala hilo. Mofu kuna madaraja, katika bajeti yako Mheshimiwa Waziri sijaona hapa daraja la Mofu au daraja la Mto wa kwenda Masagati. Naomba atuangalie Wanakilombero, tuna matatizo ambayo yametukera miaka mingi tangu tupate uhuru. Jamaa walikuwa wanasema ukitaka kukaa katika mji usikae Kusini, kama pale Dar es Salaam usikae sehemu kama za Mbagala huko Serikali inawasahau. Kusini kuna matatizo na sisi Tanzania tumekaa Kusini, tunaona tunasahaulika, barabara zetu haziendelezwi miaka na miaka. Tunaomba Serikali ituone kwa sababu na sisi tunalipa kodi kama watu wengine.

Mheshimiwa Spika, sina mengi zaidi na sitaki kuwanyima watu wengine muda wao. Ahsante sana na naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante nashukuru kwa kutukopesha muda, kwa hiyo, tunakuja kwa Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na Mheshimiwa Dokta Augustino Mrema atachangia.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie katika hotuba ya Waziri wa Ujenzi. Lakini awali ya yote naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri sana na mawasilisho mazuri sana na kila Mbunge nafikiri aliyemsikiliza jana, anakubali kwamba aliwasilisha vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba niwapongeze sana Mameneja wote Tanzania nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia barabara zetu. Lakini naomba nimpongeze sana Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa wa Mwanza Engineer Kadashi kwa usimamizi ulio makini kwa barabara zote zilizo chini yake. Lakini nina ushauri kwa Wahandisi wa Wilaya na nisimsahau Mhandisi wangu wa Wilaya ya Kwimba Ndugu Magesa. Nimewapongeza Wahandisi kwa maana ya Mameneja wa *TANROADS* wote kwa sababu wao ndio wanaosimamia fedha zote zinazoombwa. Kati ya shilingi trilion 1.4, shilingi Trilioni 1.2, ni fedha za miradi ya maendeleo ambazo zitakwenda kusimamiwa na Mameneja wa *TANROADS*. Nawasihi sana Mameneja hawa wa *TANROADS* fedha hizi ni fedha nyingi sana, tunaomba mwende mkasimamie vizuri, sisi Wabunge pamoja na wananchi tunataka kuona ubora wa barabara zitakazotengenezwa kupitia fedha hizi na kwa kufanya hivyo mtakuwa mmetusaidia sana.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine naomba kuishukuru Serikali kwa dhati kwa kutenga fedha sh. 732,000,000/= kwa ajili ya daraja la Maligisu. Naishukuru sana Serikali najua kazi iliyobaki ni kwenda kuvisha tu hiyo sahani. Mheshimiwa Waziri kwa heshima kubwa namwomba sana angalau apate siku moja twende akalione daraja hilo. Daraja hili limetengenezwa na mkandarasi Mtanzania lina urefu wa mita 108, Kanda ya Ziwa hamna daraja la namna hiyo. Ni Mtanzania huyu kazi yake ni nzuri sana Kashele *Contractor.* Namwomba tena Mheshimiwa Waziri apatapo nafasi basi twende aone kazi iliyofanyika pale kwa sababu wamepeleka fedha nyingi, Sh. 732,000,000/= si pesa kidogo kwa fedha ambazo tunagawana humu ndani. Lakini niwaombe wenzangu kweli kabisa pamoja na maneno mengi sana hii bajeti ni bajeti ya mwaka 2011/2012 na sio Mpango wa Miaka Mitano. Narudia bajeti hii ni bajeti ya mwaka 2011/2012 sio Mpango wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, nina uhakika hizi fedha tulizopitisha sisi hapa kwa sababu tulianzia kwenye Wizara ya Fedha tukapitisha, sasa Waziri wa Ujenzi hana fedha zingine zaidi ya hizi hata tukimnyofoanyofoa hapa hawezi kupata fedha zingine na hapa tulipo hatuwezi kubadilisha chochote kile. Nawasihi wenzangu tulioingia humu zamani, barabara hazikuwa hivi, jamani tumefikia pazuri mno. Hizo kilomita zilizosemwa barabara za zamani nyingi zilikuwa hazipitiki si kusini, kaskazini wala magharibi. Lakini leo wapo watu wengine na nawasihi sana nchi hii ni nchi yetu sote, mnapoanza kujenga barabara za kusini tusilalamike, mnapoanza kujenga barabara za kaskazini tusilalamike. Hivi wale wa Kigoma, Tabora barabara zao tunataka zisijengwe. Lakini Waheshimiwa wengine wanasema hapa eti barabara hii kwa nini mwaka huu haikupewa fedha, hivi tukishafikia kundi fulani likaanza kusema kwamba kwa nini fedha hizi zinakwenda sehemu fulani. Nashauri sana kama nilivyosema kwamba bajeti hii ya mwaka 2011/2012 na sio Mpango wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, tuombe kama ambavyo Ndassa namwomba Mheshimiwa Waziri. Nimwombe Mheshimiwa Waziri barabara zifuatazo ambazo naomba aziingize mwakani, najua tumepangiwa fedha za kipindi hiki lakini hazitoshi. Barabara ya Fulo inayopita Sumve mpaka Nyambiti, barabara hii Mheshimiwa Waziri anaijua vizuri sana tangu mwaka 1995. Namwomba kwa sababu kule Fulo inaunganika na ile barabara ya Mchepuo ya kutoka Usagara kwenda Kisesa ambapo itakwenda kugusa lami. Sasa nakuomba barabara hiyo iimarishwe kwa sababu za kiuchumi. Barabara ya pili ni Magu-Bukwimba-Jojilo-Mabuki na hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kuiwekea lami tangu mwaka 2005. Alikuja pale Ngudu akatamka mwenyewe. Sio mwaka huu hapana mimi nasema ndani ya miaka mitano. Tuna mwaka 2012, 2013, 2014 na 2015, basi angalau barabara ile ya kutoka Magu-Bukwimba-Jojilo-Mabuki basi ahadi ya Mheshimiwa Rais itimizwe iwekwe kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingine, hili ni ombi kubwa tunacho chanzo chetu cha maji pale Ihelele. Tumeweka fedha zetu pale zaidi ya sh. 270,000,000,000/=, lakini miundombinu ya barabara pale sio mizuri kwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Sayansi na Teknolojia, kwa jina la utani

Mawe Matatu. Barabara hiyo inatoka Mwanangwa-Misasi-Buhigo mpaka pale Ihelele kwenye chanzo cha maji. Magari mengi yanapita kwenda pale kwa sababu ni sehemu kubwa. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri Magufuli na najua akiamua anaweza hebu sasa aiwezeshe barabara hii iweze kupitika muda wote. Barabara ya Bukwimba-Kadashi-Maligisu mpaka Kabila kwa Mheshimiwa Limbu naomba na yenyewe itengewe fedha za kutosha. Fedha zinazotengwa kwa kweli zitatosha kwa sababu ya uchache wake, lakini barabara hizi tungeweza kuziimarisha zaidi.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ni hii barabara ya Magu-Bukwimba-Ngudu-Jojilo iko kwenye mpango wa *PMMR***.** Nimepita juzi mwezi Mei, mkandarasi aliyepewa kazi hiyo sijui labda ndio utaratibu. Nimemkuta yuko na mkokoteni na jembe la mkono anafukia mashimo. Nilimwambia Mhandisi wangu wa Wilaya nikamtafuta Mhandisi wa Mkoa bahati mbaya nimemkosa, lakini je, huo ndio utaratibu? Lakini niombe miradi mikubwa mikubwa hii yote inayokwenda Wilayani au Mikoani tuwape Mameneja wa *TANROADS* wa Mikoa na Wilaya wazisimamie. Barabara hizi kusimamiwa kutoka Makao Makuu hata ukiwauliza wa Mkoa wanasema aah! Wakubwa wako kule ndio wanajua. Mheshimiwa Magufuli hebu tujaribu kubadilisha utaratibu huu ili kusudi barabara hizo ziweze kusimamiwa vizuri zaidi. Nashauri sana naomba sana, lakini nirudie la mwisho Wahandisi au Mameneja wa *TANROADS* Mikoa tunawapa shilingi trilioni 1.2 kwa ajili ya miradi ya barabara, naomba sana barabara hizi zisimamiwe vizuri. Mkandarasi mkorofi yule asiyefanya kazi zake vizuri ili fedha hizi zionekane vizuri kwamba zimefanya kazi yake vizuri, naomba utaratibu wa kumsimamisha na kumfukuza ufanyike. Tusioneane aibu hizi fedha ni nyingi sana Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo kwa sababu huu ni Mfungo Mtukufu wa Ramadhani niwatakie kila la kheri wananchi wangu wa Mantale, Malya, Kalalo, Nyambiti na wengine wote waliofunga mwezi Mtukufu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Spika, baada ya maneno hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Awali kabisa nitoe shukrani za pekee kwa Waziri na Msaidizi wake pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa bajeti hii vizuri. (*Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Tunduru tuna mtandao wa barabara, lakini kwa masikitiko makubwa fedha ambazo zinatengwa kwa ajili ya kutengeneza barabara zetu za Halmashauri kwa kweli ni chache sana ukilinganisha na ukubwa na urefu wa barabara zile. Naiomba Wizara ijaribu kuangalia upya *allocation* ya fedha kwa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kwa kweli hazitoshi. Nitatoa mfano, kuna barabara mbili za muda mrefu sana hazijaweza kupata fedha, barabara ya kwenda Misechela na mwaka huu tulikuwa tumeazimia Mheshimiwa Rais tumpeleke kule, sasa miaka kumi barabara hii haijapata fedha, sijui Rais atafikaje kule. Rais mwenyewe alisema nipelekeni hata kule kwenye barabara mbovu ili iwe changamoto kwa wale ambao wanasimamia barabara hizo na sisi tumeazimia safari hii tumpeleke Misechela, sasa kazi kwenu.

Mheshimiwa Spika, tunazo barabara za Mkoa Wilaya ya Tunduru, barabara hii mojawapo inatoka Tunduru Mjini inakwenda Malasi mpaka Chenga ili iungane na barabara inayokwenda Sasawala Wilaya ya Namtumbo. Tulitarajia kwa sababu ni barabara ya Mkoa basi matengenezo yaonekane ya kimkoa mkoa. Tunashukuru kwa kazi kubwa inayofanywa na *TANROADS* Mkoa kuiangalia barabara hii, lakini kutokana na uwezo mdogo walionao wa kifedha wanalazimika kila mwaka kuweka vifusi. Malalamiko haya nadhani si ya kwangu peke yangu, Wabunge wengi wamejaribu kulizungumzia hilo. Kwa hiyo, tunaomba Mkoa wa Ruvuma kwa barabara hizi nazo mziangalie. Tunashukuru kwa kiwango kizuri kilichotengenezwa barabara ya kutoka Azimio kwenda Makande mpaka Mto Ruvuma, kwa kweli barabara ni nzuri imejengwa kwa kiwango cha changarawe.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa barabara hiyo hiyo ya Mkoa, eneo la Mbesa, tulishaomba eneo hilo ambalo maarufu linaitwa Maolela lijengwe daraja au *box kalavati.* Kwa sababu kilichofanyika pale imejengwa *drift* matokeo yake mchanga unakuja na matope yanajaa na

magari mengi yananasa pale na eneo lile linahudumia Kata zaidi ya nne. Kwa hiyo ,kama itajengwa *box kalavati* pale au daraja itakuwa ni ukombozi wa Kata ya Malasi Mashariki, Kata ya Malasi Magharibi, Kata ya Mchoteka, Kata ya Mbati na Kata ya Marumba. Eneo hilo ndilo linalozalishwa korosho, mpunga na mahindi kwa wingi sana. Naomba sana Mheshimiwa Waziri ashike kalamu yake aandike eneo hilo la Mbesa kwa ajili ya kujenga boksi kalavati.

Mheshimiwa Spika, vile vile kulikuwa na barabara ya Mkoa ya kutoka Mkapunda-Ligoma-Chemchem. Ni barabara ya Mkoa ya muda mrefu, sababu kubwa za kiuchumi zilitajwa na ndipo Taifa likaipandisha barabara hii kuwa ya Mkoa. Cha kushangaza wiki mbili zilizopita tumepokea barua kutoka *TANROADS* Mkoa kwamba barabara hii inarudishwa Halmashauri. Tulitegemea kwamba *TANROADS* Mkoa waendelee kuzichukua barabara ambazo zinatushinda sisi Halmashauri, lakini cha ajabu tunarudishiwa barabara. Naomba sana barabara hii Mheshimiwa Waziri waipokee tena, tutakwenda, tutahakikisha, tutakaa kwenye vikao vyetu vya Halmashauri, tuirudishe *TANROADS* Mkoa kwenye Bodi ya Barabara ili tuwarudishieni tena. Sisi Halmashauri hatuna uwezo wa kutengeneza barabara zilizopo, cha kushangaza mnaturudishia barabara zingine!

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Tunduru-Mangaka. Barabara hii ni ahadi kiporo na ilikuwa matarajio ya Wanatunduru pamoja na Wanaruvuma kwa ujumla. Barabara hii ionekane mwaka huu katika harakati za kujengwa na sio kama *detailed design* na *feasibility study*. Cha kushangaza sasa huu ni mwaka wa tatu, *detailed design and feasibility study*, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina.

Mheshimiwa Spika, kule kwetu ubwabwa uliolala ndiyo unakuwa wa kwanza kuliwa. Huwezi kupika ubwabwa mwingine mpya kabla hujala huu uliolala jana. Sasa cha kushangaza ahadi kiporo ambayo ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi ya 2005 – 2010, bado inaendelea tutajenga kesho, tutajenga kesho. Hatutakubaliana katika Bajeti ijayo. Hii tunaipitisha, lakini Mheshimiwa Waziri kama ataendelea kubaki kwenye Wizara hiyo ajue mwakani, kama hakuna mpango wowote wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ambayo ni ahadi kiporo nitumie lugha ile ile ya mama yangu Mheshimiwa Anne Malecela kwamba mwakani hapa hapatakalika kabisa kabisa. Naomba Mheshimiwa Waziri kwa hilo ajiandae, kwa nguvu tulizopewa na wananchi wa Tunduru basi simalizi, itaeleweka mwakani hapo hapo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunashukuru Serikali kwa kukamilisha mchakato wa ujenzi wa barabara yetu ya kutoka Tunduru hadi Namtumbo. Lakini wananchi wa Tunduru wanashangazwa. Barabara hii imegawanywa katika vipande vitatu. Tunduru Mjini-Matemanga, Matemanga-Kilimasera na Kilimasera-Namtumbo. Tulitarajia wakandarasi wawe watatu ili kuongeza kasi ya ujenzi. Lakini cha kushangaza mkandarasi amekuwa mmoja kwa vipande vyote vitatu. Mkandarasi huyu alitakiwa awe amesha-*mobilize equipments* mpaka kufikia Februari mwaka huu 2011. Lakini hadi leo hii Mheshimiwa Waziri akijaliwa kwenda hatakuta maendeleo yoyote sana sana ni ujenzi wa vibanda vibanda. Sasa kama kunakuwa na *delay* ya miezi takriban sita kesho na kesho kutwa atatoa sababu nyingine za kuchelewa. Namwomba Mheshimiwa Waziri tutakapomaliza Bunge hili ziara yake ya kwanza atembelee kipande hiki cha barabara angalau kutoa hamasa ili mkandarasi huyu aweze kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, niungane na Mheshimiwa Mteketa, kiasi huyu ni mtoto wetu, watu wa Tunduru ndiyo tuliozaa na hekima hii aliyoitoa, chimbuko lake ni kule kusini. Ukichora mstari ambao ni mnyoofu na ukaukatiza basi kule unakoelekea sura tunasema ndiyo kaskazini. Kulia kwa vyovyote utasema huku ndiyo mashariki, kushoto utasema ni magharibi lakini chini utasema ndiyo kusini na Mtu akisimama kaskazini ndiyo itakuwa kichwani, mashariki kulia kwake, magharibi kushoto na kusini ndiyo miguuni. Bahati mbaya mtu anapotaka kuoga basi maji yanaanza kuangukia kichwani kwanza yanadondokea miguuni. Kwa hiyo, maji machafu yale yanayotoka kichwani ndiyo yanakwenda miguuni. Lakini vilevile unapotawadha kwenda kuswali unaanza kichwani kwanza. Mkono wa kulia ndiyo Dar es Salaam, Mkono wa kushoto ndiyo huko magharibi inakuja kumalizia miguuni kusini.

Mheshimiwa Spika, ikitokea mtu ameanza kunawa miguuni wanaanza kumzomea kwa kumwambia sio sahihi, ndiyo haya yanayotokea sasa hivi. Kwa sababu imeanza kukumbukwa

kusini ndiyo watu wanaanza kupiga kelele kwa sababu sio stahili. Inaonekana kwamba kunawa lazima uanze kaskazini ambayo ni kichwani. Sasa leo Wizara tena imetoa michoro kabisa kwamba jamani sasa hivi tusilaumiane. Ramani ndiyo hizo zimetolewa na maeneo ambayo yamekumbukwa muda mrefu kichwani, sasa tumeanza kupeleka miguuni ambako ndiyo kusini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tafadhali sana Wabunge, sisi tulio kusini tumevumilia muda mrefu tukiwa tunasubiri hicho kichwa na mikono ya kushoto na kulia ioge vizuri hatukusema lolote. Leo Serikali ya chama hiki hiki Tukufu ikianza kutukumbuka kusini halafu watu wa kaskazini waanze kupiga kelele na sisi hatutakubali. Naomba Serikali kupitia Wizara hii iendelee kuhakikisha kwamba na kusini kunakumbukwa ile hulka ya kwamba kusini lazima kuwe kwa mwisho naomba iwe historia katika nchi hii. Tuna mambo mengi sana ya kufanya ambayo yamesimama muda mrefu, leo gesi inachimbwa. Haya *copper* imepatikana Mtwara na makaa ya mawe yamepatikana huko Liganga, yatasafirishwa na nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tuna imani kabisa kabisa kwamba Wizara hii itaendelea na msimamo wake huo wa kuhakikisha kwamba maeneo yaliyosahauliwa nayo yanakumbukwa tena kwa nguvu zinazostahili.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Kwa hiyo, unakubaliana na mimi Mungu hana ubaguzi. Maana hizo *copper, gas* mbona ziko huko? Ahsante. Sasa nimwite Mheshimiwa Dokta Augustino Mrema na Mheshimiwa Eng. Ramo ajiandae.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kabla sijachangia hoja ya Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Spika, ulipokuwa Uingereza kuna mambo yalitokea katika Bunge hili, hayapendezi. Pamoja na watu kueleza matatizo waliyotumwa na wananchi wao ikatokea hoja kwamba Mrema ni kibaraka wa CCM, tena nikatajwa kwa jina na Mbunge wa CHADEMA, Mheshimiwa Chiku Abwao. Kwanza nasema, hiyo ni kashfa na matusi kwa Chama cha Mapinduzi. Chama cha Mapinduzi hakihitaji Mrema awe kibaraka wao wala wakala wao na Mheshimiwa Chiku Abwao uliyosema hivyo umesahau fadhila mwaka 1995 nilikubeba, niliku-*recommend* ukawa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chiku Abwao, kaa chini na Mheshimiwa Mrema itabidi baadaye urudi kwenye hotuba yako. Sio hii.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Tunavunjiana heshima hivi hivi. Jambo ambalo linatangazwa Tanzania nzima Mrema ni kibaraka wa CCM eti kwa sababu mimi ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Yalisemwa Bungeni na jana kwenye magazeti yameandika. Naomba nieleze yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, katika Bunge la Tisa CHADEMA walikuwa na Wabunge 11, CUF Wabunge 30, Mbunge mmoja wa TLP lakini mbona CHADEMA nyie mlipewa Kamati mbili. Mheshimiwa Dokta Slaa alipewa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mrema tukianza kuzungumza kitu ambacho si chenyewe…

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nitaendelea hapo, nataka nilieleze hili kwa sababu ni *very serious,* sio binafsi.

**SPIKA:** Tutakupa nafasi nyingine, naomba ukae chini kidogo. Ninachokisema tukianza lugha ya kugongana hapa na mwingine atataka kujibu. Ninachokisema kuna nafasi zinazotolewa kwa ajili ya vitu hivyo tu ambavyo ni rasmi. Hapa wananchi wangependa kusikia wewe unataka kusema nini. Kwa hiyo, ningeomba sana hii iondoe kwanza uendelee na mjadala, utaratibu mwingine unaweza ukafuatwa.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Sasa naomba nirudi kwenye uchaguzi wa mwaka 2010. Kule kwenye Jimbo langu la Vunjo, picha inayojaribu

kutengenezwa hapa ni kwamba mimi ni kibaraka wa CCM. Katika uchaguzi ule, Rais Mheshimiwa Dokta Jakaya Kikwete alipata kura 27,000 kwenye uchaguzi wa Rais, Dokta Slaa alipata kura 22,000 kwa hiyo kule Vunjo Rais wangu ni Jakaya Mrisho Kikwete. Haiwezi kuwa kosa kwa kumuunga mkono Rais Jakaya Kikwete na kushirikiana naye katika maendeleo ya Vunjo na Tanzania nzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kule Vunjo katika uchaguzi wa Ubunge nilichaguliwa kwa kura 29,000, CCM mgombea wao alipata kura 17,000 na CHADEMA mnaoniandama kura 6,000. Kwa hiyo, Mbunge aliyechaguliwa kule Vunjo ni Augustino Lyatonga Mrema. Kwa hiyo, nikitaka maendeleo lazima nishirikiane na Rais Jakaya Kikwete, haiwezekani nishirikiane na mtu mwingine yeyote ambaye haongozi Serikali. Sasa kule Vunjo kazi ambayo imefanyika ni nzuri na sina sababu ya kutomuunga mkono Rais wangu na Waziri wa Ujenzi pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huyu Rais ni mzuri Mheshimiwa Jakaya Kikwete, alipofika kule Vunjo mwaka jana alitoa ahadi kwamba atajenga barabara Marangu Mtoni, Kilema Kaskazini, Kirua Vunjo Magharibi mpaka barabara ya Kawawa na leo ahadi ile nimeiona kwenye kitabu hiki. Kule Kawawa mpaka Kiruwa Vunjo Magharibi kilomita kumi na amekwishaanza na barabara inatengenezwa na sasa uko kwenye utaratibu wa kuweka lami. Pale Marangu Mtoni kwenda kule nyumbani kwangu karibu na soko la Kilema, ukiangalia kwenye kitabu hiki kuna kilomita tano za lami. Kwa nini nisimpende huyu Rais, kwa nini nisimsifu, kwa nini nisishirikiane na yeye? Kumuunga mkono ndiyo unaonekana kibaraka, kwani lazima nipambane au kupigana na yeye kwa jambo lipi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sio hayo tu kwa huyu Rais, maji safi ya kunywa Himo kwenye kampeni yake kaahidi sh. 150,000,000/= ndizo ninazozingojea, watu wa Himo wanywe maji. Kuna Hospitali ya Wilaya inajengwa pale Himo, nzuri kubwa kwa nini nisimsifu Rais Jakaya Kikwete. Juzi nilikuwa nazungumzia kuwa na soko la Kimataifa hapa. Kuna sh. 93,000,000/= wameanza kujenga *fence*, kujenga soko la Kimataifa pale njia panda Himo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sio hayo tu, hata ukiangalia Halmashauri yangu ya Moshi inafanya kazi nzuri katika kutengeneza barabara. Barabara ya Kilema Pofo kwenda Kilema Hospitalini ingawa hajakamilika vizuri, lakini Serikali imetoa sh. 51,000,000/-. Kwa hiyo ina maana kama fedha nyingi zitakuwa zimeletwa na Wizara ya Ujenzi, barabara zangu kule Vunjo zitatengenezwa, moja ni hii na ndiyo nataka nisisitize Waziri wa Ujenzi anisaidie kwa kuniongezea fungu, barabara hiyo iko kwenye eneo muhimu ambapo wananchi wanaihitaji sana.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna barabara ya Uchira- Kisomachi kwenda Kwa Ralia, kilomita 11. Tayari sh. 80,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya kutengeneza barabara hiyo kwa nini nisiwasifu, kwa nini nisiwapende? Kuna barabara ya kwangu pale Marangu-Komera-Kiraracha kilomita saba zinatengenezwa kwa changarawe. Hongera sana mwendelee na hiyo barabara mpaka ikamilike. Kilacha–Matala–Msae kilomita 12 imekwishaanza, ni ya moramu, itengenezwe ikamilike. Lole–Kikere–Marela kule Mwika kilomita nne, tayari imeshaanza. Hongesa sana Waziri, aendelee kutuongeza hela kule. Kilema sokoni kwenda Maua kilomita tatu na yenyewe imeshaanza. Himo-Makuyuni–Lotima imekwishaanza kilomita saba. Kahe–Soko Kiomu kilomita 10.5 na yenyewe imeshaanza. Kawawa–Yamu–Nduoni kilomita 6.5 na yenyewe imeshaanza. Mabungo–Kanjoni kilomita 4.5 imekwishaanza, Marangu–Sembeti kilomita 6.3 imekwishaanza, Paukula–Kilema kilomita 4.5 na yenyewe tayari imeanza kutengenezwa. Kwa hiyo, nina kila sababu ya kuunga mkono Serikali na kuunga mkono Serikali sio kuwa kibaraka, sio kuwa kikaragosi. Kwa nini mnanivunjia heshima kwa Watanzania, *why*? Kwani lazima tukubaliane kila kitu kinachofanywa na chama kingine jamani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna mambo tunazungumza hapa, hii *sitting allowance* tunazopeana hapa, kuna watu wameamua wazipeleke huko wanakojua wao; za kwangu nimeamua kuzipeleka Kanisani na kwenye Misikiti, kosa nini? Parokia ya Uwomboni nimeshaipa Sh. 1,000,000/=, hizi *sitting allowances,* Parokia ya Sinza nilikwenda kuchangisha Sh. 20,000,000/=; nikachangia Sh. 1,000,000/=, Parokia ya Nganjoni nimechangia Sh. 500,000/=, Usharika wa Loleni ni Sh. 1,000,000/=, Usharika wa Mangaria sh. 500,000/=, Usharika wa Lowiri Sh. 500,000/=, Bishop Moshi *Memorial Centre* Sh. 300,000/=, hata juzi nilikuwa kwenye kwaya ya Nkhungu hapa nimetoa Sh.

100,000/=. Sasa siwezi kuonekana ni kibaraka kwa sababu nimesema hela hizo za *sitting* nipewe niwapelekee watu wangu wa Vunjo, hilo sio kosa. Kwa hiyo, tunaweza tukatofautiana lakini ni Mpinzani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nimeamua niyaseme hapa kwa sababu ninazogomwa hapa. Ukiitwa na Rais Jakaya Kikwete kwenda kwenye Mkutano Mkuu wa CCM inaonekana umekwenda kucheza ndombolo. Lakini Rais wangu aniite kwa nini nisiende? Au kama kuna watu wengine wana sera zao kwamba nchi haitawaliki je, ni lazima niwaunge mkono? Sikutumwa na wananchi wa Vunjo kuja kufanya vitendo vibaya kwenye Bunge au nje ya Bunge vya kufanya Serikali isitawalike, sio kazi yangu hiyo, sio biashara niliyotumwa na watu wangu. Hata maandamano narudia tena, hakuna mtu anayekataza maandamano, lakini nimewaambia jamani kutokana na uzoefu wangu, Waziri wa Mambo ya Ndani, Waziri wa Kazi na Maendeleo ya Vijana na Naibu Waziri Mkuu, uzoefu ninaouona yaliyotokea Misri, Tunisia, Libya, Madagascar, Somalia nchi zimevurugika na Serikali zimeangushwa. Walianza na maandamano ya amani. Kwa nini nakatazwa nisitoe maoni yangu? Hiyo ni demokrasia gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa, ni lazima tuwe na utararibu wa kuongoza nchi hii kwa sababu kama haya yanayotokea katika nchi zingine yangetokea hapa kwa nini tunafikiri kwamba madhara yaliyotokea kule hayawezi yakatokea hapa? Ndiyo tahadhari ninayotoa kama kiongozi mzoefu wa Serikali za nchi hii. Kwa hiyo, nasema haya kwa sababu naona naandamwa hapa bila sababu na wananivunjia heshima bila sababu. Kuwa kibaraka wa CCM maana yake ni nini na unasema ndani ya ukumbi huu na unanitaja kwa jina? Kama kuwa Mwenyekiti wa Kamati, ndiyo nikauliza mbona Bunge la Tisa na nyie mlipewa Uenyekiti, kwani na nyie mlikuwa wakala na vibaraka wa CCM? Kwa nini nikipewa Uenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu za Serikali za Mitaa na jana tulikutana, tunafanya kazi nzuri kwenye Kamati yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba radhi nilianza na hilo kwa sababu ya uchungu kwamba Bunge sasa badala ya watu kuleta hoja za kusaidia wananchi, tunaamua kugeuza Bunge kuwa mahali pa uchochezi, kutukanana na kuvunjiana heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii, ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimemruhusu Mheshimiwa Mrema aseme alivyosema kwa sababu alishawahi kuwa Naibu Waziri Mkuu. Kwa hiyo tuendelee na *Engineer* Ramo Makani.

**MHE. *ENG.* RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, nami nikushukuru kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuwa miongoni mwa wachangiaji waliopata fursa hiyo asubuhi hii kwa ajili ya kuchangia hoja iliyopo mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niungane na wale walioipongeza Serikali kwa kiwango kikubwa kabisa, kwa kuweza kutenga Bajeti ambayo ni Bajeti rekodi kwenye Bajeti za Wizara zote mwaka huu. Ninaamini kabisa hili linatokana na ukweli kwamba barabara au mtandao wa barabara ni chachu ya maendeleo, kwa sababu ni dhahiri kwamba kwa kuwa mtandao mzuri au mtandao bora zaidi wa barabara hata sekta nyingine zitawezeshwa kwa urahisi zaidi na kwa ubora zaidi zikiwemo sekta ya kilimo, viwanda, madini na nyinginezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii pia kuikumbusha Serikali kwamba kujenga mtandao wa barabara wa jumla ya kilomita 12,000 ambalo ni ongezeko la asilimia mia moja kutoka mtandao wa kilomita 60,000 za lami, hii ni changamoto kubwa sana ambayo inataka maandalizi makubwa. Wapo wengine wamesema kama walipochangia hapo awali kwamba wanasubiri miujiza kwa sababu wanaona hii ni kazi kubwa sana, nami naungana nao kwamba hii ni kazi kubwa sana lakini nataka kusema mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba inawezekana.

Mheshimiwa Spika, hii itawezekana tu kama mambo yafuatayo yakiwa ni mchango wangu yatazingatiwa. Tunahitaji kufanya vizuri zaidi katika hatua mbalimbali ambazo ni za muhimu katika mchakato wa kujenga barabara. Kama ilivyo kwa miradi mingine ya ujenzi lakini sasa kwa sababu tunazungumzia barabara zaidi basi nizungumzie barabara.

Mheshimiwa Spika, tunahitaji kudhibiti migogoro ya kimkataba inayotokana na miradi ya ujenzi, tunahitaji kudhibiti ucheleweshaji wa ukamilishaji wa ujenzi wa barabara, tunahitaji kudhibiti gharama zinazotokana na ujenzi wa barabara, tunahitaji kufanya vizuri zaidi katika kudhibiti uhafifu wa barabara, lakini haya yote hayawezekani bila kuzingatia kwamba wanaopaswa kuzingatia hayo, wote kwa ujumla kila mmoja wao anatakiwa kutimiza wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi ya ujenzi na sasa tunazungumzia barabara zaidi una miguu mitatu, kama ya stuli au mafiga matatu tunayoyazungumzia wakati wa uchaguzi. Kwanza kuna mwenye mradi mwenyewe, mtekelezaji wa mradi ambaye kwa ujenzi wa barabara ni Serikali, pili kuna wahandisi washauri wanaofanya usanifu na wanaosimamia, tatu kuna mtekelezaji mwenyewe anayefanya kwa mikono yake na miundombinu yake au mitambo yake ambaye ni mkandarasi.

Mheshimiwa Spika, hawa watatu kila mmoja akitimiza wajibu wake sawasawa miradi ya ujenzi inakwenda sawasawa, lakini tatizo linalojitokeza ni kwamba aidha, kila mmoja hatimizi kiwango fulani au sehemu fulani ya majukumu yake, ama mmoja kuwa mzigo kwa wengine hali ambayo itasababisha matatizo ya utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Spika, kila mmoja ana wajibu wake lakini wanategemeana, kila mmoja anaweza kuwa ni tatizo kwa wenzake wawili, lakini tukijenga mfumo mzuri utakaoweza kuwaunganisha wote watatu hawa hakutakuwa na matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo kweli hata siku moja kwamba mkandarasi peke yake anaweza kusababisha mradi kuanguka, mhandisi mshauri anakuwa wapi na Serikali yenyewe kama mtekelezaji wa mradi anakuwa wapi. Siyo kweli hata kidogo kwamba mhandisi mshauri peke yake anaweza kukwamisha mradi na hivyo hivyo kwa Serikali. Ningependa kwa sababu ya muda niseme haraka haraka kwamba yapo majukumu mengi kwa kila mmoja, lakini jukumu kubwa kwa Serikali ni kuhakikisha kwamba fedha kwa ajili ya mradi huo ipo na inapatikana wakati wote au wakati sahihi itakapokuwa inahitajika kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili niseme kwamba Bajeti iliyotajwa hapa kwa maana ya kwenye karatasi, Serikali ihakikishe kwamba fedha hiyo inaenda kweli. Tukipeleka asilimia arobaini au asilimia 60 matokeo yake yatakuwa ni dhahiri na hakutakuwa na sababu ya kusema kwa nini hatukufanikiwa katika utekelezaji wa miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, upande wa washauri na wahandisi wengine wanaoshiriki kwenye mradi, hapa sitazungumzia wahandisi kwa maana ya Mameneja wa Mikoa tu peke yake nataka kuzungumzia wahandisi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, dhana ya kwamba wataalam wazalendo hawawezi tumeizungumzia mara nyingi sana na mimi naomba nirudie kwamba hii ni dhana potofu tuondokane nayo kabisa. Wahandisi wa Tanzania waliopikwa vizuri kitaaluma halafu wakapitia utaratibu wa kusajiliwa wakaiva, wakifanya kazi yao chini ya kiwango, sababu siyo kukosa utaalam labda inaweza kuwa ni matatizo mengine na hasa matatizo ya kimaadili, lakini nataka kusisitiza kwamba ni vema tukajikita katika kuhakikisha kwamba tunatumia watalaam na makampuni ya ndani kwa sababu nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sababu moja kubwa iliyotajwa haraka haraka ni kwamba tunakusudia kukuza uwezo wa nchi wa kujenga uwezo wa ndani wa kuweza kutekeleza miradi hiyo siku zijazo, lakini pia tunakusudia kukuza uchumi, kwa sababu fedha nyingi tunazosema kwamba zimeingia kwenye utekelezaji wa miradi ya barabara hatimaye zitabaki hapa ndani badala ya kwenda nje. Pia barabara ukiijenga ikawa mpya imekamilika siku za usoni inahitaji matengenezo, inahitaji kui-*repair* na unahitaji kuifanya iweze kufanya kazi yake kama ilivyokusudiwa kwenye usanifu na *maintanance*, kwa hiyo ukishirikisha watalaam wa ndani unapata faida kubwa kwa sababu baadaye wao ndiyo watakaochukua jukumu hilo na kwa hiyo hutapata shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipozungumzia juu ya mfumo wa kuweza kufanya hii miguu mitatu yote ikafanya kazi sambamba nilikuwa nazungumzia hasa haja ya kuboresha namna

tunavyoweza kufanya udhibiti na ukaguzi, dhana ya udhibiti na ukaguzi isichukuliwe kama ni dhana ya kutaka kukomoana au kutaka kukwamishana, tuichukue kwa mtazamo chanya, kwamba hii ni njia ya kuzuia zaidi kuliko ya kutibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaweza kuona kasoro nyingi wakati wa utekelezaji wa miradi kama tutatengeneza mfumo bora zaidi wa kuweza kusimamia na kuweza kukumbushana, hakuna namna nyingine yoyote isipokuwa kwa kuhusisha taasisi za Serikali ambazo zipo ikiwemo Bodi ya Usajili wa Wahandisi, Bodi ya Wakandarasi, lakini pia Baraza la Tafa la Ujenzi na nyingine nyingi, hizi ziwezeshwe na zipewe uwezo wa kuweza kusimamia vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyotangulia kusema mzigo wa kujenga kilomita 12,000 siyo lelemama, kwa hiyo tunatakiwa kuboresha katika kila eneo ambalo litashiriki katika kuwezesha kwamba miradi hii inakwenda sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono kabisa utaratibu wa Serikali wa kumtumia Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* katika kusimamia masuala mbalimbali ya utekelezaji wa miradi na matumizi ya fedha za umma. Lakini nilisema wakati wa semina elekezi Ubungo, nashukuru *CAG* amechukua hatua aliweza kutekeleza lile wazo nililosema kwamba afanye kazi kwa kushirikisha pia taasisi nyingine. Ninayo taarifa muda mfupi uliopita alisaini *memorandum* na *PPRA* kwa ajili ya shughuli za manunuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba fanyeni hivyo hivyo kwa upande wa watalaam kupitia Bodi ya Usajili wa Wahandisi kwa sababu peke yake hawezi. Hii ni dhana ya kusema kwamba kama unataka kwenda kumkagua mwalimu ukimpeleka daktari ambaye hajawahi kufundisha hata siku moja na hajui zana na taratibu za kufundisha hawezi kukagua vizuri. Kwa hiyo, kila taaluma inaweza kufanya ukaguzi vizuri zaidi ikiwa inakaguliwa na wale wahusika wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda naomba nizungumzie juu ya suala la utekelezaji wa miradi kama hii ambayo ni ya kihandisi kwamba unahusisha wahandisi zaidi. Umefika wakati sasa wa kuwa na chombo cha juu kabisa kama ilivyo kwa *CAG* upande wa mambo ya uhasibu na mambo ya *auditing,* lakini pia kwa uhandisi sasa imefika wakati tuwe na mhandisi ambaye atakuwa kwenye *apex*, kama vile tunavyokuwa na daktari au tunavyokuwa na mtaaluma mwingine yeyote yule katika ngazi ya Taifa. Tuwe na *Chief Engineer*, tunaweza kutafuta jina lingine lolote lile lakini iwe ni *Apex Authority* ya kuangalia masuala ya uhandisi kwa Taifa zima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imetokea bahati mbaya kidogo kwamba hatukuweza kubadilishana taarifa na Mbunge mwenzangu wa Tunduru Kusini lakini naomba niboreshe maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Tunduru – Namtumbo. Imekatwa vipande vitatu ni sawa, lakini mkandarasi ni mmoja kwa maana ya taasisi, lakini taarifa nilizonanzo nimezifuatilia kwa kina ni kwamba kila kipande ya vile vipande vitatu mkandarasi anafanya utaratibu wa kuwa na *resources* zinazojitegemea katika kila kipande, menejimenti tofauti, *equipment* tofauti na *mobilization* inakwenda namna hiyo. Mimi nimekuwa wa mwisho kutoka Jimboni, mwenzangu alitangulia, *equipment* zimeanza kuingia na zilizo nyingi zipo baharini ndani ya wiki mbili hivi zitakuwa zimefika kulingana na taarifa nilizoweza kuzikusanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tunduru - Mangaka vilevile nikiwa huko hata wiki moja haijatimia tulifanya mkutano wa mwisho na *JICA* na *ADB mission* tayari wameshafanya majadiliano ya kuangalia masuala ya mazingira pamoja na uhusishaji wa huduma za jamii, ahadi ni kwamba mpaka kufika mwezi Januari, 2012 tayari watakuwa wamepata maelekezo kutoka makao makuu ya hizo *missions* lakini pia ndani ya mwaka mmoja kuanzai Januari, 2012 mkandarasi atakuwa *site*. Hii ni taarifa ambayo mwenzangu alikuwa hana, naomba kuiboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa naomba Waziri achukue maombi yafuatayo ya kukamilisha miradi nitakayoitaja hapo siku za usoni, daraja la Kalulu bado linaendelea kujengwa lakini linasuasua naomba aongeze *speed* ya kuweza kukamilisha daraja la Kalulu, tunalo daraja la

Fundimbanga bado halijaanza lakini hili nitaomba pia lijengwe kwa utaratibu ambao tumeanza kuutumia kama tulivyofanya kwa upande wa daraja la Kalulu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia barabara ya kutoka Mji Mwema kupitia Mindu kwenda mpaka Ngapa inatokea Nachingwea, naomba pia hii iingizwe kwenye mpango. Barabara nyingine ni ya kutoka Mkowela, Tinginya, Ngapa nayo pia iweze kutiliwa mkazo wa kuweza kukamilishwa kwa ajili ya manufaa ya Wilaya yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa kwa maombi ya jirani yangu kuweza kuhusisha pia ombi lifuatalo ili barabara ya kutoka Songea kwenda Msumbiji upande wa nchi jirani na yenyewe uweze kuingizwa katika mpango ili kuweza kutekeleza azma ya kutekeleza vizuri sera za CCM lakini pia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijagongewa kengele tena kwa mara nyingine naishukuru sana Serikali kwa kuzingatia umuhimu wa kuufanya mtandao wa barabara ambao sisi kwa upande wa taaluma tunasema ni kama mishipa ya damu kwenye mwili wa binadamu kuwa kipaumbele. Usipoboresha barabara maana yake ni kifo kama ungekuwa unazungumzia uhai wa binadamu. Kwa hiyo, naomba jitihada hizi ziweze kuendelezwa lakini zitekelezwe kwa vitendo na hasa nirejee lile ombi langu la kusema kwamba kama tunaweza kuahirisha Bajeti maeneo mengine, lakini kwenye Bajeti ya Ujenzi fedha iliyokadiriwa itolewe yote tena kwa wakati ili Serikali iweze kutimiza wajibu wake wa kulipa makandarasi kwa wakati na kuepuka gharama kubwa katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Sasa nitamwita Mheshimiwa Kepteni John Komba na Mheshimiwa Ismail Rage ajiandae Mheshimiwa John Chiligati ajiandae, Mheshimiwa Eustace Katagira pia. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii, kwanza nitoe salamu za rambirambi kwa kijana wangu alinisaidia kwenye kampeni mwaka 2005, amefariki leo usiku anaitwa Nyandindi, Mungu amuweke mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, baada ya rambirambi hizi, nianze moja kwa moja kwa pongezi kwa Waziri wetu wa Wizara hii na Naibu Waziri wake, kwa kweli mnafanya kazi nzuri sana na Mungu awabariki sana. Kazi mnayoifanya mnaifanya Serikali yetu isikike, itukuke na iwe hai wakati wote ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu hapa wanahangaika sana kutulinganisha sisi na Kenya na Uganda, halafu wengine ni wasomi tena wasomi pengine kuliko mimi, wengine ni wanasheria, wengine wana historia, wanasahau kwamba Kenya ilikuwa koloni la Waingereza, Uganda ilikuwa *protectorate* ya Waingereza na Tanganyika ilikuwa ni *territory* la Waingereza, kwa maana sisi tulikuwa chini ya udhamini tu. Lakini wenzetu Waganda walikuwa kama vile wamepewa walelewe na Wakenya ndiyo hasa ilikuwa ni nchi yao kabisa, ni kipande kutoka Uingereza kimemeguka kimeenda kukaa Kenya. Kwa hiyo, Waingereza kazi yao ni kusaidia Kenya iwe kama Uingereza, hiyo watu wamesahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana walipotoka hapa waliacha msomi mmoja au wawili, ndiyo maana hata Baba wa Taifa elimu yake ya juu alikwenda kuisomea Uganda ambako waliamua kuweka elimu huko siyo Tanzania, sasa mnapotulinganisha sisi na Kenya, sisi tunatakiwa tupongezwe kwamba tumefanya mengi zaidi ya Kenya kwa sababu tumetoka chini, tumekuwa watoto maskini tumeenda mbele zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lami ambazo tunazo sisi hapa ukazibandika nchini Kenya au Uganda au Malawi, zitaenda mpaka chooni kule, vyoo vya wanawake vitaingia lami, vyoo vya wanaume vitaingia lami huko vijijini huko maana nchi hii ni kubwa sana, linaganisha tu nchi yetu na hizo na sasa hivi tunaunganisha nchi yetu katika barabara za lami ujue ni namna gani ambavyo nchi yetu tumechupa kuliko Kenya, kuliko Uganda. Sisi tulikuwa ni watoto yatima, tumefanya kazi nzuri,

hatuionei aibu na baada ya kuwa watoto yatima bado tukasema pamoja na uyatima wetu tukomboe wenzetu, kwa hiyo bado hela zetu zinakomboa wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukipima kazi ya ukombozi peke yake uiweke katika pesa maana ninyi ni wasomi hapa ni shilingi ngapi? Hela zile tungeziweka tuziingize kwenye biashara ya maendeleo ya nchi yetu tungekuwa wapi sisi? Usingetulinganisha na Kenya wala Malyasia, tungekuwa mbali sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unapozungumza utaratibu mzuri ama nchi nzuri kama Botswana, Angola, *South Africa,* ujue kwamba ule uchumi wao uujumlishe ndiyo Tanzania, hiyo ndiyo kazi iliyofanyika hapa nchini kwetu. Kwa hiyo, naomba sana tusizungumze kutoka hewani. Wale watoto wanaokuja kusoma Bunge hapa wapate na elimu hii kwamba Tanzania iliyopo hapa ndiyo imefanyakazi yote hiyo, tusiondoe historia hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nirudi kwenye barabara, kwanza nashukuru wapo wenzangu hapa jana, leo wanaongea kwa jazba kisa kitu kidogo tu kwamba na sisi Kusini tumekumbukwa eti kwa lami kidogo kidogo hii. Wenzetu lami zinaingia madizini tunawaangalia, lami zinaingia kwenye vilabu vya pombe tunawaangalia, lami zinaingia kwenye ma-*hall* ya madisko tunawaangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo tumepata eti iende *Mbamba bay* basi watu wanasema hapa, ubaguzi, tulibaguliwa sisi bwana siyo ninyi na sisi tulikaa kimya, tulitulia na siyo kwamba tulikuwa hatukusoma tulikuwa na viongozi wakubwa akina Mzee Kawawa si walikuwa huko? Lakini walisema peleka kwanza huko kwingine, tulikuwa na moyo wa utulivu na ninyi mtuvumilie sasa, tena ninyi ndiyo mseme kwamba sasa ni wakati wa watu wa Kusini wakomboke, walitukomboa sasa tuwakomboe na wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, leo mnasimama hapa mnatoa hoja kwamba eti sisi tunapendelewa, tunapendelewa nini sisi? Rukwa ni maskini kabisa, Rukwa ni ya kwanza katika mazao, wanalima mahindi, wanalima mpunga, wanavua samaki Ziwa Rukwa, Ziwa Tanganyika, lakini namna ya kutoa mahindi kupeleka Dar es Salaam ni kazi kubwa sana hiyo.

Leo wanatengeneza ohoo, tunapendelewa jamani dhambi kwa Mungu. Tusifanye hivyo sisi wote ni Watanzania kale kanguruwe samahani waislam wamefunga, kale kasungura tulikubali kaliwe Kaskazini sisi tulikaa kimya tulikubali. Sasa kale kasungura kaelekezwe Kusini na nyie mkubali. Msipige kelele tu hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Songea - Mbinga tunashukuru imeanza kujengwa, mkandarasi yule anafanya kazi vizuri, tunaona sasa inakwenda vizuri ahsante sana. Barabara ya kutoka Mbinga kwenda *Mbamba Bay* nimeiona humu lakini haina mkandarasi kule nataka tu waniambie Waheshimiwa Mawaziri wote kwamba lini hasa barabara kutoka Mbinga kwenda *Mbamba Bay* kwa lami itajengwa maana fedha zimetoka, nimeziona kwenye kitabu. Lakini ni lini hasa nikienda pale nikawaambia wananchi wa Nyasa wale na Wamatengo kwamba kazi hii inaanza mara moja. Kwa hiyo, niliikuwa nataka jibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kuna barabara ambayo Rais mwenyewe aliahidi, mimi nilikuwepo siku hiyo barabara ya kutoka Songea kwenda Mitomoni Rais amekwenda mpaka kwenye daraja ambalo mama Jenista Mhagama alijenga daraja lile kwa nguvu zake mwenyewe ambalo sasa linaunganisha Tanzania na nchi ya Msumbiji kupitia Mkoa wa Nyasa. Rais amefika mpaka pale na alitaka kuvuka lile boti lilikuwa dogo alisita kuingia. Tukasema ukimwagika tutakubeba akasema unanidanganya. Kwa hiyo, aliahidi kwamba itawekwa lami miaka minne iliyopita mpaka leo lami haijawekwa. Kwa hiyo, mnatuweka sisi Wabunge wa upande huo katika wakati mgumu sana. Tunaomba ahadi ya Rais ambayo ilikuwa ya uchaguzi uliopita ikamilishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mwambao kutoka Lituhi kwenda *Mbamba Bay* kwenda Chiwanda barabara ile ni ya mpakani, kama mnakumbuka mwaka 1964 Banda alidai maeneo yote haya ni ya kwake kuanzia kule Kyela kwa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kule ni

kwake, unafika Manda huku kwa Mheshimiwa Deo Filikunjombe ni kwake, kwangu mimi kule kote maeneo yale ya kwake. Mwalimu aliamuru Jeshi lijenge barabara ya muda, yapo madaraja ya muda kule, nina hakika kabisa Mheshimiwa Spika wewe ni shahidi ulishakuwa Mkuu wa Mkoa katika Mkoa ule, ninachokisema unaweza kukishuhudia hapa. Ile barabara watu wale ni duni, duni dunika, ni watu duni sana. Usinione mimi mnene hapa watu wangu duni kweli kweli. Basi kuliona kwamba hili ni basi linatembea mwambao ni miaka mitatu tu iliyopita tangu Uhuru. *(Makofi)*

Kwa hiyo, wewe fikiri uduni wao uko namna gani? Kwa hiyo, naomba sana hii barabara ipo chini ya *TANROADS* lakini imefunguliwa tu haijaanza matengenezo naomba muiwekee mkakati wa kuitengeneza, ni barabara ya mpakani na sasa hivi mnaona Malawi maandamano kila siku walimuondoa Banda wakasema ni dikteta, wakamuondoa sijui nani wakamuweka huyo mdemokrasia, leo hawataki hata kumuona. Wanaandamana kumuondoa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Wapi huko?

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Malawi. Wale wanadai kwamba ardhi hii ya kwetu ni yao. Sasa wasije wakaandamana wakapanga siku moja maandamano yakaanzia Lituhi kwenda *Mbamba Bay* maana wanasema ni nchi yao. Kwa hiyo, naomba sana barabara hiyo itengenezwe ili majeshi yetu yaende kule ili wana ulinzi wetu watembelee vizuri ili wananchi wetu uchumi wao uweze kuinuka. Barabara ya kutoka Lituhi kwenda Chiwindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niliongea siku moja na Naibu Waziri wa Wizara hii maana yeye na mimi tuna- *share show* moja, naye ana watu duni kama mimi tu. Hakuna barabara inayotuunganisha kutoka Wilaya mpya ya Nyasa, Wilaya ya Ludewa mpaka Wilaya ya Kyela matokeo yake juzi tungempoteza Mbunge hapa, Mheshimiwa Deo Filikunjombe alitaka kwenda kuwaona wananchi wake kwa kutumia boti kutoka Manda kwenda Lupingu alizama na kuogelea maskini hajui, Wanyasa wale wakaenda kumuokoa angekufa tungetangaza tanzia hapa. Mbunge anajitahidi kwenda kuwasaidia wananchi wake kwa kutumia mtumbwi. Hebu *just imagine* hakuna barabara, tungepoteza Mbunge katika Bunge hili hili, tungelia humu, Mheshimiwa Deo Filikunjombe kama yupo ananisikia atatoa ushahidi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii yote ni kwa sababu alikosa barabara ya kwenda kuwatembelea akaamua potelea mbali ajitose kwenye maji hata kuogelea lakini Mwenyezi Mungu kamsaidia amepona. Naomba barabara iwepo kutoka *Mbamba Bay* mpaka Kyela inawezekana kabisa. Inawezekana kwa sababu katika Ilani ya CCM kuna ujenzi wa Daraja la Ruhuhu nimeliona kwenye kitabu hiki, lakini sijaona fedha zake.

Ninaomba kwa sababu hii ipo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya miaka hii mitano tukijenga daraja lile ama tuta lile la Mto Ruhuhu itatusaidia sana kutoboa barabara kutoka Ludewa kwenda Kyela. Kwa hiyo, naomba sana kwa vile ipo kwenye Ilani ya Uchaguzi tusipuuze kwa sababu wananchi wale hawahitaji kusikia kuna CHADEMA, wala kuna *NCCR Mageuzi,* wale ni CCM damu damu. Kwa hiyo, tusiwapoteze bila sababu za msingi kwa sababu ya barabara tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ipo barabara ndani ya mpakani kutoka Nyoni kwenda Kingelikiti, kwenda Tingi, kwenda Dapoli, kwenda Lipalamba, kwenda Mipotopoto, kwenda Mitomoni ambako napakana na Mheshimiwa Jenista Mhagama. Barabara hiyo ni ya mpakani na ya ulinzi, inalinda mpaka wa Tanzania na Msumbiji barabara hiyo watu wa *TANROADS* walikwenda kufanya utafiti kwamba barabara ipandishwe daraja iwe barabara ya Mkoa. Mpaka leo hatujapata jibu lake. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, utakapokuwa una-*wind up* uniambie mmefikia wapi katika kupandisha hadhi barabara ya Nyoni, Kingilikiti, Tingi Dapoli, Lipalamba, Mpotopoto, Mitomoni mpaka kule kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama ili iunganishe na iwe barabara pia ya Msumbiji na Tanzania. *(Makofi)*

Naomba niwashukuru kwa Daraja la Lwekei nimeona fedha zake. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri nikuambie kwamba wale vijana wako wanafanya kazi nzuri, daraja linakwenda vizuri *two way traffic* yaani hawa wanakwenda, hawa wanarudi baada ya miezi miwili darala lile litakuwa ni zuri na la kisasa kabisa katika Mkoa wa Ruvuma, tunakushukuru sana kwa hili. *(Makofi)*

Mwisho kabisa, ingawa najua hili ni suala la Mbunge mwenzangu lakini ni Waziri sasa, Waziri hawezi kusema mwenyewe hapa, lazima sisi tumsemee hapa. Mheshimiwa Dkt. John Nchimbi, kero kubwa ya wananchi wa Songea ni *stand* ya Songea. Mji wa Songea ni Manispaa lakini hauna fedha ya kutosha kama Mbinga, Mbinga ina uwezo lakini inahitaji Serikali Kuu isaidie Manispaa ile, *stand* ya Songea Mheshimiwa Nchimbi kama atakosa Ubunge mwaka 2015 ni kwa sababu ya *stand* ya Songea. Kuna mashimo juu ya mashimo yeye hawezi kusema hapa lakini mimi naweza kusema, Mheshimiwa Jenista Mhagama anaweza kusema, Mheshimiwa Ramo Makani anaweza kusema na wengine wanaweza kusema. Tunamsemea ni kijana mzuri, uwezo mkubwa kabisa lakini anaangushwa na *stand* ya Songea Mjini, naomba mpeni lami pale hata mapipa yeye atajua na Halmashauri yake namna gani ya kujenga *stand* yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache nawashukuruni sana, Serikali hii idumu na wala tusiwe na wasiwasi, kelele za mlango zitapigwa sisi tutalala tu hakuna shida na mwaka 2015 tutapangusa na kesho kutwa Igunga ndio mtaona ushahidi wake. Ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, naomba radhi sauti yangu si nzuri naumwa mafua leo. Awali ya yote mimi kama Mbunge wa Tabora na kwa niaba ya Wabunge wote wa Mkoa wa Tabora naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu tangu tupate Uhuru Mkoa wa Tabora ulikuwa umesahaulika sana. Lakini kutokana na uzuri wa Chama cha Mapinduzi kutengeneza Ilani nzuri ya Uchaguzi na kutokana na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, aliwaahidi wananchi wa Tabora kwamba kuanzia Bajeti ya mwaka huu barabara zote zinazounganisha Mkoa wa Tabora na Mikoa, mingine itajengwa kwa kiwango cha lami. Nilikuwa naangalia Kitabu cha Bajeti hapa ambacho Mheshimiwa Waziri amesoma ukurasa wa 23, naomba kunukuu; “Barabara ya Nzega - Puge kilomita 56 imetengewa hela.” Kilichonifurahisha zaidi Waziri ameweza kuthubutu kuweka tarehe ya barabara hii kuisha yaani tarehe 29 Oktoba, 2012. Hawa watu Mungu awajalie sana. Barabara ya Puge - Tabora kilometa 58 na yenyewe vile vile imeshatengewa fedha na inatazamiwa kuisha tarehe 29 Oktoba, 2012. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi haikuishia hapo barabara ya Tabora - Nyahua kilomita 85 zimetengwa fedha na zenyewe barabara hii tutakabidhiwa tarehe 29 Julai, 2013. Nataka kumuahidi Mheshimiwa Dkt. John Magufuli na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe leo nitakapokwenda kusali swala ya *Tarawei* nitawaombea dua Mwenyezi Mungu awajalie sana watu hawa. Naungana na ndugu *Captain,* Mikoa ya Magharibi na Mikoa ya Kusini tulikuwa tumesahaulika kana kwamba hatupo Tanzania. Lakini sasa ni lazima tuwe na shukrani kwa uamuzi mzuri uliofanywa na Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninamuomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuongea kuna taarifa zimetolewa jana kwenye *television* ya *TBC1,* nimepigiwa simu jana usiku na leo asubuhi kidogo kuna taarifa ambayo mimi siamini kama ni sahihi kwa sababu nilifanya ziara kwa kushirikiana na Naibu Waziri wa Wizara ya Ujenzi kutembelea wakandarasi wote hao watano ambao wanajenga barabara kwa kiwango cha lami kutoka Tabora kwenda Urambo, kutoka Tabora kwenda Nzega, kutoka Tabora kwenda Nyahua na wakati tulipokwenda fedha walizokuwa wanazihitaji kwa ajili ya *mobilization* walishapata. Sasa jana kwenye *TV* nimeona eti sina hakika lakini nitaomba Waziri ajaribu kunipa ufafanuzi jambo hili kwa sababu nimesoma kwenye kitabu cha Bajeti cha mwaka jana zilitengwa fedha zaidi ya shilingi 11,000,700,000 nina hakika hawa wakandarasi walipata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nilitaka vilevile kutoa ushauri kwa Wizara ya Ujenzi katika hii mikataba wanayotengeneza mkandarasi ukishampa mkataba ule haina tofauti na fedha taslimu kwa sababu mkandarasi anachukua ule mkataba akiupeleka benki anapewa fedha. Sasa sioni kwa nini anakwenda kuchukua fedha benki akafanye miradi mingine wakati Serikali ikichelewesha fedha kidogo wanakaa wanatupigia kelele. Utaratibu wa fedha za Wizara zitatoka baada ya leo na *Inshallah* Wabunge wenzangu wote nina hakika mtaunga mkono na itapita haraka ili hawa wanaodai fedha zao kuanzia kesho waanze kupata fedha zao na uzuri Bunge hili lina watu makini

sana walisharekebisha huko utaratibu siyo kama zamani mpaka Bunge liishe ndio wanalipwa fedha zao. Leo mambo yakiwa mazuri tu basi kesho *cheque* zinatoka kama kawaida. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nina imani kabisa kwamba Waziri atakapokuwa ana-*wind up* atuhakikishie wananchi wa Tabora kwa sababu Mheshiumiwa Dkt. Harrison Mwakyembe alipofanya mkutano wa hadhara pale Tabora Mjini aliwahakikishia watu wa Tabora kwamba ikifika mwaka 2014 mimi nitakuja Bungeni kwa bajaji, mimi nina hamu sana ya kuja kwa bajaji hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitaka kuongelea suala la mizani. Mizani kwa kweli imekuwa kero kwa watu wengi wanalalamika. Nilikuwa nafikiri wakati umefika sasa tuige kwa wenzetu mambo mengine mazuri wanayoyafanya. Sasa hivi nchi jirani za Kenya na Uganda mabasi hayasimami tena kupima mizani. Tunaomba mabasi ya abiria angalau yapewe heshima kama ni lazima basi kuweka mizani wawekewe pale kwenye *stand* yao ya Ubungo kabla hawajaondoka ili wapime pale pale ndani ya kituo chao kuliko wanapopita barabarani waweze kuwahi. Nasema hivyo kwa sababu gani, kuna mabasi yanayotoka Tabora kwenda Dar es Salaam yanafika pale Kibaha kwenye mizani saa 12.30 foleni ya pale wanatoka saa moja na nusu au saa 1.45 wakati mwingine na wakati mwingine mpaka saa tatu. Kwa hiyo, unakuta mabasi yanachelewa yanaingia Dar es Salaam usiku. Mimi nafikiri ni wakati muafaka wa hizi mizani kuziangalia. *(Makofi)*

Lakini jambo lingine ningependa kutoa ushauri kwenye Wizara hii kwa kweli inafanya kazi nzuri na fedha wanazozipata wanazitumia vizuri ni wakati muafaka kwenye *high way* zetu tunazozijenga sasa hivi tuweke *road tolls* badala ya kukaa tunategemea kila siku *road toll* ni ya kwenye mafuta tu, tuweke *road tolls* kwenye magari haya makubwa yanayopita kutoka nje ya nchi kwa sababu wanatumia barabara zetu na wananunua mafuta wakati mwingine mara chache sana au wanakuja na mafuta kutoka nchi jirani kwa hiyo, wanatumia barabara zetu bure. Kwa hiyo, ukiweka *road toll* kwa ajili ya kulipia barabara zetu kwa kweli huu mfuko wa barabara utaweza kusaidia na kuboresha barabara zetu hasa Mikoa ya Kusini na Mikoa ya Magharibi ambayo kwa kweli tulikuwa tumesahaulika kwa muda mrefu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimefurahi kwamba kuna nyumba za Serikali Tabora pia zinajengwa hasa kwa Waheshimiwa Majaji wangu. Ningependa kuwapongeza kabisa na kama nilivyosema tangu hapo awali Bajeti hii ya mwaka huu walahi ina raha ya peke yake hasa hii ya Wizara. Kwa hiyo, hata nguvu ya kuendelea kuongea sina kwa sababu furaha niliyokuwa nayo nina hakika sasa wananchi wa Tabora adha waliyokuwa wanaipata ya barabara sasa itakuwa haipo. Napenda kuunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza niseme naunga mkono hoja kwa niaba ya wananchi wa Manyoni kwa sababu nisipounga mkono wananishangaa kwa kuwa mambo ambayo Wizara hii inafanya kule Manyoni wanayaona na ushahidi tu upo kwenye jalada la kitabu cha Bajeti mkiangalia jalada lake huko mbele, ile barabara ipo Manyoni kwa hiyo wakinisikia siungi hoja mkono watanishangaa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuunga mkono hoja napenda niwapongeze Waziri, Naibu Waziri wake *comrade* Mwakyembe na timu yake yote. Kwa kweli mnafanya kazi nzuri sana na Mungu awabariki, maneno yanayosemwa semwa yasiwavunje moyo, songeni mbele, mnafanya kazi nzuri, barabara zinaonekana kila mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ladda tu niseme jambo moja ambalo nimelisikia tangu jana, hili la wengine sijui wapi sisi kusini, Kaskazini, Magharibi, Mashariki jamani lugha hii si sawa sawa. Bajeti hii ukitazama kwa kweli imegusa kama ni Mashariki, kama ni Magharibi, kama ni katikati kama ni Kusini imegusa kila eneo. Kwa hiyo, hii lugha ambayo imeanza kutokea hapa kwamba kuna baadhi ya maeneo yametengwa, baadhi ya maeneo yamesahauliwa, baadhi ya maeneo yamependelewa nadhani si lugha nzuri, tunawagawa wananchi, tunawachanganya wananchi si sawa sawa. *(Makofi)*

Tunayo miaka mitano ya kutekeleza mipango ambayo ipo katika Ilani ya Uchaguzi. Hii ni Bajeti ya kwanza katika miaka mitano, sasa Bajeti hii ya kwanza haiwezi ikagusa kila mtu na

barabara yake, kuna miradi ya mwaka wa kwanza ipo humu, kuna mwaka wa pili, mwaka wa tatu, embu tuwe wavumilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wale waliotoa miongozo jana, naomba sana akiwemo na rafiki yangu Mheshimiwa Ole-Sendeka, nakuomba sana rudisha moyo hii ni Bajeti ya kwanza katika Bajeti tano. Kwa hiyo, naomba sana hizi lugha ambazo zinatugawagawa kwa kweli haziisaidli nchi, hazisaidii wananchi, tuwe wamoja, Bajeti zipo tano, hii ni moja katika bajeti tano, tuwe wavumilivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niseme tu kwamba kazi ambayo inafanywa na Wizara hii ya kufungua nchi yetu kwa barabara ni moja ya misingi au vichocheo muhimu sana katika kuleta maendeleo, ni kama elimu. Unajua wanaposema Tanzania tuna rasilimali nyingi sana, kwa nini ni maskini, vipo baadhi ya vitu ambavyo tukivifanya, tutakwamka tu. Kikubwa kabisa ni elimu maana ujinga ndiyo kizingiti kikubwa sana. Lakini la pili ni hili la barabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jinsi ambavyo barabara zinavyotengenezwa na akina Magufuli, haya ndiyo mambo ambayo yataleta maendeleo na kazi wanayoifanya ni kazi nzuri. Mkoa wa Singida kwa mfano, tulikuwa ni moja ya Mkoa ambayo tupo nyuma sana kimaendeleo na moja ya sababu ilikuwa ni barabara tu, tulikuwa *not rechargeable,* sasa kama mtu huwezi kutoka, huwezi kuingia wawekezaji hawawezi kuja, mazao hamuwezi mkauza, hakuna barabara, maendeleo yatatoka wapi?

Mheshimiwa Spika, lakini nafurahi kusema kwamba Mkoa wa Singida sasa zinaanza kufunguka, barabara kutoka Dodoma mpaka Manyoni imeshakamilika tayari na imo katika jarada la kitabu chetu, Manyoni - Singida tayari imeshakamilika tunashukuru, Singida kuendelea mbele kule mpaka Mwanza kule tayari imeshakamilika tunashukuru. Sasa hivi barabara ya Singida, Babati, Minjingu mpaka Arusha kuna makandarasi watatu inafanyia kazi, tunashukuru. Mambo yanakwenda kwa nini tusiunge mkono Bajeti hii na Wanasingida wanaona. *(Makofi)*

Lakini vilevile sasa hivi kuna barabara ambayo imeanza kutengenezwa kutoka Manyoni inakwenda Itigi, Chaya mpaka Tabora, kazi imeshaanza. Kwa hiyo, mambo haya watu wanaona na hata watu wanaposema Serikali ya awamu ya nne haijafanya chochote ni uongo wa mchana, watu wanaona haya mambo. Kwa hiyo, *comrade* Magufuli songa mbele. Watu hawataki maneno wanataka barabara na barabara zimo humu, songa mbele. Unatekeleza Ilani ya Uchaguzi vizuri na Mungu anaona kama watu wengi hawaoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile tunashukuru kwamba ile barabara inayotoka Makongorosi mpaka Lugwa, Itigi mpaka Mkiwa imo katika Bajeti hii kwa maana ya upembuzi yakinifu, tunaomba upembuzi ufanyike ili Bajeti zijazo na yenyewe sasa iwemo katika mpango wa kuwekwa lami ili tukamilishe ule mzunguko kwamba sasa Mkoa wa Singida huweze kufika kwa lami kutoka katika Mikoa yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo moja kidogo ambalo katika hii barabara ya Manyoni, Itigi, Chaya, Tabora, mkandarasi ameshaanza kufanya kazi, tatizo ambalo tunaliona ambalo naomba *comrade* Magufuli ulitazame, sasa kwa sababu Manyoni, Itigi, Tabora, barabara mpya inatengenezwa, hii ya zamani imeshaachwa kutoka Manyoni kwenda Itigi na kwenda mbele zaidi mpaka Chaya kwa sababu zamani sasa haitengenezwi ni mashimo matupu, tunaomba wakati mpya inatengenezwa hii ya zamani basi ipitike hili niombe rasmi na kwa sababu najua *comrade* wewe ni msikivu, nadhani hili utalisikia. *(Makofi)*

Sasa baada ya shukrani zote hizo na kutoa mambo ambayo yanafanyika, sasa tuje katika maombi. Barabara mpya ya kutoka Dodoma, Manyoni, Singida ilipofika Manyoni, ilipita pembeni ya mji, kwa jinsi walivyo *design* ile barabara. Sasa ile ya zamani iliyokuwa inapita katikati ya mji, hiyo nayo tunaiombea, ombi lilishakuja kwako Mheshimiwa Waziri, kwamba na yenyewe...

**TAARIFA YA SPIKA**

**SPIKA:** Kuna nini Ole-Sendeka, maana yake yupo kwake kule, sasa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE- SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nimeomba taarifa. Kanuni ya 68(8)…

**SPIKA:** Ni nini mwongozo, utaratibu, taarifa. Kuhusu taarifa.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, nimelazimika kuomba taarifa kwa mujibu wa Kanuni ya 68(8) na nimelazimika kwa sababu ni mara ya tatu sasa, wachangiaji waliokuwa wakichangia Mheshimiwa Mbunge mmoja aliomba Mwongozo hapa kwako, uli-*comment* na sina haja ya kujibu hoja iliyosemwa na Spika, lakini Mheshimiwa kaka yangu na mtu ninaemuheshimu sana aliyekuwa akichangia sasa hivi ameedelea kuasa kana kwamba Mwongozo niliouomba jana ambao ulikuwa unasubiri majibu ya meza, nilikuwa nalenga kuigawa nchi hii kwa misingi ya uelewa au kwa misingi ya kupotosha Utaifa na kutokutambua nia na dhamira ya Serikali yetu ya kuunganisha nchi katika Mikoa na hasa katika Mikoa ya pembezoni kwa kuunganisha kwa barabara ya lami. *(Makofi)*

Niliomba Mwongozo kwa nia ya kuweka mambo vizuri ya kuonesha kwamba yapo maeneo katika nchi hii ukiacha barabara za Kitaifa ambayo yamependelewa na narudia kusema ukisoma hotuba ya Waziri katika ukurasa wa 14 na 15 zipo barabara nilizotoa mfano kama za Kilimanajro zilizogawanywa ukitoka, nisome ukurasa wa 14 kwa ruhusa yako, ningeweza kukuonesha, ningeweza kukuonesha upendeleo wa wazi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Naomba Mwongozo tu, unataka kusema nini?

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa yangu niliyokuwa naitoa ni kwamba Mheshimiwa aliyekuwa anasema, nataka nikueleze Mwika Kiraracha kilomita 34 nenda hapo mbele ukurasa wa 14, utakuta barabara nyingine ya barabara ya Sadala Masama kilomita 12, nenda Kibosheshine mpaka kwa Rafaeli kilomita 43, nenda Kiluo, Nduoni, Marangu kilomita 31, nenda barabara ya Kawawa, nataka kuonesha upendeleo ili kuweka haki sawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge naomba ukae kwanza. Hivyo sivyo unavyoulizwa Mwongozo, kwanza jibu lako sisi hatujakujibu, lile hatujakujibu, wenzio wanachangia tu. Tuombe uvumilivu, huo sio utaratibu unaousema. Sasa wewe unataka tukuongoze nini? Kwa sababu lile la Mwongozo wa jana, hujajibiwa Mheshimiwa, kwa hiyo, ningeomba sana tumuache yule aendelee kujadili, hujajibiwa ule Mwongozo wa jana. *(Makofi)*

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. nilichokuwa nasema tu ni kwamba ndugu zanguni ni Bajeti ya kwanza katika Bajeti tano, tujenge uvumilivu tu, kama jambo halikufanyika mwaka huu, bado mwaka wa pili, mwaka wa tatu, bado mwaka wa nne mpaka mwaka wa tano jamani. Si kwamba barabara zote mwaka wa kwanza zinazotakiwa kujengwa mwaka huu, wapo Watanzania wenzetu tu ambao na wenyewe vilevile wanatushangaa tunapolalamika. Nadhani na naomba tu tuvumiliane jamani, nchi yetu wote hii, tudumishe umoja wetu na ustaarabu wetu. Kwa *speed* hii wanayokwenda akina Magufuli baada ya miaka mitano, tuwape nafasi, nina hakika kwa ndugu yangu Ole-Sendeka itafika, nina hakika kabisa kabisa, wote tupo hapa na tunapanga sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa nazungumzia suala la barabara mpya ya lami, imepita pembeni ya mji, kwa sababu ile ya zamani iliyokuwa inapita katikati ya Mji wa Manyoni, ile tulikuwa tumeiombea, tumeandika barua katika Wizara ya Ujenzi na bahati nzuri wakati wa kuzindua barabara mpya alipokuja mwaka jana mwishoni, Mheshimiwa Waziri Mkuu akatoa ahadi mbele ya Wanamanyoni kwamba na ile ya zamani iliyokuwa inapita katikati ya mji ambayo si ndefu sana, kilomita nne, tano tu kwamba na yenyewe itawekwa lami. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ile kauli na ahadi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Magufuli sidhani kwamba utaiweka pembeni, najua mwaka huu kwa barabara ile haimo kwenye kitabu hiki. Hii kengele hii tuligawana na Mheshimiwa Ole-Sendeka?

**SPIKA:** We endelea tu.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, najua katika Bajeti hii ya mwaka huu, hii barabara ninayoisema haimo na kwa sababu zipo Bajeti zingine zinakuja nne, Mheshimiwa Magufuli basi naomba sana hii barabara iwemo kwa sababu ni kilio cha watu wa Manyoni. *(Makofi)*

Ombi la pili, tunayo barabara ambayo inakwenda kwenye tarafa inayoitwa Tarafa ya Nkonko ambayo ipo pembezoni, hii barabara inatoka Manyoni, inakwenda Nkonko, inakwenda Sanza inakwenda mpaka Ikasi. Hii barabara ina umuhimu wa kipekee kabisa, nashukuru mwaka uliopita ilianza kutengenezwa, ninachoomba mwaka huu vilevile, nimeona imetengewa fedha kidogo, lakini naomba tuletewe mkandarasi ataitengeneza vizuri kwa sababu ndiyo barabara pekee yake inayohudumia Tarafa ya Nkonko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ya barabara hii ni daraja pale Sanza kuna daraja. Nimeona limetengewa pesa katika Bajeti hii kama shilingi milioni 145, lakini ninachoomba wataalamu kwamba daraja pale limeshajengwa mara tatu, linasombwa na maji. Embu waulize wenyeji wawaeleze tabia ya ule mto, ule mto una tabia ya kuhamahama, kila wakijenga daraja linakuja kusombwa na maji, naomba safari hii kabla kazi hii haijaanza, wakae na wazee wapate historia ya ule mto ili tusiendelee kupoteza pesa za Serikali, kila mara wanajenga daraja halafu linasombwa na maji, lakini nashukuru watu wa Sanza kama wananisikia kwamba daraja lao lipo katika ndani Bajeti ya Mheshimiwa Magufuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tulishaomba ipandishwe barabara inayotoka Chukuyu inakwenda Majiri, inakwenda mpaka Ikasi, inakutana na hii ninayoisema, ili ombi limeshakaa Wizarani miaka mitatu Mheshimiwa Magufuli la kupandisha hadhi barabara hii, naomba safari hii sasa lile ombi letu likubalike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimeona katika Bajeti kwenye ukurasa wa 91 wanao utaratibu wa mafunzo ya ujenzi wa barabara za vijijini kwa kutumia nguvu kazi yaani *labour based technology.* Nadhani jambo hili, Mheshimiwa Waziri ni jambo zuri sana, kule vijijini, barabara za vijijini ebu tufundishe wananchi kutengeneza barabara wenyewe kama wanavyofanya *TASAF. (Makofi)*

Barabara za *TASAF,* barabara zinatengenezwa na wanavijiji na wanalipwa. Kwa hiyo, tukifanya hivi tutapata mambo mawili, tutapata barabara nzuri, wanajengwa vizuri tu kwa sababu tunasimamiwa na wataalam, tutapata barabara na wananchi watalipwa kwa hiyo itakuwa ni ajira na barabara za vijijini zinaweza zikaajiri watu wengi sana.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hili la kutengenza barabara kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi ni jambo jema, tulisukume kwa nguvu zetu zote kwa sababu barabara za *TASAF* zilizojengwa kwa utaratibu huu ni mzuri na mpaka sasa bado zinafanya kazi mpaka sasa. Zingine ni nzuri kuliko za wakandarasi. Kwa hiyo, naomba jambo hili mlisukume kwa nguvu sana kwa sababu ajira nyingi sana zitapatikana kama barabara zitajengwa kwa teknolojia ya kutumia nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, katika barabara yetu hii ya ukanda wa kati ambayo inahudumia mikoa karibu kumi, inahudumia nchi nne, inahudumia bidhaa za Uganda, Burundi na *DRC.* Sasa barabara hii ina usumbufu mwingi na ucheleweshaji mwingi sana wa mizigo, kinachochelewesha mambo mawili, moja lipo katika Wizara ya Mheshimiwa Magufuli la mizani, la pili lipo Wizara ya Mambo ya Ndani la *traffic*. Kwa hiyo, gari likishabeba mizigo bandarini, linakwenda labda Burundi au Rwanda, huko njiani unakumbana na mizani mingi mno. Kutoka tu Dar es Salaam mpaka katikati, mpaka Singida kuna vituo karibu saba vya mizani. Sasa je, mpaka afike Rusumu kule mpakani na Burundi kule, mizani mingapi, vituo vingapi? Kwa hiyo, kila mzani pale watatumia saa mbili, saa tatu, kila mizani. Sasa rafiki zangu polisi wa *traffic* ndiyo usiseme, kilomita kumi tayari *traffic,* simama, wiki nzima gari halijafika Burundi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante umeshamalizia Burundi, ahsante sana. *(Kicheko*)

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante, shukrani na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu na mimi nichangie katika hoja hii. Nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na timu yake yote, nawapongeza kwa kuandaa Bajeti nzuri na hata mwisho wa kitabu wameweka *pictorial diagrams* nzuri za kuonesha kila Mkoa ambazo zinafafanua vizuri jinsi barabara zilivyogawiwa katika kila Mkoa na katika kila sehemu ya Tanzania. Lakini nawapongeza kwa kuendesha Wizara hii muhimu vizuri sana. *(Makofi)*

Nakumbuka katika Bunge lililoanza mwaka 1995, Wizara ya Ujenzi ilikuwa Wizara ya matatizo sana, Wizara iliyokuwa inalalamikiwa sana. Lakini kwa usimamizi mzuri na uendeshaji mzuri, leo hii kila anayesimama anasema kwamba Bajeti ya Wizara hii ipite bila kupingwa na bila kupunguzwa, nawapongeza sana waendeshaji wa Wizara hii ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kyaka, Bugene, Kasulo katika Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Karagwe, labda nieleze kidogo, juzi juzi nilisimama nikaongea juu ya umeme, lakini nikaongelea sehemu ambazo zimo katika Jimbo la Karagwe kwa mwenzangu ambaye tunashirikiana Mheshimiwa Blandes, watu ambao wana nia isiyo nzuri kule Karagwe wakaanza kuhoji na kusema kwa nini hakuongea Mheshimiwa Blandes. Waelewe kwamba tunashirikiana vizuri, mimi na Mheshimiwa Blandes katika kutetea maslahi ya Wilaya mama ya Karagwe na Wilaya mbili zote, Wilaya ya Karagwe na Wilaya mpya ya Kerwa. Kwa hiyo, wasianze maneno ya kushangaa, wajue kwamba sote ni wamoja, letu ni moja la kuitetea Wilaya ya Karagwe na Wilaya mpya ya Kyerwa. Kyaka, Bugene na Kasulo tunashukuru Serikali kwamba sasa kazi imeanza katika kisehemu cha Kyaka kwenda mpaka Bugene kinajengwa kwa kiwango cha lami kilomita 59. Tunaomba kazi iendelee kutekelezwa vizuri, mkandarasi aliyepo asimamiwe vizuri ili tupate barabara nzuri. *(Makofi)*

Lakini pia kipande cha Bugene kwenda mpaka Benako, fedha ipo ya upembuzi yakinifu, tunaomba kazi hii ianze ili mbele ya safari na hiki kisehemu kijengwe pia kwa kiwango cha lami ili sehemu yetu ifunguke pale Mkoani Bukoba, lakini pia ifunguke kuelekea kule Kasulo kuteremka mpaka kwenda Kahama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mugakorogo, Bugomola mpaka Murongo. Hii barabara ina mtandao wa kutoka katika sehemu ya Karagwe kwenda katika Wilaya mpya ya Kyerwa, fedha za upembuzi yakinifu zipo, tunaishukuru Serikali pia, tunamshukuru Mheshimiwa Waziri, lakini tunaomba pia haya mambo yasibaki ndani ya vitabu, upembuzi uanze ili fedha zitafutwe na hii ijengwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bugene – Nkwenda - Murongo. Mheshimiwa Rais katika ziara zake za kikazi wala sio za kampeni amesimama pale Murongo tarehe 19 Januari, 2009 na pia alisimama pale Isingiro akihutubia mkutano mkubwa tarehe hiyo hiyo ya tarehe 19 Januari, 2009 kwa upendo mkubwa akawaahidi wananchi kwamba hii barabara itajengwa kwa kiwango cha lami, lakini pia amekuja tarehe 28 Agosti, 2010 katika mkutano mkubwa wa hadhara pale Nkwenda akazidi kurudia kwamba wananchi wangu hii barabara naiangalia ili ijengwe kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kyerwa wamenituma nikumbushe maneno haya ya Mheshimiwa Rais ili barabara hii ifanyiwe maandalizi ya kujengwa katika kiwango cha lami. Barabara hii inaunganisha Wilaya ya Karagwe na Wilaya ya Kyerwa Wilaya mpya. Inaunganisha nchi yetu na nchi ya Uganda. Lakini pia barabara hii ina *traffic density* kubwa sana. Lakini pia eneo hili lina uchumi mkubwa sana. Tunaomba, nasimama hapa kwa niaba ya wananchi wa Kyerwa nikikumbushia na kumwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie hili suala na alipe uzito unaostahili hasa kwa kuwa na maneno ya Mheshimiwa Rais kwa watu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara inayopita kwenye Mlima wa Rwakunuka *(Rwakunuka escapement),* pamoja na shukrani kwamba ujenzi umeanza pale kwenye kilima cha Rwakunuka, lakini naleta kilio cha Wanakyerwa. Hiki kilima alipitia Mheshimiwa Rais mwenyewe tarehe 19 Januari, 2009. Aliona mwenyewe jinsi kilima kile kilivyo cha hatari sana. Aliona mwenyewe jinsi

makona yalivyo mabaya sana. Aliona mwenyewe kwamba ukitokea utelezi wakati wa mvua wananchi wamo katika hatari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kilima hiki urefu wake ni kilomita nne tu lakini sasa hivi baada ya mimi kufuatilia kwa *TANROADS* mkoani kila mara nimekuwa nikienda *TANROADS* mkoani. Nikumbushie ahadi ya Mheshimiwa Rais imekuwaje? Mbona ujenzi haujaanza? Mbona utekelezaji haujaanza? Mwishowe sasa mkandarasi yupo, ameanza kujenga, lakini kinachojengwa hata siyo kilomita moja, kinachojengwa pale ni mita 700 tu kutoka kwenye hizo kilomita nne, kwa hesabu za kawaida ndogo tu, hata kama hujaenda shule. Kama *speed* hii ya kujenga kile kilima cha Rwabunuka cha kujenga mita 700 kwa mwaka, itakuwa miaka mitano au miaka sita kabla ya hicho kilima hakijajengwa kukamilishwa. Lakini pia itakuwa mpaka aliyeahidi Mheshimiwa Rais ametoka madarakani, amemaliza muda wake kabla ya hicho kilima hakijajengwa barabara ikakamilika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kushukuru kwamba shughuli imeanza naleta kilio cha Wanakyerwa kwamba angalau kazi ya maana ifanyike angalau ijengwe nusu ya kilomita nne waanze na kilomita mbili, mwaka wa pili wajenge kilomita mbili nyingine. Lakini mita 700 hata kilomita moja haitimii, naomba Mheshimiwa Waziri asikie kilio hicho na ajitayarishe atenge pesa kiasi fulani angalau kilomita mbili zijengwe. Wananchi wa Kyerwa wanasikia kilomita 52 zinajengwa kwingine. Kilomita 70 zinajengwa lakini wenyewe zawadi yao waliopewa na Mheshimiwa Rais ya kilomita nne, hata hiyo haijengwi kwa ukamilifu, inabidi wasubiri waangalie tu mita 700. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa upendeleo maalum. Atenge pesa ili kazi hii iweze kufanywa na kwisha kwa wakati muafaka. Hili likifanyika litasaidia biashara kati ya Wilaya ya Kyerwa na nchi ya Uganda na itasaidia pia wananchi wanaoishi upande mmoja wa mlima ambao ni wakulima stadi kabisa, wanazalisha sana kahawa, washawishike sana kuleta mazao yao kuuza katika sehemu ya Tanzania kuliko kuyapeleka sehemu nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba haya niliyoongelea yote, Mheshimiwa Waziri ayawekee maanani na mimi niseme kwamba ninaunga kabisa mkono hoja yake ya leo. Nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kushukuru sana kwa kupata nafasi hii adimu ya kuchangia leo Wizara hii na nianze kwa kweli kwa kupongeza Wizara kwa kufanya kazi kubwa katika nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na sote ni mashahidi barabara ni muhimu na nichukue nafasi hii kushukuru sana barabara ambazo zimekuwa zikijengwa na zinazoendelea kujengwa na hususani kwa niaba ya wanawake wote ninaowawakilisha wa Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Iringa kutokea Wilaya ya Ludewa, Makete na Njombe yenyewe. Nasema hivi kwa sababu wazalishaji wakubwa wa mazao vijijini ni akinamama, kama wanazalisha na akinamama hao wanakosa masoko hususani ya mahindi kwa mfano akinamama wa Ludewa wakikosa soko la mahindi, akinamama wa Makete wakikosa soko la mahindi na mbao tunazopasua na Njombe inakuwa ni changamoto kubwa. Kwa hiyo, nashukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Pia nichukue nafasi hii kushukuru barabara ya Dodoma – Mtera - Iringa. Barabara hii imekuwa ni changamoto kubwa, lakini imeanza kushughulikiwa sasa hivi wanaanza *feasibility study* na sisi kwenye kikao cha *RCC* na kikao cha *Road Board* cha Mkoa tuliijadili sana. Tunaomba wale wakandarasi wafanye kazi hiyo mapema na kwa haraka, kwa sababu Wabunge wengi wanaotoka Mkoa wa Mbeya, wanaotoka Mkoa wa Ruvuma, Rukwa wanazunguka hadi Morogoro, lakini kumbe *short cut* ipo. Tungeweza kufika mara moja wanatoka kule wanakuja kulala pale kwetu Iringa na Njombe tunawapokea vizuri na kesho yake wanakuja Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini wanatoka, wanapita watu wa Ruvuma au watu wa Rukwa wanapita Mkoa wa Njombe, wanapita Mkoa wa Mbeya waje Mkoa wa Morogoro, unapita mikoa

minne. Kwa hiyo, niiombe Wizara, maeneo ambayo tunaweza tukapata *short cut* za kuingia mkoa kwa mkoa yapewe kipaumbele. Nitumie nafasi hii kusema kwamba hata Mkoa wa Dar es Salaam hivi Watanzania wote tukishakwenda Dar es Salaam lazima tupite Ubungo? Ukiwekewa jambo Ubungo pale unapita wapi? Hatuwezi kupita *entrance?* Wengine wanaingilia Ubungo, wengine wanapitia Bagamoyo, wengine Kibaha unaingia Dar es Salaam. Lakini leo hii Watanzania milioni 40 akisema anaenda Dar es Salaam wewe msubiri tu Ubungo. Hamna *short cut* nyingine kwa ajili ya usalama tupate *entrance* za kutosha kwenye Mikoa na Wilaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na nitumie nafasi hii kusema kwamba tumepata Mkoa mpya wa Njombe, Mkoa huu unahitaji barabara tena za lami, barabara inayopita pale ni moja tu ya Taifa ambayo inaunganisha Tanzania - Zambia. Lakini Mkoa wa Njombe na Wilaya zake tunahitaji barabara za lami. Niishukuru sana Makete, Rais alitupa barabara pale ya lami, inatusaidia sana. Lakini tuunganishe basi Makete na Kyela. Wilaya na Wilaya, tuunganishe Ludewa na Makete. Sasa mtu ukitaka kutoka Ludewa kwenda Makete lazima uje Njombe kwanza. *You are talking of three to four hours,* halafu utoke Njombe uingie Makete *you are talking of three to fours again* ni sawa sawa na mtu kutoka Ludewa mpaka Dar es Salaam saa nane kwenye mkoa mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakuomba sana *Madam Speaker* hili uliangalie na ulisimamie sana. Haiwezekani kamkoa kamoja tu ukitaka kwenda Wilaya na Wilaya utumie saa nane, utoke uende. Kwa hiyo, kwa niaba ya wananchi wa Makete na Ludewa wameniomba sana Mheshimiwa Waziri watusaidie barabara ya kuunganisha Wilaya ya Makete na Wilaya ya Ludewa kwa sababu barabara ikiwa salama inapitika, unaokoa muda. Wenzetu Waingereza wanasema *time is money* kwa sababu utaweka mafuta ni gharama, utasafiri saa tatu *lunch time* itafika itabidi ukale chakula. Upo na wananchi tena na kadhalika na huduma zingine *you see!* Lakini kumbe barabara ingekuwa salama na safi, unatumia muda mfupi. *We save money*, uchumi zile hela zinafanya uwekezaji tunalipa *TRA* nchi inapata mahela. Hapo mambo yanakuwa *super.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, niombe sana, najua hii ni Wizara ambayo imeshikwa na watu *smart.* Kwa hiyo, hamtaniangusha barabara ya Ludewa - Makete iunganishwe Makete kwenda Wilaya ya Kyela Mbeya pale *short cut* tupate vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendelee kusema barabara ya Itoni – Ludewa - Manda. Barabara hii ya Itoni inakwenda mpaka pale Lusitu, Kata ya Madope, Mlangali, Mangi, Luana, Mkomi Ng'ombe, Lwilo mpaka Manda.

Hii barabara ni muhimu sana. Barabara hii inakwenda kwenye ile Wilaya yenye madini ya Mchuchuma na Liganga. Madini haya si ya wananchi wa Ludewa peke yake, ni ya nchi nzima ya Watanzania na tunasema wawekezaji waje. Madini ya Mchuchuma na Liganga yameingia kwenye Ilani, yapo kwenye *vision 2020-2025 - Millenium Development Goals.* Kwenye *internet,* masuala ya Mchuchuma na Liganga yapo lakini bila miundombinu inayoeleweka bado ni changamoto *Madam Speaker*, ni changamoto kubwa. Hivi kweli tuna maanisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, habari ya Mchuchuma na Liganga Waheshimiwa Wabunge wenzangu ni mashahidi. Wengine hapa tumeanza kipindi kilichopita tumesikia Mchuchuma na Liganga, mwaka huu Mchuchuma na Liganga na mwakani Mchuchuma na Liganga, hivi lini inaanza ku-*take off* ndugu zangu? Kila mwekezaji akija anauliza reli iko wapi? Tunabaki tunatazamana. Kiwanja cha ndege kiko wapi? *You know I am coming from Johannesburg, you know I am coming from UK, I need to invest.* Huwezi kumweka mwekezaji saa tatu asafiri kwenda barabarani *three hours.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwanja vya ndege tunahitaji. Kwa hiyo, kwa kweli niwaombe sana na huu utaratibu nchi kama Tanzania halafu hatuna *airline* inakuwaje? Ukitaka kwenda Kenya, upande *South African Airways* maana yake utakwenda Johannesburg kwanza ndiyo urudi Nairobi. Umewachangia *KQ Kenyan Airways.* Ukitaka kwenda Nairobi…

**SPIKA:** Hiyo ni kesho hiyo.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kwa kuwa Mawaziri wote wapo na wananisikia, niombe sana na pale Ludewa tunaomba *air wing* moja Mchuchuma na Liganga bila *air wing* itakuwa ni changamoto. Barabara tunaomba i-*take off* mapema hii barabara ya Itoni - Ludewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara hii tumeijadili kwenye kikao cha *RCC* na tumeomba iwe *up graded*. Mheshimiwa Waziri *estimate* zipo mezani kwako pale tumeshakuletea. Tunaomba kipaumbele. Katika Bajeti hii barabara ya Itoni - Ludewa imepangiwa shilingi milioni 150 kilomita nane. *Are we serious 150?* Maana yake ni *earth road.* Ile ni hela ya *public community partnership* labda tukiingia wakati wa shughuli ndogo ndogo. Lakini kwa kweli barabara hii inahitaji kipaumbele maana ni kwa maslahi ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hawa wawekezaji wa Mchuchuma na Liganga huwezi kuwaweka siku mbili walale njiani, watoke Dar es Salaam waje walale Iringa halafu tena useme ngoja kwanza tuangalie kama mvua imenyesha ama haijanyesha. Leo imenyesha subiri mpaka kukauke kauke ndiyo twende, twende Mundindi pale kwenye madini ya Mchuchuma na Liganga leo imenyesha sana, maana tutakwama. Huko lazima tutoke. *(Makofi)*

Kwa hiyo sisi tutakuletea rasmi, tumeshaleta lakini tutafuatilia na *documents* za kikao cha *RCC* na *Road Board* tutakuletea rasmi Mheshimiwa Waziri na wewe una ushirikiano sana na Mkoa huu mpya. Tunaomba sana barabara hii kwa kweli ni muhimu. Madini haya ya Mchuchuma na Liganga kweli kabisa pasipo miundombinu ya barabara itaendelea kuwa changamoto ya kutosha. Barabara hii tunaomba hata wakati wa ujenzi ipanuliwe, maana kuna ule mlima unaitwa Gangi Tolole, Jongo Jongo na pale panaitwa Kona Setani, maeneo haya yana kona kali, yanafanana na Kitonga. Sasa maeneo haya bila kuweka utaratibu mzuri lami inayoeleweka na *traffic light* ikiwezekana maana ikiwa *single road* lazima mmoja akae huku kuchungulia amwambie yule wa chini subiri na kuna eneo linalokwenda Lupingu barabara ile ni changamoto kubwa. Juzi juzi hapa mwaka jana kuna watu wamefariki gari ilitumbukia.

Mheshimiwa Spika, tunaomba ule upana ufanane na ile barabara ya Kitonga ili gari mbili ziweze kupishana, maana madini ya chuma yatakayokuwa yanasombwa kule yatahitaji *semi trailer, semi trailer* inahitaji *space* ya kutosha. Kwa hiyo, sisi tutawapa ushirikiano mkubwa, nguvu kazi, rasilimali watu, vijana wapo tayari kabisa kujitolea kwa moyo wote. Lakini changamoto kubwa ya Mkoa wa Njombe hususani Wilaya ya Ludewa na Makete ni barabara, tunaomba sana sana kwa kweli maeneo hayo yazingatiwe. *Feasibility study* ianze mapema kabisa, barabara hii ifanye kazi kwa maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini pia wakati wa ujenzi wa barabara ni muhimu tukazingatia, yapo maeneo ya kupita baiskeli, yapo maeneo ya kupita pikipiki, yapo maeneo ya kupita wanyama. Ukienda barabara za nchi zingine yaani hampishani na pikipiki hapo, ng'ombe, baiskeli hapo hapo, upo utaratibu.

Sasa barabara zetu ng'ombe anapita mbele, kushoto baiskeli, huku pikipiki, ajali zinakuwa nyingi. Haya ni mambo ambayo ni ya kusaidiana saidiana, tunaweka sehemu huko pembeni. Kunakuwa hamna ajali, unasikia mara watoto wamegongwa. Wengine mnatoboa pale chini ya barabara, watoto wa shule wanapita salama kabisa, hamna ajali. Mambo yanakuwa safi kabisa. Kwa hiyo, tunaomba sana mambo haya ni ya kuzingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo lingine muhimu niombe maeneo ya mizani. Makambako pale, magari yanasimama sana. Yale magari yanayosimama kama yamezidisha mizigo zile faini zile hazilingani na bei ya barabara ya lami kilomita moja. Taarifa nilizonazo barabara ya lami kilomita moja ni kama milioni 400. Lakini mtu akizidisha mzigo amekwishatoka nao Tunduma – Zambia - Malawi akifika Makambako amekwishaharibu barabara, utamwambia faini kiasi kadhaa. Kile kiasi anacholipa hakifanani na uharibifu, *we have to do something Madam Speaker. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini mimi najiuliza mzigo umezidi kwenye mzani, mbona hatuoni mbao zinashushwa, viazi vinashushwa, bidhaa kwamba huu mzigo ume-*over load* shusheni, mkashushe mje mchukue? Sasa hii *over loading* wanapunguzaje? Ndiyo swali langu maana yake

kila wanaozidisha mizigo gari limepita. Sasa mbona huwa hatuoni ma-*godown* haya ambayo mizigo inatulizwa pale wewe ume-*over load? (Makofi)*

*Madam Speaker,* niombe sana hizi barabara ni za kuzitunza sana maana ni za gharama kubwa. Tuzitunze vizuri, wengine ambao hatujapewa barabara eneo la Ludewa tunalia. Kwa hizi ambazo tunazo barabara tuzitunze. Tunaomba sana Mkoa huu mpya wa Njombe wenye Wilaya ya Ludewa, Makete na Njombe yenyewe kwa kweli mtusaidie. Sisi tukipata barabara tunaahidi Serikali kilimo tulichokuwa tunakifanya na akinamama wenzangu yale mashamba tunayolima ya viazi na mahindi tutalima maradufu maana bidhaa zetu zitakwenda mpaka *East Africa Common Market. (Makofi)*

Lakini leo hii tunalima mahindi, tunategemea *SGR food* ndiyo waje wanunue Ludewa. Hamna watu wengine. Wafanyabiashara wanaishia Makambako kwenye lami na Kunzombe. Ludewa - Makete hawaji wanasema barabara hazipitiki. Sasa yale mazao, *godown, warehouse* tuna vihenge. Vihenge vile ikinyesha mvua ndiyo hivyo, tunaomba Serikali mtusaidie barabara hizo. Wafanyabiashara waje wanunue mahindi, waje wanunue viazi na mbao tunazopasua Kumakete na Ludewa waje waje barabara. Changamoto hizi zinapelekea sisi wananchi, utakuta tunatoka Ludewa uje ulale Njombe, maana ile barabara unatoka saa 12 unafika saa 8.

Mheshimiwa Spika, safari ya kwenda Dar es Salaam lazima utenge ya kulala *guest* njiani. Unalala siku moja njiani. Lakini kumbe barabara ingekuwa salama aah, unatoka siku hiyo hiyo *time is money* umeokoa hela, tunasomesha watoto. Lakini *over head expenses* ya mwananchi mmoja ni kubwa mno. Gharama za uendeshaji tu maisha kutokana na miundombinu na changamoto za barabara kiuchumi. *(Makofi)*

*Madam Speaker,* nakuomba sana utusaidie sana kwa kweli habari ya barabara Kunzombe *Madam Speaker* utusaidie. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ameshindwa kusema kwamba ananisemea na mimi. Pale Itoni ndiyo kwangu hasa. Wale wanaokwenda kuchimba madini watakuja kwenye starehe Njombe, sasa wanakujaje? Kwa hiyo, tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Naomba nimwite Msemaji wetu wa mwisho mchana huu Mheshimiwa Iddi Azzan. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. IDDI M. AZZAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kwenye Wizara hii. Niendelee kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Kinondoni, lakini niendelee kuwapa pole wakazi wote wa Dar es Salaam ambao hivi sasa ninapozungumza wapo kwenye foleni, kwenye misongamano ya magari, wanashindwa kuwahi kazini, wanashindwa kuwahi hospitali, nawapa pole sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee naomba nichukue nafasi hii kuipongeza sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Nampongeza sana Mwenyekiti wa Kamati hiyo pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo na yule aliyesoma Taarifa ya Kamati hiyo, jana. Nampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kweli tunataka mabadiliko ya ukweli ya kuondoa msongamano wa magari Dar es Salaam, basi maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge, yangechukuliwa kwa uzito unaostahili, tatizo la msongamano Dar es Salaam lingeondoka. Lakini tumekuwa ni wazuri sana kwenye kuongea, utekelezaji unakuwa sivyo. Wananchi wa Dar es Salaam wanaendelea kuteseka, kuumia, kwa sababu ya msongamano mkubwa uliopo. Tunaathirika kiuchumi kwa sababu, ya msongamano ambao upo. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, pamoja na mambo yote wanayofanya na matatizo yote ya barabara yaliyopo nchini, lakini Dar es Salaam ni lazima iangaliwe kwa upendeleo wa pekee, na siyo upendeleo, Dar es Salaam itendewe haki kwa sababu, pato kubwa la nchi hii karibu 80% ya pato la Taifa linatoka Dar es Salaam. Leo Dar es Salaam mnaitengea Shilingi bilioni tano kwa ajili ya kuondoa msongamano. Huo ni mchezo wa kuigiza. Naomba sana Serikali, kama kweli tunataka kuondoa tatizo hili, tunataka uchumi wetu ukue, kuondoa umasikini kwa wananchi wetu, basi ni lazima tuboreshe miundombinu na kuondoa msongamano uliopo Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumekuwa mafundi sana wa kuongea, tumeanza kuzungumzia suala hili la msongamano Dar es Salaam tangu nimeingia Bungeni. Wenzetu wa Kenya walianza juzi tu, lakini hivi ninavyozungumza tayari wameshazindua barabara yao ya juu, yaani *fly over,* tayari imezinduliwa, inafanya kazi. Sisi bado tuna hadithi tu hizo hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kasungura ni kadogo kama tunavyosema, kwamba tugawane kasungura hako kadogo, lakini kasungura hako kadogo ni nani anakafuga? Yule anayefuga si ndio anatakiwa apate angalau kanyama kakubwa kidogo? Dar es Salaam ndiyo tunaofuga huyo sungura, kwa maana ya kutoa pato kubwa la nchi hii. Kwa hiyo, ni lazima tuiangalie Dar es Salaam kwa namna ya pekee kabisa. Msongamano umezidi, Mheshimiwa Waziri amesema hapa kwamba tunajenga *fly over TAZARA.* Lakini *fly over* ambayo anaizungumza ni pesa ambazo tunatarajia kupata kwa wahisani, pesa kutoka Japan, *JAICA! (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi juzi Japan wamepatwa na tatizo kubwa sana, uchumi wao umeyumba. Kwa hiyo, kuna mawili, ama wanaweza wakakubali kutusaidia ama wakakataa. Hivi wakikataa, tunafanya nini? Katika hela zetu za pato letu la Taifa, hela zetu za ndani, tunashindwa kweli kutenga Shilingi bilioni 20 kwa ajili ya kujenga *fly over* moja, tunangojea wafadhili, Wahisani watusaidie! Namna hiyo hatuwezi kwenda ikiwa kila kitu cha msingi cha maana kinangojea wafadhili, kwa kweli hii sio sawasawa. Naiomba sana Serikali iliangalie kwa makini sana suala hili, kwamba Dar es Salaam iangaliwe kwa jicho la huruma ili tuweze kuondoa msongamano, kuondoa matatizo yaliyopo pale. Tatizo ni kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wametenga pesa katika hizo Shilingi bilioni tano kwa ajili ya kumalizia baadhi ya barabara. Kuna barabara ya Maziwa, Kigogo kutokea Jangwani na Yanga kule, ilianza kujengwa, mara hii imetengewa pesa ili ikamilike. Ujenzi wake unasuasua, umechelewa. Yapo baadhi ya maeneo wananchi waliahidiwa kulipwa fidia, lakini imekuja kusemwa kwamba fidia haitalipwa. Wananchi pale wamegoma na mwisho wa siku watakwenda Mahakamani, ujenzi ule utazidi kusimama. Kwa nini tuliwaahidi kuwalipa fidia mwanzo halafu hivi sasa tuseme hatutaki kuwalipa fidia? Naomba sana, kama tuliwahidi mwanzo, wakafanyiwa tathmini nyumba zao tena mara mbili, mara ya kwanza walifanyiwa tathmini wakarudia tena kufanya tathmnini, basi walipwe wale wananchi fidia yao ili barabara ile iweze kukamilika, ujenzi ule ukamilike, tusaidie barabara ziwe zinapitika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, iko barabara ya Dampo, Kigogo kwenda Dampo kutokea *Mandela Road.* Ni barabara ambayo inaondoa msongamano sana, ni zile barabara ambazo tuliomba muda mrefu zitengenezwe ili kuondoa msongamano, *Ring Roads.* Lakini cha ajabu kwenye bajeti ambayo imeletwa hapa, eti imetengewa pesa kwa ajili ya kutengenezwa kwa kiwango cha changarawe. Sasa ninajiuliza, ni changarawe gani? Hivi sasa ilipo ni changarawe, unatenga pesa kwa ajili ya changarawe! Yaani changarawe, maana yake ni nini? Unaweka nini pale? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini unapojenga barabara ya changarawe Dar es Salaam, kwenye eneo la makazi ya watu, maana yake ni nini? Unataka kuwauwa watu! Uwajengee barabara ya changarawe ili mavumbi yaingie kwenye nyumba za wananchi waathirike! Kwa hiyo, tathmini zenu mnazofanya za kujenga changarawe, mfanye na tathmini pia za afya kwamba, barabara ile ya changarawe tukiijenga wananchi wataathirika vipi?

Kwa hiyo, naomba sana suala hili la kujenga barabara ile kwa kiwango cha changarawe sikubaliani nalo. Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam hawakubaliani nalo! Ninyi Wabunge mnaokaa Dar es Salaam pia hamkubaliani nalo. Kwa sababu barabara ile inaondoa msongamano, ni barabara ambayo inapitwa na magari mengi. Huwezi ukafananisha barabara ile na barabara ya changarawe labda tutakayoijenga kwenye maeneo mengine, Chato au Kyela au sehemu nyingine. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kule magari yanayopita unayahesabu! Yanapita magari manne, magari matano, magari sita, magari kumi, magari ishirini. Pale yanapita magari mengi, zaidi ya magari 5,000 kwa siku. Sasa yale mavumbi, unajua ni kiasi gani yanawaathiri wananchi? Kwa hiyo,

nawaomba sana hilo suala lenu la changarawe ondoeni. Barabara ile tuliomba lami tangu mwaka juzi ijengwe kwa kiwango cha lami ambacho tulikubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Moroko – Mwenge, Mwenge – Tegeta, naishukuru Serikali, ujenzi umeanza kutokea Mwenge kwenda Tegeta, lakini asili ya barabara ile, na sikushangaa sana kwa sababu Mheshimiwa Mbunge mmoja jana alisema kwamba Mheshimiwa Waziri amezoea yeye anaanza kwa kinyumenyume huku. Kwa hiyo, ameanzia Mwenge kwenda Tegeta, sina tatizo, lakini kuna kipande cha kutoka Moroko kuja Mwenge, naomba kipande kile kiwekwe kwenye mpango haraka na kusiwe na sababu. Maana sababu zitakuwa kuna majengo, kuna tathmini, kuna hiki, hapana! Iliwekwa ijengwe, basi iwekwe hivyo hivyo kwa maana ya kujengwa. Kama mliweza kujenga Ubungo kwenda Kimara, mkavunja nyumba nyingi za walalahoi pale na barabara ikajengwa, tuliposema ijengwe ilijengwa, leo tunapata taabu gani? Kigugumizi gani cha kujenga Moroko kuja Mwenge? Naomba iwekwe kwenye mpango, hata kama kuna ghorofa la mtu, livunjwe, barabara ile ijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Uhuru ambayo iko Ilala ina historia. Imezungumzwa miaka mingi. Leo tunakwenda miaka 50 ya Uhuru, barabara haipitiki! Barabara ya hovyo hata yule aliyetupa uhuru wakati huo akija hivi sasa anaona hakuna mabadiliko yoyote! Kwa hiyo, naomba na barabara ile tulishaisema siku nyingi, mlishaiweka kwenye mpango, sijui ni kitu gani? Sijui ni kigugumizi gani mnashindwa kuikamilisha barabara ile? Tunaomba ikamilishwe, ijengwe kwa kiwango kizuri ili kweli ionekane ni barabara ya uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la wadau wengi kusimamia masuala ya usafiri Dar es Salaam, Kamati imezungumza, *SUMATRA,* sijui Jiji, sijui watu gani, hizo daladala mnazozikamata kutwa, ndio mnazizidishia msongamano, kwa sababu ukisimamisha tayari umeweka msongamano. Hivi hamwezi kutengeneza mpango ikawa kuna taasisi moja tu inayofanya kazi hiyo? Lazima kuwe na mambo yote haya kwenye masuala ya usafiri. Naomba hili liangaliwe kwa makini kama ambavyo ilipendekezwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge, hili suala la kupunguza misongamano na kuondoa kero kwa wananchi wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakubaliana tena na mawazo ya Kamati kwamba, Jiji la Dar es Salaam sasa liangaliwe kwa namna ya pekee. Ikiwezekana tuunde Wizara Maalum kwa ajili ya Jiji la Dar es Salaam. Ndivyo yalivyo majiji mengine kwenye nchi nyingine. Ukienda Nairobi pale utakuta kuna Wizara ambayo ni maalum kwa ajili ya Jiji la Nairobi. Kwa hiyo, tungekuwa na Wizara hiyo ingeweza kutusaidia. Kwa hiyo, mliangalie kwa makini, mawazo mazuri sana ya Kamati yametolewa. Wajibu wa Serikali ni kuyafanyia kazi na utekelezaji uanze, kuliko kuanza kuwa na maneno mengi, utekelezaji unakuwa sio sawasawa, wananchi wa Dar es Salaam wanazidi kuumia, wanazidi kuteseka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Polisi - Mabatini najua iko chini ya Halmashauri. Tumeipangia pesa mara nyingi kutegemea hela za *Road Fund* ili ijengwe, pesa hizo ama hamzileti, ama mnazileta mnavyotaka ninyi, matokeo yake, barabara ile mpaka leo haipitiki. Ni mbovu kupita maelezo! Namwomba sana Mheshimiwa Waziri, barabara ya Polisi - Mabatini ifanyiwe haraka kwa maana ya hela hizi za Mfuko wa Barabara, zipelekwe ile barabara ijengwe kwa kiwango cha lami ili kuondoa msongamano kwenye barabara ya Ali Hassan Mwinyi. Ni barabara nzuri ambayo inaweza kusaidia matatizo, kuondoa msongamano Sinza, kuondoa msongamano Ali Hassan Mwinyi, lakini pia, maana baadaye najua Spika atasema labda namsemea, lakini pia barabara hiyo Mheshimiwa Spika wetu, ndiyo barabara yake anayopita kwenda nyumbani kwake. Ni kero kubwa! Akienda na gari dogo ni shughuli! Kuna mashimo makubwa ya ajabu! Hivi mnataka Spika wetu akae wapi? Tukampangie *Movenpick?* Hapana! Atakaa kule kule Kijitonyama kwake, lakini barabara itengenezwe. Ikitengenezwa barabara itamsaidia yeye, lakini itawasaidia na wananchi wa Kijitonyama, itawasaidia na wananchi wa Sinza na wananchi wote wanaopita njia hiyo. Nami ndio Mbunge wake Spika tukiwa Dar es Salaam, lazima nimsemee. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Barabara ya kutokea Banana ambayo inakwenda kutokea Mbezi Mwisho, hii barabara ipeni kipaumbele, ipeni umuhimu, kwa sababu foleni zote za *Morogoro Road* zitapungua. Foleni zote za Ubungo – Kimara zitapungua kama tutajenga barabara ya Banana,

Kinyerezi na kwenda kutokea Mbezi mwisho, itasaidia kuondoa Msongamano sana. Hata ukiamua sasa malori yanayotoka Bandarini, yasipite *Mandela Road,* yasipite *Morogoro Road,* yapitie Banana, yaende *Airport.* Banana yanatokea Mbezi Mwisho, yanaendelea na safari. Itasaidia sana kuondoa msongamano, kuondoa matatizo kwa wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho nisisitize tena kwenye daraja la Kigamboni. Hadithi zimekuwa ni nyingi! Mbunge aliyekuwepo mwanzo alipigania daraja hili, kaondoka, kaja mwingine, anapigania daraja hili, naye asije akaondoka kabla ya kujengwa kwa daraja hili. Kama kweli kuna mpango huo wa kujenga wameshapatikana *NSSF,* basi shughuli hizo ziendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, katika Kitabu cha Waziri kwenye ukursa wa 152, ameonyesha pesa kwa ajili ya *compensation* au fidia kwa ajili ya *fly over* za *TAZARA* na Ubungo. Sasa kinachonishangaza na kunisikitisha, fedha hizi Shilingi milioni 96, unaweka ndiyo *compensation* kwa ajili ya ujenzi huo wa *fly over!* Mbona hatuelewi? Shilingi milioni 96 unafanya nini? Ama ni hela ambazo mmeweka tu basi mpite mtembelee tu, mzilezile ziishe? Kwa maana ya *compensation,* haisaidii! Shilingi milioni 96 unafanya nini? Umeweka Shilingi milioni 96 *fly over* mbili za Dar es Salaam, wakati huo huo umeweka Shilingi milioni 96, ujenzi sijui wa kitu gani Kyaka! Sasa unaifananisha Kyaka na Dar es Salaam? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, niendelee kusisitiza tena kwamba suala la msongamano Dar es Salaam, sio suala la kufanyia masihara, sio suala la kufanyia mchezo. Tuwe *serious* kuondoa msongamano Dar es Salaam ili wananchi wetu waweze kufaidika kwa maana ya kukuza uchumi wao na pato la Taifa liweze kukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Ni Mbunge wangu huyo, asiponisemea nitamnyima kura. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, mnakumbuka tumesema tunarudi saa 10.00 jioni, siyo saa 11.00 tena? Tunarudi saa 10.00 na tukirudi wanaanza kutoa ufafanuzi wa hoja mbalimbali mlizotoa. Kwa hiyo, napenda kusitisha Kikao cha Bunge, mpaka saa 10.00 jioni.

*(Saa 07.13 mchana, Bunge lilifungwa mpaka Saa 10.00 jioni)*

*(Saa 10.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu nauelekeza kwenye mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba Wizara kwa dhati kabisa ikubali kuipokea barabara ya Mlalo– gwelo-Mlola, Makanya Milingano hadi Mashewa iwe chini ya barabara za Mkoa katika Mkoa wa Tanga. Barabara hii inahudumia Majimbo manne ya Wabunge wa Mlalo, Lushoto, Bumbuli na Korogwe Vijijini. Barabara hii ni muhimu kiuchumi, kijamii na kiutamaduni. Naomba sana jambo hilo lipewe umuhimu sana.

Mheshimiwa Spika, pili, naishukuru Wizara kwa kutenga fedha za barabara ya Mombo–Lushoto Magamba *Section*. Ni kweli fedha zilizotengwa ni kidogo sana lakini tunashukuru. Hata hivyo, ni vema zikatengwa fedha za kutosha ili mradi huo ukamilike kuepuka ongezeko la gharama. Pia naomba barabara hiyo ifike eneo la Mkuzi ambako Rais mstaafu ana makazi yake, ni budi tuwaenzi viongozi wetu wastaafu na wachapakazi.

Mheshimiwa Spika, tatu, tatizo la msongamano wa magari jijini Dar es Salaam ni zito, naipongeza Serikali kwa uamuzi wa kujenga barabara za juu kwa juu *(flyover)* eneo la Ubungo na TAZARA. Nashauri pia eneo la Mwenge lianze kufikiriwa kujengwa daraja la juu. Pia utafutwe uwezekano wa kujenga daraja eneo la makutano ya UWT na Morogoro *road*. Miji mingine ya Mwanza na Arusha ianze kuandaliwa.

Mheshimiwa Spika, nne, naipongeza Wizara kwa hotuba na bajeti safi, nawatakia utekelezaji mwema wa mafanikio.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JENISTA J. MHAGAMA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa miradi mikubwa ya *MCC,* Mkoani Ruvuma ikiwepo mipango inayotekelezeka iliyokwishaanza ya ujenzi wa barabara ya Peramiho Mbinga Mbamba Bay.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Mpakani Mkenda (Tanzania – Msumbiji). Barabara hii imepewa ahadi ya kujengwa kwa lami na Mheshimiwa Rais. Nina maswali mawili; upembuzi utakwisha lini na barabara itaanza kujengwa lini kwa kiwango la lami?

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Mkoa wa Ruvuma kwa ujenzi wa barabara katika Halmashauri bado ni kidogo. Hali ya udongo na mvua inasababisha barabara nyingi kushindwa kudumu, magari yanayobeba mahindi yanasaidia sana kuharibu barabara. Serikali haiwezi kufikiria kuongeza fungu la ruzuku ya barabara katika Halmashauri ya Wilaya, Mkoa wa Ruvuma ili isaidiwe kuokoa barabara za Mkoa huo?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Makambako-Songea katika Ilani ya uchaguzi, barabara hii imepangiwa kujengwa upya katika bajeti ya mwaka huu, sijaona fedha yoyote iliyotengwa. Naomba maelezo ni lini barabara hiyo itaanza kujengwa upya.

**MHE. PUDENCIANA W. KIKWEMBE**: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika Wizara hii katika eneo la Wakandarasi ambao Wizara hii imekuwa ikiwateua na kuchagua ili waweze kufanya kazi za ujenzi na barabara.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na ulalamikiwaji wa Wizara hii kutoka kwa wananchi kwa jinsi wakandarasi hao wanavyoteuliwa kwa maana kwamba kumekuwa na upendeleo katika uchaguzi huo na pia wakandarasi wengi wamekuwa hawana uwezo kwa maana ya elimu ya kutosha ya namna ya kufanya kazi hizo, yaani kumekuwa pia na ujenzi wa majengo chini ya viwango.

(a) Je, Serikali inasemaje kuhusiana na hilo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kukabiliana na hali hiyo?

(c) Je, Wakandarasi wa aina hiyo (wachakachuaji) wanachukuliwa hatua zipi baada ya kugundulika kwamba wamefanya udanganyifu?

(d) Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuhakikisha kwamba inachukua hatua madhubuti katika kuondokana na hali hiyo ili kuepusha majanga yanayoweza kutokea kutokana na hali hiyo? Kwa mfano, majengo yanayojengwa chini ya kiwango?

(e) Serikali inajipangaje kuhakikisha kwamba shughuli hizo (hasa majengo ya Serikali) zinakuwa chini ya taasisi za Serikali kama Magereza, J.K.T ili pia taasisi hizo ziweze kujiendesha na kulipunguzia mzigo Serikali? Badala ya kuwapa wakandarasi ambao wamekuwa wakijinufaisha kwa maslahi yao na si kwa Taifa kwa ujumla?

Mheshimiwa Spika, naunga hoja mkono.

**MHE. DAVID E. SILINDE**: Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kuhusu ahadi ya Rais J.M. Kikwete ya ujenzi wa daraja la Kamsamba kwenda Kilyamatundu. Februari, 2009 Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alitembelea Jimbo la Mbozi Magharibi, ambapo aliahidi kujenga daraja linalokatisha Mto Momba toka Kata ya Kamsamba kwenda Kijiji cha Kilyamatundu ndani ya miezi sita, lakini mpaka sasa ujenzi huo bado

haujaanza, ikiwa watu wanaendelea kufa kutokana na mamba wakali walio wengi katika mto huo. Je, katika mwaka huu wa fedha Serikali itafanyaje?

Mheshimiwa Spika, pili, ni ujenzi wa barabara za kutoka Ntungwa kwenda Chilulumo mpaka Mkulwe na barabara ya kutoka Kakozi mpaka Kapele. Barabara hizi hazipitiki kabisa na wananchi wamekata tamaa na Serikali yao. Hivyo, tunaomba katika mwaka huu wa fedha zitengwe fedha ili barabara hizo zijengwe kwa kiwango cha changarawe ili nao waone wanathaminiwa katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni ujenzi wa vivuko kutoka Kata ya Chitete kwenda Kata za Chilulumo na Mkulwe. Endapo tutajenga Kivuko katika maeneo hayo tutapunguza umbali wa wananchi kuzunguka na kupitia eneo la Jimbo la Mbozi Mashariki kufuata huduma mbalimbali, hivyo basi tunaomba kujengewa kivuko eneo hili ili tusaidie wananchi hususan akinamama wanaofariki wakati wa masika kutokana na kujaa maji mto huo, wakijaribu kuepuka umbali kutafuta huduma. Mheshimiwa Waziri naomba nipatiwe majibu kama linawezekana.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ABDALLAH SHARIA AMEIR:** Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe kwa kuchaguliwa kuwa Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri sana inayofanya kwa ujenzi wa barabara hapa nchini. Kwa Wizara hii kwa jitihada zake naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, mimi ni mkazi wa Zanzibar na Tanzania bara, Mkoa wa Mara, Wilaya ya Bunda katika kuishi kwangu na kutembea sehemu mbalimbali za Tanzania Bara, kwa upande wa Wilaya ya Tarime kuelekea katika mgodi wa dhahabu wa Nyamongo, kuelekea Mugumu, Wilaya ya Serengeti, Barabara hiyo ni muhimu sana kwa uchumi wa nchi na wananchi wake lakini barabara hii iko katika hali mbaya sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuitengeneza barabara hiyo ili kuwaondoshea shida wananchi wanaotumia barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba sana kazi ya ukandarasi hata kampuni za ndani zinaweza kufanya kazi hizo kwa ufanisi zaidi na kutoa ajira kwa Watanzania kwa nia ya kujenga uchumi wa nchi na wananchi kuliko kila kazi za ujenzi kupewa kampuni kutoka China tu na wazalendo kukaa ofisini bila kazi yoyote huku wakilipa leseni na kodi nyingine bila kuwa na kazi. Je, kuna uhalali gani wa kazi za ujenzi kupewa Kampuni za China tu?

Mheshimiwa Spika, naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi kuhusu masuala haya. Ahsante sana.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa mara ya tatu naomba sasa nichangie katika suala zima la nyumba za Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunaona nyumba nyingi za Serikali zinajengwa kwa lengo la kuwasaidia wananchi wa Tanzania wapate makazi bora. Lakini utaratibu wa upatikanaji wa nyumba za kawaida si wazi sana na pia wananchi hawajui wanapewa akina nani na kwa vigezo gani? Hali inavyoonekana nyumba zile wanaopewa si Madaktari, Walimu wala Manesi, wanaopewa ni sekta nyingine nyingine za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa mtazamo wangu naona utaratibu wa ugawaji wa nyumba za Serikali hauko wazi (si wa uwazi na ukweli). Naomba niishauri Serikali yangu, sasa ifanye utaratibu wa kugawa nyumba kwa kuweka mizani sawa kama ni Wizara basi Wizara zote wafanyakazi wake wapewe nyumba kama itakavyopangiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa kwa wananchi wa kawaida katika zoezi la ugawaji wa nyumba jinsia izingatiwe. Naomba wanawake wapewe umuhimu wa kipekee kwa kuwa wao ndio walezi wa familia.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nitoe masikitiko yangu juu ya Wizara inavyoshindwa kuwajibika katika kudhibiti wapangaji wake. Wapangaji wa nyumba za Serikali wamekuwa wanamiliki nyumba kama zao na wanaweza kufanya wanavyotaka hakuna wa kujibu. Mfano, nyumba za Kisasa Dodoma, nyumba hizi kuna ambazo hazina watu zimeota manyasi mpaka kumekuwa msitu. Pia nyumba nyingine zimetolewa vioo na nyingine zimevunjwa milango. Naomba Serikali iangalie nyumba hizi ni urithi wa Watanzania walio wengi. Naomba niulize Serikali yangu sasa, je hizi nyumba zinatuletea faida na ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, naomba nishauri juu ya viwango vya ujenzi. Nyumba zinazojengwa ziwe madhubuti (imara), nyumba nyingi zinajengwa kwa haraka na kukosa uimara. Naomba nitoe mfano, nyumba za Waheshimiwa Mawaziri, Ma-*DC* na Ma-*RC*. Mimi binafsi sijazipenda kabisa na inawezekana zikawa imara lakini kwa kufananisha na zile nyumba za zamani za viongozi zilizopo Oysterbay naona zile zilikuwa bora zaidi kuliko hizi za sasa.

Mheshimiwa Spika, nikiwa kama mkazi wa Jimbo la Kigamboni naomba nipewe maelezo ya uhakika badala ya kusikia sikia tu. Je, Kigamboni kuna nyumba za Serikali au majengo yasiyokwisha ya Serikali? Naomba nijue kama ni kweli na kama zipo Halmasharuri ya Wilaya ya Temeke inaelewa hivyo? Je, wana Temeke wangapi wanaishi katika nyumba hizo? Naomba majibu yangu niyapate pamoja na idadi yote ya majengo yaliyopo Mkoa wa Dar es Salaam na yawe yamechaguliwa Kimanispaa.

Mheshimiwa Spika, sasa niingie katika suala la ujenzi holela. Ujenzi usio na mpangilio ndio chanzo cha matatizo. Naishauri Serikali yangu tufanye kazi kwa ushirikiano. Kwa muono wangu naona Wizara ya Ardhi inasababisha hasara kubwa kwa Wizara ya ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu Wizara ya Ardhi inapimia watu viwanja barabarani na kuwapa Hati miliki. Wakati wa ujenzi wa barabara wanavunjiwa na wana hati miliki. Mfano, Mzee Sinde Mbagala, Mbalinga *Investment, Kobil* Mbagala, Shule za Sekondari St. Anthony na St. Mary's Mbagala (JKT japo nasikia hawa walilipwa (sina uhakika). Je, Serikali haioni hili ni tatizo? Kwa kweli ushirikiano ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ya Ujenzi, TAMISEMI, Sheria na Katiba, Ardhi na Mazingira zikae pamoja kusaidiana kwa kutatua matatizo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja lakini ushauri wangu uzingatiwe na nitaunga mkono zaidi nikipata ufafanuzi mzuri wa hoja zangu. Ahsante sana.

**MHE. DKT. HAJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Spika, napenda kwanza nimpongeze Waziri wa Ujenzi na timu yake yote ya *Management* na Watumishi wa Wizara kwa hotuba nzuri na utekelezaji wa bajeti iliyopita 2010/2011. Napenda nichangie hotuba katika sehemu za huduma za vivuko na barabara.

Mheshimiwa Spika, katika sehemu 145 ya hotuba imeeleza ukarabati wa vivuko na kuvitaja vivuko hivyo. Ningependa kumkumbusha Waziri kwamba kivuko cha MV Kilombero ni muda sasa kimeonesha kupungua uwezo wa kiutendaji. Hivyo basi, nashauri nacho pia kuwemo katika orodha ya vivuko ambavyo vinahitaji matengenezo. Kivuko hiki cha *MV* Kilombero kama hakitofanyiwa matengenezo makubwa msimu huu kitakwenda kuishia kushindwa kutoa huduma.

Mheshimiwa Spika, Wizara katika mpango wa matengenezo ya barabara kwa mwaka 2011/2012. Katika barabara za Mkoa wa Morogoro, barabara ya Malinyi – Lupiro haikutengewa fungu la matengenezo au ukarabati. Naomba Wizara ya Ujenzi irejee bajeti yake na kuiona barabara hiyo ya Lupiro – Malinyi, ambayo kutokana na mvua za msimu uliopita zimeharibu kiasi kikubwa na baadhi ya sehemu zinapitika kwa shida.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. JAMES D. LEMBELI:** Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima kabisa kuanza mchango wangu kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. Naunga mkono kwa sababu kazi iliyofanyika katika kipindi cha 2010/2011 inaonekana ni ya kuwapa matumaini Watanzania. Mtandao wa barabara za lami na zile za mkoa umeongezeka kwa kiwango kikubwa vilevile *Pave* na *Unpaved regional roads*.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi, naishukuru Serikali kwa kusikia kilio kikubwa cha wananchi wa Jimbo la Kahama ambapo katika kipindi cha miaka minne Serikali imepandisha hadhi barabara mbili kutoka za Wilaya kuwa za Mkoa. Barabara hizo ni Kahama – Chambo na Nyandekwa – Uyogo hadi Nsunga. Kupanda hadhi kwa barabara hizi kunafanya jimbo la Kahama kuwa na barabara tatu za Mkoa.

Hata hivyo, napenda kujua ni kwa sababu gani barabara ya Nyandekwa–Uyogo-Nsunga imetengewa fedha za kutengeneza kilomita 12 tu wakati barabara hii ni mpya na ina urefu wa kilomita zaidi ya 90. Naomba kujua ni eneo gani la barabara hii ndio litatengenezwa kwa mujibu wa bajeti hii?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA**: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri inayoifanya ya kujenga barabara mbalimbali kwa kupitia Wakala wake *TANROADS*. Barabara ndiyo mishipa ya damu ya uchumi wetu. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara *TANROADS* na Mfuko wa Barabara. Najua mahitaji ni mengi wakati fedha ni kidogo sana. Katika hali hii bila shaka mnaongozwa na *priority areas* bila kusahau *Regional and District balancing* ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ambalo napenda nichangie, ni umuhimu wa Wizara kuwa macho na makini wakati wa kutoa *contracts* za ujenzi wa barabara kwa waombaji. *Contractors* wengine wanaweza kuwa matapeli au siyo waaminifu. Kwa hiyo, baada ya kutoa *contract* kunahitajika usimamizi makini sana na kupiga vita rushwa ya aina yoyote katika ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, ambalo ni muhimu sana kwangu pamoja na wananchi wa Ngara ni utekelezaji wa ahadi ya Rais ya kujenga barabara kwa kiwango cha lami ya kutoka Mnzani (Nyakahura) kupitia Buseke, Keza, Rulenge hadi Murugarama, Wilayani Ngara. Ahadi hiyo ilitolewa na Mheshimiwa Rais Dokta Jakaya Mrisho Kikwete mwaka jana (2010) wakati wa Kampeni za uchaguzi Mjini Ngara na katika mji mdogo wa Rulenge.

Mheshimiwa Spika, nimekuwa nikiwasiliana na Mheshimiwa Waziri kuhusu jambo hili na jibu lake siku zote ni usiwe na wasiwasi kaka yangu.

Mheshimiwa Spika, katika Bunge hili la bajeti niliuliza swali la nyongeza kuhusu utekelezaji wa ahadi hii ya Rais ya kutupatia barabara ya Lami kutoka Mnzani-Rulenge hadi Munigarama, jibu la Mheshimiwa Naibu Waziri Dk. Harrison Mwakyembe lilikuwa fupi *but to the point,* naomba nimnukuu: “Mheshimiwa Mbunge wa Ngara usiwe na wasiwasi, subiri utafurahi mwenyewe wakati wa kusoma bajeti ya Wizara ya Ujenzi.” Mwisho wa kunukuu. Nilichofanya ni kumuandikia ki- *note* kuhusu kauli hiyo na akanijibu kwa kurudia maneno yake ya hapo juu.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Ngara walifurahishwa sana na kauli hiyo ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Walinipigia simu na kuniandikia *messages* za kunipongeza. Jambo la kusikitisha ni kwamba barabara hiyo haimo katika bajeti ya Wizara 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa barabara hii kujengwa kwa kiwango cha lami ni kwamba licha ya kuleta maendeleo makubwa kwa wananchi wa Ngara, lakini nchi ya Burundi kwa miaka mingi imetamani sana barabara hii ingekuwa ya lami ili waweze kupitisha mizigo yao kwa urahisi kuliko ilivyo sasa ambapo malori yao ya mizigo yanakwama kwenye milima mirefu iliyoko kwenye barabara ya sasa.

Mheshimiwa Spika, pia Kabanga *Nickel* ni mradi mkubwa sana duniani na uko Ngara. Katika utajiri wa *Nickel*, Kabanga *Nickel* ni ya pili duniani ikitanguliwa na Canada tu. Barabara hii ya Mnzani Keza, Rulenge hadi Murugarama ikiwekewa lami itasaidia sana katika usafirishaji wa mizigo ya Kabanga *Nickel* kwenda bandari ya nchi kavu ya Isaka.

Mheshimiwa Spika, naiomba sana Serikali ione umuhimu wa barabara kama mshipa muhimu wa damu wa uchumi wetu kwa kuzingatia umuhimu wa biashara kati yetu na nchi ya Burundi na pia umuhimu wa mgodi wetu wa Kabanga *Nickel* bila kusahau maendeleo ya Wilaya ya Ngara na Wilaya ya Biharamulo.

Mheshimiwa Spika, nawatakia kazi njema ya kuujenga uchumi wetu kwa kuimarisha miundombinu ya barabara. *God bless you*.

**MHE. RITTA E. KABATI**: Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kwanza kumpongeza Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Dokta Pombe Magufuli; Naibu Waziri Dokta Harrison Mwakyembe; Katibu Mkuu, Balozi H. Mrango; Naibu Katibu Mkuu Dokta John Ndunguru pamoja na Watendaji wote wa Wizara kwa hotuba yake nzuri na jinsi alivyoiwasilisha kwa umahiri mkubwa katika Bunge letu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu hali ya barabara hapa nchini. Niipongeze sana Serikali kwa kazi nzuri inayofanywa kwa ujenzi wa barabara na madaraja katika maeneo mbalimbali ambao unaendelea hapa nchini. Kwa mfano, angalau unaweza kusafiri kutoka Tunduma–Mwanza au Dar es Salaam mpaka Mwanza na kwingineko bila matatizo makubwa tofauti na kipindi cha nyuma. Naomba nitoe ushauri wangu kuhusiana na barabara hizi zinazosimamiwa na Halmashauri za Miji na Majiji.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi nyingi zinajengwa bila kiwango na zilizojengwa pia usimamizi wake matengenezo hayafanyiki kwa wakati, nafikiri hauendani kutokana na ufinyu wa bajeti na wataalam.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Serikali zile barabara muhimu zingeamishiwa *TANROAD* na hasa zile barabara ambazo zinategemewa na uchumi wa nchi hii.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wetu wa Iringa ni kati ya mikoa inayotegemewa kwa kilimo cha mazao ya chakula na Biashara. Ningeomba Serikali itoe kipaumbele kwa barabara za Wilaya ya Mufindi, barabara zinazozunguka msitu na Kiwanda cha Mgololo na barabara zinazokwenda katika Kiwanda cha Chai na ikiwezekana zijengwe kwa kiwango cha lami. Pia barabara za Jimbo la Kilolo. Jimbo hili ni kati ya Majimbo ambayo yana uzalishaji mkubwa sana wa kilimo cha nyanya, vitunguu, matunda, mahindi, shayiri na kadhalika lakini barabara zake wakati wa mvua hazipitiki kabisa na kusababisha magari makubwa kukwama muda mrefu katika barabara hizo. Kwa kuwa uwezo wa Halmashauri wa kujenga barabara hizo kwa kiwango cha lami ni mdogo, basi zihamishiwe *TANROAD* ili kukuza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia kuhusu barabara ni Wakandarasi kutolipwa kwa wakati na huenda kunasababisha hata baadhi ya miradi hiyo ya ujenzi kutokamilika kwa wakati na kutokuwa na kiwango cha kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu bomoa bomoa inayoendelea hapa nchini. Hili ni tatizo ambalo linahitaji elimu na umakini mkubwa sana kwa sababu kutoelewa sheria za barabara kunafanya wananchi kuonekana kama wanaonewa na kusababisha kuichukia Serikali yao. Pia kwa wale waliotakiwa kulipwa fidia. Pia fidia zinapochukua muda mrefu inakuwa ni kero kubwa sana kwa wananchi wetu. Ningeishauri Serikali kuweka alama maalum ambayo itakuwa kielelezo cha kutoguswa kwa maeneo hayo na kama mtu atavamia bila kujua basi ubomoaji ufanyike mara moja. Pia fidia zilipwe mara moja ili kama mtu amebomolewa nyumba yake au chumba cha biashara, ile fidia atakayolipwa iweze kumsaidia.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na malalamiko makubwa sana ya wananchi kutolipwa fidia za mali zao kwa muda mrefu tunaomba jambo hili lipatiwe kipaumbele sambamba na ulipaji malimbikizo ya madeni kwa Wakandarasi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni vyombo vya habari viliripoti kuhusu ubomoaji wa Jengo la *TANESCO* kuwa lipo katika *road reserve* na linastahili kubomolewa. Je, kwa nini Wizara haikuchukua tahadhari mapema wakati wa ujenzi wa jengo hilo? Kwa kuwa jengo hilo ni la thamani kubwa na ukichukulia maanani *TANESCO* kwa sasa ina mzigo mkubwa wa deni la *Dowans* kwa nini ubomoaji huo usihamishiwe upande wa pili ambako kuna Wizara ya Maji yenye majengo siyo na thamani kama hayo? Ili kuepusha hasara katika ubomoaji wa jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii pia kuishukuru Serikali kwa ujenzi wa barabara ya Dodoma–Iringa kwa kiwango cha Lami lakini ujenzi wa mradi huo wa hiyo barabara umezingatia haki ya wananchi wanaopisha ujenzi wa barabara hiyo kulipwa fidia ya mali zao.

Mheshimiwa Spika, pia nilitaka nipatiwe majibu kuhusu mpango wa ujenzi wa barabara ya lami kuelekea katika hifadhi iliyopo Ruaha. Hifadhi ambayo ni ya pili kwa ukubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu ujenzi wa maeneo ya mapumziko na vyoo. Ningependa kujua kama Serikali ina mpango au mkakati wowote wa kujenga maeneo ya mapumziko katika barabara zetu, kwa kuwa kuna uharibifu mkubwa wa mazingira na udhalilishaji mkubwa kwa abiria wanapotaka kujisaidia (au wanaita kuchimba dawa) naomba hili lipewe kipaumbele ni pamoja na kutoa hadhi kwa barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kupata ufafanuzi. Kumekuwepo na taarifa za kutatanisha kuhusiana na ubomoaji wa mabango ya Halmashauri. Je, ni nani kati ya Halmashauri na Wizara anayehusika. Kwa kuyaondoa mabango hayo hamwoni kuwa mtakuwa mmewapotezea Halmashauri chanzo chao cha mapato? Kwa sababu Halmashauri nyingi nchini hazina mapato ya kutosha kukidhi haja zao na mabango ni chanzo kikubwa sana kinachosaidia hata matengenezo ya barabara zao.

Mheshimiwa Spika, baada ya mchango huo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii ili nitoe mchango wangu katika Wizara hii ya Ujenzi. Naanza na msongamano katika Jiji muhimu sana la Dar es Salaam. Msongamano wa Jiji la Dar es Salaam ni mkubwa sana kiasi ambacho unatia hasara Taifa kila siku mamilioni ya shilingi.

Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari unachangia wafanyakazi wa Serikali kuchelewa maofisini pamoja na wafanyakazi wa sekta ya binafsi. Kama haitoshi wafanyabiashara vilevile wanapata usumbufu. Ufanisi haupatikani katika miundombinu kama hii. Ni lazima miundombinu mbadala ipatikane haraka sana, itakayowezesha kuondoa msongamano wa magari. Kwanza ni lazima tuondoe Wizara zote muhimu zilizopo katika jiji la Dar es Salaam na kuhamishiwa Dodoma ambapo Serikali ina mpango wa kufanya Makao Makuu ya Serikali na kwa kuwa Tanzania si maskini wa ardhi, tuanzishe mji mwingine ambao ujengwe kitaalam utakaokuwa na miundombinu yote. Barabara pana sana mbili mbili kutoka kila upande na barabara za juu. Tukifanya hivi msongamano utakwisha.

Mheshimiwa Spika, bomoa bomoa ya nyumba ovyo ovyo ambazo zinadaiwa zipo katika (*ROAD RESERVE*) naomba nipate maelezo ya kina kuhusu tatizo hili, kwa sababu mamlaka husika zipo inakuwaje inajengwa nyumba mpaka inamalizwa watu wanakaa tena kwa miaka mingi sana, halafu Serikali inabomoa. Sasa najiuliza mtu huyu kibali cha ujenzi kapata wapi? Wakati anaanza ujenzi je, hakuonekana? Baya kabisa Serikali inabomoa na halipwi, hii sio haki na ni uonevu.

Mheshimiwa Spika, sasa nazungumzia matuta pamoja na rasta. Pamoja na nia nzuri ya Serikali ya kupunguza ajali barabarani kwa mwendo wa kasi. Lakini utaratibu si mzuri wa kujenga matuta na rasta. Mfano mzuri, tuangalie barabara ya Dar es Salaam Dodoma. Kama utafanya

tathmini ya kina utagundua ina matuta karibu sitini (60) pia ina rasta karibu mia na hamsini (150) katika sehemu tofauti. Sio mbaya lakini izingatie sehemu muhimu za jamii kama masoko, shule na vijiji. Pia matuta yajengwe katika mfumo salama kwa magari na watu yasiwe makubwa sana. Rasta ni hatari kwa usalama wa magari, rasta zinaharibu gari. Mfano, utakuta matuta yamejengwa maporini ambamo hamna vijiji vyovyote ni kero na usumbufu. Naomba Serikali iangalie upya mfumo wa matuta na rasta barabarani upangwe vizuri pasipo kusababisha usumbufu ambao si lazima. Ahsante.

**MHE. GREGORY G. TEU:** Mheshimiwa Spika, ahadi za Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete wakati wa kampeni za Urais 2010 pamoja na ahadi zilizoko kwenye Ilani ya Uchaguzi Ibara ya 4(64)(e) ni kuweka lami barabara ya Mbande–Kongwa (*Junction*) hadi Mpwapwa (kilomita 50). Ili kutekeleza ahadi hii, kwa kuanzia ni lazima upembuzi yakinifu na usanifu ufanyike. Je, kazi hii ya upembuzi yakinifu na usanifu wa barabara hiyo itaanza lini? Ni kiasi gani cha fedha kimetengwa kwa kazi hiyo? Ningependa nihakikishiwe utekelezaji wa ahadi ya ujenzi wa barabara hii kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na kuahidiwa na Mheshimiwa Rais.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kupata fursa hii ya kuweza kuchangia hoja iliyopo mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Waziri mwenye dhamana, Mheshimiwa John Pombe Magufuli kwa jiitihada kubwa ambazo amezionesha katika kuendesha Wizara hiyo. Nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Biharamulo Magharibi kuna ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita 154 Kigoma hadi Lusahunga kwa kiwango cha lami. Ujenzi huu unaendelea vizuri na kwa kiwango kinachoridhisha sasa. Sidhani katika shughuli hii pamoja na yote niliyoyaeleza hapo juu kumekuwepo na kasoro mbalimbali katika utekelezaji wa mradi. Aidha, kasoro hizi hazipaswi kujitokeza au kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, katika mambo ambayo Watanzania wengi wanahitaji kutendewa katika kazi hizi ambazo ni za mikataba na mashirika au nchi za nje ni:-

(a) Kutokuwepo kwa mikataba kati ya Wakandarasi hawa na wafanyakazi wa kawaida. Hii imepelekea kutokuwa na uhakika wa ajira kwa maana ya kuanza kazi asubuhi na kufukuzwa jioni na hii kupelekea kutokuwa na uhakika wa ajira na ujira mdogo au usiofaa.

(b) Bima ya matibabu. Hii imetokea wafanyakazi hawa wakiumia kazini hawapewi huduma stahili ya matibabu na wanapopata ulemavu basi hakuna fidia ya ulemavu au hasara wanayoipata kazini!

(c) Ulipaji wa fidia stahili kwa wananchi. Ni dhahiri mikataba hii inagharimu pesa nyingi mno. Hivyo, wananchi wapewe fidia stahili kulingana na sheria na mikataba ya Kimataifa.

(d) Uharibifu wa mazingira. Aidha, kumekuwepo na suala zima la uharibifu wa mazingira na hususan mazingira yale ambapo kifusi kinachotwa mashimo haya hayasawazishwi na hivyo kutengeneza madimbwi makubwa na kama yapo jirani na makazi ya wananchi inakuwa hatari kwa watu na mifugo katika sehemu hiyo na pia inakuwa sehemu ya mazalia ya mbu na hivyo kufanya suala la malaria kuwa tatizo kubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa kutenga fedha toka vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya kujenga barabara hizi. Aidha, napongeza hatua za kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Biharamulo (Kalelezo) hadi Uyovu kilomita 112. Barabara hii itasaidia sana kurahisisha mawasiliano na kufungua soko la mazao kwa wakulima. Naomba ujenzi huu uanze haraka sana na ufanyike kulingana na mkataba ulivyopangwa. Aidha, kwa kilomita 12 ambazo hufanywa ndani ya Makao Makuu ya Wilaya husika ambapo barabara hiyo hupita, basi naomba shughuli hiyo ifanyike kwa usahihi na kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hizi. Aidha, madaraja na mitaro ya maji itengenezwe vizuri na hivyo kufanya barabara hizi zidumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuishauri Serikali kuhusu suala la mizani. Mizani yetu imekuwa haifanyi kazi vizuri, gari linalobainika kujaza uzito mkubwa linaishia kutozwa faini tu na kuruhusiwa kuendelea na safari. Huku ni kuvunja sheria kwani taratibu ni kwamba gari hili likibainika basi, pamoja na kutozwa faini gari hili lishushe au lipunguze mzigo na ndiyo liruhusiwe kuendelea na safari. Haikubaliki kuona gari hili mzani mmoja linakuwa na vipimo tofauti kiasi ambacho kinatoa nafasi ya rushwa na uharibifu mkubwa wa barabara. Suala hili lipewe umuhimu mkubwa mno.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, nami pia napenda kuchangia maoni yangu kuhusu bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi. Nichukue fursa hii kuipongeza Wizara na Serikali kwa ujumla kwa jitihada kubwa inazozifanya ili kuhakikisha miundombinu ya barabara na madaraja inaimarishwa na kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kuelezea maoni yangu kuhusiana na ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Mfumo unaopendekezwa na *PPP* ni muafaka na mzuri, kwani utaifidia Serikali kupata fedha kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili na pia *NSSF* itazidi kukuza mtaji wake. Tunaelewa kwamba ipo mipango ya kujenga Kigamboni kuwa *Satelllite Town* bila Daraja hili kwa kweli itakuwa ni ndoto. Wawekezaji watashindwa kuja. Hivyo basi ni rai yangu kwamba ujenzi huu uanze na kukamilika haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, napongeza Serikali kuhusiana na miradi ya kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam kwa mipango mizuri, ili ujenzi wa barabara za juu kwenye makutano ya barabara maeneo ya TAZARA na Ubungo. Ni uamuzi mzuri isipokuwa fedha zilizotengwa kiasi cha Shilingi Bilioni 5.02 ni ndogo sana. Kiasi hiki kinaweza kujenga takriban kilomita 5–6 tu za lami, huku ukizingatia Dar es Salaam wanachangia zaidi ya 80% ya pato la Taifa hili. Vilevile zipo taarifa za takwimu kwamba kuwepo kwa msongamano kunasababisha hasara ya Sh. 4,000,000,000/= kwa siku, hivyo ni vyema juhudi za makusudi zifanyike ili kupata fedha popote pawezekanapo kwa ajili ya kuboresha zaidi barabara.

Mheshimiwa Spika, kwenye bajeti hii pia pesa kiasi cha sh. 96,000,000/= zimetengwa kwa ajili ya kulipa fidia wakazi wa Ubungo watakaopitiwa na mradi wa *DART* ni fedha ndogo sana. Nina mashaka na azma hii haitekelezeki. Nyumba ya gharama ya chini ni takriban Shilingi Milioni 10-25, sasa milioni 96 ni fidia kwa nyumba ngapi? Ni vyema kiwango hiki kiangaliwe ili usumbufu na uonevu usijitokeze.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuelezea haya, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri wa Ujenzi, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na wafanyakazi wote.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Waziri Mkuu nilichangia eneo la Wizara ya Ujenzi. Nilichangia maeneo yafuatayo:

(a) Msongamano Dar es Salaam;
(b) Fidia barabara ya Kilwa Road;
(c) Mabango Dar es Salaam; na
(d) Mahusiano mema.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na Msongamano Dar es Salaam. Katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri ukurasa wa sitini imeonesha zimetengwa Bilioni tano na ishirini elfu (5,020.55) Mheshimiwa Waziri Bilioni tano ni sawasawa na Kilomita tano kwa kilomita moja Shilingi bilioni moja.

Mheshimiwa Spika, Dar es Salaam ndio nchi, uchumi wa Tanzania unategemea, ni namna gani ukisoma taarifa ya Kamati ya Miundombinu inaelezea ni namna gani msongamano wa Dar es Salaam unavyoathiri uchumi na kufanya pato la Taifa kushuka kwa hiyo, pesa hizi zilizotengwa kwa ajili ya msongamano hazitoshi naomba kama mna dhamira ya dhati ya Dar es Salaam mtafute pesa za kutosha.

Mheshimiwa Spika, Kasma Na. 2326 inahusu *Road Flyovers Compensation for TAZARA and* Ubungo Shs.96,444,475.00/=. Katika bajeti iliyopita ilionyesha hii *Flyover* ya *TAZARA*-Ubungo ingekuwa imeshaanza, sasa sijui kiasi hiki cha pesa a alichoonyesha Mheshimiwa Waziri au walichotenga wanakusudia kulipa akina nani kwa sababu ni kidogo mno kutokana na kazi hii haionyeshi kama kazi hii wanaipa umuhimu.

Mheshimiwa Spika, pili ni kuhusu fidia, barabara ya Kilwa *Road*. Mheshimiwa Waziri katika bajeti zilizopita Serikali ilikubali kulipa watu wote walioathirika katika barabara ya Kilwa *Road* na watu walishaanza kulipwa, lakini katika uongozi wako nimesikia ukitoa kauli tofauti na viongozi waliopita katika Wizara hiyo kwamba huwalipi watu wa Kilwa *Road* wale waliobakia. Kwa hiyo, tunaomba utakapofanya majumuisho utupe msimamo wako kuhusu malipo ya watu wa Kilwa *Road*.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kuhusu suala la mabango ambalo amekuwa akitamka Mheshimiwa Waziri kwenye vyombo vya habari, viongozi wa Dar es Salaam wakiwemo Wabunge wa Dar es Salaam ambao mimi ndio Mwenyekiti wao na Mameya tunamshauri ni vema tukae na yeye tukashauriana, tukizingatia mabango ni sehemu kubwa inayotupatia mapato katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, nne ni mahusiano mema. Mheshimiwa Waziri, ni vyema katika utendaji wake wa kazi akawa na mahusiano mema na wenzake nikiwa na maana ya Wabunge ni wenzake, ni vema akiwa na jambo lolote akawasiliana na Wabunge wa Mikoa inayohusika na jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, namtakia Mheshimiwa Waziri maisha marefu, kazi njema na Mungu akujaalie kwa kila unaloliomba.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU**: Mheshimiwa Spika, msongamano wa magari Dar es Salaam ni kero kubwa sana na husababisha hata upotevu wa mapato. Serikali ina mpango gani wa kuondoa kero hii? Magari mengine wala hayana umuhimu ni aina ya watu wanaozurura tu kwa nini tusiige nchi zingine kwa kutoza *congestion fee*. Tunasherehekea Uhuru miaka 50 lakini barabara ya Uhuru Dar es Salaam mpaka leo Serikali haina mpango nayo wakati ni barabara ya *TANROAD*.

**MHE. BERNADETA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nipende kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa hotuba nzuri iliyoandaliwa kwa ufasaha na kuwasilishwa kwa viwango vya hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, pili, naipongeza Wizara hii kwa ubunifu, utendaji na mipango mizuri, iliyowezesha kuwa na mtandao mkubwa wa barabara zilizotengenezwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kujitahidi kuhamasisha wanawake kujiunga na kundi la wengine ili waweze kushiriki katika matengenezo ya barabara pamoja na jitihada hizo, bado walengwa wengi hawajafikiwa.

Kwa kuwa Mkoani Kagera viko vikundi vya wanawake ambao wanapenda kushiriki ukandarasi wa barabara. Je, Waziri ataahidi na ni lini atatuma wataalam wake waje kutoa mafunzo ya ukandarasi Mkoani Kagera na kunihakikishia kuwa nitapata taarifa, ili tusaidiane kuvitambua vikundi hivyo na baadaye kuweza kuvifuatilia ili vifanikiwe?

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara inayofanya kazi nzuri na kazi zinazoonekana. Imenisikitisha kuona bajeti ya maendeleo ni 1,250,976,939,000/=, ili kutekeleza miradi ya maendeleo, lakini zaidi ya nusu ya fedha hizo yaani 629,870,193,000/=, zinategemea ufadhili kutoka nje. Hii ina maana kuwa kama wafadhili wakishindwa kutoa fedha au wakichelewa kuzitoa, mipango mizuri hii itashindikana.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kwa Serikali, Wizara hii ipewe fedha za ndani, ili mipango yake itekelezwe kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ABIA M. NYAKABARI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi ngumu inayofanywa na Wizara hii ya Ujenzi, napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja na kwa kuwa jana nilijisahau kuunga hoja baada ya mchango wangu imenibidi nikiri kwa maandishi kuwa naunga hoja mkono, lakini niliiomba Serikali kuzingatia hizo barabara nilizosema Kalamba-Nzite – Ilemba, Mtowisa, Mfinga, Mamba, Usevya hadi Sitalike na Barabara ya Legeza Mwendo, Mambo Kenya, Ulumi, Mwimbi, Katazi, Mwazye, Ilula na Kaengesa pamoja na barabara ya Nkundi, Kate kwenda Wapembe kwenye Samaki Ziwani, la sivyo Chama cha Mapinduzi kitakuwa katika hali ngumu ya uchaguzi ya mwaka 2015 na hasa upande wa Wampembe.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, miundombinu ya barabara ni nyenzo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi au jamii yoyote ile. Inashangaza kuona Wizara hii imegawanyika katika Wizara mbili yaani Ujenzi na Uchukuzi. Nilitegemea miundombinu ya reli, ndege, bandari zingekuwa ndani ya Wizara moja ili ufuatiliaji uwe mzuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, msongamano wa barabara Dar es Salaam ni jambo la kusikitisha kwamba Dar es Salaam Jiji linaloingiza 70% ya pato la Taifa lakini msongamano huu unapunguza sana pato hili. Kama sehemu ya kilomita tano mtu anatumia saa moja na nusu au mbili kwa gari. Wananchi wengi sasa imebidi kubadili tabia mfano, kuamka alfajiri sana ili kuwahi foleni mfano, kuwa barabarani saa 11 alfajiri na kukaa katika *bars* hadi saa tatu hadi nne usiku ili kukwepa foleni. Matokeo yake ndoa zimekuwa na matatizo na kufanya watoto wasionane na wazazi wao hususan baba kwani wanaondoka wamelala na wanarudi usiku watoto wamelala.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa kuhusu *flyovers* lakini imechukua muda mrefu sana. Ushauri ni kuwa kwanza *feeder roads* zirekebishwe na ziboreshwe ili kupunguza msongamano mfano barabara za Kinondoni na za Ilala. Pamoja na mipango mizuri ya Serikali lakini imekuwa ni kama ndoto za mchana. Ahadi zimekuwa nyingi lakini hakuna utekelezaji. Serikali ilianza mpango wa barabara tatu ambao ilishindikana.

Mheshimiwa Spika, suala la matuta lina kero kubwa sana. Sijaona nchi yoyote yenye utaratibu wa kuweka matuta eti kwa kuwa mtu kagongwa. Matuta si suluhisho la ajali bali ni kuongeza ajali na kuharibu magari. Ni lazima barabara ziwe na alama ili madereva wazione na wapita njia waone. Inasikitisha kuona alama hazipo, hivyo madereva kushtukia matuta tena makubwa na kusababisha ajali.

Mheshimiwa Spika, pamekuwa na tabia za magari kutokuwa na *reflectors* ili hata inapotokea ajali au gari kuharibika alama ziwepo ili kuwatahadharisha wengine. Matokeo yake kumekuwa na ukatwaji wa miti na kuweka barabarani tena mikubwa na hata wakiondoka huacha matawi makubwa barabarani hivyo kuchafua barabara na hata kusababisha ajali.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri iliyojaa takwimu na inaeleweka, kwa maana hiyo naunga mkono.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo juu, naomba Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi kwa barabara zifuatazo kama zitabebwa na Serikali (TANROAD) au kuwekewa lami:

(a) Sengerema hadi Geita kupitia Buchosa, Nyamazugo, Nyehunge, Nzela hadi Geita;

(b) Mwanangwa hadi Salawi (Shinyanga) kupitia Misasi;

(c) Busisi hadi Kakora kupitia Ngoma, Nyang'hwale, Kharumwa, Nyang'holongo hadi Kakora;

(d) Geita hadi Kahama kupitia Bukoli; na

(e) Kisamba (Magu) hadi Kijilishi kupitia Badugu,

Nyahuhande, Nyangili, Mkula hadi Kijilishi

Mheshimiwa Spika, barabara zote hizo tano naomba Waziri atoe ufafanuzi katika barabara hizi ni zipi za Changarawe na zipi ziko tayari kutengenezwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, kuhusu daraja la juu (*flyover*) Mabatini, Mwanza. Mji wa Mwanza umekuwa na watu wengi sana na unakua kwa haraka. Serikali haioni kuwa ni wakati muafaka sasa kujenga daraja hilo la juu ili kupunguza msongamano wa watu na magari yanayosababisha wananchi kuchelewa shughuli zao mbalimbali na hasa kuwahi kazini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya Sabasaba hadi Kayenze. Katika upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza, barabara itokayo hapo hapo Uwanja wa Ndege kuelekea Igombe hadi Kayenze itafungwa na haitatumika tena. Halmashauri ya Jiji la Mwanza ilishaandaa barabara itakayotoka *Airport* kupitia Kiseke, Kahama, Igombe, hadi Kayenze na baadaye kuungana na barabara kuu itokayo Mwanza hadi Musoma kupitia Kisesa (town).

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ile barabara ya awali itokayo Uwanja wa Ndege hadi Kayenze tayari ilikuwa ya *TANROAD* je, *TANROAD* wako tayari kuichukua kama barabara yao sasa badala ya ile ya kwanza? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAJI JUMA SEREWEJI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kabla sijakwenda kwenye hoja yenyewe, kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mwanakwerekwe naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana hotuba hii kwa hatua iliyochukua hasa kwa ujenzi wa barabara. Ingawa bado Mikoa na Wilaya kadhaa zina matatizo na barabara lakini tulipofika panafaa kupongezwa. Ila sasa Serikali izidi kujitahidi na kuendeleza barabara zilizobaki.

Mheshimiwa Spika, namuomba Waziri wa Wizara ya Ujenzi ijitahidi sana kuwalipa fidia kwa wananchi ambao wanawabomolea nyumba zao ili kuondosha usumbufu.

Mheshimiwa Spika, alama za barabarani zinazoonyesha mbele kuna matuta, *zebra cross* na mpindo mkali. Alama hizi lazima ziboreshwe kila wakati ili zioneshe vizuri na pale ambapo hazipo aidha, kwa paipu kutolewa au mabango kuanguka parekebishwe haraka sana kwa sababu alama zile ndizo zinaepusha ajali. Alama ya matuta barabarani mengine huwa hayaonekani kutokana na kufutika kwa rangi nyeupe ambayo inajulisha kuwa pana tuta. Matuta hayo yapitiwe mara kwa mara na kuwekwa rangi ili yaonekane vizuri pamoja na *zebra cross* nazo vile vile hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nazidi kuunga mkono hoja hii. Ahsante.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa sina budi kumpongeza Waziri, Mheshimiwa John Pombe Magufuli; Naibu Waziri, Mheshimiwa Harrison Mwakyembe, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri sana ambayo wameisoma hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, naanza mchango wangu kuchangia kuhusu tatizo la mizani za barabarani. Kuna usumbufu mkubwa sana katika hili zoezi la upimaji mizani barabarani mpaka kusababisha kuwepo na msongamano wa magari makubwa kupaki barabarani. Nashauri sehemu za mizani zijengwe nje ya barabara kubwa.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ninalopenda kuchangia ni kuhusu msongamano wa magari katika miji mikubwa hasa Dar es Salaam na Mwanza. Nashauri kuwa barabara zote zilizopo katika miji hiyo zipelekewe *TANROAD* ili ziweze kuhudumiwa na kupunguza msongamano

uliopo. Wananchi wamekuwa wakipata matatizo makubwa sana na kusababisha usumbufu na kero kwa wafanyakazi na wanafunzi kukerwa katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Spika, pia natoa ushauri mwingine kuwa angeteuliwa Mshauri kwa ajili ya kuangalia tatizo linalosababisha msongamano huo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata wasaa huu ili niweze kuchangia kwa njia ya maandishi kutoa maoni yangu juu ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii inazo changamoto nyingi ikiwemo ujenzi wa barabara ambao unaambatana na ubomoaji wa nyumba zilizoko pembezoni mwa barabara kwa mujibu wa sheria. Suala hili la ubomoaji wa nyumba umeleta malalamiko na tafrani kubwa kutokana na zoezi lenyewe, miongoni mwa jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi wa barabara zetu sio jambo la dharura, ningeshauri Wizara izingatie ushauri wa Rais Jakaya Kikwete alioutoa wakati alipokuwa akitembelea Wizara hii ya Ujenzi kwa kutoa kauli kwamba wananchi wasibomolewe nyumba za kupisha ujenzi wa barabara hadi wawe wamelipwa kwanza fidia zao na wapatiwe muda wa kuondoka.

Mheshimiwa Spika, watendaji wa Wizara hii wanapobomoa nyumba za wananchi tena kwa kutozingatia hali halisi ya ubinadamu na kuwaacha hawana mahali pa kuishi ndiyo yanayopelekea wananchi kuichukia Serikali yao kwa kuona kwamba inawanyanyasa ndani ya nchi yao. Naishauri Wizara ifanye upembuzi yakinifu wa kujua inahitaji kujenga barabara ngapi? Zipi na mahali gani ili kama kuna watakaobomolewa nyumba zao waandaliwe vema tena mapema kabisa ikibidi iwe ni miaka miwili kabla.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam ni jiji linalokua kwa kazi na hasa ikizingatiwa kwamba ni jiji la kibiashara zaidi pamoja na shughuli nyingi za Kiserikali ziko Dar es Salaam. kwa maana hiyo basi, naiomba Wizara hii kama Waziri alivyoainisha vipaumbele vyake katika hotuba aliyoiwasilisha isiwe ni maneno tu, Jiji la Dar es Salaam lifanyiwe mkakati wa makusudi na wa dharura ili kushughulikia suala la msongamano wa magari, kwa kufanya hivi tutakuwa tumeokoa mamilioni ya fedha yanayopotea kila siku kutokana na msongamano mkubwa wa magari na hasa ikizingatiwa sana kwamba Mkoa wa Dar es Salaam unachangia pato kubwa sana la Taifa kuliko mikoa mingine yote.

Mheshimiwa Spika, pia mitaro ya maji machafu itengenezwe vizuri ili kuepusha mafuriko katika barabara zetu hususan Dar es Salaam ambapo barabara zimekuwa zikishindwa kupitika nyakati za masika.

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Kilwa maeneo ya Mivinjeni imekuwa na matatizo naiomba Wizara iiangalie barabara hii na hasa eneo la Mivinjeni. Hali kadhalika kuwepo na udhibiti wa baadhi ya magari mazito kutumia barabara zisizo za viwango vyao kwani hili nalo limesababisha uharibifu wa miundombinu, pia Serikali isipokee barabara ambazo haziko katika viwango ikibidi Mkandarasi atimuliwe na badala yake watafutwe Wakandarasi wenye uwezo mzuri, hali hii italipunguzia Taifa hasara ya mabilioni yanayopotea kila mara kwa kukabidhiwa barabara zisizo na viwango.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichangie katika Wizara hii ya Ujenzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nitachangia kuhusu barabara iliyo katika hadhi ya Mkoa inayotoka Tabora – Mambali – Bukene – Itobo – Nzega. Barabara hii sasa hivi inapitiwa na magari mengi sana karibu mara tano ya kawaida yake, hii ni kutokana na kwamba barabara ya Nzega–Tabora haipitiki kwa sasa kutokana na kwamba imeharibika sana.

Mheshimiwa Spika, hoja iliyopo hapa ni kwamba, Serikali inapaswa iwe na mpango wa dharura wa kuhakikisha barabara hii inapata nyongeza ya bajeti ili iweze kutengenezwa mara kwa mara kuweza kuhimili idadi kubwa ya magari ambayo yote sasa yamehamia barabara hii ya Nzega – Itobo – Bukene – Mambali hadi Tabora.

Mheshimiwa Spika, bila kuweka bajeti ya nyongeza na ya dharura kuirekebisha barabara hii ni wazi kwamba kutokana na idadi kubwa ya magari na mengi yakiwa na uzito unaozidi tani 10 zinazoruhusiwa kupita barabara hiyo, barabara hii inaharibika sana kwa kipindi kifupi na isipodhibitiwa barabara hii itaharibika na itakuwa haipitiki kabisa. Ushauri wangu ni kwamba, bajeti itakayotengwa katika barabara hii ya Nzega – Itobo – Bukene – Mambali – Tabora izingatie ongezeko kubwa la magari, mabasi na malori ya mizigo zaidi ya tani 10 ambayo yote sasa hivi yanapita barabara hii.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Bukene tunafurahia magari na mabasi mengi kupita barabara ya Bukene lakini tunataka tuwe na uhakika kuwa barabara hii itatengenezwa ili haya magari yaweze kupita muda wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kwa maandishi. Kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali, Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuchapa kazi vizuri lakini pia kutuletea bajeti nzuri ya matumizi ya mwaka huu 2011/2012. Baada ya pongezi hizo naomba kuishauri Serikali katika mambo yafuatayo:-

Barabara kuu zinazojengwa na wakandarasi wa nje. Barabara hizi huchukua watu wengi wanaofanya kazi mbalimbali kwa kipindi chote cha ujenzi wake. Ni mara nyingi inaonekama wakandarasi hawa wakiwaajiri watu kutoka nje, hata kwenye nafasi ambazo Watanzania wana uwezo nazo. Serikali ingeweza kufaidi sana kwa vijana wengi wasio na ajira kuajiriwa katika ujenzi wa barabara hizi. Naishauri Serikali kwanza kufuatilia jambo hili kwa karibu ili wananchi wake wasio na ajira wafaidike zaidi.

Ulinzi wa barabara zilizojengwa. Serikali inatumia fedha nyingi sana za walipa kodi katika ujenzi wa barabara nchini lakini cha kusikitisha barabara hizi baada ya kujengwa zimekuwa zinaachwa bila ulinzi na utunzaji kiasi kuwa huharibiwa na watu wasiokuwa na nia njema wanaopitisha magari makubwa kupita kiwango na uwezo wa barabara, jambo linalopelekea barabara hizi kuharibika sana na kwa muda mfupi. Pia utaratibu wa kutunza na kusafisha mifereji iliyojengwa na wakandarasi hao. Nashauri mifereji hii kwa kupitia Halmashauri zao wakabidhi Serikali za Mitaa ambazo ndizo ziko kwenye mitaa na barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukubwa au urefu wa baadhi ya barabara: Mheshimiwa Spika, zipo baadhi ya barabara zinazotengewa fedha za kutengeneza kwa kiwango cha lami urefu wa kilomita 0.5. Jambo hili lina madhara yafuatayo:-

(a) Barabara moja inatengenezwa kwa kipindi kirefu sana kumalizika na haionyeshi *impact* mwisho wa siku.

(b) Kutokana na urefu mdogo Serikali inapotangaza tenda Wakandarasi walio na uwezo mzuri na mkubwa hawajitokezi na hivyo Serikali kuchukua wakandarasi wasio na ubora wa kutosha. Nashauri Serikali kupanga kutengeneza barabara chache kwa urefu utakaoonekana kwa kipindi fulani (mfano mwaka mmoja) na kuhamia katika barabara nyingine kwa mwaka unaofuata. Hii itaonyesha au itakuwa na *Impact* kubwa na wananchi watafurahia maana kazi itaonekana.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha mchango wangu huo.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja hii. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wasaidizi wake kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kuifungua nchi kwa barabara.

Pamoja na pongezi hizi ninayo maoni na maombi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni kuhusu barabara ya mchepuo Manyoni Mjini kilomita tano. Barabara hii ndiyo iliyokuwa inatumika kabla ya ujenzi wa barabara mpya, tumewasilisha ombi kwa Wizara hii ili iwekwe lami. Aidha, wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu anazindua barabara mpya (Dodoma–Manyoni) alitoa ahadi ya Serikali kwamba itawekwa lami. Wananchi wa Manyoni wanasubiri utekelezaji. Wakati lami inasubiriwa, kwa sasa barabara hii imeharibika mno, ina mashimo makubwa, tunaomba TANROADS (Mkoa wa Singida) waifanyie ukombozi angalau ipitike vizuri kwani kwa sasa hivi ni kero iliyo katikati ya Mji.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kuhusu kupandishwa daraja barabara ya Chikuyu Mjini – Ikasi. Barabara inayounganisha Mkoa wa Singida (Ikasi) na Mkoa wa Dodoma (Chaliigongo) inayoanzia katika *trunk road* (Chikuyu–Mjini–Ikasi–Chiliigongo ipandishwe daraja iwe ya *TANROAD*. Ombi hili tayari lilipitishwa katika Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Singida na sasa tunasubiri uamuzi wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kuhusu uanzishwaji wa vituo vya ukaguzi wa magari ya mizigo iendayo nchi za nje. Kutokana na usumbufu na ucheleweshaji wa magari ya mizigo iendayo nje ya nchi *(Transit Cargo)* Serikali kupitia Wizara yenu (Ujenzi), Wizara ya Uchukuzi na Wakala wa kufanikisha biashara ukanda wa kati *(Central Corridor Trade Facilitation Agency)* mmeanzisha mpango wa kuweka vituo vichache vitatu (3) vya ukaguzi wa magari ya mizigo iendayo nje *(Transit goods Inspection Centres)*, vituo hivyo ndipo patakuwa na mizani, vituo vya forodha, ukaguzi wa uimara wa magari *(Traffic vehicle Inspection)* na kadhalika badala ya sasa ambapo magari hayo yanasimamishwa katika mizani mingi, *Police check points* nyingi na hivyo kusababisha usumbufu wa ucheleweshaji wa usafirishaji mizigo.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa kuanzisha vituo hivi ni muhimu sana katika kufanikisha biashara ya ndani na nje, lakini nataka kujua mpango huu utaanza lini? Vituo hivyo vichache vitakuwa wapi? Je, mradi huu umetengewa fedha kiasi gani katika bajeti hii ya 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kazi kubwa inayoifanya kwa ujumla wake, ukweli mnahitaji pongezi kubwa, kwa Jimbo la Nkenge tumeona kazi yenu, Daraja la Kajai lakini hela ya kumalizia imetengwa ndogo mno. Kwa kuwa sehemu hiyo ni ya kutitia vema ikajengwa kwa kiwango cha lami hasa kilomita za Daraja.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Daraja la Kabingo litengenezwe kama Rais alivyoahidi. Tuliambiwa wakati wa kampeni kuwa fedha zimekwishatengwa Sh. 200,000,000/= mpaka sasa hakuna kilichofanyika. Ushauri wangu ni kwamba, naomba daraja hilo lijengwe kama Rais alivyoahidi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Spika, nami niungane na wenzangu kuchangia Wizara hii ya Ujenzi. Pamoja na maelezo mazuri ya Waziri wa Ujenzi nina haya ya kuchangia kwa uchache.

Mheshimiwa Spika, bajeti ya Wizara imejaa maelezo yake bajeti hii ina mapungufu makubwa mno kulingana na mahitaji ya vifaa. Katika vitabu vya bajeti utaona kuwa katika shilingi trilioni 2.8 zilizotengwa kwa miundombinu, shilingi trilioni 1.5 ni kwa Wizara ya ujenzi peke yake. Hili ni jambo la kusikitisha katika bajeti hii kubwa ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali haikuangalia sehemu nyingi hapa nchini zenye maslahi ya kuipatia nchi mazao ya chakula na biashara, kwa hiyo, kuzipatia bajeti ya fedha kwa ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Mfano, katika Mkoa wa Dodoma na Wilaya zake hasa Wilaya ya Kondoa haina sehemu hata moja iliyotengewa fedha kwa ajili ya kutuwekea lami wananchi wa Kondoa.

Mheshimiwa Spika, fedha zote zinazotengwa kwa ajili ya kuweka lami Dodoma, utaona bado hazihusishi Jimbo la Kondoa. Hali hii bado inadidimiza uchumi wa wananchi wa Kondoa kwa kushindwa kusafiri na kusafirisha mazao hasa kipindi cha mvua kinapoanza.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kuwa uchumi wa nchi hii huletwa na wananchi wa nchi hii, hivyo yapaswa kuimarisha miundombinu yote hasa maeneo ya vijijini kunakotoka mazao hususan Jimbo la Kondoa. Wananchi wa Kondoa wanapata shida kwa kukosa barabara za lami, nauli zimekuwa zikipanda siku hadi siku pia, matokeo yake maisha kwa ujumla kwa wakazi wa Kondoa ni magumu sana kwa sababu ya ubovu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na huruma ya Mheshimiwa Rais ya kuwa tujengewe barabara kiwango cha lami kutoka Bicha mpaka Stand bado agizo la Rais halijatekelezwa. Bado Waziri Mkuu pia alituonea huruma akaagiza tujengewe barabara ya lami toka Bicha mpaka Darajani lakini agizo lake halijatekelezwa mpaka leo.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa ina jumla ya kilomita za mraba 13,210 ndani ya eneo hilo kilomita 1500 za barabara zipo chini ya Halmashauri. Pamoja na jitihada za Halmashauri kutaka kujenga hizi barabara bado umekuwa mzigo kwa kuwa kila mwaka Kondoa huletewa fedha kidogo za maendeleo. Umefika wakati muafaka sasa Serikali kuzichukua barabara za pembezoni ambazo zinaunganisha Kondoa na mikoa ya Singida na Arusha na Manyara kwani kwa bajeti inayopangiwa Halmashauri ya Kondoa si rahisi kujenga barabara hizi muhimu zinazounganisha Kondoa na Mikoa ya jirani ya Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kujenga barabara hizi kutainua sana uchumi wa wananchi hivyo dhana nzima ya MKUKUTA itaweza kutekelezeka. Halmashauri kwa sasa inazidi kutanuka kwa maana ya idadi ya watu kuongezeka, hivyo na shughuli za kiuchumi zikiwemo kilimo pia zinakua. Hivyo, ni vema Serikali ikauangalia Mji wa Kondoa kwa jicho la huruma katika ujenzi wa barabara ya lami ili na sisi tuone kwamba kodi tunazotoa kwa Serikali zinatunufaisha watu wa Kondoa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na msemo wa Serikali kuwa Sungura ni mdogo kuna uwezekano mkubwa na kubana matumizi yasiyo ya lazima ikapatikana fedha ya kuniwekea lami ya angalau kilomita mbili tu Kondoa Mjini. Mfano, tunajua Ofisi lazima iwe na vifaa lakini ukiangalia kwenye Kasma 410502 na Kasma 410503 yamebadilishwa maneno tu kwenye mahitaji ya ununuzi wa samani za ofisi na ununuzi wa meza, viti na kabati.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine, Idara ya Utawala na Kitengo cha Uhasibu na Fedha. Vitengo hivi viwili tu utaona mfano, wakati Idara ya Utawala posho ya kazi ya ziada wameomba Sh. 109,500,000 (Milioni moja na tisa na laki tano) wenzao kitengo cha Uhasibu na Fedha wameomba Sh. 68,400,000 (Milioni sitini na nane na laki nne). Haya ni matumizi makubwa sana ya fedha na ni sehemu ndogo sana kati ya mamia ya Kasma yake, matumizi mabovu ya pesa.

Mheshimiwa Spika, pesa hizi zibanwe kuendana na mahitaji halisi ili Mji wa Kondoa upate hizo kilomita mbili tu za kuanzia kwa pale Kondoa Mjini angalau kutekeleza agizo la Rais na Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kitengo cha Uhasibu na Fedha (Kifungu 1002). Kwenye Kasma 220103 Gharama za uchapishaji na ununuzi wa karatasi za kudurufia 4,800,000 na wakati huo huo wameomba katika Kasma 220109, gharama za uchapishaji na kudurufu Sh.10,325,000/=. Huu ni mtindo uliozoeleka watumishi wengi wa Serikali kwa sasa kama njia ya kujitafutia fedha ambazo zinatengenezwa kwa mianya ya wizi na kuliibia Taifa. Ahsante.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali hii imewekeza fedha nyingi sana katika miradi mbalimbali kama vile kilimo na hata utalii ili kuwaletea maendeleo wananchi na pesa hizi hatupendi zipotee bila kufikia malengo haya. Lakini shabaha hii inakumbwa na changamoto ya kutokuwepo kwa barabara za uhakika na za kupitika muda wote kutoka katika maeneo hayo ya uzalishaji. Hata hivyo, barabara hizi ni kubwa kiasi kwamba haziwezi kuhudumiwa na Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili kufanikisha shabaha ya Serikali kikamilifu lakini pia kuthamini mabilioni ya fedha ambayo Serikali imewekeza namwomba Waziri atueleze kama yuko tayari kuzipitia barabara zote ziendazo kwenye miradi mikubwa ya Serikali na hatimaye kuzijenga katika viwango bora vitakavyohimili usafirishaji kwa maana ya zihudumiwe na Serikali kuu kwani Halmashauri zetu hazina ubovu kifedha.

Aidha, mfano mzuri ni barabara ya Mradi wa Kilimo Kwanza Kitanga, Miradi ya Umwagiliaji Titye na Rungwe mpya pamoja na ile ya Kilimo na Utalii – Kagerankanda katika Jimbo langu la Kasulu Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda mrefu sasa nchi yetu imekuwa ikitumia barabara kusafirishia mizigo mizito badala ya reli na maji kama ilivyo kwa nchi zingine hali inayopelekea barabara zetu ziharibike mara kwa mara. Sasa basi, ili kulinda barabara zetu zidumu kwa muda mrefu, namwomba Waziri atueleze ni mikakati gani ya makusudi kabisa na ya haraka iliyowekwa ili kuboresha bandari muhimu ya Kigoma sambamba na kuinusuru reli ya kati ili hatimaye mizigo mizito ya kwenda DRC, Burundi na hata Rwanda iweze kusafirishwa kwa njia ya Reli, kwa lengo zuri la kulinda barabara zetu ziweze kudumu angalau kwa muda mrefu ikiwemo barabara yetu ya Kidahwe–Nyakanazi ambayo itajengwa katika bajeti hii Mungu akipenda iwapo tu mambo yatakwenda kama yalivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wazo zuri ni wazo zuri tu, hata kama linatoka kwa shetani, leo tunapozungumzia jinsi ya kuondoa tatizo la msongamano Jijini Dar es Salaam. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa John Magufuli na timu yake kwa kuwa hotuba yake imejumuisha mawazo mazuri ya Injinia James F. Mbatia aliyewahi kutoa ushauri wa kitaalam wa namna ya kujenga miundombinu ya usafiri wa treni kwa wakazi wa Jiji, kutoka Pugu–Gongolamboto–Vingunguti-Buguruni mpaka kituo kikuu cha kati, pia kutoka Ubungo mpaka Kituo kikuu cha kati, ushauri ambao aliutoa mwaka 2010. Hivyo basi, hii inaonyesha kwamba kila Mtanzania anao wajibu na haki ya kuishauri na kuijenga nchi yetu, hasa ukizingatia kwamba Tanzania ni yetu sote. Kwa hiyo, haitokuwa vibaya kama mawazo haya mazuri yaliyotolewa na Injinia James F. Mbatia yakawa ni changamoto kwa wananchi, Watanzania wote wenye taaluma mbalimbali nao watoe mawazo yao badala ya kulalamika na kunyoosheana vidole tu bila kutoa ufumbuzi na hatimaye nchi yetu itapata maendeleo na itazidi kuwa mahali pazuri pa kuishi.

Ahsanteni sana na Mungu awabariki sana sana.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kuboresha miundombinu ya barabara, majengo na mitambo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kufahamu hatua iliyofikiwa ya ununuzi wa Kivuko cha Kilambo ambacho tenda yake ilitangazwa mwezi Juni, 2010. Kivuko hiki ni muhimu sana kwa wananchi wa Mtwara waendao Msumbiji kwa shughuli za biashara na wapiga kura wangu ambao wanalima ng'ambo ya pili ya Mto Ruvuma hasa kutokana na kivuko kilichokuwepo kuzama miaka miwili iliyopita.

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010–2015 inaeleza kuwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi itanunua vivuko vya Msangamkuu, Rusumo na Kilambo na zabuni kwa ajili ya vivuko hivyo ni kama nilivyoeleza hapo juu ilishatangazwa Juni, 2010 ukurasa wa 33 wa Hotuba ya Waziri inakitaja Kivuko cha Ilagala, haya ni makosa ya uchapaji au ndio Kilambo? Ningependa kupata ufafanuzi kivuko cha Kilambo kitakamilika lini kwa sababu nakala ya Gazeti ya Tangazo la zabuni ninayo kwa ajili ya rejea.

Mheshimiwa Spika, napenda kupata ufafanuzi juu ya hatma ya nyumba 15 zilizoachwa na Mradi wa *RIPs* ambazo *TBA* imezikodisha kwa *Aurtumus* wakati Mkoa wa Mtwara una tatizo kubwa sana la nyumba kwa watumishi hasa Majaji na Madaktari.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, Wizara ione umuhimu wa kujenga kwa kiwango cha lami barabara ziendazo kwenye nyumba ya Rais Mstaafu Awamu ya Tatu na eneo ambalo tunatarajia kujenga nyumba ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili ambazo zote zipo Msasani Penisula.

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena, naunga mkono hoja.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara nchini. Pamoja na pongezi hizo napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuweka matuta (*Humps*) barabarani. Naamini tumeendelea utaratibu wa kuweka matuta barabarani kwa sababu tu ya ukosefu wa nidhamu ya uendeshaji gari kwa upande wa madereva. Hivyo, dawa pekee ni matuta barabarani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Jimbo la Mbozi Mashariki ambalo hupitiwa na barabara kuu iendayo Zambia (*TANZAM- HIGHWAY*) kwa karibu kilomita 65. Eneo hilo la barabara lina vijiji au sehemu ambazo ni hatari sana kwa maisha ya binadamu. Maeneo hayo ni Kijiji cha Ihanda na Lumbila (Ruanda). Tumekuwa tunapoteza maisha ya Watanzania wengi sana kwa kugongwa na magari. Hali ni mbaya zaidi eneo la Ihanda ambalo sasa ajali za magari zimekuwa kama jambo la kawaida.

Mheshimiwa Spika, vikao vya Halmashauri ya Wilaya na *Roadboard* vilikubali maeneo hayo yawekwe matuta. Meneja wa *TANROARD* Mkoa wa Mbeya alishaagizwa alipeleke suala hili Wizarani, alithibitisha kwamba alishalipeleka ombi hilo Wizarani. Nataka kujua tatizo ni nini hadi leo matuta hayajawekwa katika maeneo hayo? Je, Wizara hii inafurahia kuona wananchi wasio na hatia wanaendelea kufa kwa makosa ambayo siyo ya kwao? Ni lini sasa matuta yatawekwa eneo la Ihanda na Lumbila (Ruanda)?

Mheshimiwa Spika, nawasilisha na sitaunga mkono bajeti hadi nipate jibu la faraja kwa wananchi wa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, nilipata bahati ya kutembelea Wilaya ya Muheza, nilipata pia bahati ya kutembelea barabara ya Muheza–Amani. Barabara hiyo imefanyiwa majaribio ya ujenzi kwa kutumia teknolojia cha *terrazyme* kwa kiasi cha kama kilomita nne tu.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa maelezo ya wahandisi wa barabara lakini pia na kwa maelezo mazuri niliyoyapata kwa Mbunge wa Muheza Mheshimiwa Mntangi, ujenzi wa barabara kwa teknolojia hii unapunguza gharama za utengenezaji kwa gharama kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, gharama za kutengeneza kilomita nne kwa kiwango cha changarawe, zinakadiriwa kuwa Sh. 80,000,000/=, wakati ambapo gharama za kutengeneza urefu huo huo wa kilomita nne wa barabara kwa kutumia *terrazyme* inakadiriwa kuwa Sh. 50,000,000/= *What a save*! Punguzo la karibu asilimia 37.5. Kama kazi ingesimamiwa vizuri bado gharama zingeweza kupungua zaidi. Aidha, inasemekana kwamba barabara inayojengwa kwa *terrazyme* inaweza kudumu kwa miaka hadi mitano bila kufanyiwa matengenezo yoyote. Wakati zile zinazotengenezwa kwa changarawe hukarabatiwa (matengenezo makubwa) karibu kila baada ya miaka mitatu. Hivi kama kuna unafuu kama huo kwa nini basi Wizara isianze kutumia teknolojia hiyo ya *terrazyme* katika kujenga barabara zetu? Je, kwa nini sasa hata barabara hiyo ya Muheza–Amani ambayo imefanyiwa majaribio ya *terrazyme* isijengwe yote kwa teknolojia hiyo hiyo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu wizi kwenye mizani au rushwa. Bado barabara zetu siyo salama sana. Pamoja na jitihada za kujenga barabara nchini, lakini tusipodhibiti uzito mkubwa wa magari yanayopita kwenye barabara hizo ambayo pia ni mengi, tutasababisha uharibifu wa barabara.

Mheshimiwa Spika, inashangaza sana kana kwamba tuna mizani (nyingi sana kwenye barabara kuu) za kupima uzito wa magari, hata hivyo, kwa sababu ya rushwa au wizi wa watumishi wa mizani magari yenye uzito mkubwa sana huruhusiwa kupita kwa kitu kidogo.

Nashauri, ili barabara zetu zidumu uadilifu kwa wafanyakazi wa mizani usisitizwe. Aidha, wale watakaopatikana na makosa hayo wafukuzwe kazi mara moja, maana hao wanahujumu barabara zetu. Pia gari zitakazokamatwa na uzito kupita kiasi zipigwe adhabu kubwa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa nyumba za Serikali, napongeza sana hatua ya Serikali kuamua kujenga nyumba kwa viongozi wa Serikali, lakini pia kujenga na kuziuza kwa watumishi wake. Hata hivyo, ujenzi wa nyumba hizi unaofanywa na *TBA*, Magereza, SUMA-JKT, una kasoro nyingi sana. Najua *TBA* ndiye msimamizi wa ujenzi wa nyumba hizo. Tatizo kubwa hapa ni usimamizi mbovu wa nyumba hizo. Nyumba nyingi ni mbovu sana, zina nyufa sana katika sakafu pamoja na kuta. Aidha, nyumba nyingine zinavuja, mabafu mengi hayapeleki maji sawa sawa, kazi ya mabomba mbaya! Lakini pia unapowaita viongozi wa *TBA* kwa ukarabati hawatokei kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, nashauri, kuwe na usimamizi madhubuti wa ujenzi wa nyumba za Serikali, zile zinazohitaji ukarabati kama za hapa Dodoma basi zikarabatiwe mapema.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Waziri kwa hotuba yake nzuri inayotia matumaini katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie hoja hii kwa kumwomba Waziri na wataalam wake waone umuhimu wa kuipandisha daraja barabara ya kutoka Buhingo hadi Ihelele kilipo chanzo cha maji yaendayo Shinyanga na Kahama na baadaye Nzega, Igunga na Tabora.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa barabara hii inayoanzia Mwanangwa – Misasi – Buhingo hadi Ihelele kwenye chanzo cha maji Wizara ione umuhimu wa kuitengeneza kwa kiwango cha lami na mwaka huu itengewe pesa kwa kuifanyia matengenezo makubwa ili iweze kupitika kwani imeharibika sana. Hii imesababishwa na ukweli kwamba barabara hii ni ya magari ya tani 10, lakini malori makubwa yanayopeleka madawa kwenye mitambo ya maji yana uzito wa zaidi ya tani 40.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri na Wizara yake waone umuhimu wa kuitengeneza barabara hii maana ni *strategic*. Huwezi kuwa na mradi wa zaidi ya bilioni 200 wa maji machafu ushindwe kuweka miundombinu ya kuhudumia.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuchukua fursa hii ku-*appreciate* kuwa Serikali sasa imegundua Kigoma nako wapo walipa kodi maana nchi inafikia miaka 50 ya uhuru ndio kunakumbukwa kwa kujengewa barabara za lami kwa lengo la kuufungua Mkoa wetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango iliyopo napenda kufahamu ni lini barabara ya Kigoma, Kasulu, Kibondo hadi Nyakanazi itajengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, tatizo la miradi ya barabara kuchukua muda mrefu linasababishwa na Serikali kutotoa pesa kwa wakandarasi kwa muda unaotakiwa, hali hii inasababisha baadhi ya miradi gharama zake kuzidi zaidi ya nusu ya gharama ya awali kwa visingizio mbalimbali ikiwemo upandaji wa bei ya vifaa vya ujenzi kutokana na shilingi yetu kuendelea kushuka na dola kupanda kila siku.

Mheshimiwa Spika, suala lingine, wakandarasi wengi hutaka kulipwa kwa dola badala ya shilingi yetu. Lakini ndani ya Bunge hili tulipitisha azimio la malipo yote hapa nchini yafanyike kwa pesa yetu. Je, Serikali haioni kuwa wakandarasi wanalipwa pesa nyingi kutokana na *exchange*

*rate* kubadilika. Tofauti na makubaliano ya awali ambapo Serikali imekuwa imejiandaa kwa *exchange rate* iliyopo wakati wa kuingia mkataba?

Mheshimiwa Spika, kwa nini baada ya kufunga mkataba na makubaliano ya malipo usiwekwe wazi Serikali italipa kwa *exchange rate* ya wakati ambao mkataba umeingiwa ili kunusuru Serikali kulipa pesa nyingi kuliko makubaliano ya awali?

Mheshimiwa Spika, kuhusu daraja la Kivukoni (Kigamboni). Ni muda mrefu sasa tunasikia juu ya daraja kujengwa eneo la Kigamboni. Naiomba Serikali ituambie ni lini ujenzi wa daraja hilo utaanza?

Mheshimiwa Spika, *TEMESA* imetekelezwa katika mikoa mingi hapa nchini imebaki kuwa kama barabara, mafundi wamekimbilia katika gereji binafsi vifaa havipo. Lakini Serikali inaendelea kununua magari kila kukicha je, yanafanyiwa *service* na kutengenezewa wapi? Kwani magari yananunuliwa lakini *TEMESA* inaendelea kufa. Ni dhahiri kwamba Serikali inapeleka magari yake kutengenezwa katika gereji binafsi na gharama imezidi kuwa kubwa. Hii sio sahihi, *TEMESA* iboreshwe na Serikali ilipe madeni yote kwa *TEMESA* ili ifanye kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu madeni ya Wizara hii, kupitia *TANROADS* taarifa inaonesha kuwa mpaka Machi, 2011 madeni waliyokuwa wanadaiwa na wakandarasi pamoja na fidia kwenye miradi mbalimbali ya barabara yalikuwa yamefikia kiasi cha Shilingi billion 446.47 (USD 297.6M) hilo ni ongezeko la 38.8% katika robo hiyo ya mwaka na hii ina maana kuwa ongezeko hili la madeni lilikuwa ni kwa wastani wa USD 1M kila siku (takriban shilingi bilioni moja na nusu kwa kila siku)

Mheshimiwa Spika, lakini pia taarifa ya Mkurugenzi Mkuu wa *TANROAD* tarehe 19 Mei, 2011 madeni yaliongezeka hadi kufikia bililioni 454, kiasi hiki ni kikubwa tofauti na kile kilichopangiwa mwezi Machi, 2011.

Mheshimiwa Spika, Serikali iangalie upya suala hili kwani badala ya kujenga barabara mpya tutakuwa tunalipa madeni na fidia.

Mheshimiwa Spika, lengo la mizani limekiukwa. Mizigo katika magari inazidishwa uzito matokeo yake wanalipa *fine* lakini lengo la mizani sio hilo, ni kulinda barabara zetu ili zisiharibike kwa kuelemewa na uzito tofauti na viwango vilivyowekwa. Tujivunie kazi ya usahili ya kulinda barabara. Mfano mzuri, ni barabara ya Dar es Salaam-Chalinze imeharibika kwa uzito wa magari ya mizigo. Ifike wakati reli ifanye kazi ya kubeba mizigo, barabara ibebe mizigo isiyo mizito.

Mheshimiwa Spika, *TBA* kazi yake ni nzuri lakini mbona majengo ya *UDOM* yamepata ufa mapema haikuyasimamia? Je, ikiwa walisimamia watachukuliwa hatua gani kwa kutosimamia viwango?

**MHE. DKT. ABDALLAH O. KIGODA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ujenzi wa barabara Mkata–Handeni, Korogwe-Handeni unaendelea ingawaje kwa kasi ndogo. Tunaishukuru Wizara kutekeleza suala la ulipaji fidia kwa wananchi walio kando kando ya barabara. Kimsingi barabara hizi maeneo mengi zimewafuata wakazi na hivyo kuwa na uhalali wa kulipwa fidia zao. Eneo la Suwa-Amani-Mazingira-Mkata na Vibaoni bado hawajalipwa fidia. Eneo la Kilole na Bagamoyo bado hawajalipwa fidia. Elimu ya awali ilitolewa kwa wananchi hawa watalipwa na wengine *infact* wameshalipwa. Kwa hali hii tunaomba zoezi hili likamilike ili ujenzi wa barabara uende kwa kasi inayohitajika. Kauli ya wananchi wengine kutokulipwa fidia wakati wengine wameshalipwa litaondoa utekelezaji wa utulivu wa ujenzi wa barabara. Ni vema Wizara ikajenga imani ya wananchi ya kutabirika. Aidha, ni vema barabara hii ikapimwa kwa umuhimu wake kiusalama, kiuchumi na hivyo kukazania utekelezaji wake wa haraka.

Mheshimiwa Spika, naomba ahadi ya Naibu Waziri Ujenzi, Mheshimiwa Mwakyembe tulisafiri nae kwenye eneo la barabara ili akaone hali halisi.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naunga mkono hoja.

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *TEMESA*, wakala huu ulianzishwa ili magari yote ya Serikali yaweze kufanyiwa *service* kule au kutengenezwa. Zilitumika fedha nyingi sana kujenga na kuzinunulia vifaa katika kila mkoa. Lakini *machine* zile zipo tu pale zinapigwa kutu na wafanyakazi wapo pale tu wanalipwa mishahara bila kufanya kazi. Cha kusikitisha zaidi magari ya Serikali yakihitaji matengenezo inabidi yaende *TEMESA* ndio wayapeleke katika *garage* za watu binafsi kwa ajili ya matengenezo, je, hii ndio kazi ya *TEMESA*? Kasoro za *TEMESA* zilitengenezwa kupunguza gharama, tunaona katika *report* ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali 2009/2010 (*CAG*), matengenezo kupitia karakana za watu binafsi ziligharimu Sh.176,722,089/=, hizi ni pesa nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri *TEMESA* iwezeshwe na fedha wanazodai kupitia taasisi mbalimbali walipwe ili waweze kununua vifaa vya kisasa magari ya Serikali yaanze kutengenzwa *TEMESA* hii itarudisha ajira nyingi kwa Watanzania sababu kwenye karakana za Kichina wameleta hata wakwanguaji rangi kutoka China. Je, Wizara mnashirikiana na uhamiaji kujua wafanyakazi hawa wanaofanya kazi ambazo Watanzania wangeweza kuzifanya?

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Daraja la Kigamboni. Imekuwa ni wimbo wa Taifa sasa kila mwaka kwa kipindi cha miaka sita, sasa Serikali imekuwa ikisema daraja hili litajengwa tena na *NSSF*. Je, mkakati wa ujenzi huo umefikia wapi usafiri wa kivuko ni wa matatizo *especially* kivuko kimoja kimeharibika. Naomba majibu ya uhakika, siyo majibu ya kila siku Serikali ipo katika mchakato.

Mheshimiwa Spika, barabara zinazojengwa kwa kiwango cha lami. Barabara nyingi nchini kwa mfano, barabara ya kutoka Dar es Salaam kupitia Mlandizi mpaka Chalinze. Barabara ile ni mbovu sana ina mabonde na kupelekea *accidents* nyingi sana sababu haikujengwa kwa kiwango. Je, mkandarasi huwa hatoi *guarantee* kwamba, barabara itatumika kwa miaka mingapi kabla ya kuharibika? Au ni sababu gani zinapelekea barabara ile kuwa na mabonde kwa kiasi kikubwa hivyo?

Mheshimiwa Spika, panakuwepo na ajali nyingi sana zingine zikiwa ni uzembe wa madereva lakini nyingine zinaweza kuzuilika. Kwa mfano, barabara zote kuu zijengwe (*Dual carriage way)* na pawepo na *permanent* ya ku-*park* endapo ni gari iliyopata matatizo. Malori mengi yanaweka majani wakati gari imeharibika kwenye kilima, madereva wanaokuja nyuma hawaoni mbele na kupelekea ajili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya *Old* Bagamoyo *Road*. Barabara hii pale karibu na *TMJ* Hospital kuna kadaraja ambacho tumekuwa tukikipigia kelele kwa zaidi ya miaka mitano sasa. Mvua zikinyesha huo ni daraja na maji yanajaa pale, barabara ile ni ya *TANROAD*, je tatizo ni nini? Hivi Serikali (*TANROAD)* imeshindwa kuweka daraja pale au mpaka ajali mbaya itokee watu wapoteze maisha ndio hatua ichukuliwe. Je, si vizuri kuzuia? Pia ni kwa nini mashimo yaliyopo kwenye barabara hiyo hayazikwi mapema mpaka yachimbike sana ndio waje wajaze mchanga?

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa nyumba za Serikali. Ni kitu cha kusikitisha kila mwaka zinajengwa nyumba za Serikali lakini kuna nyumba za Serikali ziliuzwa kwa bei ya kutupwa. Kwa mfano, nyumba nyingi zilizopo Osterbay na kadhalika zimegeuzwa matumizi na kuwa karakana au gereji za kuuzia magari, hii ni aibu. Je, ni kwa nini nyuma zilizouziwa viongozi na kugeuzwa matumizi zisirejeshwe Serikalini na kupangiwa viongozi wengine. Kwa kuwa nia ya Serikali ni kuhamia Dodoma, ni kiasi gani cha Serikali kilichotengwa na kwa W izara zipi kwa ajili ya ujenzi hapa Dodoma?

Mheshimiwa Spika, kuhusu matumizi ya mashangingi kwa watumishi wa umma. Magari haya yanakuwa ni gharama ya hali ya juu na mzigo kwa Serikali. Kulifanyia shangingi moja *service* ni sawa na kununua *Toyota Corola* la milioni tatu pale Japan. Pia matumizi ya mafuta ni ghali sana.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba, Wizara iangalie magari ya bei nafuu kwa ajili ya watumishi au watumishi wakopeshwe magari ili wayatunze na kuyajali. Hii itapunguza matengenezo yasiyo ya lazima. Mawaziri, Katibu Wakuu wakopeshwe magari na gari ya ofisini iwe ofisini na itumike wakati wa saa za kazi tu? Hii itapunguza matumizi mabaya ya gari za Serikali.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMMED:** Mheshimiwa Spika, fedha kwa ajili ya miradi ya barabara. Miradi ya ujenzi inachukua sehemu kubwa ya bajeti ya Serikali zote duniani na ndio maana nchi nyingi hata matajiri zinaweza kukabiliana na tatizo hili kwa njia ya *BOT, PPP* na *Consession Arrangments.* Serikali yetu kwa kupitia Bunge limepitisha sheria ya *PPP* ambayo bado haijaanza kutekelezwa kama ilivyokusudiwa kutokana na urasimu ulivyo Serikalini. Hivyo, nashauri kuwa mbali na kitengo kilichoko kwa Waziri Mkuu, Wizara ifanye maamuzi ya kina na miradi ya ujenzi wa barabara na madaraja ambayo wawekezaji watakuwa tayari kuijenga kwa njia hizo nilizozitaja. Pia Wizara, baada ya kuanzishwa maeneo hayo, iyatangaze kwa wawekezaji kwa kupitia mitandao na vyombo vya habari lakini hasa kwa ofisi za Balozi zetu ili wasaidie kuwatafuta wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ifanye juhudi ya kupata taaluma hii katika nchi za India, China, UAE na kadhalika, lakini pia itumie uzoefu wa makampuni ambayo yana uzoefu katika miradi hii kama *SNC* ya Canada na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara zetu. Barabara zimekuwa hazina umadhubuti, kutokana na kuelemewa na shehena za magari ya mizigo ambayo yameongezeka kutokana na reli yetu kushindwa kutoa huduma inayostahili. Nashauri pamoja na gharama kubwa ya ujenzi barabara zenye kuchukua uzito mkubwa, lakini kwa kuwa reli itachukua muda mrefu kujengwa, Wizara iongeze viwango vya umadhubuti wa barabara ili kukabiliana na uharibikaji wa barabara mara zinapotengenezwa au kujengwa.

Mheshimiwa Spika, viwango vya ujenzi wa barabara zetu, haviridhishi kwa mfano ya Mandela au inayoelekea Mwenge na kadhalika. Wizara imewachukulia hatua gani wakandarasi? Lakini kwa nini barabara hizo hazirekebishwi baada ya kumaliza ujenzi ambao hauridhishi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wakala wa Majengo. Wakati umefika wa kutafuta teknolojia mpya za ujenzi wa nyumba nafuu na kwa haraka kwani kwa mfano *IRIS* ya Malasyia wanajenga nyumba kwa kutumia takataka za mashambani, vyuma kidogo na ambazo ni madhubuti na kwa muda mfupi nyumba inapatikana. Sheria zetu zingaliwe ili teknolojia hizi mpya ziweze kukubalika na taasisi zetu za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. OMARI R. NUNDU:** Mheshimiwa Spika, mwambao wa pwani ya Mkinga–Tanga–Pangani–Bagamoyo–Dar es Salaam una mandhari nzuri ya utulivu wa biashara na pia ni kiungo kifupi cha Wilaya na Mikoa hii na nchi jirani ya Kenya. Kasi ya maendeleo katika ukanda huu inadumazwa na kukosekana kwa barabara nzuri ya kiwango cha lami katika ukanda wote. Kwa bahati na pongezi kubwa kwa Serikali vipande vya barabara za ukanda huu zimekwishajengwa au zinaendelea kujengwa kwa kiasi cha lami. Haya ni maendeleo mema lakini ili faida ya barabara hizi ikamilike inabidi kipande cha barabara ya Tanga – Pangani ambayo ni takriban maili 32 tu nacho pia kijengwe mapema kwa kiwango cha lami. Ujenzi wa barabara hiyo ulikuwemo kwenye ahadi ya Rais mwaka 2005 – 2010 na kuwekwa katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2010 – 2015.

Mheshimiwa Spika, kumejitokeza matatizo ya ulipwaji fidia wananchi waliobomowa nyumba zao kufuatia maagizo ya Serikali ili kupitisha ujenzi wa barabara ya Tanga-Horohoro. Wananchi hao wanadai kuwa waliahidiwa kulipwa tangu mwanzoni mwa mwaka 2010. Naomba suala hili lishughulikiwe mapema kuepusha migogoro ya kijamii na kisiasa.

**MHE. DKT. SEIF S. RASHID:** Mheshimiwa Spika, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu naomba kwanza nipongeze hotuba ya Mheshimiwa Waziri na utendaji wa kazi uliokwishafikiwa hadi sasa na mipango ya uboreshaji wa barabara zetu unaotegemewa katika kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, maendeleo ya nchi yatakuwa zaidi kama mazingira ya uwezeshaji yanakuwepo kabla ya mahitaji. Hii ni kusema barabara ziwepo za ubora zaidi kabla ya ongezeko kwa mfano wa magari yanayotumia barabara hiyo, lakini pia ni lazima mgao wa uwepo wa barabara uwafikie watu wote kwa uwiano na usawa.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa maendeleo ya barabara za ndani ya Wilaya kugawana kwa usawa kama ilivyofanywa kwa ujenzi wa Shule za Sekondari kwa kila Kata.

Mheshimiwa Spika, nasema wazi kwamba sipo tayari kuunga mkono hoja kama tutaendelea kuona Wilaya fulani zinatofautiana sana katika ujenzi wa barabara za lami. Hii si haki kabisa. Wakati umefika kwamba kila Wilaya ikapata kasma ya ujenzi wa barabara za lami za kiwango fulani kama vile kilomita 15 au zaidi na wale ambao tayari wanazo watusubiri wengine kwa uboreshaji huo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya za Mkoa wa Kilimanjaro zina barabara za lami za urefu mwingi zaidi wakati wengine hata zile za changarawe bado ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, nataka niambiwe kama Serikali itatekeleza kwa ubora ujenzi wa barabara ya kutokea Ikwiriri kupitia Mkongo hadi Mloka kwa haraka zaidi ili vijiji hivi zaidi ya 14 vinufaike mazingira wezeshi za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika miaka ya 1960 barabara ya kutokea Muhoro hadi Mbwera gari ilikuwa inafika, hivi leo Barabara hiyo ni kitendawili na kwa namna nyingine ni kitega uchumi kwa wakandarasi uchwara wanaolipwa fedha na Serikali kila mwaka lakini barabara hiyo haipitiki.

Mheshimiwa Spika, Rufiji imevumilia kuona wengine wakipiga hatua za vijiji vyao kufikiwa na barabara kuwezesha magari kufika, lakini Wilaya ya Rufiji upande wa *delta* umekuwa ni changamoto na kugharimu fedha nyingi kutumika kwa mafuta ya boti na kuipa hasara Serikali kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, uwiano wa maendeleo ni muhimu sana na mwelekeo wa bajeti ya ujenzi wa barabara kwa upendeleo wa kuona Mkoa wa Kilimanjaro ukiwa na barabara nyingi sana za lami na bado zinaendelea, wakati sisi kule Rufiji tukipata tabu sana bila ya mafanikio ya barabara ya changarawe, kutoka Ikwiriri hadi Mloka, Utete–Ngarambe. Nasema siungi mkono hoja na naitaka Serikali kurekebisha hili.

Mheshimiwa Spika, Serikali imetumia fedha nyingi bila ya sababu ya kujenga gati ndani ya Mto Rufiji upande wa Mkongo ambayo haitumiki. Hivyo, naitaka Serikali kurudisha fedha hizo mlizozipoteza ili Warufiji wanufaike nazo kwa ujenzi wa barabara kutokea Nyamwage hadi Utete na Kibiti-Utete iwe ya lami. Nitaridhia bajeti hii kama tutakuwa na uwiano wa maendeleo ya barabara na sio kuwekeza fedha zote kwenye mikoa michache na kuacha wengine tukiwa watazamaji.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi sipo tayari kuunga mkono uwekezaji wa Mkoa wa Kilimanjaro ukiongezeka kama ulivyoainisha na kuendeleza utofauti wa maendeleo baina ya maeneo ndani ya nchi moja. Nataka na sisi Warufiji tufike Mtwara kwa gari kama ilivyokuwa miaka ya 1960, barabara ya Ikwiriri–Mloka inatengewa fedha sio tu kwa kutimiza ahadi ya Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni ila ni haki yetu ya msingi kutokana na kodi zetu.

Mheshimiwa Spika, nataka jibu ni kiasi gani kimetengwa kwa barabara ya Mloka – Ikwiriri na ujenzi unaanza lini na ni lini Warufiji tutafika Mtwara kupitia Muhoro kwa gari na feri ya Utete imetengewa kiasi gani cha kuiwezesha kivushe wakulima na wagonjwa hadi usiku?

Mheshimiwa Spika, suingi mkono hoja hadi nitakapopata majibu ya kuridhisha kwa maendeleo ya nchi yetu.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Spika, *what goes around comes around!* Kuna tetesi kuwa wajanja fulani wamepeleka *TANROADS*, *invoice* ya zaidi ya bilioni za fedha kwa

jina la SOGEA, kuwa ati SOGEA haikulipwa kwa miradi iliyofanya zamani. Naomba liangalieni hili, nawapenda sana ninyi wawili na nchi inawapenda na kuwahitaji sana. Kama ipo hiyo *invoice* ni bomu.

**MHE. DIANA MKUMBO CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, napenda kutumia nafasi hii kwa njia ya maandishi kuwapongeza Waziri wa Ujenzi Mheshimwa John Pombe Magufuli, Naibu Waziri wa Ujenzi Dokta Harrison Mwakyembe, Katibu Mkuu pamoja na watendaji wote walioshiriki kuandaa bajeti hii nzuri yenye lengo la kuwapunguzia wananchi tatizo la barabara kwa viwango mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, vile vile nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitampongeza Meneja wa Barabara, Mkoa wa Singida Ndugu Kangole. Nampa pongezi hizi kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida kwani daima amekuwa makini, mwadilifu na moyo wa kujituma katika kutekeleza majukumu yake ikiwemo kutengeneza maeneo korofi kila yanapojitokeza. Mwenyezi Mungu amjalie asije akabadilika.

Mheshimiwa Spika, pili, ni ahadi ya Waziri Mkuu kutengeneza Barabara ya kuingia na kutoka Manyoni Mjini. Napenda kumkumbusha Mheshimiwa Waziri mwenyewe kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu Mizengo Peter Kayanza Pinda alipokuwa akizindua barabara ya kutoka Dodoma hadi Manyoni aliahidi kutengeneza barabara ya kuingia na kutoka Manyoni Mjini na Waziri aliyekuwa ana dhamana wakati Mheshimiwa Dokta Shukuru Kawambwa alikubali na alikiri kuwa fedha zipo. Suala la kusikitisha ahadi hiyo hadi leo haijatekelezwa na sababu hazijulikani.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wameingiwa na hofu, mashaka na kukosa matumaini na Serikali yao namwomba Mheshimiwa Magufuli Waziri mwenye dhamana kutoa majibu yenye matumaini kwa wananchi wa Manyoni wakati akijibu hoja za Wabunge hapo kesho jioni.

Mheshimiwa Spika, tatu, ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka Mkiwa, Itigi, Rungwa inayounganisha Mkoa wa Singida na Mbeya. Wananchi wa Wilaya ya Manyoni na Mkoa wa Singida kwa ujumla wamefurahia sana ahadi ya Serikali ya kujenga barabara hii niliyoitaja hapo juu kwa kiwango cha lami. Hivyo basi, napenda kufahamu kupitia bajeti hii zimetengwa shilingi ngapi na ujenzi utaanza lini. Wananchi wa Mkoa wa Singida wana imani sana na Mheshimiwa Magufuli Waziri mwenye dhamana, hivyo tunategemea sana majibu mazuri wakati akihitimisha bajeti yake ili nami nisimsumbue wakati wa vifungu.

Mheshimiwa Spika, nne ni ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami ya Singida, Ilongero, Mtinko, Nkungi, Kidarafa hadi Hydom ahadi ya Mheshimiwa Rais. Kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida ninampongeza sana Mheshimiwa Dokta Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa upendo aliouonyesha kwa wananchi wa Singida, wakati wa kampeni ya Urais aliahidi kujenga barabara niliyoitaja hapo juu. Alitoa ahadi ya kuanza na ujenzi wa barabara hii kwa kuanzia na kilomita thelathini akianzia Singida hadi Ilongero. Napenda kujua fedha za ujenzi huu zimetengwa shilingi ngapi na ziko Mfuko upi?

Mheshimiwa Spika, tano, ujenzi wa barabara ya Shelui, Sekenke, Ntwike, Doromoni hadi Ibaga. Napenda kuikumbusha Serikali kuwa barabara hii ni kubwa na ni ya muhimu sana kwa sababu imepitia kwenye vijiji vingi vyenye wakulima wazuri, wafugaji wazuri na wavuvi. Jambo la kushangaza Wakala wa Barabara (*TANROADS*) wanahudumia kilomita 21 tu ambazo zinaishia katikati. Kwa nini barabara hii isihudumiwe na *TANROADS* yote ili kuleta sura na huduma nzuri kwa wananchi hawa wengi wenye shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Nasubiri majibu ya kaka yangu Mheshimiwa Magufuli au Mheshimiwa Dokta Mwakyembe sitaki kugombana nao wakati wa vifungu.

Mheshimiwa Spika, sita, maombi ya kujengewa daraja la Sanza, barabara ya Mkoa ya Manyoni, Heka, Sanza hadi Chaligongo. Napenda kuipongeza Serikali kwa kazi zake nzuri za kutengeneza barabara hii kila inapoharibika. Bali natoa masikitiko makubwa kwani Serikali imesahau kutengeneza daraja la Sanza ambalo lilibomolewa na mafuriko ya mvua miaka mingi

iliyopita. Kubomolewa kwa daraja hili wananchi wanapata shida sana kwani magari husitisha safari kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ya CCM inawajali wananchi wake namwomba Mheshimiwa Waziri alipokee tatizo hili kwa moyo wa huruma na ikiwezekana kipindi cha bajeti hii kabla hakijamalizika twende pamoja na Mbunge wa Jimbo akaangalie tatizo hili ambalo lina uzito wa pekee. Nasubiri majibu ya Serikali wakati wa kujibu hoja hapo kesho jioni. Tena barabara hii inaunganisha na Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, saba, barabara ya Singida, Mwankoko, Mgungira hadi Iyumbu. Naipongeza sana Serikali kwa kuipandisha daraja barabara niliyotaja hapo juu kuwa barabara ya Mkoa. Napenda kuiomba Serikali kuitengeneza barabara hii kwa kiwango cha lami angalau kilomita kumi yaani Singida Mjini hadi Mwankoko ili kuleta hadhi ya Manispaa wakati Serikali inaendelea kukusanya nguvu za kuijenga barabara yote kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, nane, ni madhara ya matuta barabarani. Napenda kuungana na ushauri wa Kamati ya Miundombinu kuwa matuta ya barabarani yanaharibu magari sana. Hivyo, ni bora yaondolewe na suala la mwendo kasi litafutiwe ufumbuzi mwingine.

Mheshimiwa Spika, tisa, fedha za barabara za Halmashauri. Napenda kuiomba Serikali kuongeza kiwango cha fedha zinazotengwa kwa ajili ya barabara za Halmashauri za Iramba, Singida na Manyoni kwani kila wanapoomba fedha wanapewa kidogo tu kinyume na maombi yao. Hii inakwamisha sana ujenzi na ukarabati wa barabara ambazo ziko chini ya Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Spika, napenda kumalizia kwa kuunga mkono bajeti hii nikiwa na matumaini kuwa Mheshimiwa Magufuli pamoja na Mheshimiwa Dokta Mwakyembe kwa dhamana waliyonayo wataujali mchango wangu na kwamba watanipa majibu yenye matumaini kwa Watanzania.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Spika, ni kweli Serikali yetu inafanya kazi kubwa na inastahili pongezi. Tatizo uwekezaji katika barabara umeonekana umelalia sehemu kidogo ya nchi (*skewed*) na kuacha sehemu kubwa. Bajeti hii nilitazamia ingesaidia katika kurekebisha hali.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma uliacha barabara ya Njombe-Songea hakuna barabara yenye lami kabisa. Wakati barabara za kuelekea mipakani kwa Mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ziliwekwa lami muda mrefu, hakuna juhudi za dhahiri kwa Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, maoni maalum. Serikali inaonesha dhamira ya kutengeneza barabara ya lami Mbinga – Mbambay. Hii itapita Nyomi na hivyo kuacha barabara ya maeneo makubwa ya uzalishaji ya Nyomi, Maguru, Langira, Kirare na Mkoka. Mheshimiwa Rais aliahidi kutengeneza kwa kiwango cha lami barabara ya Nyomi – Maguru Mkoka. Barabara nyingine ni Mbinga – Litembo (hapa kuna Hospitali kubwa). Naomba Wizara ifanye taratibu za kutekeleza hili. Niliongea na Mheshimiwa Waziri mapema mwaka huu na hivyo naomba maelezo ya utekelezaji. Naomba pia barabara zifuatazo zitengenezwe kwa kiwango cha lami. Kigonsera – Matiri – Mbaha, Kitai – Ndanda – Lituhi (pana mradi mkubwa wa makaa ya mawe). Barabara kutoka Matiri – Mbaha itachepushwa kukwepa mteremko mkubwa. Wananchi wamekwishaanza.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi zinafaa sasa zishughulikiwe na *TANROADS*. Mbinga – Mpepai, barabara hii inatakiwa kutengewa fedha zaidi ili itengenezwe kwa kiwango kizuri. Kitai – Litumbandyosi, Litembo – Kitai – Mzuzu (imesahaulika sana), Mbinga - Ngune – Ngumbo.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma ni Mbinga zaidi ni maeneo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Sioni na sielewi kwa nini yawe maeneo ambayo hayana umeme na hayana barabara, hii haikubaliki. Bajeti ijayo iangalie na itende haki.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. AGGREY D.J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Waziri wa Ujenzi kwa hotuba yake nzuri ambayo ameitoa asubuhi ya leo. Ni ukweli usiopingika, kwamba maudhui ya hotuba hii yamelenga kutekeleza kwa haraka Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2010 – 2015. Aidha tunampongeza Mheshimiwa Harrison G. Mwakyembe kwa ushirikiano wa hali ya juu anaoutoa kwa Mheshimiwa Waziri na hivyo kusababisha ufanisi wa hali ya juu katika Wizara.

Mheshimiwa Spika, kipekee tunaishukuru Serikali kwa kukubali barabara ya Sanya Juu – Kamwanga ianze rasmi kwa kututengea Shilingi bilioni 1.8. Ni matumaini yetu kwamba mwanzo huu utaweka nuru mpya katika kuinua hali ya uchumi hasa katika eneo la utalii. Sisi wananchi wa Siha tunauunga mradi huu mkono na tutatoa kila aina ya ushirikiano ili mradi huu uweze kutekelezwa kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara ya Ujenzi na kwa umuhimu nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri John Pombe Magufuli na Naibu wake Mheshimiwa Harrison Mwakyembe, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wakuu wa Vitengo vyote vya Wizara.

Mheshimiwa Spika, ukurasa wa 68 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imebainisha wazi kuwa kutakuwa na ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kilomita 14 kutoka Kilindoni *Airport* hadi Utende kwa thamani ya Sh.1,899.60 milioni.

Mheshimiwa Spika, kwanza nashukuru sana kwa Serikali kuanza mradi huo. Lakini wasiwasi wangu ni kuwa kwa pesa hizo zilizotengwa na ukiangalia kuwa ujenzi ndio unaanza, ulipaji fidia kwa nyumba au mali zitakazoathirika na ujenzi huo na hasa ukizingatia malighafi nyingi hutoka nje ya Wilaya ya Mafia kuwa pesa hizo ni ndogo mno. Hivyo, ningependa kupata maelezo zaidi.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kujua fidia hiyo itaanza kulipwa lini na watapewa siku ngapi kwa ajili ya matayarisho ya kuhama na kupisha ujenzi wa barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, ni kuutakia kheri na mafanikio uongozi wote wa Wzara na wataalam wao wote ukiongozwa na Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli, Waziri.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kujipanga vizuri kutekeleza miradi ya barabara nchini.

Mheshimiwa Spika, naomba kupata ufafanuzi kuhusu barabara ya Mkiwa – Itigi – Rungwa – Makongorosi. Barabara hii imeonekana kupimwa na mafundi wa barabara kwa kile kinachoitwa upembuzi yakinifu au usanifu. Lakini haionyeshwi popote kwa mwaka 2011/2012. Aidha kwa ujenzi wa lami au kutafutiwa fedha au hata kwa *routine maintenance* chini ya barabara za mikoa zilizotengewa fedha.

Barabara hii imeachwa kwa kusahauliwa au ni makusudi kwa sababu kuacha bila maelezo au mipango yoyote inatia shaka sana na kuonyesha jinsi Serikali isivyotambua umuhimu wa barabara hii hata kabla na baada ya uhuru. Kutoka Mkiwa – Itigi – Mlongojii – Doroto – Lulanga – Itagat – Ukimbu (Kayui) – Mtakuja – Makale – Mitundu – Kalangali – Kiyombo – Kirumbi – Mwamagembe – Kiutanula – Rungwa – mpaka Kambi Katoto – Makongorosi, takriban vijiji 20 haviwezi kuachwa tu bila kuwa na barabara ya kupitika kwa mwaka mzima. Kilimo cha tumbaku, alizeti na mazao ya misitu kama mbao, asali na nta na kadhalika, yanahitaji kusafirishwa kwenda masika na kadhalika. Pia kuna mbuga za akiba za Rungwa/Kizigo na Muhesi ambazo hutegemea barabara hii muhimu kufanya doria na watalii na makampuni zaidi ya tisa ya uwindaji. Ni eneo lenye utajiri wa rasilimali lukuki. Pia barabara hii ni kiungo kati ya Mkoa wa Mbeya na Singida.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itenge fedha kwa mwaka wa fedha 2011/2012, vinginevyo kuna hatari ya barabara hii kutopitika wakati wa masika zinazoanzia Novemba.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Manyoni – Itigi – Chaya imeanza kujengwa, nashukuru lakini imepangwa kumalizika 2013. Hoja hapa ni kuwa wakati barabara hii inajengwa, ile ya zamani imetelekezwa. Hali ya barabara ya Manyoni – Itigi – Chaya (*the current one*) ni mbaya na imeachwa kwa maelezo kuwa barabara mpya inajengwa.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara itenge fedha za *routine maintenance* ya barabara hii 2011/2012 wakati ujenzi wa barabara mpya unaendelea. Sioni popote kwenye jedwali kuonyesha imetengewa fedha za matengenezo ya kawaida na ya dharura. Bila shaka *TANROADS* walisahau hilo.

Mheshimiwa Spika, kambi ya Mchina ya Mkiwa na *Quarry* ya Mlima Iwelewele na Majengo ya Mhandisi Mkazi pale Iwelewele yakabidhiwe kwa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni. Hili nimeliandikia kwa Mheshimiwa Waziri na *Director General (DG)* wa *TANROADS*. Mpaka kati ya Wilaya ya Manyoni na Ikungi ni daraja lenye mto karibu na kibao cha barabarani kinachoonyesha Kijiji cha Mkiwa. Tokea ukoloni mpaka ni kijito na hata *GN* ya Serikali inasema hivyo. Kodi za kitongoji cha Iwelewele ilikusanywa na Mwanangwa wa Baraza la Itigi, Wilaya ya Manyoni na wananchi wa Ikungi wanajua hilo.

Mheshimiwa Spika, Serikali yafaa itambue kuna Mbunge wa sasa wa Singida Mashariki ni Mbunge mgumu ambaye Mkoa wa Singida haujawahi kupata toka uhuru. Ni msumbufu, ananisumbua nisipate nafasi ya kuongoza wananchi wa Jimbo langu. Serikali itambue hilo kwa kunisaidia kudhibiti mipaka ya Jimbo langu. Nikionekanekana kushindwa na matatizo na yeye kufaulu atapata kibali machoni mwa wananchi wa Jimbo langu na wengine watakuwa wanapeleka matatizo yao kwake maana tunapakana kwa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, hilo likitokea, Chama chetu kitayumba katika chaguzi zijazo. Naomba hili lipatiwe ufumbuzi kwa kuyakabidhi maeneo tajwa hapo juu kwa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wake wote kwa kazi nzuri ya utayarishaji wa hotuba hiyo, ambayo Mheshimiwa Waziri ameiwasilisha vizuri na kwa ufasaha na umahiri mkubwa, na uwezo huo mzuri Mheshimiwa Waziri anao, nampongeza. Naomba kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ujenzi wa barabara unasimamiwa na Wizara ya Ujenzi, hivyo hata ahadi ya Rais (njia) utekelezaji wake unasimamiwa na Wizara yako. Mheshimiwa Rais Mstaafu, Mheshimiwa Mkapa wakati wa utawala wake wa Awamu ya Tatu, alifika Zanzibar kwa ajili ya uzinduzi wa njia (barabara) itokayo Mtoni kwenda Amani (*round-about)* ambayo njia hiyo (barabara) ilijengwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), na alipoizundua ilikuwa ina njia mbili ya kuingia na kutoka na kutomalizika. Hivyo, alitoa ahadi ile barabara ambayo haijakamilika Serikali ya SMT kwa kupitia kauli yake ndio itakayoikamilisha, barabara hiyo ilikuwa imebaki kilomita tatu. Hivi sasa ni mwaka wa nane tokea (2003 – 2011). Naiomba Wizara yako kuliangalia suala hili kwani hata Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete analikubali suala hili na kuahidi kutekeleza ahadi hiyo, lakini bado kuna kigugumizi katika ujenzi huo. Ingawa taarifa ipo inayoeleza kwamba SMT imetenga fedha za ujenzi huo, lakini fedha hizo zimekwamia wapi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika kitabu chako zijaona barabara (njia) ziendazo kwa kasi. Msongamano wa magari Dar es Salaam ni tatizo kubwa. Ningeliomba ukatujulisha nini tatizo hadi leo barabara hizo zimekuwa gumzo bila ya kujulikana kwanza kwake na kumalizika.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji wa wanawake katika kazi za barabara katika ukurasa wa 37 na ukurasa wa 92 umezingatia jinsia kwa kuwashirikisha wanawake. Naipongeza Wizara kwa ajili ya kuona kwamba wanawake pia wana uwezo katika kulijenga Taifa lake, kwa kuwaongezea

ujuzi wa kuwapa mafunzo ya ukandarasi kwa kampuni 15 za wanawake kama ushiriki wa wanawake katika kazi ya ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, vile vile natoa pongezi kwa Wizara kwa kuwahamasisha wanawake kutoka katika Mikoa mbalimbali na kuwapatia mafunzo ya ukandarasi kwa kutumia teknolojia ya nguvu kazi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MOSSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Kasulu, mpango mkakati unaonyesha wazi kuna siasa ndani yake inayolenga kuwapora wana Kigoma fedha za ujenzi wa barabara hiyo na kuzipeleka Nyakanazi Mkoa wa Kagera. Hili linadhihirika katika Vitabu vya Mipango vya Wizara vya mwezi Mei, 2011, vilivyoonyesha kuwa ujenzi uanzie Nyakanazi kuja Kibondo *then* Kasulu kuelekea Mpanda kupitia Kanyani na Uvinza. Ilivyopangwa kuwa ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Kasulu – Nyakanazi, Wizara ina dhamiria nini wakati inajua kabisa kuwa barabara ya Kidahwe – Kasulu (km50) iliyotengewa fedha tangu mwaka jana 2010/2011 ni tofauti na hiyo ya Nyakanazi – Kibondo – Kasulu – Kanyani – Uvinza – Mpanda?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa ni vizuri sana Serikali ikawa "*stable"* kwa kuheshimu mipango yake na siyo kuwa kama kinyonga. Hivyo shilingi bilioni sita (6) na ushee za mwaka jana kwa ajili ya ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Kasulu zitafutwe na kupelekwa Kigoma ili ujenzi huo uanze Kidahwe kuelekea Kasulu *as it was planned and passed by the Parliament.* Aidha, Wizara ya Ujenzi iepuke tabia ya kuhamisha fedha kama inavyotaka kufanya kwa barabara hiyo eti ujenzi uanzie Nyakanazi Kagera huku ikijulikana wazi kuwa Nyakanazi sio Kigoma na barabara hizo kama nilivyofafanua ni mbili tofauti.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, naishauri Serikali isikubaliane na ushauri wa Mheshimiwa Serukamba (Mb) na Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu anayeshauri kuwa ujenzi wa barabara uanzie popote huku akiwa amelenga Nyakanazi kwa sababu alishadhamiria hivyo tangu siku nyingi bila kujali kuwa tayari Kidahwe – Kasulu ilishatengewa fedha tangu siku nyingi badala yake zingatieni ushauri wa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete unaofanana na ushauri wangu kwa maslahi ya wana Kasulu Kigoma na Tanzania kwa ujumla wake hasa ikizingatiwa kuwa, Mkoa wa Kigoma ulisahauliwa sana hasa barabara hiyo ya Kidahwe – Kasulu. Hizo shilingi bilioni mbili (2) za mwaka 2011/2012 zitumike kwa barabara hiyo kama mlivyoandika kuanzia Kidahwe – Kasulu – Nyakanazi.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, naomba Wizara ione kuwa hata wana Kasulu wanastahili lami kama wana Kagera Nyakanazi na Kigoma Mjini kwa akina Mheshimiwa Serukamba.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. ABDULSALAAM S. AMER:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kujua barabara toka Kilosa hadi Mikumi itaanza lini, pia barabara ya Morogoro - Iringa *High way* inapita katika Mji Mdogo wa Mikumi lakini katika Mji Mdogo wa Mikumi hakuna *bumps* hata moja zaidi ya ile iliyoko kwenye mizani ya Mikumi. Naomba Wizara ifanye kila iwezavyo kuweka matuta kwani kila mara hutokea ajali kutokana na kukua kwa Mji huo mdogo wa Mikumi. Napenda matuta yawekwe unapoingia Mji wa Mikumi ukitokea Morogoro na mengine katika Njia Panda itokayo Kilosa na Kilombero. Naomba Wizara izingatie maombi yangu.

Mheshimiwa Spika, nasisitiza barabara ya Miyombo – Lumuma katika awamu ya kwanza haukufanyika kihalali. Barabara hiyo ipo katika Wilaya ya Kilosa Mkoa wa Morogoro na yote ni Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tatizo hiyo barabaraba inapita katika Majimbo mawili, Jimbo la Kilosa la Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Jimbo la Mikumi ambalo ni langu. Sehemu ya Jimbo langu la Mikumi wameruka. Je, katika bajeti hii, hawataruka barabara inayopita Jimbo la Mikumi?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ALPHAXARD K.N. LUGOLA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kujenga barabara kwa wingi katika nchi hii na hivyo kufanya mtandao mrefu na mkubwa wa barabara za lami ambapo sasa bajaji inaweza ikatoka Dar es Salaam hadi Musoma kupitia Dodoma bila tatizo au kutoka Tanga hadi Mutukula.

Aidha, naipongeza Wizara kukubali kuijenga barabara ya Bunda – Kisorya – Nansio yenye urefu wa 118 km kwa kiwango cha lami. Pia, naipongeza Wizara kwa kuanza kuifanyia upembuzi yakinifu barabara hiyo ambapo katika Kitabu cha hotaba ya bajeti, nimeona shilingi 40,000,000 zimetengwa kwa ajili ya upembuzi yakinifu (rejea ukurasa 141 katika Kitabu cha hotuba na ukurasa 138 katika kasma 4132, Mkoa wa Mara katika Kitabu cha Mpango na Bajeti ya mwaka 2011/2012 (Randama). Naiomba Wizara ihakikishe fedha hizo zinatumika kama zilivyokusudiwa kwani pia barabara hii ni ahadi ya Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni vivuko katika Jimbo la Mwibara ambapo katika ahadi ya Rais alituahidi kivuko kipya cha Rugezi – Kisorya kwani kilichopo ni kibovu na kinaweza kuhatarisha usalama wa maisha ya wananchi. Aidha, Kisiwa cha Nafuba chenye shule, zahanati na makazi mengi ya watu kuna tatizo la usafiri hasa katika usafirishaji wa vifaa vya ujenzi wa shule, zahanati na nyumba na usafiri wa wananchi mfano wanafunzi waendao Bara kusoma Sekondari ya Kata – Nansimo na watumishi kama Walimu, Waganga, Afisa Uvuvi). Naomba kivuko kati ya Kisiwa hiki cha Nafuba na KiJiji cha Nansimo ambapo tayari kuna maegesho yaliyokuwa yanatumika wakati wa meli iliyokuwa inabeba na kusafirisha marobota ya pamba. Kwa vile boti la MV Ukarra ipo, naomba tupatiwe boti hiyo sisi wana Mwibara ili kutatua tatizo la usafiri kati ya Kisiwa cha Nafuba na Nansimo.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la usafiri kati ya Iramba, Jimbo la Mwibara na Majita, Jimbo la Musoma Vijijini ambapo pametengwa na rasi ya maji ya Ziwa Victoria. Hali hii imedumu kwa muda mrefu na hivyo kutupa gharama kubwa za usafiri kwani lazima ukiwa na gari uzunguke kutokea Wamba uende Bunda, uende Musoma na baadaye uende Majita takriban 150 km. Tunaomba kivuko eneo hili ili kunusuru hali hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. ZARINA S. MADABIDA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kupongeza Serikali kwa kazi nzuri ya kusambaza barabara Tanzania nzima maana barabara ni maendeleo.

Mheshimiwa Spika, nakubali wazo la Kamati ya kuunda aidha Wizara au Idara itakayoshughulikia msongamano maana miji inakua. Hii itawezesha tuwe na *Traffic Management System* ili kuwe na mtitiriko wa magari muafaka.

Mheshimiwa Spika, napongeza suala la *Flyover* lakini naomba tufikirie *over/under pass* kwa sababu ni rahisi na zinaweza kutekelezwa kwa muda mfupi. Wakati tukingoja hizo *over/under pass*, hali sasa hivi ni mbaya sana na Serikali inaweza kutatua kwa kurekebisha njia za ndani lakini pia kwenye makutano kama navyoonyesha sasa hapa chini:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, Temeke. Daraja la Malindi/BP, ni ufumbuzi wa foleni ya Kilwa Road, hata zikijengwa barabara kama ilivyoorodheshwa kwenye hotuba haiwezi kufungwa kwa sababu magari yote ni lazima yapite hapa. Hata daraja la Kigamboni haliwezi kutatua kwa sababu magari yatapita hapo hapo darajani.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa maungo *(junctions)* ya Chang'ombe *(VETA), TAZARA* na kujenga barabara ya Jet (Mchicha) ambayo inatoka Temeke na kutokea *Pugu Road* karibu ya *Air Port*.

Mheshimiwa Spika, Kinondoni. Daraja la *Salender* ni lazima lipanuliwe. Serikali imepanua barabara nyingi lakini zote zinakutana *Salender Bridge* lakini kusaidia hili basi barabara ya Msasani – Tanesco na nyingine za ndani ni lazima zijengwe.

Mheshimiwa Spika, Daraja la Mabibo linatoa uwezo wa kuondoa msongamano Ubungo kwa watu wanaotoka barabara ya *Port Access* toka *TFDA*/Mkapa *Processing Zone* kutokea Maziwa ambayo watatumia watu waendao Magomeni, Mikocheni, Mwananyamala na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kujenga barabara muhimu zinazotokea Wilaya tofauti, Kimara – Chuo Kikuu, wanaokuja toka *Morogoro Road* kwenda Wilaya ya Kinondoni; Samaki Wabichi - Goba – Kimara na Dar es Salaam – Bagamoyo – Msata.

Mheshimiwa Spika, Ilala. Barabara ya Uhuru – Buguruni -*Port Access* ina hali mbaya sana, ndiyo maana viongozi waliokuwa wanapitishwa hapo sasa hawapitishi. Ukurasa wa 155, unazungumzia km.1, sijui hii ni kutoka wapi hadi wapi, sehemu mbovu ni zaidi ya km.1. Barabara hii siyo tu itengenezwe bali inahitaji pia kupanuliwa iwe *two line*.

Mheshimiwa Spika, *juction* ya Mandela na Buguruni iwekwe taa na ipanuliwe ili iweze kupeleka magari njia tatu – Airport, Vingunguti na Ubungo.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo *(TBA).* Kuna tuhuma nyingi kuhusu nyumba za Wakala wa Majengo, zinapangishwa wafanyabiashara badala ya wafanyakazi wa Serikali, wapo Wachina, Ndugu, jamaa ambao siyo wafanyakazi wa Serikali. Nataka nipate takwimu Wakala wa Majengo ina nyumba ngapi zinakaliwa na wafanyakazi na ngapi zimepangishwa watu wengine na kwa nini zipangishwe watu wengine au wafanyakazi wa Serikali wote wana nyumba?

Mheshimiwa Spika,TAMESA – Wakala wa Ufundi na Umeme, *Strategic Plan* ya 2005 – 2010 iliundwa *Agency* hii ihudumie nyumba za Serikali kwenye ufundi na umeme, lakini vilevile kuweka ufanisi kwenye vivuko vyetu ikiwa ni pamoja na matengenezo. Je, vivuko hivyo ajira zake zina sura ya Kitaifa? Nasikia hakuna utaifa bali ni Kimkoa kwa misingi kwamba wengi wanatoka Mkoa mmoja hasa viongozi. Nina maswali mengine na *concerns* zifuatazo:-

- Naomba nijue Watendaji Wakuu kwenye kila kivuko anatokea wapi?
- Makusanyo ya vivuko yanaenda wapi? Kwa mwaka 2010/2011 ni kiasi gani kilikusanywa?

- Ni kwa nini mpaka leo mradi wa *ticket handling machine* haujaanza au ni kweli kuwa mradi unahujumiwa kwa sababu vinatumika vitabu *pair* mbili, moja ya Serikali na nyingine ya watu binafsi?

- Nimeona mwaka 2010/2011, *Agency* ilipangiwa shilingi bilioni 1.3, je, wale walizalisha kiasi gani? Serikali ilianzisha *Agency* (Wakala) ili kupunguza mzigo wa Serikali, je, ni kwa kiasi gani Wakala hii inaisadia Serikali kimapato?

- Ukaguzi wa ndani unaonyesha shilingi bilioni 2.6 ilitumika kulipia madeni hewa, je, ni kweli na hatua gani zimechukuliwa?

Mheshimiwa Spika, fidia, ukurasa wa 152, fedha zimetengwa kwa ajili ya fidia ya *TAZARA* na Ubungo shilingi milioni 96.4, hizi ni za kulipia nini? Maana fedha hizi huenda zikaweza kulipia labda nyumba moja au hata hiyo moja isitoshe, je, Serikali kweli imepanga au kuna tarakimu zimekosewa? Wasibomolewe watu kabla ya fidia kulipwa na fidia iwe inayokubalika na pande zote mbili na fidia ikitolewa watu wapewe muda wa kutosha ili waweze kujenga nyumba nyingine lakini vilevile Serikali iwape viwanja mbadala vya kujenga nyumba nyingine.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Mbagala barabarani wamekuwa wanahangaika, *justice delayed is justice denied*. Kwa nini Serikali haitoi tamko ili wajue hatma yao na tamko la Serikali liendane na vielelezo ili suala hili lifikie mwisho. Viongozi kadhaa walishatamka kuwa watalipwa, basi Serikali iondoe huu utata na kuwawekea heshima viongozi wake. Wananchi wanahitaji kujua hatua yao, je, Serikali italipa riba, mabadiliko ya thamani na mfumuko wa bei?

Mheshimiwa Spika, mimi nalima shamba kiJiji cha Vikawe, nyumba zote zimewekewa X pamoja na Msikiti na Kanisa (vyote vina majengo makubwa) na ni mipya kabisa sasa hii barabara inajengewa akina nani? Pia kama ni fidia ilipwe haraka na maamuzi yawe ya haraka ili tusiwafunge wanaotaka kuendeleza wasifanye hivyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Watendaji wabovu. Kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu Watendaji katika Mikoa mbalimbali, Serikali iache kuleana, ichukue hatua kwa haraka ili wananchi waendelee kuwa na imani na Serikali yao.

**MHE. CHRISTOPER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, inaelelekea sasa nchi yetu imeanza kuonyesha dalili ya kuugua ugonjwa wa upendeleo katika ugawaji wa rasilimali za nchi. Dalili zipo katika sekta nyingi ila naomba kujikita kwa siku ya leo kwenye sekta ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, natambua na kuamini juu ya mpango wetu wa kitaifa wa kujenga barabara za lami kuunganisha Mikoa yote nchini. Utaratibu huu ni muhimu sana kwa maslahi mapana ya nchi ukizingatia kwamba kwa muda mrefu hatujaweza kuunganisha Mikoa mingi ya pembezoni mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Simanjiro kwa upande wa Mashariki na Kaskazini imepakana na Wilaya za Same, Mwanga, Moshi Vijijini, Hai, Arumeru na Monduli. Umbali wa kutoka Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro hadi kwenye Machimbo ya Madini ya Tanzanite Mererani ni wastani wa km 20. Kutokana na umuhimu wa kiuchumi na ubovu wa barabara hii, Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa na Rais wa Awamu ya Nne, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kwa nyakati tofauti waliahidi kujengwa kwa kiwango cha lami. Aidha, usanifu wa kina ulikamilika. Kwa mwaka wa fedha 2010/2011, ilitengwa shilingi bilioni mbili (2,000,000,000) ili ujenzi uanze kwa kiwango cha lami. Kinachoshangaza katika hotuba ya Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. John P. Magufuli sio tu haipo kwenye orodha ya ujenzi bali pia haipo kwenye orodha ya miradi iliyokamilisha usanifu wa kina wa mradi. Fedha zilizotengwa mwaka 2010/2011 hazijatolewa na ukienda kwenye Kitabu cha Maendeleo imepangiwa shilingi milioni 157 tu.

Mheshimiwa Spika, sina wivu na miradi miwili hata mitatu inapoelekezwa kwenye Majimbo ya Watanzania wenzangu. Tabu ninayoipata ni pale ambapo maeneo jirani nami tena isiyo na umuhimu mkubwa wa kiuchumi zinapopangiwa miradi mingi wakati jirani zao wakibaki kuwa watazamaji tu. Rejea Kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Dkt. John P. Magufuli 2011/2012, ukurasa 14, 15 na 28 kama mfano.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa pamoja na ahadi ya Mheshimiwa Benjamin W. Mkapa miaka 16 sasa na ahadi ya Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete ya miaka sita (6) sasa, wakati wa Kampeni ya Rais mwaka 2010, Mheshimiwa Dkt. Jakaya M. Kikwete aliahidi barabara hiyo kuanza kujengwa katika bajeti ya mwaka 2011/2012 na kuongeza kuwa barabara hiyo haitaishia Mererani tu bali itajengwa hadi Lendanai.

Mheshimiwa Spika, inakera kuona barabara inajengwa kutoka Moshi Vijijini na kuishia mpaka wa Moshi Vijijini *(TPC)* na Simanjiro. Katika bajeti ya mwaka 2011/2012, inaonekana usanifu wa barabara ya Mbauda (Arusha) hadi Losunyai hapa napo ni mpakani mwa Wilaya ya Arumeru na Simanjiro. Katika bajeti hii ya mwaka 2011/2012, nimeona ujenzi wa barabara ya Monduli Jeshini hadi Lolkisale, hapa napo ni mpakani mwa Simanjrio na Monduli. Hali hii haijengi Utaifa bali inasimika mbegu mbaya ya upendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mipango ya bajeti huwa na utaratibu mrefu kuanzia kwa wataalam hadi Bungeni, ni vizuri Waziri atazame upya mgawanyo wa barabara za Vijijini ili uwepo

uwiano kwa nchi mzima na kuzingatia mchango wa kiuchumi na wingi wa watu pamoja na ahadi za muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, narudia tuendelee na mtandao wa kuunganisha Mikoa lakini bado ni rai yangu kuwa Wilaya za wafugaji, Simanjiro na Kiteto nazo zinahitaji barabara ya lami.

Mheshimiwa Spika, ombi langu la mwisho ni kuomba Serikali itupie macho kwa haraka barabara ya Makutano hadi Butiama ambapo pana historia ya Muasisi wa Taifa letu Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere.

Mheshimiwa Spika, naomba maelezo ya Serikali.

**MHE. EUSTACE O. KATARIGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima kwa kuandaa bajeti nzuri na kuwasilisha kwa umahiri.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa uendeshaji mzuri wa Wizara na hasa kazi kubwa ngumu na muhimu ya kujenga barabara.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bugene – Nkwenda – Kaisho – Murongo – Uganda. Katika mikutano miwili kwa nyakati tofatuti Mheshimiwa Rais aliwaeleza wananchi kuwa barabara hii itajengwa kwa kiwango cha lami. Barabara hii ina "*very high traffic density*", inabeba uchumi mkubwa, inaunganisha Wilaya ya Kyerwa (mpya) na inaunganisha Wilaya ya Karagwe, inaunganisha Tanzania (kupitia Karagwe) na Uganda.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais kwenye ziara yake ya kikazi alipitia kilima hicho ambacho kipo kwenye barabara ya Bugene – Kaisho – Muronga. Tarehe 19.1.2009 aliagiza kiwekwe lami kwa jinsi kilivyo hatari. Alikumbushia tena tarehe 28.8.2010 kwenye mkutano wa hadhara pale Nkwenda. Urefu wa kilima ni kilimometa nne (4) tu. Ujenzi umeanza lakini kwa urefu wa 0.7 km. Hii ni sehemu ndogo sana, hata kilomita haitimii. Wananchi wa Kyerwa tunaomba itengenezwe angalau kwa *phase* mbili, tupeni zawadi yetu toka kwa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, kazi ya Wizara ni nzuri.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Ludewa, nampongeza Waziri Magufuli na Naibu wake Mheshimiwa Mwakyembe kwa utendaji wao mzuri wa kazi. Watanzania tunawaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ludewa ni mbovu sana na inasikitisha kuona kwamba leo Tanzania na Wanaludewa wanatimiza miaka 50 ya Uhuru bila ya kuwa na hata kipande kimoja cha lami.

Mheshimiwa Spika, katika Mkoa wa Iringa, Wilaya zote zina barabara za lami, Iringa Mjini wana lami, Iringa Vijijini wana lami, Mufindi wana lami, Njombe wana lami, Kilolo wana lami, Makete wana lami, ni Wilaya ya Ludewa tu ndio haina hata kilometa moja ya lami. Hii ni dhambi kwa Wanaludewa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba barabara ya lami kutoka Njombe hadi Manda kupitia Ludewa Wilayani.

Mheshimiwa Spika, barabara ya lami toka Njombe – Ludewa itachangia sana katika kukuza uchumi wa Watanzania kwani itakuwa ni nyezo muhimu katika utekelezaji wa miradi ya Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. SALOME D. MWAMBU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kuipongeza hotuba ya Wizara ya Ujenzi na kuunga mkono moja kwa moja.

Mheshimiwa Spika naipongeza Wizara kwa kazi nzuri, Mawaziri pamoja na Watendaji wote.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo ya kutoa tamko mapema kabla ya utekelezaji, wananchi wanahitaji wapewe maelezo mapema mfano zoezi la kuweka alama za 'X' kwenye nyumba, vibao na majengo ya Serikali. Wananchi wanapojenga, Watendaji wa Wizara huwa wanalielewa, je, kwa nini wasielimishwe mapema ili wasiharibu mali na fedha zao kujenga? Pili, Waheshimiwa Wabunge tunapata shida sana kwani hata sisi tunakuwa hatuna majibu sahihi.

Mheshimiwa Spika, wakandarasi wazawa wapewe nao tenda za ujenzi wa barabara na wakopeshwe mitaji ili kuwajengea uwezo. Tufike mahali tuache kuwapuuza wasomi wetu. Kwanza, wataongeza ajira kwa Watanzania kuliko wageni wanaajiri watu wao. Pili, wataongeza pato la Taifa fedha itabaki hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara ifanye utaratibu wa kuzichukua barabara ambazo zimeshindikana kutengenezwa na Halmashauri za Miji mfano barabara ya Iguguno – Katumbili – Lyelyembo – Yulansoni hadi Msingi. Barabara hii inapita katika bonde linalozalisha mazao vya vyakula na biashara. Wananchi wanashindwa kupeleka mazao kwenye soko. Wanalanguliwa kwa bei ya hasara. Haiwezi kutengenezeka hata miaka zaidi ya kumi ijayo, haitatengenezeka. Sijaona kama barabara hii kama imepewa mgao wa fedha, pamoja na kuiombea fedha kama ombi maalum. Naomba nipewe jibu na Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha.

Mheshimiwa Spika, katika mradi wa ujenzi wa barabara ya lami imekuwa ni hali ya kusahau zile barabara zinazoingia katika Mji, haziwekwi lami. Yaani barabara ya lami inapita nje ya Mji, mfano barabara ile ya kuingia Iguguno na kutoka haikuwekwa lami, matokeo yake magari ya abiria hayaingii ndani abiria hushushwa mbali na Mji na hii inasababisha, abiria kuporwa mali zao na vibaka, majambazi au kusababisha gharama za kulala mjini Singida. Pamoja na Mheshimiwa Rais kutoa ahadi mwaka 2008 na 2010 kuwa iwekwe lami ndogo lakini bado Wizara haijatekeleza.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri awatamkie wananchi wa Iguguno lini Wizara itatekeleza au imekataa agizo la Mheshimiwa Rais?

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchangia haya, naomba kuunga hoja asilimia 100.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, miezi kadhaa iliyopita nilipeleka barua Wizara ya Ujenzi yenye kichwa cha habari nyumba za lililokuwa Shirika la Saruji Tanzania. Barua ilikuwa na Kumb.Na.BG/MJK/03/010.

Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi katika barua husika, iliyokuwa na viambatanisho mbalimbali ni kutaka kujua mustakabali wa zilizokuwa nyumba za Shirika la Saruji Tanzania ambazo kwa mujibu wa mkataba wa mauzo zilibaki Serikalini, chini ya usimamizi wa *PSRC* na hatimaye kuhamishiwa *Tanzania Building Agency (TBA).*

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Saruji ya Wazo Hill *(TPCC Ltd)*, ni mpangaji wa nyumba za lililokuwa Shirika la Saruji, kama walivyo wapangaji wengine. Hivi karibuni wananchi wangu ambao nao ni wapangaji wa *TBA* (kwa sasa) wamekuwa wakisumbuliwa na Kampuni ya Saruji ya Wazo kana kwamba nyumba husika zimeuzwa kimyakimya.

Mheshimiwa Spika, katika maelezo yangu kwa Wizara, nikaambatanisha ushahidi ufuatao kuthibitisha ninayoyaandika ili kama kuna pahali pamekosewa hatua stahiki ichukuliwe ili kuweza kuokoa mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwanza, barua toka Wizara ya Miundombinu, Wakala wa Majengo Tanzania yenye Kumbukumbu namba. GA.114/228/01/18 ikielezea kwamba nyumba husika zimerejeshwa rasmi Serikalini kutoka *PSRC* tarehe 7 Novemba, 2007 kwa barua yenye Kumbukumbu namba PSRC/1/12/64 .

Pili, kumbukumbu ya kikao cha Waziri Mkuu na Mawaziri kuhusu uuzwaji wa nyumba za *TPCC* cha tarehe 15/02/2005, Kumb.Na.CAC 406/510/01/30 kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji *TPCC*. Pamoja na kwamba mengine barua husika inabainisha wazi kwamba kutokana na mkataba wa mauzo ya *TPCC Ltd* nyumba (*residential estate)* ziliondolewa na kukabidhiwa Shirika la Saruji Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kikao husika kilipewa taarifa juu ya utaratibu wa kupangisha eneo la makazi/nyumba *(residential estate)* kutoka katika kiwanja kikubwa (Plot 1, 4 na 7) kilichokuwa mahsusi kwa ajili ya kiwanda *(industrial plot)* chenye hati miliki namba 42336 zilikwisha kamilika lakini hatua ya kutoa hati mbili mbadala bado haujatekelezwa!

Mheshimiwa Spika, tatu, barua toka *TPCC Limited (Twiga Cement)* ya tarehe 21 October, 2007 yenye Kumb.Na.TPCC/GM/2 kwenda kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi ikimtaarifu kwamba kipande cha Ardhi namba 1, 4, na 7 *Wazo Hill* kinamilikiwa na Kampuni chini ya hati namba 42336 lakini kama sehemu ya mchakato wa ubinafsishwaji imekubalika kwamba kiwanja husika kigawanywe/kitenganishwe mara mbili na sehemu ya makazi ya watu itabaki Serikalini.

Mheshimiwa Spika, naomba nipate maelezo ya kina hapa nimeelezea sehemu tu ya viambatanisho! Kwa kuwa najua Mheshimiwa Naibu Waziri anayajua haya na nilishampa taarifa na viambatanisho vyote! Naomba nipate kauli ya Serikali kuhusiana na mustakabali wa nyumba hizo!

Mheshimiwa Spika, kuna ujenzi unaoendelea wa barabara ya New Bagamoyo (Kawawa JCT – Tegeta) yenye urefu wa km. 17. Nitumie fursa hii kushukuru kama Mbunge wa Jimbo husika na kupongeza kwa kuwa kukamilika kwa barabara hii kutasaidia sana kupunguza msongamano wa magari katika barabara hii.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa hotuba ya Waziri jumla ya shilingi milioni 88.619.20 zimetengwa zinazojumuisha ujenzi, malipo ya fidia na kuhamisha huduma za jamii kwenye eneo la ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na sintofahamu miongoni mwa (baadhi ya) wananchi kuhusiana na malipo ya fidia. Naomba nipate maelezo toka wa Waziri juu ya mchakato mzima wa malipo ya fidia kwa walioathirika, utagharimu kiasi gani na malipo hayo yataanza kutolewa lini.

**MHE. CHRISTINA L. MUGHWAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata fursa hii ili nami nitoe mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuzungumzia kero kubwa ya msongamano katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, wakazi wa Jiji la Dar es Salaam wanapata usumbufu mkubwa wa usafiri kutoka eneo moja hadi lingine kutokana na miundombinu finyu ya barabara na isiyokidhi mahitaji ya usafiri katika Jiji hilo. Muda mwingi sana hupotea barabarani kutokana na msongamano wa magari, watu wanachelewa sana kufika sehemu zao za kazi jambo ambalo linaathiri sana uchumi wa nchi ukizingatia kuwa Dar es Salaam ndiyo Jiji lenye wakazi wengi na shughuli nyingi za uchumi.

Mheshimiwa Spika, natambua kuwa Serikali iko katika mchakato wa kuleta mradi wa mabasi yaendayo kasi, mradi ambao hata hivyo umechukua muda mrefu sana kukamilika. Kinachoshangaza ni kuwa mradi huu wa mabasi yaendayo kasi utafanikiwa vipi ilhali barabara ni finyu? Mabasi haya yatapita katika njia zipi ili yaende kasi?

Mheshimiwa Spika, wakati nchi zinazoendelea zinatumia usafiri wa treni ziendazo kasi katika Miji Mikuu, kwa nini sisi tunafikiria usafiri wa mabasi ambao hautatuondelea tatizo la usafiri katika Jiji letu Kuu? Kwa nini Serikali isifikirie usafiri wa treni katika Jiji la Dar es Salaam kwani baadhi ya miundombinu ya treni tayari ipo na haitumiki mfano njia ya reli inayotoka katikati ya Jiji hadi Ubungo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali pia ifikirie usafiri wa majini ili kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. Wakazi wa vitongoji vya Bunju, Boko, Mweni na Tegeta wanaweza kutumia usafiri wa boti kufika katikati ya Jiji.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuzungumzia suala la bomoabomoa inayotekelezwa na Wizara hii ya Ujenzi ili kupisha miradi ya barabara. Pamoja na nia njema ya jambo hili, bomoabomoa imesababisha hasara na umaskini mkubwa kwa wananchi waliokumbwa na zoezi hilo.

Mheshimiwa Spika, limekuwa ni jambo la kawaida kwa Serikali yetu kuwabomolea na kuwahamisha wananchi bila kuwalipa fidia wanayostahili. Naiomba Serikali isiwe inachukua hatua ya kuwabomolea na kuwahamisha wananchi ilhali wakijua kuwa hakuna hela ya kuwafidia wananchi.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wangu wa Singida hivi sasa unaunganishwa na Barabara Kuu za kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza na ile ya kutokea Arusha hadi Mwanza. Hizi ni Barabara Kuu ambazo kwa kiasi kikubwa zitachochea uchumi wa Mkoa wa Singida. Niiombe sasa Serikali iziangalie barabara za ndani na za Vijijini za Mkoa huu ambazo hazijaguswa kabisa katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Singida ambao ni Mkoa ulio nyuma sana kimaendeleo wanahitaji kupewa kipaumbele katika miundombinu ya barabara zake hasa za Vijijini ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi. Kipekee naiongelea barabara kutoka Ikungi hadi Londoni ambako kuna machimbo ya dhahabu na barabara hii ina matumizi makubwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukuwa nafasi hii kuipongeza Serikali kwa juhudi zake katika ujenzi wa barabara nchini, chini ya Waziri, Naibu Katibu Mkuu wa Naibu wake pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo, nina machache ya kuchangia ili kuboresha maendeleo ya nchi yetu. Barabara ni mtandao ambao unakuza na kuboresha uchumi na kuongeza au kusukuma maendeleo ya wananchi na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam na Miji mingine kama Mwanza, Arusha inakabiliwa na tatizo kubwa la msongamano wa magari. Hii pengine inatokana na kuathiriwa kwa miundombinu ya barabara ambazo Serikali ilichelewa kuziboresha hadi Miji imezidi kukua. Je, ni lini italetwa mipango na bajeti ya Wizara hii itakayoonyesha ni lini ujenzi wa barabara za kisasa *(flyovers)* utaanza kwa Mkoa wa Pwani, naomba nipatiwe majibu.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo gani katika ujenzi wa kilomita 60 za barabara ya Ndundu – Somanga? Suala la kila baada ya muda kusogezwa tarehe ya kumalizika ujenzi huo zinadumaza maendeleo ya Mikoa ya Lindi, Mtwara na sehemu ya Mkoa wa Pwani. Naomba niambiwe tarehe ya uhakika ya kumalizia ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, miundombinu na ujenzi wa barabara za lami kwa Mkoa wa Pwani ambao una Wilaya za Rufiji, Kibaha Mjini na Vijijini, Mafia, Kisarawe, Bagamoyo na Mkuranga unasuasua sana au kama haupo. Je tatizo ni nini? Naomba maelezo.

Mheshimiwa Spika, kuna ujenzi wa barabara unaotarajiwa kujengwa kwa Wilaya ya Mafia na kuna baadhi ya nyumba ambazo zimewekwa alama ya kuonyesha nyumba hizo zitabomolewa, Je, kwa nini mpaka leo wananchi hao ambao nyumba zao zimewekwa alama hawajui ni kiasi gani na lini watalipwa au ujenzi huo utaanza? Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na usomaji mahiri. Pia nawapongeza Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya bajeti.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri na kasi ya utekelezaji wa miradi iliyoahidiwa na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015. Katika Wilaya ya Bagamoyo ujenzi wa barabara ya Bagamoyo – Msata kwa kiwango cha lami unaendelea kwa kasi lakini mradi ambao tuna shida nao sasa ni ujenzi wa barabara ya Mkuranga – Saadani – Pangani – Tanga. Ujenzi wa barabara hiyo kwa kiwango cha lami umeahidiwa katika Ilani. Kwa changamoto za bajeti, najua ujenzi wa barabara hii hautaweza kutekelezwa mara moja lakini mategemeo yetu ni utekelezaji wa awamu. Matarajio yetu yalikuwa ni tengeo katika bajeti ya mwaka huu kwa ajili ya ujenzi wa madaraja na hasa ujenzi wa daraja la Wami katika barabara hii ya Mkuranga – Saadani – Pangani – Tanga. Hicho ndicho kiungo kikubwa cha usafiri katika barabara hiyo. Napenda kupata maelezo ya Wizara juu ya mpango wa ujenzi wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. PEREIRA A. SILIMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia kwenye hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niipongeze Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya, hongera! Pamoja na pongezi hizo, naomba nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ni suala la uwezeshaji *(empowerment)* wa Makandarasi wazawa. Pamoja na jitihada zilizopo za kuwawezesha Mainjinia wazawa, bado naomba jitihada za kuwawezesha na kuwajengea uwezo ziongezwe. Nasema hivi nikijua faida kubwa ya jambo hili kiuchumi na uhaulishaji wa teknolojia.

Mheshimiwa Spika, pili, ni udhibiti kwenye *weighbridges*. Ujenzi wa barabara ni wa gharama kubwa na Serikali yetu inatumia hela nyingi sana kwa ujenzi. Kwa umuhimu huo, Serikali imeweka miundombinu kuwa ni kipaumbele cha kwanza. Kuna tatizo kubwa katika utunzaji wa barabara zetu kazi ambayo ingerahisishwa kwa kupima uzito wa mizigo kwenye vituo vyetu.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba vituo hivi havijatimiza madhumuni ya uwepo wao baada ya kuona barabara nyingi zinachimbika na kuharibika kutokana na magari kuzidisha uzito. Bado kuna matatizo kwenye vituo hivi na kuna dalili ya upokeaji wa rushwa. Hatua lazima zichukuliwe ili kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, tatu ni barabara mkakati. Ili nchi yetu ipate faida ya kila barabara inayojengwa, ni lazima tujenge barabara baada ya kuridhika kwamba barabara hizo ni za kimkakati na kichocheo halisi cha kufungua maeneo mengine. Pamoja na kuingiza siasa jambo hili, bado kigezo cha kimkakati kitumike katika kuamua barabara ipi ijengwe kabla ya ipi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kutoa masikitiko ya wananchi wa Jimbo langu kuhusu bomoabomoa na alama za 'X' zilizotanda katika maeneo yao. Masikitiko ya wananchi ni makubwa katika suala hili na kwa kweli bomoabomboa inasababisha chuki kubwa sana kwa Serikali ya CCM na CCM yenyewe. Kuna haja kubwa ya kuliangalia upya jambo hili na kutumia hekima na busara katika kulitekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na bomoabomoa, lipo tatizo la fidia kwa wale wanaobomolewa nyumba zao. Fidia inayolipwa haikidhi haja, inalalamikiwa na wananchi wengi. Kuna haja ya kuangalia upya vigezo vinavyotumika katika kuandaa fidia kwa wananchi husika.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *TANROADS* kwa kazi nzuri wanayoifanya ikiwa ni pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *TANROADS* Mkoa Singida. Kinachokwamisha utendaji mzuri ni fedha za bajeti hazipelekwi kwa wakati wake au kukosa kabisa kupelekwa Mkoani na kusababisha kero na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi. Naomba fedha zipelekwe katika wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, narudia kushukuru kwa kuipandisha daraja barabara ya Mwankokoro – Mtunduru – Mgungira hadi Iyumbu kuwa ngazi ya Mkoa. Hata hivyo, barabara hii inahitaji matengenezo mapya pamoja na madaraja matatu muhimu, kutenga fedha za ukarabati haitoshi kwani hii ni barabara mpya. Naomba sana barabara hii itengewe fedha za kutosha ili iweze kupitika kwa mwaka mzima kwani barabara hii inaunganisha Mkoa wetu na Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Spika, kuna malalamiko mengi kuhusu ujenzi wa barabara za Wilayani na Vijijini na ni kwa sababu ya utaalam mdogo na uhaba wa fedha lakini pia upo ubadhirifu mkubwa wa fedha, mara nyingi *value for money* haipatikani. Ushauri wangu ni kuanzisha Wakala/*Agency* itakayoshughulikia barabara za Wilayani na Vijijini ambayo itakuwa na wataalam na fedha za kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, tatizo la Makondarasi kujenga barabara chini ya viwango linasikitisha sana na linaendelea siku hadi siku, hivi tatizo ni nini? Kwa nini Serikali inawalinda?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuipongeza sana Wizara hii kwa kazi nzuri inayofanyika. Nashukuru pia jitihada za Wizara katika kuziona barabara za Igawa – Ubaruku – Mbarali na barabara ya Rujewa – Madibira – Mafinga. Nawashukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kuzipa kipaumbele barabara hizo nilizozitaja kwa kuzipangia fedha kwa kiwango cha lami. Naomba chondechonde barabara hizo ni muhimu kwa kusafirisha mazao ya wananchi kutoka mashambai/viwandani, kupeleka mchele mzuri unaolimwa Kata za Rujewa, Ubaruku, Songwe, Imalilo na Kata ya Madibira.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi nilizotoa, bado yapo matatizo makubwa ya mtandao wa barabara Wilayani Mbarali. Barabara hizo zimeombewa fedha na Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali kwa vile ni muhimu sana kwa kusafirisha mazao ya Mpunga kwenda sokoni na maeneo mbalimbali ya nchi kwenye upungufu wa chakula. Barabara zenyewe ni barabara za ndani ya Wilaya, barabara ya Itipingi – Kangaga km.14, imeombewa shilingi milioni 40. Manienga – Matemela - Ipwani – Luwango – Ibengele, imeombewa shilingi milioni 45, hizi zipo Kata ya Mawindi na Ipwani. Kata ya Mahongole – Igalako – Mwatenga – Kilambo, km.10 zimeombewa shilingi milioni 50. Kata ya Rujewa, barabara ya Rujewa – Nyeregete, kurekebisha madaraja, zimeombwa shilingi milioni 25. Kata ya Mapogolo, barabara ya Ukwavila – Ifushilo/Mapelemehe barabara ya kuelekea maeneo ya mashambani zimeombwa shilingi milioni 30. Kata ya Mlombweni, barabara ya Mapogoro – Magigiwe km. 6 zimeombwa milioni 35. Kata ya Utengule/Luhanga, barabara ya Igurusu – Utengule – Luhanga – Madundasi imeanza kutengenezwa na *TANROADS* lakini kazi haiendelei kwa sababu ya kukosefu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ni muhimu sana kwa kusafirisha mazao kutoka mashambani lakini zimepangiwa bajeti ndogo sana. Naomba Serikali isaidie fedha zinazotumwa Wilayani Mbarali walau ziongezeke ili barabara hizi ziweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Spika, nawatahadharisha Waheshimiwa Mawaziri wasikubali kubomoa nyumba za watu eti walijenga ndani ya eneo la barabara. Ni kweli lakini makosa yapo pande zote, Serikali haikuwaona wanapojenga? Msikubali kupongezwa kwa hili lina laana. Manung'uniko ya watu maskini ambao wamevunjiwa nyumba zao hata kama sheria itawabana lakini machozi yao ni chukizo kwa Mwenyezi Mungu, hamtakuwa salama. Wabomolewe nyumba zao hakuna ubishi ili kuboresha barabara lakini walipeni. Mawaziri hawa wapo juu sana lakini hili litawachafualia, Chama kitachafuka na Serikali pia kumbukeni hizi ni zama za ushindani. Sisi tunapokea maoni ya watu wengi, mtuamini, ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, sikubaliani na hoja hii kutokana na sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa barabara kutoka Musoma – Makutano – Butiama – Nyamuswa - Natta - Fort Ikoma – Mugumu - Mtu wa Mbu – Loliondo (maarufu Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo) Mto wa Mbu, bado halijapatiwa ufumbuzi. Serikali naona bado inasuasua. Tanzania ni nchi huru kwa nini basi watu wa nje watuzuie kujenga barabara ya lami kutoka Butiama kwenda Mto wa Mbu kupitia Serengeti? Ninao ushahidi kwamba nchi jirani (Kenya) inapanga *campaign* chafu barabara hii isijengwe eti kwa kuwa wanyama Serengeti wataathirika. Barabara hii hayati Mwalimu Nyerere aliipigia kelele ijengwe kwa kiwango cha lami bila kujali kelele za Wakenya, Marekani au Wajerumani. Waziri Magufuli aliwahi kuambiwa na Mwalimu Nyerere barabara hii lazima ijengwe. Leo ni miaka 11 bado barabara hii haijajengwa. Inaonekana wazi kwamba Serikali imekuwa legelege kwa suala hili.

Mheshimiwa Spika, iwapo Wazungu na Wakenya wanawapenda wanyama wa Serengeti kiasi kikubwa hivyo basi kwa nini wasijenge *Tunnel* lenye urefu wa kilometa 54 kwenye eneo la utata Mbugani ili barabara ipite chini na kuwaaachia wanyama kupita juu bila kuathirika? Kama wazo la kujenga *tunnel* litakubalika basi hizo fedha ambazo zingetumika kujenga *tunnel* zitakuwa mbadala, kwa nini zisitumike kujenga barabara ya Mugumu – Sirori – Simba (Kiagata) hadi Kirumi?

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri kuhusu urefu wa barabara hiyo yaani Makutano – Natta – Mugumu – Loliondo – Mto wa Mbu ina makosa makubwa kiasi kwamba haieleweki barabara hii ina urefu gani. Je, ni kilometa 452 kama inavyosomeka *paragraph* 49 ukurasa 28 au kilomita 328 kama inavyosomeka ukurasa wa 63 *paragraph* 113?

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri anasema "Katika mwaka wa fedha 2011/2012, jumla ya shilingi milioni 791.50 fedha za ndani zimetengwa kwa ajili ya kukamilisha usanifu na shilingi milioni 843.31 kwa ajili ya maandalizi ya kuanza ujenzi wa lami kwa sehemu ya Makutano - Natta (km 50)". Urefu anaousema Mheshimiwa Waziri si sahihi. Urefu wa barabara kutoka Makutano hadi Natta ni kama ifuatavyo:- Makutano – Butiama (Km.18.966), Butiama – Nyamuswa (Km.17.196), Nyamuswa – Mgeta (Km.23.6) na Mgeta – Natta (Km.29.9), jumla ni Km.89.9. Sasa kama Waziri hajui urefu wa barabara nzima ni kilomita ngapi wala urefu wa barabara Makutano – Natta, je, hotuba hii kweli ni sahihi kutokana na upungufu niliouainisha hapo juu? Sioni kwa nini niunge mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, bajeti hii pia haikuwatendea haki wananchi wangu wa Musoma Vijijini. Ni mwaka jana ambapo Waziri Magufuli akiwa Waziri wa Mifugo aliwaahidi wananchi wangu wa Bwai Kaitururu (Mugango) baada ya kuona shida ya usafiri kwenye barabara ya kutoka Musoma – Busekela (Majita) kwamba barabara hiyo inahitaji ujenzi upya. Mheshimiwa Magufuli aliniahidi angefanya kila njia tupate barabara bora, je, ahadi hii mbona haijatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, pia Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete alipotua na helkopta huko Nusekela Majita, aliwaahidi wananchi wangu kwamba barabara ya Musoma – Mugango – Muranga – Busekela inahitaji ijengwe kwa kiwango cha lami. Je, ahadi hizi zitatekelezwa lini?

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwa sababu nilizozitoa sioni kwa nini niunge mkono hoja hii.

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Spika, kivuko cha Mto Kilombero ni kibovu huwa kinasumbua sana, mara kwa mara kinahatarisha maisha ya watumiaji. Napendekeza Wizara ikifanyie ukaratabi wa kina kivuko hiki au kinunuliwe kipya. Tusisubiri mpaka watu wapoteze maisha ndio tuchukue hatua. Thamani ya maisha ya wanadamu ni kubwa kuliko kisingizio cha fedha Serikali inachotoa.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete mara mbili ameahidi kukamilisha ujenzi wa Daraja la Mto Kilombero. Nimestushwa na bajeti iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa daraja hili eti shilingi bilioni moja kwa ajili ya daraja hili wakati daraja hili linahitaji kiasi cha shilingi bilioni 45. Kutengewa shilingi bilioni moja ni usanii mtupu. Hivi shilingi bilioni moja *out of* 45 zitafanya nini? Magufuli *be serious on this.*

Mheshimiwa Spika, Wizara imefanya usanii mwingine kwenye barabara aliyotuahidi miaka nenda rudi kuwa itajengwa kwa kiwango cha lami, eti sasa hivi imetengewa shilingi milioni 200 kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Mkamba (Kidatu) *to* Ifakara. Hivi shilingi milioni 200 inajenga nyumba au barabara ya kiwango cha lami? Magufuli acha usanii *once again*. Milioni 200 zinajenga barabara ya kilomita ngapi na ya aina gani?

Mheshimiwa Spika, hivi huo ujenzi wa nyumba Kilombero hawazihitaji? Mbona sijawahi kuona nyumba zozote zikijengwa Wilayani kwetu?

Mheshimiwa Spika, napenda kujua hivi ni vigezo gani vilivyotumika kuamua ugawaji wa fedha kwenye ujenzi wa barabara na madaraja?

Mheshimiwa Spika, msongamano Dar es Saalam ni kero ya muda mrefu. Ujenzi wa *DART* uharakishwe.

Mheshimiwa Spika, nini hatma ya UDA?

**MHE. SALIM HEMED KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii muhimu. Naomba waendelee na kazi hiyo hiyo au wazidishe kidogo ili malengo ya Wizara yafikiwe kwa urahisi na kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu miradi ya barabara, malengo ya Wizara ni pamoja na kuunganisha Miji Mikuu yote ya Mikoa kwa barabara za lami ifikapo mwaka 2017/2018, haya ni malengo makubwa lakini yanayohitaji fedha nyingi ambazo Serikali haina. Napendekeza Serikali ikope katika Taasisi za Fedha za ndani na nje ili ijenge barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubora wa barabara zetu, nyingi zinajengwa chini wa viwango hivyo tunapoteza bure rasilimali chache za Taifa hili. Naiomba Serikali isizikubali barabara ambazo Makandarasi wameboronga na Wakandarasi hao warudishe hela waliyopewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam lina msongamano mkubwa wa magari kutokana na barabara za ndani (*feeder road*) kuwa hazipitiki. Inawezekana barabara hizo ni za Halmashauri lakini kwa kuwa uwezo wao ni mdogo, jukumu bado linabaki kwa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majengo, Tanzania bado haijapiga hatua kubwa katika majengo makubwa hasa katika Miji Mikuu kama Dar es Salaam, Mwanza, Arusha na kadhalika. Usanifu wa majengo bado haupendezi. Mahali ambapo panatakiwa majumba ya *“vertical”* tu (yaani magorofa) kunaruhusiwa kujengwa nyumba ndogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Wabunifu Majengo, tunataka Wabunifu Majengo wenye sifa sio wenye vyeti tu. Tatizo la wataalam wengi wanadangaya. Majengo yanaporomoka ovyo kwa kukosa utaalamu. Sasa lazima tubadilike, mipango yetu iendane na ubora.

Mheshimiwa Spika, barabara za changarawe ziwe ni kwa muda mfupi tu kwa sababu zinahitaji matengenezo ya kila mwaka hivyo kupoteza rasilimali nyingi za Taifa.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ya kuhakikisha kuwa barabara zetu zinajengwa kwa kiwango cha lami. Nampongeza Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Harrison Mwakyembe, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Dodoma – Babati yenye urefu wa Km.261 zimetengewa shilingi milioni 10,226.41 tu kwa mwaka huu wa fedha na fedha zilizotengwa zitatumia kujenga km.62 kati ya km.261. Hata hivyo, pesa zilizotengwa haziwezi kukamilisha ujenzi wa km.62 hizo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009/2010 zilitengwa shilingi bilioni 42 hazikufanya kazi yoyote; mwaka 2010/2011 zilitengwa shilingi 9,564,500,000, kadri miaka inavyosogea mbele thamani ya shilingi inashuka barabara hii pia inazidi kupangiwa kiasi kidogo cha fedha. Serikali ione aibu kujenga barabara hii yenye historia ya kipekee kwa kusuasua (*The Great North Road*).

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu aliagiza Wizara zianze kujenga majengo yao Dodoma ili kuiwezesha Serikali kuhamia Dodoma. Je, Waziri, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli haoni kuwa anakaidi agizo hilo kwa kujenga nyumba 28 za Serikali Jijini Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa kuanzisha Bodi ya Mfuko wa Barabara. Bodi hii inafanya kazi kubwa ya matengenezo ya barabara zetu pamoja na ufinyu wa bajeti. Naishauri Serikali kuiongezea fedha Bodi hii ili iweze kukamilisha malengo yake.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Ujenzi inawasababisha Watanzania wanaosafiri kwa kutumia barabara kuchafua mazingira. Siamini kuwa Wizara imeshindwa kujenga vyoo kandokando ya barabara kuu ili wasafiri wasiendelee kuchafua mazingira kwa kujisaidia ovyo pembezoni mwa barabara.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msongamano wa magari Dar es Salaam ni kubwa na la muda mrefu. Kila siku magari yanashushwa bandarini, miundombinu ya Dar es Salaam ni ileile; ni zaidi ya miaka kumi Serikali imekuwa ikiahidi kupunguza msongamano wa magari kwa kujenga barabara za *flyovers;* mabasi yaendayo kasi, njia ya reli; usafiri wa boti na kadhalika. Tumechoka kusikia mipango na mikakati, wakati ufike sasa wa kuona utekelezaji. Watanzania wanatarajia kuona miradi yote hiyo ikitekelezwa. Katika nchi nyingine watu binafsi au Makampuni binafsi hutengeneza barabara kisha hutoza kiasi kidogo kwa watumiaji kwa ajili ya kurudisha pesa zao kisha barabara hukabidhiwa kwa Serikali, kwa nini tusifanye hivyo kwa kusaidia ukuaji wa haraka wa uchumi wetu?

Mheshimiwa Spika, Serikali itukumbuke katika barabara ya Mpwapwa Gulwe – Kibakwe – Chipogoro. Barabara hii ni mbaya mno kwa sababu haipitiki kabisa. Hivi karibuni gari limepinduka kutokana na ubovu huo; maeneo hayo yana mazao mengi mno hivyo wakulima wanashindwa kufikisha mazao yao kwenye soko.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko, napenda kuelezea hisia zangu juu ya mgawanyo wa ujenzi wa barabara kwa Mikoa na Wilaya hata Majimbo. Nimejaribu kupitia Kitabu cha Hotuba ya Wizara hii kwani ukipitia mgawanyo wa miradi ya ujenzi wa barabara utagundua upendeleo mkubwa uliotumika katika *allocation* kati ya Mikoa na Mikoa, na utaona Mikoa ambayo mingi inaongoza katika kuzalisha mazao ha hata ile yenye rasilimali zenye kuleta fedha katika kukuza uchumi wa nchi yetu kama madini, bado zimeachwa kando kabisa. Cha ajabu Mikoa ambayo tayari ilishapata vipaumbele hapo nyuma bado imeachwa kando.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kujua ni vigezo gani vimetumika kwani hata mgawanyo wa ujenzi wa barabara kati ya Wilaya na Wilaya ndani ya Mkoa pia kumeonyesha *bianess* kubwa sana. Hata ndani ya Jimbo, mgawanyo wa barabara ndani ya Jimbo ume-*favour* sehemu wanazotoka viongozi (Mbunge) na katika ngazi ya Wilaya na Mkoa ime-*favour* zaidi sehemu ambazo wanatoka viongozi wa Serikali na maswaiba wao. Hii inatia fedheha sana na walakini na sintofahamu kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia kwenye hili, naomba ku-*site case* ya Mkoa wa Mara ambapo nitafanya *comparison* kati ya Mkoa na ndani ya Mkoa. Ndani ya Mkoa wa Mara Mgawanyo umekuwa *very biased* kati ya Wilaya na Wilaya na hata pia ndani ya Jimbo mgawanyo huu pia umeonyesha vipaumbele vyake, hivi vimezingatia vigezo gani kwani kuna maeneo ambayo ndio kitivu cha uchumi katika sehemu husika na nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mgawanyo wa Jimbo la Tarime, Wizara imetenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa barabara ya Nyamwaga – Mumba - Itinyo – Kagonga *Road* ambayo ipo

katika kiwango cha changarawe na mabonde ni mengi kuliko maelezo. Cha ajabu hii barabara walau imeshatengenezwa kwa kiwango hadi cha changarawe, ndio barabara pekee kwenye Jimbo ambayo imejengwa ili kuunganisha Jimbo kwa maana ya kutoka Makao Makuu ya Jimbo kwenda kwenye viunganishi vya Jimbo au Tarafa na Kata ambapo ndipo uchumi wa Jimbo kwa maana ya uzalishaji wa mazao na shughuli nyingine kama mbao na madini na hivyo kuweka umuhimu wa kuwa na miundombinu mizuri ili kuweza kusafirisha mazao, mifugo na binadamu na iweze kupitika kwa kipindi chote kwa maana ya wakati wa kiangazi na masika.

Mheshimiwa Spika, barabara ambayo inakarabatiwa ni ambayo inaelekea sehemu ambayo Mbunge wa Jimbo Mheshimiwa Nyambari Chacha Nyangwine anatokea na hata *biasness* hii niliona kwenye mgao wa umeme pia ulipelekwa maeneo hayohayo. Sasa hapa swali ni je sehemu zingine za Jimbo hazina sifa hizi za kupewa miundombinu ya babaraba na umeme? Maana maeneo tajwa ni yale ambayo pia Mheshimiwa Mwera alikuwa akitoka na sasa Mheshimiwa Nyangwine. Swali *allocation* ya kutengeneza au kujenga hizi barabara haizingatii *basic creteria* ambazo wataalam wa Wizara husika wakati wa *allocation* au wanatumia zaidi *technical know who* na sio *know how?* Yaani zaidi ni *lobbying* na kujuana? Hivi jamani sehemu kama Nyamongo barabara ya Nyamwanga inapita na kwenda Muiba hadi Itonyo bila aibu ya ku-*divert* na kwenda hadi Nyabigena – Kemanja hadi Nyamongo maana hali pale ni mbaya na ni barabara iendayo mgodini lakini inasitikisha sana tena sana. Naomba majibu.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wakazi ta Tarime na wananchi wa Tanzania wote wanaofanya shughuli za maendeleo katika Jimbo la Tarime, naomba Wizara itamke ni lini wataweka na kutengeneza barabara ya Nyamwaga ambayo inaanzia Tarime Mjini - Nyamwaga – Nyamongo hadi Mto Mara na ukizingatia uwekezaji yaani *Barrick African Gold Mines* alishaonyesha utayari wake kujenga hii barabara iwapo Serikali itasaidia kufanya upembuzi yakinifu. Hivyo pamoja na upungufu huo, naomba Wizara isaidie sana kuhakikisha barabara hii inajengwa.

Mheshimiwa Spika, pili, Mheshimiwa Magufuli, Waziri alishaahidi kuwa ataingiza kwenye mpango wa bajeti ya mwaka huu barabara ya kuanzia *Security Road* - Rorya – Susani – Mwema – Nyantira hadi Kegonga. Hii itasaidia sana kwa uchumi wa Tarime na Rorya. Barabara hii inaweza kuanzia kujengwa kuanzia Rorya – Susani – Mwema – Sirani. Naomba majibu katika majumuisho ya Waziri kama barabara hizi mbili zitawekwa lami.

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kuna hizi barabara bado hazipo katika hadi ya kuwa chini ya *TANROADS,* zipandishwe ili ziweze kukarabatiwa ili kuinua uchumi wa Jimbo la Tarime kama viunganishi vya Tarafa na Kata husika na Mji wa Tarime ambapo ni Makao Makuu ya Halmashauri ndogo ya Mji. Pia ni viunganishi na Jimbo la Rorya na nchi jirani ya Kenya.

Mheshimiwa Spika, barabara ambazo naomba zipandishwe daraja au kama zipo chini ya *TANROADS* basi zitengenezwe walao hata kwa kiwango cha changarawe kwani wakazi wa maeneo haya wanateseka sana na ubovu wa barabara hizi. Hivyo, naomba sana barabara ya kuanzia Magena kupitia Nyandoto – Karotambe – Kiongera – Nabirongo – Kijiweni hadi Rorya (Nyanasanda); pia barabara hii ni muhimu sana na haipitiki kwa uharibifu uliopo na ukizingatia wananchi wa Susani na Mwema wenye kutoka koo za Wanchari ikitokea kukawa na vita za koo za Warenchoka na Wanchari basi mawasiliano yanakatika kati ya Waanchori na Tarime Mjini kwani hutegemea barabara ya Security Road - Rorya – Susan – Sirari ambayo walau ipo katika *level* ya changarawe. Barabara hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, vilevile barabara nyingine ni ile ya kutokea Msati kupitia Nyandoto – Malale – Kikomoni – Matamakwe hadi Songambele kwenye soko kubwa lililopo Kata ya Susani ambapo Wanatarime wengi na Wakenya huja mnadani kila Jumapili na Alhamisi. Hii ni muhimu sana enzi za miaka ya themanini na tisini ilikuwa ikitumika lakini baadaye ikatelekezwa na hasa daraja la mto Mlale ndilo linalotesa maana lile la mto Moni limeshajengwa ambalo hupeleka na kuuwa watu wanaopita eneo lile wakati wa masika.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kuwa kuwepo na *strategy* ya kuboresha barabara za Vijijini ili kurahisisha usafirishaji wa mazao kutoka kwenye *production source* hadi kwenye *warehouses* ambapo ndipo pa kuuzia mazao au bidhaa zingine.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu utengenezaji wa *flyover* ili kuondoa *congestion* kwenye miji mikubwa kama Dar es Salaam ambapo nchi hupoteza mapato makubwa na kupunguza *production rate* kwenye kazi na pia matumizi makubwa ya mafuta. Tunaweza kuiga hata nchi jirani ya Kenya, Nairobi, nilipotembelea juzijuzi hapa niliona kweli wana dhamira ya kweli. Hivyo Serikali ni bora iwe na dhamira ya kweli na siyo *quantification* tu ya *figure* na maneno mazuri ambayo huishia kwa nadharia kila mwaka. Uchumi wa nchi utakuwa tu kama miundombinu ya barabara itaboreshwa vizuri. Tukumbuke kama Wizara hii ndiyo *a major pillars* na *heart* ya Wizara zote na pia ndio inachangia uchumi mkubwa sana kwa nchi yoyote ile. Hivyo ni bora itazamwe kwa jicho hili muhimu la kuwa *backbone* ya huduma nyingine kwani bila barabara imara *no movement from one point to another.* Ukienda hospitali lazima upite barabarani, shuleni, ofisini na hata shambani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza sana Waziri wa Ujenzi pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kujenga barabara zetu vizuri bila ya ubaguzi. Barabara zinajengwa kila Mkoa wa Tanzania, hivi sasa kuna Wakandarasi na wanaendelea na ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ni Wizara chachu kwa maendeleo ya sekta nyingine. Wizara hii ni Wizara ambayo inafanya kazi nzuri na ni tegemeo kubwa katika nchi yetu, kwani ikiwa hakuna barabara kunakuwa na usumbufu mkubwa wa usafiri kwa watu na hata mizigo. Wakulima wengi wanazalisha mazao mengi katika maeneo yao, lakini wanashindwa kuyapeleka masokoni kwa sababu ya kukosa usafiri, barabara zikiwa mbovu shughuli za maisha zinashindwa kufanyika, maisha yanakuwa magumu kwani magari yanashindwa kufika katika maeneo yao na wananchi wanapata tabu ya usafiri na mizigo yao.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali barabara za Jiji la Dar es Salaam zipelekwe kwenye *TANROADS* kwani Halmashauri ya Jiji wameshindwa kuzitengeneza pamoja na kuzishughulikia. Imekuwa ni aibu kubwa kwani ni Jiji ambalo lina wakazi wengi na pia wageni wengi sana. Nchi yetu inapata aibu kubwa kwa wageni wanaokuja nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho namalizia kwa kusema kuwa *TANROADS* wana uongozi ulio makini sana, wachapa kazi nzuri sana na ni wa kuigwa mfano katika utendaji wao wa kazi.

**MHE. KULUTHUM J. MCHUCHULI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kuleta katika Bunge lako Tukufu hotuba ya Wizara ya Ujenzi ili nasi Waheshimiwa Wabunge tupate kuchangia ili kuboresha hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia katika vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, ubora wa barabara za lami zinazojengwa. Kumekuwa na malalamiko mengi kuwa barabara nyingi kuu zinazojengwa kuwa zipo chini ya kiwango, hili tumelishuhudia katika barabara za Kilwa Road, kutoka maeneo ya Bandari hadi Mbagala ambapo barabara hii baada ya kutumika kwa muda mfupi tayari imeanza kuharibika.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kuna sababu nyingi zinazopelekea barabara kujengwa nchini ya kiwango ikiwepo ya Wakandarasi Washauri kutosimamia vizuri ubora wa kazi zinazofanywa na Mkandarasi husika aliyepewa dhamana ya kujenga barabara kwa sababu ya kutopewa malipo yake kwa wakati. Je, Serikali inawaeleza nini Watanzania wanaosubiri kwa muda mrefu kupata barabara bora kwa ajili ya kuwapunguzia adha ya usafiri kama wananchi wanaoishi maeneo ya Mbagala? Je, Serikali imeshidwa kusimamia vizuri mipango yake inayopanga yenyewe?

Kuhusu mizani za barabarani, tunatambua umuhimu mkubwa wa kuwepo kwa mizani za kupima uzito wa magari barabarani lakini mizani hizi kwa sasa zinaonekana kama hazina tija kwa sababu kumekuwepo na tuhuma nyingi za rushwa kwa watumishi wanaofanya kazi katika vituo hivi. Kwa mfano, gari inatambulika kuwa inazidisha uzito lakini kinachofuata ni mwenye gari kutoa rushwa na kuruhusiwa kuendelea na safari ili lizidi kuendelea kuleta uharibifu badala ya kutozwa faini na kupunguza sehena ya mzigo ambao umezidi. Sasa je, Serikali inawaeleza nini wananchi juu ya uharibifu wa barabara unaendelea kwa makusudi kutokana na usimamizi mbovu wa watendaji wake? Nashauri Serikali iboreshe haraka teknolojia za kisasa ambazo zitawezesha ufuatiliaji wa kina wa utendaji wa vituo vya mizani kutoka Makao Makuu ili vitendo vya rushwa vikomeshwe.

Suala lingine, matuta barabarani ni muhimu sana kwa ajili ya kupunguza mwendo kasi wa magari hasa katika maeneo ya watu wengi na kwenye miteremko mikali. Ushauri wangu ni kwamba pawepo na vipimo maalum vya matuta na aina maalum kwa nchi nzima kwa sababu matuta mengi ni makubwa sana na matuta aina ya *chips* yanaharibu sana kwa mfano katika kiJiji cha Mwarusembe – Mkuranga kuna tuta kubwa sana ambalo sasa inakuwa kero kwa watumiaji wa barabara hii.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kusuasua kwa umaliziaji wa kipande cha barabara ya Ndundu Somanga, km.60. Wananchi wa Mikoa ya Pwani – Rufiji Lindi, Mtwara wamechoshwa na ahadi za kila siku za umaliziaji wa kipande hiki kikorofi.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, ukurasa wa 60 ameonesha pesa ya umaliziaji wa kipande hiki. Naishauri Serikali (Wizara ya Ujenzi) kuhakikisha kwamba barabara hii inakwisha mwaka huu (2011) kama ilivyoahidiwa ili tuweze kuwakomboa wananchi wa Kusini katika kufungua milango ya uchumi ili kuondokana na umaskini wa makusudi tunaopewa watu wa Kusini.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri. Aidha, nampongeza Katibu Mkuu na Watendaji wa Wizara kwa maandalizi mazuri ya hotuba.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mipango mizuri ya Wizara hii, napenda kupata ufafanuzi wa jambo lifuatalo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kamanga – Sengerema Mjini, barabara hii imeahidiwa na Mheshimiwa Rais wakati wa Kampeni mwezi Julai/Agosti 2010 kwamba itajengwa kwa kiwango cha lami. Naomba nipewe ufafanuzi ni lini ujenzi huo utaanza. Ahadi ilikuwa kwamba ujenzi huo ungeanza mara tu baada ya kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Usagara – Geita ambao tayari umeshakamilika.

Mheshimiwa Spika naomba matengenezo ya Busisi – Nyang’hwale – Nyang’holongo yafanywe kwa umakini kabla ya mvua kuanza kunyesha.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sengerema ni ya Halmashauri lakini kwa asili ya udongo wa eneo hili fedha zinazotengwa kupitia Halmashauri hazitoshi hivyo imeendelea kuwa kero kwa miaka kadhaa. Naiomba Wizara ione namna ya kutenga fedha maalumu ili zitusaidie kuimarisha barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA:** Mheshimiwa Spika**,** kuhusu Bodi ya Usajili wa Wabunifu wa Majengo na Wakadiriaji, utendaji wa Bodi hii si wa kuridhisha na hauko wazi sana. Naomba waboreshe utendaji wao. Kuthibitisha hoja yangu hii, Taasisi ya MIST – Mbeya, Idara ya Ubunifu wa Majengo iliomba usajili *last year* na mpaka leo hawajapata jibu la uhakika. Mimi

mwenyewe nimefuatilia jambo hili jibu ambalo nilipewa ni kwamba *regulations* mpya hazijakamilika.

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kuchukua muda mrefu kukamilisha *regulations* hizo. Vinginevyo haitakuwa na maana ya kutunga sheria wakati *regulations* zinachukua muda mrefu. Pia mawasiliano sio mazuri baina ya Bodi na waombaji. *Feedback* ni muhimu sana kwenye vyombo kama hivi.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Usajili wa Wahandisi, naomba Bodi ihamasishe shughuli zake kwenye Vyuo Vikuu na Vyuo vya Ufundi, huko ndiko ma-*engineers* wanatengenezwa. *Presents* ya Bodi ni muhimu sana kwenye Vyuo Vikuu. Ni muhimu kuwahamasisha *Engineering Student's* kujisajili kwenye *ERB*. Ni muhimu *ERB* kuanzisha au kusaidia kuanzisha Vyama vya Kihandisi vya Wanafunzi *(Student Engineering Society*) hii itasaidia *graduate students* kujiunga na *ERB*.)

Mheshimiwa Spika, pia ni muhimu kuhakikisha Walimu wanaofundisha *engineering* (masomo ya *engineering*) kwenye Vyuo Vikuu wamesajiliwa na *ERB*. Vinginevyo Wahandisi wanafunzi hawatakuwa na viwango vizuri. Pia naomba *ERB* ipunguze urasimu kwenye kusajili *Engineering Lecturers* na *Engineering Graduate Students.*

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iboreshe *efficiency of Road Inspection Department.* Tunatengeneza barabara kwa pesa nyingi, lakini matengenezo siyo mazuri sana hasa kwenye MaJiji kama vile Dar es Salaam. Kama tutazifanyia *repair* barabara zetu kwa wakati tunaweza ku-*save a lot of money*. Kwa hivyo utendaji wa *Road Inspection Department* ni muhimu sana kuzikaguwa barabara zetu. Vinginevyo usipojenga ufa, utajenga ukuta. *Road maintenance plan* ni muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho nawashukuru kwa kazi nzuri.

**MHE. SUSAN L.A. KIWANGA:** Mheshimiwa Spika, naanza kuchangia kwa masikitiko makubwa na mshangao jinsi Wizara hii ya Ujenzi inavyofanya kazi na inavyojibu maswali hapa Bungeni na uhalisia wa bajeti ya Wizara 2011/2012. Tarehe 11/7/2011 katika swali langu la msingi kuhusu barabara ya Kidato – Ifakara, Ifakara – Mlimba – Madeke mpakani Njombe, niliomba Serikali ijenge barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Majibu ya Wizara ya tarehe 11/7/2011 nanukuu:- "Serikali katika mwaka huu wa fedha itajenga barabara ya Ifakara – Kidatu km. 80 kwa kiwango cha lami na Ifakara – Mlimba hadi Madeke kwa kiwango cha changarawe".

Mheshimiwa Spika, nimeptia bajeti Kitabu cha IV, hotuba ya Waziri na Randama, Serikali imetenga shilingi milioni 210.830 kwa barabara ya Kidatu – Ifakara. Je, kwa nini Serikali imedanganya wananchi wa Kilombero? Je, kwa namna hii tutaiamini vipi Serikali? Nahitaji maelezo ya uhakika.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kilombero ni wakulima, wafugaji waliohamia na wafanyabiashara, pia wako watumishi kama Walimu na Wauguzi lakini pamoja na kuvumilia shida ya barabara isiyopitika kwa mwaka mzima, sasa wamechoka kuona maendeleo yanakuwa maeneo mengine na wao wanateseka kwa bei ndogo ya mazao, gharama kubwa kwa nauli, kukosa kabisa usafiri kutokana na barabara mbovu. Hii imejitokeza hasa yalipotokea mafuriko Kata ya Mofu, Idete, Mbingu na Mngeta. Magari ya kawaida hayakuweza kupeleka chakula na mahitaji muhimu hadi magari ya Jeshi yakapeleka mahitaji hayo. Wanawake na watoto wagonjwa wanafia njiani kwa kukosa barabara ambayo ingewawezesha kuwafikisha hospitali ya St. Fransis Ifakara kwa matibabu.

Mheshimiwa Spika, barabara ni kichocheo kikubwa cha kuondoa umaskini kwa Watanzania walio wengi wanaoishi Vijijini. Huwezi kutenganisha Kilimo Kwanza na ukuaji wa uchumi, kuondoa umaskini na uboreshaji wa barabara. Hivyo Wizara hii ni chanzo kikubwa cha kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Spika, kuwepo na utambuzi wa barabara zote nchini na foleni, mgao sawa kila Mkoa na Wilaya ili kila Wilaya ijue mgao wake au zamu yake ni lini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa daraja la Kilombero litagharimu takriban shilingi bilioni 50 na kwa bajeti ya mwaka huu zimetengwa shilingi bilioni moja na kidogo hivyo kutokana na bajeti ndogo na kwa kuwa kivuko kilichopo ni kibovu, hivyo basi nashauri Serikali iwaokoe wananchi wa Kilombero na Ulanga kwa kuwapatia kivuko imara ambacho kitatoa huduma kwa muda wote, wanaposubiri ujenzi na umalizaji wa daraja hilo. Ahsante.

**MHE. RAMADHANI HAJI SALEH:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kutufikisha katika Bunge lako Tukufu tukiwa hali ya uzima wa afya. Pia naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa kazi kubwa anayoifanya katika kujenga nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hotuba hii nikijikita kwenye ujenzi wa barabara katika kuunganisha Mikoa yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Wakandarasi ambao wanapewa tenda za barabara zetu, wanahitaji kuangaliwa vizuri kwani Wakandarasi hao ndio wanaosababisha ucheleweshwaji wa ujenzi wa barabara, kiasi kwamba baadhi ya Mikoa wamekata tamaa kuwa barabara zao zitajengwa. Wakandarasi hao wanapochukua tenda ili kujenga barabara hizo baada ya kufanikiwa, baadhi yao huenda hadi *site* ambayo wamepangwa na kuanza kusafisha barabara hiyo, kiasi kwamba wakazi wa eneo hilo kuhisi kuwa barabara imo kwenye matengenezo. Baada ya kitendo hicho, Wakandarasi hao ambao sio waaminifu wanaishia hivy hivyo bila kumalizia barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, ukifanya upembuzi wa hali hiyo unaweza kukuta Wakandarasi hao hawajalipwa fedha zao, sijui ni Hazina ndio wanaochelewesha fedha hizo. Naomba Waziri achukue hatua kali dhidi ya wafanyakazi wazembe kwani hawa ndio wanaozorotesha maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine naomba kumkumbusha Mheshimiwa Waziri awe makini sana katika malipo ya wanaobomolewa nyumba zao kwa ajili ya kupitisha barabara. Kumekuwa na malalamiko juu ya malipo hali inayopelekea kuwa raia wanakosa imani na Serikali yao hali ya kuwa bila ya raia wema hakuna Serikali. Namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuwa makini katika eneo hili; ni kero kubwa kwa wananchi wa kila eneo ambalo linapita barabara.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Tabora una hali ngumu sana kiusafiri kutokana na barabara zote zinazoingia katika Mkoa huu kutokuwa na lami. Tunaisihi Serikali kuwalipa makontrakta ili waanze kazi ya ujenzi wa barabara ya Nzega – Tabora – Itigi – Tabora, Tabora – Ndono – Urambo – Kigoma. Hakika tuna hali ngumu sana.

**MHE. AMINA A. CLEMENT:** Mheshimiwa Spika, naomba kuiuliza Serikali, ni kwa nini barabara zinapewa Mkandarasi anayetambulika na kupoteza fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi kiwango cha lami, baada ya muda sio mrefu sana barabara hiyo inaharibika kwa kuchimbika wakati Mkandarasi alipewa kila alichoomba kwa ajili ya ujenzi huo? Je, Serikali inachukua hatua gani pindi hali hiyo ikitokea? Naiomba Serikali inapofunga mkataba na Mkandarasi pia waweke *garantee* ili inapotokea barabara kuharibika kabla ya makubaliano matengezo ya maharibiko ayabebe Mkandarasi huyo ili Serikali ipunguze mizigo na hasara za makusudi.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ishirikiane na Wizara ya Ardhi, kabla haijagawa viwanja wapimiwe kabisa maeneo ya barabara ili bomoabomoa isiwepo tena. Hii inaipa mzigo mkubwa Serikali ya kulipa fidia, naomba hili liangaliwe kwa kina.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Spika, natoa hongera kwa Mheshimiwa Waziri, hotuba imeandaliwa vizuri sana na kwa umakini mkubwa. Imepangiliwa vizuri na inaeleweka vizuri kabisa.

Mheshimiwa Spika, nina tatizo na changamoto mbili zinazoikabili Wizara hii na ninao ushauri mdogo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto ya ufinyu wa bajeti, ingekuwa vema Serikali ikawatumia watu binafsi watengeneze baadhi ya barabara Mijini na kuweka mfumo wa tozo kwa watumiaji ili tozo hii ikusanywe na kuwalipa waliotengeneza barabara hizo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, changamoto ya barabara zetu kujengwa kwa kiwango cha lami kisha kubomoka ndani ya muda mfupi hata kabla ya miaka mitatu kwisha, mfano mmoja ni barabara ya Kibiti – Lindi ambayo inabomoka maeneo yanayokaribia Nangurukuru. Pia barabara ya Dodoma - Nzega imebomoka sana maeneo ya Sekenke na Shelui na katika barabara zote hizi ukipita utakuta matengenezo yanaendelea. Je, ni nani anagharamia matengenezao hayo? Ushauri wangu kwa Serikali iwe makini wakati wa kuteua Wakandarasi na kutengeza mkataba, Mkandarasi ahusike na matengenezo yote yatakayohitajika ndani ya miaka mitano. Pia Mhandisi atakayekubali kukabidhiwa barabara iliyo chini ya viwango achukuliwe hatua kali.

Mheshimiwa Spika, barabara za mipakani zinaonyesha utofauti mkubwa kati ya eneo la Tanzania na nchi jirani. Kwa mfano mpaka wa Namanga na ule wa Sirari, ule upande wa Tanzania ni wa kiwango cha chini, je, nini sababu za tofauti hizi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HAROUB MUHAMMED SHAMIS:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu (SW) kwa rehma na neema zake nyingi anazoendelea kunijalia. Kwa hakika neema za Mwenyezi Mungu kwangu ni nyingi kiasi cha kushindwa kuzihesabu, ni wajibu wangu kabisa kusema *Al Hamdu Lillah.*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwa upeo na uono wake wa kiuongozi kwa kuona uchapakazi wa Mheshimiwa Magufuli na kuamua kumrudisha katika Wizara hii muhimu kwa uchumi na maendeleo ya nchi kwa ujumla. Hongera Dkt. Magufuli, chapa kazi kwa dhati bila kujali itikadi za vyama vyetu la muhimu ni kujenga nchi kwa pamoja ili kuondoa janga kuu la umaskini wa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na jitihada za Serikali zinazosimamiwa na Wizara hii, zipo changamoto za kuangaliwa.

- Bajeti ya Wizara iwe inaongezwa mwaka hadi mwaka.

- Usimamizi katika miradi uimarishwe.

- Uhakiki kwa Wahandisi wa Shauri (*Consultant Engineers*) ufanyike ili wafanye kazi kwa niaba ya anayejengewa na sio kwa nayejenga.

- Adhabu kwa Wakandarasi na Wahandisi Washauri zitolewe ili kuweka nidhamu na thamani ya kazi (*value for money and disciplie*).

- Kuwe na *“Road Patrol*” ya mara kwa mara ili kubainisha uharibifu wa barabara zetu na kuzikarabati mara moja kabla ya kuharibika zaidi.

- Kuwe na utaratibu maalum wa kuzitunza barabara.

- Magari yanayozidisha mizigo pamoja na kutozwa faini mizigo hiyo ishushwe ili kudhitibi uharibifu wa barabara zetu.

- Kuweka alama za barabarani ili kupunguza ajali.

- Matuta yawekwe kwa viwango na alama kabla ya tuta pia ziwekwe.

- Matuta aina Rasta yatolewe yanaongeza umaskini.

Mheshimiwa Spika, *reception* ya mtu ni uso na *reception* ya nchi yetu ni Jiji la Dar es Salaam. Barabara za Jiji la Dar es Salaam zinatia aibu kwa nchi yetu. Naishauri Serikali barabara zote katika Jiji la Dar es Salaam ziwe chini ya Wizara ya Ujenzi (*TANROADS*) ili iwe rahisi kuzihudumia.

Mheshimiwa Spika, pia nashauri barabara zilizoainishwa za kupunguza msongamano Dar es Salaam wazikamilishe na kuangalia viwango vya ujenzi katika barabara hizo.

Mheshimiwa Spika, ujenzi unaoendelea wa barabara ya Jet – Rumo – Buza na kuzungukia Tandika hauridhishi hata kidogo! Uko chini ya kiwango. Ni lazima hatua za haraka zichukuliwe ili kuinusuru barabara hiyo na kuokoa fedha za umma. Inaonekane Mkandarasi huyu ana ujanja anaoutumia kwani aliwahi kupewa mradi wa barabara na akashindwa kuukamilisha, ni jambo la kushangaza Mkandarasi huyu badala ya kupewa adhabu anapewa mradi mwingine ambao nao ndio huu anaoendelea kujenga kwa kuondosha njiani! Serikali kupitia Wizara hii hasa Waziri Magufuli afuatilie tatizo hili haraka.

Mheshimiwa Spika, wakati umefika sasa na hasa kwa kuwa kuna mpango wa kuwawezesha Wakandarasi wazawa kwa kuwapa kandarasi kubwa zaidi, Serikali iwe makini katika kukagua miradi inayojengwa ili ijengwe kwa viwango stahili. Kwani ndugu zetu wazawa (kama alivyosema Mheshimiwa Waziri Mkuu) wana tatizo la kutopenda kufanya kazi na wanapofanya ufanisi (*efficiency*) inakuwa haipo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la msongamano Dar es Salaam linaelekea kuwa sugu (*chronic*), kwani wadau ni wengi mno. Napendekeza kwa Serikali tatizo la msongamano Dar es Salaam akabidhiwe Waziri Magufuli na Wizara yake tu. Wadau wengine wakabidhi kwake tena kwa haraka ili tatizo hili liishe.

Mheshimiwa Spika, napendekeza pia barabara zote ndogondogo (*streets*) za Dar es Salaam ziwe chini ya Wizara *(TANROADS)* ili zitiwe lami zote na hiyo itasaidia sana kuondoa msongamano hasa siku za mvua ambapo magari yote hupita barabara kuu tu na kuwa ni adhabu kuendesha gari Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, mimi ni Mbunge mpya, lakini kabla sijawa Mbunge nilikuwa nafuatilia sana Bunge na utendaji wa Serikali, utendaji wa Waziri Magufuli binafsi nau-*admire.* Kwa vile sasa mini ni Mbunge, nitajitahidi kuwa karibu naye ili nimpe taarifa mbalimbali za uzembe na ubadhirifu ili naye achukue hatua na nchi yetu ipige hatua katika katika maendeleo ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, nawatakia wenzangu nchini kote saumu njema.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Hanang ina sehemu ndogo sana ya barabara kuu na barabara za Mkoa. Hii maana yake ni kuwa sehemu kubwa ya barabara za Wilaya zinahudumiwa na Halmashauri, hivyo barabara nyingi zitabaki duni kwa kuwa uwezo wa Halmashuri ya Wilaya ya Hanang ni mdogo sana.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara ya Ngamu kwa upande wa Singida, ni barabara ya MKOA, itakuwa jambo jema barabara hii nayo kwa upande wa Hanang kupitia Gawidu ikaunganishwa na barabara inayotoka Katesh kwenda Mbulu yaani barabara ya Basotu. Kuna barabara inayotoka Babati kupitia Bcsodesh Wilayani Hanang hadi Hitbadawa na hatimaye Iramba katika Mkoa wa Singida. Nitashukuru sana kwa barabara hizi mbili kupandishwa hadhi na kuwa barabara za Mkoa. Ikikubalika Wilaya ya Hanang ambayo hali yake ya barabara ilikuwa mbaya itasaidiwa na Mkoa.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Hanang ni moja ya maeneo ambamo ujenzi wa barabara ya lami ya Minjingu – Babati – Singida umepita. Ujenzi huu umeelekea baadhi ya wananchi

kutakiwa kubomoa nyumba zao ili kupisha ujenzi wa barabara hiyo. Mwaka 2009 Serikali iliamua kuwalipa fidia baadhi ya wananchi katika Wilaya ya Hanang ambako ndilo Jimbo langu. Baada ya hapo Serikali ilitoa tamko la kutowalipa fidia wananchi wote ambao nyumba zao zipo ndani ya mita 22.5 kutoka katika mstari wa katikati ya barabara kwa mujibu wa Sheria ya Barabara ya mwaka 1972. Hata hivyo, kuna baadhi wa wananchi wamekwishalipwa fidia na wengine kuahidiwa na Serikali kulipwa na tathmini ya thamani ya nyumba zao imefanywa tayari na wamefahamishwa kwa barua. Nyumba za wananchi hao waliolipwa na walioahidiwa zimejengwa katika miaka 1960 kabla ya Sheria niliyoitaja, hatua ya baadhi ya wananchi kulipwa na wengine waliokwishaahidiwa na Serikali na sasa Serikali imetoa tamko la kukataa kuwalipa, imeleta chuki kubwa kwa Serikali yao. Wanauliza ni kwa nini Serikali hiyohiyo ilikubali kwa ahadi na kuwalipa wachache na kuwaacha wengine, isitoshe wengi au wote wa wananchi hao wamejenga nyumba zao kabla ya mwaka 1972 ambapo Sheria ya *Road Reserve* ya 22.5 mita haijapitishwa.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara na Waziri wangalie utaratibu wa kuwalipa wananchi waliobaki fidia hasa wale ambao Serikali ilikwishawafanyia tathmini na kukubali kuwa itawalipa fidia kwa barua. Hatua hii ya Serikali itaondoa utata uliopo na kuisaidia Serikali katika kuhimiza azma yake ya wananchi kufuata Sheria za Barabara na hasa kwa kipindi hiki ambacho Serikali imepanua *road reserve* kutoka mita 22.5 hadi mita 30. Namhakikishia Waziri atakapotekeleza hili atakuwa amesaidia wananchi kuendelea kuenzi na kuipenda Serikali yao. Naleta viambatisho pamoja na mchango wangu huu.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kuchangia hoja hii kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi pamoja na Naibu wake. Pia nawapongeza Mheshimiwa Katibu Mkuu na Watendaji wake wote kwa kazi nzuri wanayofanya ya kutengeneza barabara.

Mheshimiwa Spika, katika kazi inayofanywa ya ujenzi wa barabara, naomba Serikali isiwavunjie wananchi nyumba zao kabla ya kuwalipa fidia ili waweze kuandaa mazingira mengine ya kuishi. Pili, je, Serikikali inakuwa iko wapi mpaka wananchi wanajenga hadi kumaliza ndiyo baadaye wanawaambia kwamba wamejenga kwenye eneo la barabara au amejenga kwenye eneo la wazi au vinginevyo? Kwa nini tumuache mtu ajenge mpaka afikie hatua kubwa bila kumtaarifu kwamba sehemu unayojenga sio stahiki?

Mheshimiwa Spika, viwango wanavyolipwa wananchi wakati wanapotakiwa kuvunjiwa nyumba zao ili kupisha barabara havilingani na thamani ya nyumba zao na hii hupelekea manung'uniko makubwa kwa Serikali kwamba baadhi ya wananchi hawapewi haki zao kulingana na nyumba zao, naiomba Serikali ifanye kazi ya ziada ili haki itendeke.

Mheshimiwa Spika, barabara zetu nyingi hazijengwi katika kiwango kilichobora ndio sababu kila baada ya muda tunalazimika kutia viraka na kupoteza fedha nyingi za Serikali. Hii inatokana na kutokuwa na usimamizi na uwajibikaji. Naomba Watendaji wetu wasimamie vizuri wanapotoa kazi kwa Makandarasi ili udhaifu uonekane mapema kabla kazi kumalizika.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu na wananchi wa Babati Vijijini Mkoa wa Manyara. Napenda kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Mheshimiwa Mizengo Kayanda Peter Pinda kwa kazi kubwa na juhudi wanazozifanya kuendeleza mipango ya ujenzi, sekta ya barabara na majengo ambayo yanahitaji gharama kubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kwa kazi na michango yao katika Wizara ya Ujenzi, wamekuwa Watendaji wa mfano na wenye msimamo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara hii kwa sehemu mbili, moja upande wa barabara na pili majengo.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishauri Serikali kwa upande wa barabara Mkoani Manyara, tunashukuru barabara ambazo zimeombwa kupandishwa kuwa za Mkoa zingefanyiwa kazi

mapema, ni eneo ambapo Serikali Kuu haina barabara nyingi kwa kilomita na pia Wilaya huwa zinashindwa kukarabati kutokana na bajeti finyu na wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Babati, nashauri barabara kutoka Kondoa, kupitia Kash – Galapo – Mamire – Mkuta – Babati Mjini ingepandishwa daraja, inaunganisha Wilaya tatu na Mikoa miwili na ni ahadi ya Rais kukarabati eneo kutoka Galapo – Kash – Lerui. Pia barabara kutoka Bashnet – kupitia Narutana – Lukmanda - Setchet – Basoutu – Katesh – Hydom Road hadi Singida, inaunganisha Wilaya ya Mbulu, Babati na Hanang na pia Mkoa wa Manyara na Singida pia ni eneo muhimu katika muungano wa Wilaya tatu, huduma muhimu za afya na muhimu kuliko zote ni za uchumi. Ni eneo muhimu kwa kilimo na ufugaji na ni barabara ambayo haina usafiri kabisa wa abiria, wananchi hupata shida sana na Wilaya hizi tatu kushindwa kukaa pamoja na kutenga fedha ya ujenzi na ukarabati, pia inahitaji gharama kubwa. Pia barabara ya kutoka Njia panda Boay kutoka barabara ya Babati – Gidas – Bubu – Endasak. Inaunganisha Wilaya ya Babati na Hanang.

Mheshimiwa Spika, pia naomba Serikali ifanye kuweka vipaumbele katika barabara ya Babati – Kondoa – Dodoma, ni barabara muhimu na imepigiwa kelele muda mrefu lakini hadi leo hii ahadi ya kujenga kwa kiwango cha lami ni sehemu ndogo tu kutoka Dodoma hadi Mayamaya na Babati – Bonga ina wajenzi wanaofanya kazi na eneo la Bonga – Mayamaya bado. Serikali imeanzisha barabara mpya nyingi na kusahau barabara hii. Naamini kuwa Serikali itaiangalia kwa huruma na kuwasaidia wananchi wa maeneo hayo ya Wilaya na Mkoa unaotumia barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, pia naleta ombi, eneo la Dareda Kati – kwenda Dareda Mission, naomba Serikali iangalie namna ya kuiweka barabara hiyo kwa kiwango cha lami. Ni muhimu kwa sababu ya uchumi na ni eneo muhimu kwa huduma ya afya. Ni mahali penye hospitali ya Rufaa ya Wilaya ya Babati Vijijini. Wananchi wengi kutoka Hanang, Babati Mjini, Mbulu na Monduli hutumia hospitali hiyo bora na kipindi cha masika barabara hiyo huwa haipitiki na huduma hiyo muhimu kukosekana.

Mheshimiwa Spika, muhimu naomba Wizara iangalie na kutoa ushauri na mwongozo kuhusu barabara ambazo zina Wilaya mbili au tatu na Wilaya zingine hazioni umuhimu wa barabara hizo na kutopewa kipaumbele na kwa muda mrefu hazitengewi fedha na wanaoathirika ni wale wa Wilaya moja. Mfano ni Babati Mjini na Babati Vijijini, Mbulu, Hanang – Kondoa. Barabara kutoka Bonga kwenda Ayasanda, Babati Mjini kwenda Mutuka, Mamire, Babati Mjini – Kiru kupitia Dagaloloi na Imbilili, barabara ya Vibaotatu – Kiru ambayo kwa miaka 31 haijatengewa fedha na hawana mpango wa kufanya hivyo, barabara kutoka Galapo – Kash – Urui – Kondoa na Boay – Gidas – Endasak.

Mheshimiwa Spika, Jimbo langu linaathirika sana kwa sababu tunatenga fedha na kukarabari lakini Halmashauri ya Babati haitengi kabisa fedha na eneo kubwa la barabara hizi ni katika maeneo yao. Vikao vya *Mini Road Board* wameshindwa kupata muafaka. Pamoja na kuwa tumekaa mara kadhaa na huko nyumba walishakaa, tunaomba Wizara itusaidie.

Mheshimiwa Spika, lingine tunaomba maelekezo mahali Wilaya zinapotoa na kupanga fedha za barabara na ujenzi wa nyumba au majengo ya umma, kuna wadau katika maeneo hayo wenye vifaa vya ujenzi mfano wa mitambo, magari, wana ujuzi wa ujenzi wa majengo, wataalam hukataa kuomba vibali kwa kisingizio cha Sheria ya Manunuzi. Wenye vifaa wako tayari kutoa mitambo na vifaa vyao na Halmashauri ichangie mafuta na *oil (lubrcants).* Mfano tenda ikitolewa ya kuchonga kilomita tano, kwa fedha hiyohiyo hao wadau wangechangia ingechongwa kulomita kumi na tano na kwa ubora zaidi kwa sababu wao pia ni watumiaji wa barabara hiyo. Katika ujenzi wa madarasa, majengo ya shule, vituo vya Polisi, ofisi mbalimbali, zahanati na vituo vya Afya, tabia hiyohiyo hutumika. Wadau wangechangia, fedha Serikali waliyotoa ikanunua vifaa vya viwandani (bati, cement, nondo, misumari) kazi kubwa zaidi ingefanyika. Wataalam hulazimika kutoa tenda kwa Wakandarasi na gharama huwa kubwa. Naamini lengo la Serikali ni kuwa na mafanikio makubwa kwa pesa wanayotoa na kamwe hawapingi kazi zaidi kufanyika kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Spika, pia tatizo la wataalam wa Wilaya kutotoa na kushauri wadau na viongozi wa eneo husika kwa kazi inayotarajiwa kufanyika. Viongozi wa eneo na wadau

wangejua kazi gani inayotarajiwa kufanywa, kwa kiwango gani, ukubwa wa kazi, wangekuwa walinzi na ubadhirifu usingetokea. Katika ziara za Ubunge tunapata malalamiko mengi sana na kuona kazi chafu bila kiwango kwa sababu wadau hawajui.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba Wizara itusaidie Jimbo la Babati Vijijini katika majengo ya watumishi Vijijini, kutoa elimu na mafunzo kwa Kamati mbalimbali za Ujenzi Vijijini ili waweze kusimamia vizuri zaidi ujenzi kwa kiwango.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara itusaidie Jimbo la Babati Vijijini katika ununuzi wa mashine moja ya kufyetua matofali ya kuchanganyia mchanga/udongo na *cement*, *hydroform blocks* na kutupatia elimu juu ya utengenezaji wa matofali hayo.

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda kuipongeza Wizara kwa kujenga barabara ya Babati –Minjingu ambayo imekamilika na kazi za mitaro na matoleo ya pembeni inaendelea. Kuna kazi ambayo haikuwepo katika mkataba wa Mkandarasi, eneo la Magugu Mjini, mitaro kutoka eneo la *SACCOS*, *stend*, Polisi, soko, hakuna njia za kutoa maji na masika maeneo hayo hujaa maji na baada ya barabara kujengwa tatizo ni kubwa zaidi. Tunaomba timu ya wataalam ije kuchunguza na kulitafutia ufumbuzi. Pia huyu Mkandarasi aweke matoleo zaidi katika maeneo hayo ili wananchi waweze kuvuka kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, nawaomba Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri waje Mkoa wetu wa Manyara wajionee hali za barabara na watushauri na pia wakiona wataamini shida tunazopata (*seeing is believing*) na wananchi wa Jimbo langu wana hamu ya kumwona Mheshimiwa Waziri Dkt. Magufuli na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza, natoa shukrani zangu za dhati kwa mara nyingine kwa ujenzi wa barabara za Kigoma. Uzalendo wenu kama Waziri na Naibu hauna mashaka hata kidogo, nawashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pili shukrani kwa barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi - Ukurasa 68 (122) na hasa kwa "*naming*" kwamba vyovyote itakavyokuwa Kidahwe – Kasulu itakuwa sehemu ya kuanzia. Hata kama pia tutakuwa na Mkandarasi atakayeanzia Nyakanazi sina tatizo. Muhimu ni kuendelea kufufua Mkoa wa Kigoma. Wasiwasi wangu ni kwamba kiwango cha fedha kilichotengwa ni kidogo sana kwa kuanzia. Naomba Waziri anipe ufafanuzi ni namna gani tutafanya kupata pesa zaidi ili kuhakikisha kuwa Kasulu inaunganishwa na Kigoma Mjini?

Mheshimiwa Spika, tatu, suala la barabara za kupanda madaraja. Bodi ya Barabara ya Mkoa Kigoma ilileta mapendekezo yake ya barabara za kupanda madaraja kama ifuatavyo:-

(1) Kagunga – Kigoma, hii inaunganisha mpaka wa Tanzania na Burundi. Naomba sana barabara hii *TANROADS* waifungue.

(2) Mwandiga – Mkongoro, hii inaunganisha barabara mbili za Taifa.

(3) Pasua – Kalinzi (kupitia Matyazo), hii inaunganisha barabara mbili za Taifa.

Mheshimiwa Spika, naomba sana barabara hizi zipande daraja. Hii ya Kagunga ni muhimu sana. Naomba Wizara ya Ujenzi iangalie hili.

Mheshimiwa Spika, sina la ziada ila naunga mkono kwa kazi yao, hongereni sana.

**MHE. YUSUPH A. NASSIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru Mola kwa kunipa umri na afya njema na hatimaye kuniwezesha kufunga swaumu ya mwezi huu wa Ramadhani.

Mheshimiwa Spika, aidha, pamoja na kuwa mdau wa wahanga wa bomoabomoa na kuomba kuchangia na *memo* ya Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda kukuomba nichangie bado haikukupendeza na kukuridhisha kunipa fursa.

Mheshimiwa Spika, naipongeza kwa dhati kabisa bajeti/hotuba ya Wizara ya Ujenzi, chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, niseme naiunga mkono.

Mheshimiwa Spika, nianze kuchangia hoja hii kwa kusema kuwa Wizara imesahau ukurasa mmoja wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2010 – 2015. Barabara ya Korogwe - Dindira hadi Soni haimo? Hili limetushangaza sana. Hivyo nimwombe Mheshimiwa Waziri pamoja na kuruka ukurasa huu watusaidie kutenga fedha za "*design"* ya barabara hii.

Mheshimiwa Spika, fidia kwa wananchi wengi wa Taifa hili zimekuwa ni suala mtambuka. Kila Mheshimiwa Mbunge aliyesimama kuzungumzia kadhia hii, alionesha kusikitishwa sana na hali hii na hakika wahusika hawalipwi kiufasaha. Aidha, kumekuwa na mfumo wa kibaguzi katika ulipaji huu kwani wananchi wa Kilole, Bogamoyo, Kwamatuku, Mkata, Vibaoni na maeneo mengineyo ya barabara za Korogwe - Handeni na Mkata – Handeni wako barabarani kudai fidia zao. Aidha, Mkuu wa Mkoa Tanga, ametuma Wakuu wa Wilaya za Korogwe na Handeni kufuatilia sakata hili.

Mheshimiwa Spika, *TANROADS* wapewe uwezo, watumishi mitambo na miongozo ya kitaalam inayoendana na mabadiliko ya kimaendeleo. Kadri nchi inavyokuwa basi na mahitaji ya miundombinu huongezeka.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Old Korogwe, Kwasamangube, Dindira, imeachwa kwa muda mrefu bila matengenezo. Nichukue fursa hii sasa kuwakumbusha Wizara/*TANROADS* kuwa, eneo hili linaunganisha Wilaya mbili na Miji ya Korogwe Mjini, Korogwe Vijijini na Bumbuli.

Mheshimiwa Spika, Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga, wananchi na hata uongozi wa Mkoa haturidhishwi na Mkandarasi *Y.N. Investiment* na *Lucky Construction* na kuwa hata Mhandisi Mshauri *(COWI*) amethibitisha udhaifu na wizi wa mchana wanaoufanya kwa Taifa hili kwa kulipwa bila kufanya kazi. *PMMR* kwa Tanga ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa ushauri kwa Wizara kama ifuatavyo:-

(1) Malori zaidi ya tani saba (7) na mabasi yasiruhusiwe kupaki nje ya nyumba.

(2) *TANROADS*, Wizara na watu binafsi wajenge *Parking Structure,* maeneo ya maengesho katikati ya Miji.

(3) Daladala zipangiwe muda wa kushusha na kupakia abiria na zisimamiwe na chombo maalum.

(4) Matuta barabarani yawe ya kiwango maalum.

(5) Mizani ziwekwe mita 500 nje ya njia kuu zetu ili kupunguza ajali na misongamano.

(6) Wizara na *TANROADS* wakishirikiana na wadau wajenge njia maalum za kugeuzia magari makubwa mabasi na kadhalika.

(7) Wizara iondoe vituo vyote vya mabasi vilivyomo kwenye njia kuu na barabara mahsusi na kuviweka mita 500 mbali na njia kuu.

(8) Iondoe vituo vya daladala karibu na *traffic light* mita 100.

(9) Wekeni "*No parking Signs*" (ishara) karibu na njia panda na palipo na taa za barabarani.

(10) Jengeni barabara za michepuo mita 150 kuruhusu magari yanayokata kushoto yaende bila kuongeza msongamano.

(11) Pigeni marufuku Maguta, Bajaji kuwepo katikati ya Miji ili kupunguza msongamano.

(12) Wizara na Taasisi zake na wadau wengine wazuie malori yanayoharibika kwenye barabara kuu na njia za pembezoni, basi yapewe si zaidi ya masaa matatu ya matengenezo, zaidi ya hapo yavutwe yawekwe pembeni kupunguza ajali na misongamano isiyo ya lazima.

(13) *TANROADS* na Wizara watunge Sheria kuzuia Madereva wasiendeshe malori kwa zaidi ya masaa kumi ili wapumzike.

(14) Wizara ianzishe *Highway Monitoring Unit* chini ya muundo wa ubia na sekta binafsi. Hii itaongeza ufanisi na kupunguza gharama kwa Wizara na Taifa.

(15) Wizara na *TANROADS* iweke mabango ya kiwango cha mwendo kasi kila baada ya kilometa tano (5).

(16) Wizara kwa kuutumia *Highway Monitoring Unit* wafanye msako wa kushtukiza kwa Madereva walevi na walioendesha magari muda mrefu.

(17) Zoezi la kukagua malori na mabasi lifanyike kila baada ya miezi sita (6) na makampuni yatakayosababisha ajali kwa uzembe waongezewe bima kwa asilimia 50% ili kujirekebisha.

(18) Barabara ya Moshi - Arusha kupitia pale Korogwe Mjini ni nyembaba sana na kila mara ajali hutokea. Wizara na *TANROADS* watusaidie kuweka mpaka na kuitanua.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii inayoonyesha utekelezaji uliopita na kazi zitakazofanyika mwaka 2011/2012. Nina uhakika, kwa jitihada za Waziri barabara hizi zitajengwa katika muda muafaka. Baaada ya utangulizi huu naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali itueleze kipande kilichobaki cha Mayamaya – Bonga, pamoja na kwamba itakuwa imeanza kujengwa, ili kukamilisha ujenzi, fedha zinatarajiwa kutoka wapi?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ya kutoka *keep left* ya Shabiby mpaka *St. Gasper* hutokea ajali mara kwa mara, ni lini Serikali itatoa au kujenga matuta ya kupunguza mwendo wa magari ili kupunguza ajali zinazotokea mara kwa mara?

Mheshimiwa Spika kwa kuwa Dodoma ndio Makao Makuu ya Serikali, ni vizuri tupate maelezo kwa nini Serikali inaendelea kujenga nyumba za Serikali ama ni nyumba za ofisi, za kuishi ikiwemo nyumba ya Waziri Mkuu Dar es Salaam? Naomba iache utaratibu huo na ujenzi wa nyumba uelekezwe Dodoma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, ni kigezo gani kilichotumika kuupatia Mkoa wa Kilimanjaro fedha nyingi sana kwa miaka miwili mfululizo yaani 2010/2011 – 2011/12 kwa kiasi cha shilingi milioni 7,190 na 1,200 kwa *unit* 7.9 tu wakati Mkoa wa Pwani umepewa shilingi milioni 865 kwa mwaka 2010/2011 na shilingi milioni 479.12 (2011/2012) kwa *unit* 82 (*km/no of bridges*). Hali hii inaleta mtafaruku mkubwa na kutokuwa na imani na baadhi ya Watendaji ndani ya Wizara. Naiomba Wizara iangalie suala hili kwani inaweza kuleta mtafaruku mkubwa ndani ya Bunge. Naomba Waziri azungumzie jambo hili kwani Wabunge wengi limewapa utata.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iangalie Wilaya ya Kisarawe kwa jicho la huruma sana. Wilaya iliyoanzishwa tangu mwaka 1907 hadi leo mtandao wake wa barabara unatia

huzuni.  Naomba zile kilometa 54 kutoka Kisarawe hadi Maneromengo zipewe kipaumbele mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, napenda kuunga mkono hoja.

**MHE. RASHID ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwepo katika Bunge lako hili na kuweza kupata nafasi ya kuwawakilisha Watanzania wa Jimbo langu la Kojani na Wazanzibar wote.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima nichukue nafasi hii kuchangia mchango wangu kwa maandishi. Pia nimshukuru Waziri wa Wizara hii kwa mpango wake mzuri aliouandaa yeye na Watendaji wa Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kupitia Serikali, kuna muhimu mkubwa wa ujenzi wa kivuko cha Feri kuelekea Kigamboni.  Sehemu hii inachukua wakazi walio wengi na wale wanaokwenda katika shughuli nyingi za kimaendeleo. Nina hakika kwa fedha ambayo inakusanywa kupitia kivuko cha Feri, fedha nyingi imeshakusanywa sasa hivi, kwa maana hiyo Serikali sasa haina sababu isiweze kushughulikia suala hili la kutengeneza mpango mzuri  wa kivuko. Kwa mpango ulioandaliwa vema na fedha zilizoidhinishwa, tunaamini kwamba Wizara hii inaweza kuendesha shughuli zake bila matatizo za ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za Mkoa, kwa mujibu wa Mkoa wangu, naona Wizara itakuwa imepiga hatua nzuri na kubwa ila tu inahitaji usimamizi uwe mzuri ili kufikia hatua iliyokusudiwa ndani ya malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba niishauri Serikali kwamba:-

- Ikamilishe fedha iliyoidhinisha kwa wakati muafaka.

- Wizara isimamie vema miradi yote iliyopanga kwa uadilifu.

- Wizara ipange na kuandaa mikataba wa Wahandisi wetu wenyewe kwani faida inapatikana nchini petu na wataalam wetu watajua jinsi gani ya kukarabati wakati barabara hizo zinapoharibika.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata japo nafasi hii ya kuchangia kwa maandishi.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja zifuatazo katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni mgawanyo wa barabara Mkoa wa Kigoma na Taifa kwa ujumla.  Ukiutazama Mkoa wa Kigoma katika ukurasa wa 229 katika hotuba ya Waziri wa Ujenzi ya mwaka 2011/2012, utaona kuwa barabara nyenye umuhimu ni inayopita Kibondo - Kasulu hadi Kigoma Mjini. Ndiyo ina umuhimu kwani hupita Wilaya zote.  Aidha, napenda kuishauri Serikali kuwa barabara hujengwa ili kuinua uchumi, hivyo wakati ujenzi wa barabara hiyo nashauri, katika bajeti hiyo ihusishe ujenzi wa barabara ya Kibondo - Mabamba na mpakani Burundi ambayo ni takriban km.39 tu ili kuwafanya wafanyabiashara wa Tanzania wanaokwenda Burundi kupitia Kibondo – Mabamba badala ya kutoka Nyakanazi hadi Kigoma Mjini ambapo zinaongezeka km.300 zaidi.

Mheshimiwa Spika, pili, mgawanyo wa rasilimali za Taifa. Katika Katiba yetu ya Tanzania, Ibara ya 8 -9 na Ibara ya 27, mgawanyo wa rasilimali unapaswa kwenda na uwiano wa nchi nzima na sio kibaguzi.  Hivyo kitendo cha barabara zaidi ya km.300 kwenda Kilimanjaro huku Kigoma bado na kadhalika, sio sahihi. Serikali iangalie upya isije ikachagua Watanzania.  Au Kitendo cha Waziri wa Nishati na Madini kugawa fungu kubwa kwenye Jimbo lake mfano zaidi ya Vijiji tisa huku Jimboni Muhambwe hata Makao Makuu ya Wilaya umeme bado, ni kuligawa Taifa.

Mheshimiwa Spika, tatu, vipimo vya magari ya mizigo mizito barabarani (mizani), napenda kupata majibu kutoka kwa Waziri kwa nini magari yakishakaguliwa yanapitiliza bila kushusha mizigo na kuendelea kuharibu barabara?

Mheshimiwa Spika, nne, utaratibu wa kugawa viwanja na Sheria za Barabara, Sheria inataka viwanja vipimwe na kupewa hati kama ilivyooneshwa katika Sheria ya Ardhi Na. 4 na 5 ya mwaka 1999. Baadhi ya Maafisa Ardhi wanapima viwanja ndani ya mita 30 kinyume cha Sheria za Barabara. Je, Serikali inachukua hatua gani? Au inawawajibisha wananchi waliojenga ndani ya M.30 na kadhalika wakati makosa ni ya Wizara ya Ardhi?

Mheshimiwa Spika, tano, kuhusu ujenzi wa nyumba za Serikali na kuhamia Dodoma. Katika hotuba ya Wizara inaonesha kuwa katika ujenzi wa nyumba 47 za Serikali ni nyumba mbili tu zitakazojengwa Dodoma na nyumba 12 zitajengwa Dar es Salaam. Nahoji kwa nini nyumba hizi zijengwe Dar es Salaam wakati Serikali imeshaonesha azma ya kuhamia Dodoma?

Mheshimiwa Spika, sita, kuhusu utekelezaji na usimamizi, naomba kumpongeza Waziri wa Ujenzi anayesimamia Wizara yake lakini napenda kutoa changamoto kuwa azidishe hapo kwani Wizara hii imepewa fedha nyingi kuliko Wizara zote, hivyo awe mkali zaidi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. EZEKIEL M. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, naomba pamoja na kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake, nichangie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, naomba mpango wa Serikali wa kujenga barabara ya Kahama – Geita (kuunganisha migodi ya Buzwagu, Bulynhulu na Geita) kwa lami uanze. Wananchi wanalalamika sana kutimuliwa vumbi na magari yanayochukua dhahabu yao.

Mheshimiwa Spika, naomba barabara za Kahama – Bulije – Mwakitolyo na Nyambula, Chela – Nyanh'olongo ziongezewe bajeti.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. KHERI KHATIB AMEIR:** Mheshimiwa Spika, mimi naomba kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa juhudi kubwa wanazozichukua kusimamia na kutekeleza azma kubwa ya Serikali hii ya Awamu ya Nne kwa kuweka mtandao wa ujenzi wa barabara kwa nchi nzima. Juhudi zao na Watendaji wa Wizara hii ni za kuigwa.

Mheshimiwa Spika, lakini hakuna zuri lisilo na kasoro au la kibinadamu lisilo na upungufu. Kwa maana hiyo, naiomba Wizara sasa ijikite katika kuangalia hali mbaya ya barabara Jijini Dar es Salaam. Mfano Pugu Road, ina hali mbaya sana, kutoka Jiji la Dar kuelekea Airport, unaweza kuchukua si chini ya masaa matatu kutokana na msongamano wa magari kwenye "*pickhour*" (saa 6.00 na kuendelea). Si hivyo tu barabara ya Uhuru - Bagamoyo *Road* – Ali Hassan Mwinyi Road. Hizi zote zina utata wa usafiri ama wa kuingia jioni au kutoka. Barabara ya Morogoro ina shida sana wakati wa kuingia Jijini, nayo waweza kuchukua zaidi ya masaa manne kutoka Chalinze kuelekea maeneo ya Mjini. Nathamini sana kazi nzuri inayofanywa na iliyokusudiwa kufanywa siku zijazo lakini naona kuna haja ya kuchukua hatua za dharura kwa muda huu kabla mipango ya kudumu kukamilishwa ili kutatua tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza kwa hatua za ujenzi wa daraja la Kigamboni zilizofikiwa pamoja na ujenzi wa barabara ya magari yaendayo kasi, *flying over* na hii nayo ikikamilika, nina hakika itapunguza msongamano kubwa wa magari Jijini. Ila nakubaliana na wazo la wachangiaji wengi la matengenezo ya barabara ndogo (*feeder road*) zinazounganisha barabara za mitaa, hizi zitasaidia kupunguza msongamano uliopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa ufupi, safari ya ujenzi wa barabara za nchini bado ndefu na jitahada za dharura na muda mrefu zinahitajika ili azma nzuri na endelevu za maendeleo ya nchi hii ziweze kutekelezwa.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waziri wa Ujenzi, Naibu wake na uongozi mzima wa Wizara hii kwa hotuba nzuri yenye maelezo ya kina na vielelezo vinavyotoa ufafanuzi wa kutosha. Aidha, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa ujasiri, umakini na kwa kujiamini katika utendaji wao wa kazi.

Mheshimiwa Spika, bomoabomoa ni kero. Hata kama wananchi wanaingia katika hifadhi ya barabara lakini je Serikali si ni jukumu lake kutunza maeneo hayo badala ya kusubiri kuja kuwabomolea watu majengo yao? Mwananchi anapaswa kuzingatia sheria lakini Serikali nayo isimamie na kuhakikisha sheria hazivunjwi. Hivyo basi si halali kuwabomolea watu nyumba zao bila fidia.

Mheshimiwa Spika, nashukuru barabara za Mkoa wa Kagera zinapitika kwa wakati wote ukiacha maeneo machache. Tunasubiri kwa matumaini ujenzi kwa kiwango cha lami na kukamilika barabara ya Kigoma – Lusahunga, Kyaka – Bugene – Kasulo, Bugene – Nkwenda – Kaisho – Murongo na Kumugakorongo – Businde Bugomora hadi Murongo. Barabara ya Kagoma – Lusahunga inasuasua muda mrefu ni vema ikakamilika katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ni ahadi ya muda mrefu ya kuweka kivuko kipya katika mto Ruvubu/Kagera eneo la Rusumo. Ukurasa wa 83 imeelezwa kwamba yatajengwa maegesho katika maeneo mbalimbali ikiwemo Rusumo lakini haonyeshi kama kuna ununuzi wa kivuko. Naomba ufafanuzi.

Mheshimiwa Spika, naomba niwatakie kila la kheri Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara na utekelezaji mwema wa bajeti yao.

**MHE. SILIVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Spika, niendelee kuishukuru Serikali kwa jitihada zake za ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Spika, Jimbo la Kibaha Mjini ndio mji mpya unatakiwa kupokea msongamano wa kila aina. Tunayo barabara ya TAMKO Mapinga kupitia Pangani, Vikawe hadi Bagamoyo, ina ahadi ya lami na ni *shortcut* kubwa ya kwenda Bagamoyo, Mbezi, Tegeta, Boko ukitokea Morogoro na Mikoa yote itumiayo njia hiyo. Itaokoa msongamano katika *junction* ya Ubungo.

Mheshimiwa Spika, Mji wa Kibaha, Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani hauna lami kabisa licha ya ahadi ya mara kadhaa ya Serikali na ya Rais mwenyewe. Wananchi wa Kibaha na hasa Pwani wanaomba sasa ahadi hii itekelezwe.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kwa Mathias - Msangani kupitia Jeshini Nyumbu na Msangani ilikuwa na lami hapo awali, sasa haina, tunaomba ijengwe.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kongowe hadi Bagamoyo kupitia *Forest* ilikuwa ya kiuchumi kwa Kata ya Kongowe, sasa haifai, naomba ifunguliwe.

Mheshimiwa Spika, suala la matuta ya barabara linaleta kero kwa kuharibu magari na hata kuchelewesha safari. Tunaomba tuwe na matuta yenye ukubwa na upana unaofanana na ulio mwepesi kupitika bila kuharibu magari *(unformunit of standards).*

Mheshimiwa Spika, bado mizani ni kero na kwa pale Kibaha inaleta msongamano mkubwa. Nashauri sasa utaratibu wa kujenga mizani uwe usiopungua km.1 pembezoni mwa barabara kuu ili magari yaingiayo mizani yawe yanapanga foleni.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LOLESIA J.M. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri kwa hotuba nzuri, bila kumsahau Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri zinazofanyika katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Geita, Mheshimiwa Rais alipotembelea Geita Mjini, Nyarugusu na Katoro aliahidi barabara za lami na barabara hizo pia zimo ndani ya Ilani ya Chama

cha Mapinduzi ya mwaka 2010 – 2015. Kwa kuzitaja ni ile barabara ya kutoka Geita – Bukoli – Kahama. Bukoli – Nyarugusu na zile kilomita mbili katika Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Geita. Nimepitia kitabu cha makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2011/2012 nimeona bajeti ya matengenezo madogomadogo tu. Napenda kupata ufafanuzi katika hili wakati wa majumuisho.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Busanda, Kata ya Bukondo, KiJiji cha Bukondo kuna gati ambalo limeanza kutengenezwa kwa muda mrefu sasa halijakamilika. Naomba Wizara iangalie namna ya kukamilisha ujenzi wa gati hili.

Mheshimiwa Spika, pia barabara ya kutoka Chibingo kwenda Bukondo ambayo iko *TANROADS* Mkoa, kwa mwaka huu waangalie namna ya kuiboresha zaidi. Kwa mwaka jana pamoja na kutengewa fedha za matengenezo lakini barabara hii haikuwa nzuri sana ukilinganisha na miaka ya nyuma.

Mheshimiwa Spika, sina la ziada, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Spika, kuna barabara katika Jimbo la Kigamboni ambazo ujenzi wake ulianza lakini kwa sasa umesimama. Napenda kujua kuna mikakati gani ya kuzimalizia barabara zifuatazo:-

(1) Mission – Kijichi – Zakhem.

(2) Feri - Mji Mwema – Somangila – Kimbiji – Pemba Mnazi.

Mheshimiwa Spika, msongamano na foleni ya magari Jijini Dar es salaam *traffic flow* ni "*unidirectional".* Sote huwa na mwelekeo mmoja wakati wa asubuhi na wakati wa jioni. Kuna umuhimu wa kugawa hizi *movements* kwa kupangilia Mji. Masoko na maduka makubwa yajengwe nje ya Mji, *Flyover* haitaondoa tatizo la foleni Jijini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vivuko vya feri, huduma ya Pantoni pale Feri, Kigamboni imekuwa kero. Huduma hii imeelemewa na idadi kubwa ya watu. Kuna haja ya kuongeza Pantoni nyingine kwa ajili ya uchukuzi wa magari na abiria. Vilevile eneo la kusubiria abiria na magari kwa upande wa Kigamboni ni dogo, linahitaji kupanuliwa na usimamizi wa mapato katika kivuko hiki unahitaji kuboreshwa. Mapato mengine yanapotea kutokana na usimamizi hafifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia ya barabara ya Kilwa. Kuna wananchi waliobomolewa nyumba zao kupisha ujenzi wa barabara ya Kilwa tangu mwaka 2002, wananchi wanataabika kulipwa fidia ya bomoabomoa hiyo. Kwa wakati tofauti Waziri aliyepita wa Miundombinu, Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa (Mb) na Katibu Mkuu wake, Omari Chombo walithibitishia wahanga hawa kuwa watalipwa fidia. Je, wananchi hawa watalipwa lini? Naomba Serikali itoe tamko rasmi kuhusu suala hili.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mwalimu John Pombe Magufuli, sambamba na vitisho vyake kuwa watakuopinga Bajeti yake atamshitaki kwa wananchi wa jimbo husika.

Natambua jitihada za Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri wa Muungano kuhusu ujenzi hususani Mkoa wa Kigoma. Hata hivyo naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kuhusu fidia, Wizara imesisitiza siku zote kusimamia sheria za hifadhi ya barabara na kusisitiza wananchi waizingatie. Nakubaliana na dhana nzima ya Wizara hii katika hili lakini naomba Wizara itambue kuwa Serikali ni moja na ina Wizara zaidi ya moja. Kuna wananchi wamejenga maeneo ya hifadhi ya barabara lakini wana vielelezo vyote vya kisheria kutoka Wizara ya Ardhi. Ni vema Wizara ya Ardhi iache kugawa viwanja maeneo ya hifadhi na hili ni muhimu Wizara ya Ujenzi badala ya kuendelea kusisitiza wananchi wazingatie sheria ni bora ianze

kutoa msisitizo huo kwa Wizara ya Ardhi. Kama Serikali inatoa viwanja maeneo ya hifadhi ya barabara halafu Serikali hiyo hiyo ibomoe nyumba za wananchi maskini kwa hoja ya kuvunja sheria ni uonevu mkubwa kwa wananchi fukara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hilo, naomba kumkumbusha Waziri madai ya fidia kwa wakazi wa Kata za Kalenge, Kazuramimba na Kandonga kufuatia ujenzi wa barabara ya Kidahwe Uvinza. Malalamiko na vielelezo kuhusu uhalali wa madai yao vipo kwa Mkurugenzi wa Bodi ya Barabara tangu mwaka jana bila majibu yoyote. Wapo waliobomoa kufuatia tangazo la awali na matokeo yake imeleta shida kulipwa fidia kwa baadhi yao lakini wengine kulipwa chini ya kiwango, napenda kukujulisha kuwa palikuwa na tatizo la tathimini, kuna upungufu mkubwa sana katika mchakato wa tathimini. Naomba Mheshimiwa Waziri madai haya yalipo yapewe uzito ili maskini hawa wapate haki zao hata kama ni kidogo.

Mheshimiwa Spika, barabara ya kilomita 50 (Uvinza – Malagarasi), utakumbuka kuwa Mheshimiwa Rais Dkt. Jakaya Kikwete kwenye ziara yake ya uwekaji wa jiwe la msingi la Malagarasi na barabnara ya Kidahwe Uvinza nilimwomba kwenye mkutano wa hadhara Kazuramimba na kwa usikivu wake alikubali kujenga kilomita 50 yaani Uvinza hadi Darajani. Naomba kauli ya Serikali kuhusu utekelezaji wa ahadi hii ya Rais kwani haimo kwenye hotuba ya 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Daraja la Malagarasi (Ilagula) mara kadhaa Mheshimiwa Waziri amezungumza kuhusu nia ya Serikali ya kuhakikisha tunapata daraja hili kama moja ya njia ya kuhakikisha tunafikia lengo la kufungua Ukanda wa Kusini mwa Kigoma kuunganisha na Rukwa. Hii ni pamoja na kufikia lengo la Mheshimiwa Rais kama alivyozungumza katika ziara yake ya kuweka jiwe la msingi barabara ya Kidahwe – Uvinza. Aidha, napenda kujua gharama za ujenzi wa daraja hili hasa kwa kuwa upembuzi utakuwa umekamilika kama ilivyoahidiwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kivuko cha Ilagala, napenda kukujulisha kuwa hali ya kivuko cha sasa ni sawa na kuweka rehani roho za wananchi wanaokitumia. Hali ya kivuko ni mbaya, kimechoka sana na mara kadhaa kinasimama. Kwenye hotuba imeelezwa kuwa mchakato wa ununuzi unaendelea, naomba kauli ya Serikali ni kwa haraka kiasi gani mchakato huu utakamilika ili kuepusha uwezekano wa kivuko kilichopo kusababisha ajali.

Mheshimiwa Spika, mwisho nashauri Serikali itazame kwa udharura tatizo la madeni kwa wakandarasi na kufikia lengo jema la ujenzi wa zaidi ya kilomita 11,000. Hii ni pamoja na kuangalia uwezekano hata wa kupunguza *reserve* ya fedha za Serikali kutoka miezi sita hadi miezi mitatu tuweze kujenga nchi hii kwani faida za ujenzi huu ni kubwa na *multiplier effects* yake ni kubwa kwa uchumi unaojitegemea.

**MHE. JOSEPHINE T. CHAGULLA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema kuweza kupata nafasi ya kuchangia kwa maandishi hotuba iliyopo mbele yetu ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, napenda pia nimshukuru sana Waziri wa Ujenzi kwa hotuba yake nzuri pia kwa jitihada zake anazofanya katika ujenzi wa barabara nchini kote, tunampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, niwashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi kwa ushirikiano wao mzuri katika ujenzi wa Taifa. Baada ya kusema haya naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete kwa kuweza kusikiliza kilio chetu cha barabara sisi wakazi wa Mwanza, Geita. Tunamshukuru sana kwa kutujengea barabara ya Mwanza – Busagara – Sengerema – Geita – Kagera.

Mheshimiwa Spika, sisi wakazi wa Geita tunajivunia sana barabara hii ambayo ni kiunganishi kizuri sana. Huwezi kuamini kwa sasa mtu analala Geita na anafanya kazi Mwanza Mjini.

Baada ya shukrani hizo, naiomba Serikali itutengenezee barabara kutoka Busisi kupitia Buyangu – Nyang'wale – Karumwa na barabara kutoka Geita – kupitia Pori la Miyenze Bunegezi – Shinyamwendwa – Ikulwa – Nyang'wale – Karumwa ziwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara hizi ni kiunganishi kikubwa sana kwa wakazi wa maeneo haya. Tunaomba sana Serikali ituangalie kwa jicho la huruma.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika barabara nilizozitaja kutoka Geita – Karumwa kupitia Nyarubele Ligembe kuna daraja kubwa. Daraja hili ni bovu sana ukilinganisha na mahitaji yaliyopo. Daraja hili limejengwa chini ya kiwango kabisa kiasi kwamba mvua zikinyesha magari hayapiti pale maana limejengwa na mbao pamoja na vyuma kidogo sana.

Mheshimiwa Spika, daraja hili la Ligembe mvua zikinyesha ni hatari sana na hasa kwa watoto wa shule ambao huwa wanasoma ng'ambo yake yaani Kijiji cha Kitongo.

Mheshimiwa Spika, namuomba sana Waziri mwenye dhamana hii aweze kututengenezea daraja hili la Ligembe Wilaya ya Nyangw'ale.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

**MHE. SELEMANI S. JAFO:** Mheshimiwa Spika, kiambatanisho cha ramani kilichopo katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa Waziri kimebainisha fika kwamba japokuwa Mkoa wa Pwani una mtandao mkubwa wa barabara za Mkoa lakini hakuna tabaka la lami katika barabara zote za mkoa kulinganishwa na mikoa mingine. Sasa naiomba Serikali ibaini tatizo hili na kufanya maamuzi sahihi katika mgawanyo wa rasilimali katika mwaka huu wa fedha kwa kuhakikisha kwamba fedha zote zilizoidhinishwa kwa Mkoa wa Pwani ili kufanikisha japo hizo kilomita chache zilizotengwa kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isione ni vyema kuweka mtandao wa barabara ya lami itakayoanzia Mlandizi Mzenga – Kisarawe ili kupunguza msongamano wa magari ya mizigo kutoka Mlandizi hadi Ubungo?

Mheshimiwa Spika, ili kukuza uchumi na kulinda thamani ya shilingi yetu ninapendekeza kwamba makandarasi wa ndani ya nchi yetu wenye uwezo wapewe kazi za ujenzi wa barabara kufanikisha ukuzaji wa uchumi kwani fedha zitabaki ndani ya nchi yetu na fedha kuhifadhiwa katika benki zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa nini Serikali isione ni vyema kutumia majeshi yetu katika ujenzi wa barabara na madarja? Tumeona ujuzi mkubwa uliopo katika majeshi yetu ambayo yanaweza kutujengea madaraja na barabara na hivyo kulinda rasilimali zetu na kulinda uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, katika kiambatanisho, eneo la ujenzi wa barabara za mkoa za lami kwa Mkoa wa Pwani ni barabara moja tu ya Kibiti – Utete, Yamuaje ndio imetengewa pesa. Je, barabara ya Kisarawe - Maneromango yenye urefu wa kilomita 54 kwa nini haikutengewa fedha kwa ajili ya matengenezo ya lami ikijulikana wazi kwamba barabara hii imeainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010?

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa sana awali ya yote shikamoni. Bajeti nimeisikia na nimeipitia kwa umakini. Naomba mnisaidie kuelewa juu ya ile barabara yetu ya Kidahwe – Kasulu.

Mheshimiwa Spika, nimeona kuwa mmetenga shilingi milion 2,108.27 tu kwa ajili ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi yenye *total kms 300.* Je, fedha hizo zitatolewa pamoja na zile za mwaka jana 2010/2011 shilingi milioni 6,086.50 ambazo zikijumlishwa na hizi za mwaka 2011/2012 yaani sshilingi milioni 6,086.50 (2010/2011) na shilingi milioni 2,108.27 (2011/2012) sawasawa na jumla ya shilingi 8,194.27.

Mheshimiwa Spika, ikifanywa hivyo na barabara hiyo ikaanza kujengwa kuanzia Kidahwe – Kasulu hadi Nyakanazi itakuwa ni hatua nzuri. Lakini mkitoa hizo za mwaka huu tu (2011/2012) shilingi milioni 2,108.27 itakuwa siyo *fair* wakubwa zangu yaani mtakuwa mmefanya uchakachuaji mkubwa wa kile kiasi cha mwaka jana yaani shilingi milioni 6,068.50 na kuwa hiyo shilingi milioni 2,108.27. Najiuliza tunasonga mbele au tunarudi nyuma? Shilingi milioni 6,086.50 ilikuwa kwa kilomita 50 tu.

Mheshimiwa Spika, naomba mnisaidie ufafanuzi iwapo itatolewa na ile ya mwaka jana au la kwa ajili ya kilomita 50 zilizokuwa zimetengewa hizo shilingi 6,086.50 kwa ajili ya Kidahwe – Kasulu.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha wakubwa.

**MHE. MAJALIWA K. MAJALIWA:** Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukupongeza kwa mipango mizuri kupitia Bajeti yako ya mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kama ulivyoeleza kwenye hotuba yako ya kutoendelea kujenga barabara za lami zaidi kwenye mikoa yenye barabara nyingi za lami na ujenzi huo sasa uelekezwe mikoa ya Kusini ikiwa Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, mkoa una wilaya muhimu ambayo inazalisha sana ya Ruangwa ambayo haina barabara hata moja ya lami.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia ramani yako kuna umbali wa kilomita 58 ili kuiunganisha wilaya hiyo na barabara kuu itokayo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, wilaya hiyo ndio inayosafirisha mazao ya chakula na biashara kwenda Mjini Lindi na Mkoa wa Mtwara.

Mheshimiwa Spika, ni vyema sasa barabara hiyo ikatengewa fedha kwa ajili ya kuijenga kwa kiwango cha lami ili wananchi wa Ruangwa hasa wakulima waweze kusafirisha mazao yao kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, ni mategemeo yangu kuwa mwisho mwa hotuba yako ya Bajeti hii nitapata marejesho ya hoja hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninapenda kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kwa kuwa makini katika kusimamia kazi zinazoendelea nchi nzima za ujenzi wa barabara za lami na zile za barabara za vijijini. Wananchi wanaridhika na juhudi hizi ili nchi yetu iweze kupitika katika maeneo mengi nyakati zote.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizi zipo changamoto zinazozikabili Serikali hususani Wizara ya Ujenzi. Ujenzi wa barabara ya Nyamwage – Somanga kwenye barabara ya Dar es Salaam – Lindi – Masasi.

Mheshimiwa Spika, umalizaji wa kilomita 60 zilizobaki umegubikwa na maswali mengi yasiyopata majibu sahihi juu ya kumalizika kwake. Mkandarasi amekuwa akilalamika kwa kutopatiwa fedha za kufanyia kazi pamoja na kuwasilisha *certificate* zake.

Mheshimiwa Spika, kazi hii haiwezi kukamilika kama Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alivyoahidi kama mkandarasi hatolipwa fedha. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie suala hili kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu alama za X na fidia za waathirika, ni kweli Mheshimiwa Waziri anafuata sheria katika kutekeleza kazi zake lakini ni lazima utu uzingatiwe katika utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, ni lazima vitisho visitumike katika utekelezaji wake inayofanya wananchi ambao hawaelewi taratibu na sheria kujawa na hofu na kusababisha maradhi ya moyo na shinikizo la damu kwa mshituko unaowakabili wakati watendaji wa Wizara ya Ujenzi wanavyowafanyia kwa vitisho wakati wakiweka alama za X.

Mheshimiwa Spika, mfano wananchi wa Mvomero wameweka X katika nyumba zao na kuonyesha kwenye nyumba zao eneo litakalobomolewa cha kushangaza watumishi wa *TANROADS* Mkoa wa Morogoro wanawatisha wananchi, hata wananchi wenye hati kuwa nyumba zao zitabomolewa bila kupata fidia. Ninao mfano wa Mzee Hilali Anton Kiteu, *Box 5 Mvomero, Plot No.367 Block 'K'* Kipogoro Mvomero *minor settlement Morogoro District.*

Mheshimiwa Spika, ningependa kupata majibu ni kwa nini wananchi kama huyu mzee Hilali asipate fidia? Ninaomba maelezo barabara ya Uliwzi ianziayo Mtwara – Tandahimba – Kimwavira – Sindamo katika Jimbo la Lindi ihudumiwe na *TANROADS* Mtwara.

Mheshsimiwa Spika, kwa sasa barabara hiyo iliyo kando kando ya Mto Ruvuma ni muhimu kwa wakazi waishio katika vijiji vya Ulindi. Cha kushangaza eneo linaloanzia Mtwara Vijijini linahudumiwa na *TANROADS* na eneo linalopita katika Jimbo la Lulindi hadi Jimbo la Nanyumbu halihudumiwi na limetekelezwa.

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Spika, wilayani kwangu Nanyumbu kuna mradi wa ujenzi wa daraja *(Construction of Lukwamba Bridge along Mnongodi – Ndenganamedi Kilimahewa – Michenjele border road* (Uk.141 – 142), Serikali imekuwa ikitoa ahadi ya ujenzi wake tangu niingie Bungeni mwaka 2006. Mara ya mwisho zilitengwa shilingi milioni 120 lakini hazikufanya kazi yoyote na hakuna chochote kinachofanyika licha ya ahadi lukuki zinazotolewa na Meneja wa *TANROADS* Mtwara. Hivyo ninaomba Wizara iwaeleze wananchi wa Nanyumbu na hasa wa Kata ya Napacho kuwa ni lini daraja hili litaanza kujengwa na ni lini litaisha kujengwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo ni matumaini yangu makubwa kuwa Serikali itatoa majibu ya uhakika juu ya suala au hoja yangu hii wakati Waziri utakapojibu hoja za Wabunge na kama sitapata majibu ya kuridhisha nitatoa shilingi kwenye mshahara wa Waziri.

Mheshimiwa Spika, hoja hii nitaunga mkono pale tu nitakapopata majibu ya kuridhisha.

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, sina budi kumshukuru Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba yake kwa vielelezo na kwa uwazi kabisa, pia sina budi kusema kwamba mpango huu unaleta matumaini kuhusu kukamilisha miundombinu iliyo muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kwa kusema kuwa utungenezaji wa barabara ya changarawe, inatia hasara kubwa kwa Serikali, kwani barabara hii sio ya muda mrefu. Napenda kutoa wazo kuwa ni vyema kujenga barabara zote za lami pamoja na kwamba kutakuwepo ucheleweshaji huu kutakuwepo na uhakika wa barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikataba, Serikali inakuwa inaingia hasara kubwa sana kwa mikataba mibovu. Mheshimiwa Waziri ninakuomba kwa makusudi uangalie vyema na kwa undani zaidi mikataba ambayo haina nia nzuri, mikataba isiingie mpaka kwanza upitiwe na wataalam maalum na hivyo kuzingatia mbinu za wakandarasi wasio waaminifu.

Mheshimiwa Spika, matuta ni muhimu sana kwa kuwadhibiti madereva kuendesha gari bila ya kujali mazingira.

Mheshimiwa Spika, nami naungana na Kamati ya Miundombinu kuondoa kabisa matuta ya rasta na pia ukubwa wa matuta kwani yanaweza kusababisha hasara kubwa kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msongamano wa magari mijini unadhoofisha uchumi wa Taifa. Suala la barabara katika miji mikuu, ni ngumu sana kayatatua pamoja na utanuzi wa barabara, na baadhi ya miundombinu, kutasaidia kidogo tu, lakini hakutaondoa msongamano uliopo sasa.

Mheshimiwa Spika, jambo la msingi ni Wizara hii kushirikiana na Wizara ya Waziri Mkuu, kutafuta njia mbadala ya kupeleka huduma muhimu maeneo mbalimbali ili kupunguza sababu za kufuatilia kila kitu miji mikuu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa ukuaji watu *(Population Expansion),* hata njia ipanuliwe lakini baadae watu wataongezeka katika maeneo hayo. Ufumbuzi mzuri kwa kuzingatia mahitaji ya watu na kuwapelekea huduma muhimu na kutanua miji mingine na kuweka huduma za muhimu katika miji mipya, ili kupunguza watu kuelekea miji mikuu kwa baadhi ya mahitaji.

Mheshimiwa Spika, ni maoni yangu kuwa mapendekezo haya kama yatazingatiwa yatasaidia kuleta mabadiliko. Ahsante sana.

**MHE. ANNAMARYSTELLA J. MALLAC:** Mheshimiwa Spika, barabara ni kiungo muhimu sana katika kuleta mafanikio ya wananchi hasa katika kurahisisha usafirishaji wa mazao kutoka shambani na kupeleka mjini kwa ajili ya matumizi na kutafuta soko. Vilevile Wizara zote ili zifanikiwe lazima ziongozwe na kusimamiwa na Wizara hii ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, unapokwenda kutafuta zahanati lazima upitie kwenye barabara, kilimo mashambani lazima upitie barabara, elimu shuleni lazima upite kwenye barabara na kadhalika hivyo Ujenzi ni Wizara nyeti sana inahitaji ipewe fedha za kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii ya mwaka 2011/2012 sijaona fedha zilizotengwa kwa ajili ya barabara za Mpanda – Karema; Mpanda – Mwese, Mpanda – Mpimbwe. Barabara hizi ni muhimu sana kwa maendeleo ya Mkoa wa Katavi. Naomba barabara hizi zisifumbiwe macho na Wizara kwani kama hazitopata huduma na kwa kuwa ni barabara za changarawe. Mvua zitakapoanza kunyesha zitaharibika vibaya.

Mheshimiwa Spika, naiomba pia Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi itenge fedha kwa ajili ya upanuzi wa barabara ya Mpanda – Mwese, kwani barabara hii ni finyu sana.

Mheshimiwa Spika, Serikali itambue kuwa barabara za vijijini ndizo zinazotoa mazao mashambani na kupeleka mjini hivyo Serikali itenge fedha za kutosha kuipatia Halmashauri ya Mpanda Vijiji ili izihudumie barabara za vijijini nazo ni barabara ya Mkokwa hadi Mnyagara; barabara ya Fikonge hadi Bugwe; barabara ya Mpanda ndogo hadi Ngoma Lusambo; barabara ya Kapanga hadi Bujombe na barabara ya Kalilankulunkulu hadi Kamsanga.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi zimekuwa zikitengenezwa bila mifereji hivyo basi naiomba Serikali inapotenga fedha za barabara itenge fedha za mifereji katika Halmashauri zote za wilaya na miji.

Mheshimiwa Spika, mwisho naiomba Serikali irudishe mpango wa zamani wa kujenga makambi ya ujenzi katika barabara kila baada ya kilomita 16. Magenge au kambi hizi zitakuwa na watu watakaofanya kazi za dharura mara tu barabara inapoharibika, mtindo huu ndiyo uliyokuwa ukitumika zamani.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kujitahidi kuboresha na kupanua barabara zetu hasa katika Jiji la Dar es Salaam bado jiji hilo linakabiliwa na upungufu mkubwa sana wa barabara kwa sababu asilimia kubwa ya watu wote wanategemea katika Jiji la Dar es Salaam kwa maofisi, viwanda na watu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, karibu asilimia ya Pato la Taifa linatoka Dar es Salaam na ndio maana hali sasa ya mkusanyiko wa watu ni mkubwa sana na ndio tatizo hilo la msongamano halitaondoka kwa sababu watu wote wanakimbilia mijini, kwa nini Serikali isitafute mipango miji

ambayo itafutwe sehemu za makazi ya watu ambayo zijengewe majumba ya ghorofa ambazo zitachukua karibu familia nyingi na pia kuondoa ofisi zote za chama katika Jiji la Dar es Salaam na baadhi ya ofisi za Serikali zijengwe nje ya Dar es Salaam kwani Tanzania ni kubwa na ina maeneo mengi sana ya wazi. Kwa nini Serikali isitilie mkazo huu wa mipango miji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mabasi ya kasi, ni rai nzuri sana ya Mheshimiwa Rais lakini tukumbuke kwamba Serikali itagharamika sana kwa fidia ya ubomoaji wa nyumba kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo ya basi liendalo kwa kasi.

Mheshimiwa Spika, ushauri, kwani haya mabasi yaendayo kwa kazi yasitengenezewa zile njia za juu, kama vile nchi za wenzetu na kama ujenzi wa daraja la Kigamboni litakavyojengwa. Lingine Serikali iwe na ule utaratibu wa kwanza kujenga majumba ya ghorofa, halafu wawahamishe wananchi walipwe fidia kwa kupewa nyumba katika ghorofa hizo kulingana familia yake. Hapo kidogo itakuwa nafuu. Halafu ndio hizo barabara zijengwe lakini ukisema umlipe fidia ahame utawalipa wangapi fidia na watu wote wamejikusanya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu majengo Dar es Salaam, tatizo Tanzania labda hatuna *plan* za miji yetu na ndio maana kila mtu anajenga atakavyo na matokeo ya sasa watu wengi, magari tele, *parking* za magari kigodo. Ili tuwe na *master plan* ya majiji ghorofa zinakuwa za aina moja tu kama nchi za wenzetu na hata kama mtu ni tajiri lakini afuate *master plan* ya mji.

Mheshimiwa Spika, leo Dar es Salaam kila mtu kajenga atakavyo shaghala bagala tu. Matokea yake hali ya nchi imebadilika, joto jingi, msongamano wa watu na magari imekuwa tafrani tu. Ni lazima tulitafutie ufumbuzi suala hili kwani ni hatari kwa nchi inayoendelea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za ndani, katika hilo hilo Jiji la Dar es Salaam baadhi ya barabara zake hazifai hata ukisema nakimbia foleni katika barabara kuu. Nijuavyo barabara zile huwa ni wajibu wa halmashauri za wilaya na wilaya zinapewa ruzuku, kwa nini hizi ruzuku hazitumiwi kwa malengo yaliokusudiwa na hakuna ufuatiliaji na ukaguzi wa kila mwaka na ndio maana wananchi wanakosa imani na Serikali yao. Kumbe watendaji ndio wanarudisha nyuma maendeleo hayo.

Mheshimiwa Spika, hotuba yako nzuri na ina malengo na mategemeo mazuri sana. Tatizo ni utekelezaji ndio mgumu na tatizo kubwa upatikanaji wa pesa ambazo mara nyingi huwa tunategemea kwa wafadhali.

Mheshimiwa Spika, mwisho ni kuhusu uzito wa magari. Katika hotuba yako Mheshimiwa Waziri umekiri kwamba kuna baadhi ya magari yana uzito mkubwa na kuna baadhi ya magari yamepigwa faini na barabara zetu tunaziona kwamba hazina kiwango cha kubeba magari yenye uzito mkubwa na maana barabara zetu utakuta zina milima na mabonde. Kwa sababu hazina uwezo barabara zetu wa kupita malori yenye uzito mkubwa.

Mheshimiwa Spika, swali ulisema kuna magari yamepigwa faini kwa kuwa na uzito mkubwa, je, magari hayo hayatembei tena na yamerejeshwa yanakotoka au yapunguzwe uzito? Je, katika mizani hakuna hujuma inayofanyika kuyaachia magari yaliyozidi uzito?

Mheshimiwa Spika, huoni kwamba kuyalea magari haya yaendelee kupita katika barabara zetu ni chanzo cha kuharibika kwa barabara hizo?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. HAMAD ALI HAMAD:** Mheshimiwa Spika, mimi zaidi katika Wizara hii ya Ujenzi naomba nisisitize kwamba kwa umuhimu wa Wizara ukizingatia ina changamoto nyingi pale tunapokuwa tukizungumzia ujenzi na au upanuzi wa barabara kwani maeneo mengi yana makazi ya watu hivi sasa jambo ambalo hulazimisha kuchukua hatua ngumu na za maamuzi magumu kwani mara nyingi huwa wameshajistawisha.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa Serikali tayari imeshaamua kwamba Dodoma ndio mji mkuu, hivyo basi ili kuonesha kwa vitendo jambo hilo, ni vyema basi kila kile Serikali inachotaka kufanya

ijiulize, maeneo gani tunataka kufanya jambo hilo na ni vyema kila wakati Serikali ikawa inafikiria kwamba ili mji uweze kuelekea kuwa mji basi au lazima pawepo na majengo ya kisasa na yenye sifa.

Mheshimiwa Spika, si vyema na haielekei kabisa kwa Serikali inayojigamba kwa utawala bora ikawa haitambui juu ya maeneo yake. Kuna mpango wa Serikali wa kujenga nyumba 28 za kisasa za viongozi katika eneo la Dar es Salaam, eneo hilo la Dar es Salaam tayari msongamano ni mkubwa na kwa kuwa tumeshaamua Dodoma kwamba ndio mji mkuu, naishauri Serikali nyumba hizo sasa zijengwe Dodoma badala ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu msongamano wa magari, hivi sasa hili imekuwa ni tatizo kubwa karibuni maeneo yote ya nchi yetu, hivyo basi ni vyema Serikali ikaunda Wizara maalum itakayosimamia na kuunda miundombinu mizuri ya kudhibiti hali hii kinyume na ilivyo hivi sasa kwamba haieleweki hasa ni nani ni mwenye jukumu hili, jambo ambalo linaleta tatizo na kuonekana ni vurugu tupu kwani wasimamizi ni wengi. Ahsante.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, hongera kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara na taasisi zote zilizo chini ya Wizara kwa kazi nzuri mnayoendelea hivyo hivyo.

Msheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri (Uk.162 – kiambatanisho Na.4) daraja la Mto Simiyu katika barabara ya Magu - Mahaha lilitengewa shilingi milioni 100 mwaka 2010/2011 ambazo hazikutolewa na mwaka huu 20011/2012 wa fedha daraja hili limetengewa shilingi milioni 96.45. Mimi nauliza fedha zilizotengwa mwaka uliopita kama zilitolewa zilifanya kazi gani na kama hazikutolewa kwa nini?

Mheshimiwa Spika, fedha zilizotengwa mwaka huu yaani shilingi milioni 96.45 zimetengwa kwa ajili gani kwani ni kidogo sana?

Mheshimiwa Spika, ni lini sasa daraja hili litatengewa fedha za kutosha na kuanza utekelezaji kama vile ujenzi?

Mheshimiwa Spika, napongeza juhudi za Wizara kuunganisha wilaya na wilaya. Mfano kuunganisha Wilaya za Magu, Kwimba, Maswa na Bariadi. Bajeti hii inatekeleza hii kwa uzuri. Nimewahi kulipigia hili kelele huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, kwa nia hiyo hiyo sikuona kwenye Bajeti hii ya mwaka 2011/12 fedha zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara itakayounganisha Makao Makuu ya Mkoa wa Mwanza na Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Simiyu. Napendekeza Wizara itenge fedha hizi katika Bajeti hii angalau kuanza ujenzi wa daraja la Mto uliopo baada ya Kijiji cha Mahana (kwa kuwa barabara ninayoshauri ichaguliwe iwe ile ya Magu - Mahaha – Bariadi.

Mheshimiwa Spika, barabara inayounganisha Wilaya ya Kwimba na Magu kupitia barabara ya Kadashi – Nyang'hanga – Lumeji Magu inasababisha kipande cha barabara kati ya Lumeji na Magu iharibike mara kwa mara. Naleta ombi maalum kwa Wizara tusaidiane kufanya ubunifu kupunguza gharama kwa kuitengeneza njia ya Magu (kwa *Area Commissioner)* – Buhumbi - Nyang'honge – Nyashana - Kadashi.

Mheshimiwa Spika, tatizo kubwa ya barabara hii ambayo ingepunguza sana pia muda wa kusafiri kutoka Magu kwenda Wilaya ya Kwimba na *vice versa)* ni kwenye mbuga baada tu ya kutoka kwenye nyumba ya Mkuu wa Wilaya. Ninaomba Wizara *(TANROADS)* watusaidie kuja kufanya tathmini ya kimahesabu za kifedha ili tuweze kusaidiana kutafuta fedha kwa ajili ya kutengeneza eneo hili walau kwa mwaka wa fedha ujao. Barabara hii ni ya Wilaya lakini naamini Wilaya haina uwezo wa kifedha na utaalamu wa kutengeneza eneo hili korofi. Hili ni ombi maalum la wananchi wa Jimbo la Magu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa fedha zilizotengwa na Wizara kwa ajili ya barabara ya Lumeji - Nyashana milioni 67.5, Magu – Kabila - Mahaha, Nyanguge - Kayenze na kadhalika. Naomba usimamizi uwe mzuri na kwa kweli wananchi na mimi binafsi naridhika na

jitihada za Meneja wa Mkoa Bwana Kadashi kwa kazi nzuri anayofanya. Ningependa kumuomba awashughulikie baadhi ya wakandarasi wababaishaji, wanaoshinda makoridoni wakizungusha wadau pamoja na hayo Bwana Kadashi amejitahidi lakini inabidi tumsaidie.

Mheshimiwa Spika, ikiwezekana nitapenda kuomba *appointment* baina yako Mheshimiwa Waziri/Naibu Waziri ukutane na Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Mwanza (mimi nikiwa Mwenyekiti wao) ili waje waeleze kero zao mbalimbali, likiwemo hili nililolitaja.

Mheshimiwa Spika, hongereni sana, *good work/welldone keep it up.* Naunga hoja mkono 100%.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kazi nzuri sana. Barabara ya kutoka Kibena - Njombe mpaka Lupembe ni barabara muhimu sana maana inaunganisha mikoa miwili, Mkoa wa Njombe na Morogoro kupitia Lupembe. Ina uchumi mkubwa sana kila siku hupita magari zaidi ya 150 – 200 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali kwa kazi nzuri inayofanya kuhusu kujenga barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, kwenye Jimbo langu Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi Mji wa Makambako kuweka lami (kilomita tano sijaona katika Bajeti hii).

Mheshimiwa Spika, katika haya mawili naomba Waziri atakapofanya majumuisho nipate majibu.

**MHE. ALI KHAMIS SEIF:** Mheshimiwa Spika, Wizara imejipangia miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara hapa nchini kwa kutegemea fedha shilingi trilioni 1.25; kati ya hizo shilingi 629,870,193,000 ni fedha kutoka nje. Wasiwasi wangu fedha kutoka nje si za kuaminika sana na kwa maana nyingine bado hakuna uhakika na utekelezaji wa miradi ambayo kwa macho inaonekana ni mingi mno. Je, Wizara inajipanga vipi pindi wahisani hawakutowa fedha kama inavyotegemewa na Wizara?

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mizani katika barabara kuu ili kuzilinda barabara zetu na uzito wa kupitiliza, inavyoonekana kuna mtindo wa baadhi ya mabasi yanapokaribia kwenye vituo hivyo baadhi ya abiria hupunguzwa kwenye mabasi, mbinu hii Wizara ya Ujenzi mnaelewa? Je, Serikali imekamata gari ngapi angalau kwa mwaka 2010/2011 zilizozidisha uzito wa magari yao?

Mheshimiwa Spika, Jiji la Dar es Salaam usafiri wa abiria imekuwa ni kero mno na wananchi pamoja na Taifa kwa ujumla tunapata hasara kutokana na usafiri wa Jiji la Dar es Salaam. Ni muda mrefu upo mpango wa mabasi yaendayo kwa kasi uanzishwe lakini mpaka leo mradi huo haujanzishwa. Nii lini mradi huu utaanzishwa?

Mheshimiwa Spika, uko mtindo wa *TANROADS* kuingia katika mikataba na makapuni ya ujenzi wa barabara bila ya kuwepo fedha, haya yametokea sana mwishoni mwa mwaka 2010, katika hali hiyo Serikali huwa ina madeni makubwa. Pia gharama za barabara huongezeka maradufu kwa mtindo wa kuingia mikataba wakati Serikali haina uwezo. Ni vyema tuwe na miradi michache lakini yenye fedha ya kuweza kuitekeleza.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweka matuta katika barabara kuu ili kudhibiti mwendo kasi. Ni suala zuri lakini matuta mengine ni makubwa kiasi ambacho gari nyingine zilizo ndogo hugoma. Ni vizuri matuta hayo yawe kwenye viwango vinavyolingana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mikakati ya ujenzi wa barabara pia suala la ubora wa barabara hizo ni muhimu, inashangaza baadhi ya barabara utaona zinafanyiwa matengenezo hata kabla ya kufunguliwa. Barabara zinatumia fedha nyingi kwa hivyo ihakikishwe kuwa barabara hizo zinakuwa kwenye kiwango kinachostahili. Ahsante.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Spika, pongezi. Kuhusu suala la msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam, hakuna asiyejua wala asiyeona kuwa Dar es Salaam hivi sasa ni Jiji la maudhi kwa suala hilo, sina haja ya kueleza sana ila nashauri ichukuliwe hatua za dharura za kuondoa msongomano hadi hapo itakapochukuliwa hatua za kudumu.

Nashauri kwamba gari zote zinazoingia jijini hasa maeneo ya Kariakoo hadi Kivukoni zisiruhusiwe kuweka *(parking)* kusiwekwe kabisa gari pembezoni ya maduka, maofisi na majumbani gari ziwashushe watu na kupangiwa sehemu maalum ya *parking*. Vilevile askari wa barabarani wakae sehemu zote zenye kukatiza magari *(keep left)* kwa njia kuu na njia ndogo ndogo wakasaidia kupitisha magari kwa mpango maalum tena wa haraka haraka na kama askari hao hawatoshi, nashauri waongezwe.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ujenzi wa Daraja la Kigamboni, kwa hili napongeza hatua zilizofikia, lakini nashauri Serikali kupitia Wizara hii kufanya maamuzi magumu, nashauri kwa huo mchango uliopatikana kutoka *NSSF,* basi Wizara ianze na ujenzi wa pesa hizo hizo kwanza na wasisubiri hadi zitimie kwani naamini ujenzi ukianza Serikali itajua wapi pesa nyingine zitapatikana au hata wahisani wataweza kujitokeza kusaidia ujenzi huo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la majengo ya Serikali, nashauri kuanzia sasa majengo yote ya Serikali yaliyokuwa hayajajengwa basi ni vyema yakajengwa Dodoma na yale ya huko Dar es Salaam yamalizwe haraka. Pia kwa kuwa sisi Wabunge kutoka Zanzibar tunakuwa tunapata taabu sana ya makazi kwa Jiji la Dar es Salaam na Dodoma, tunashauri tupatiwe nyumba za kuishi za Serikali ili kupunguza ukali wa maisha, kwani hivi sasa posho yote inaishia kukodi mahotelini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la alama za barabarani hususan rasta, imeonekana kuwa alama hizo zinaharibu sana gari za wananchi, hivyo nashauri hizi rasta ziondolewe na yawekwe matuta tu na badala ya rasta ziwekwe alama ya *zebra.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la fidia za wananchi, nashauri Serikali ifanye kwa makusudi kuwalipa watu wote ambao wanaidai Serikali yao malipo ya fidia ya nyumba na mazao kwani Serikali ikilipa fidia itatoa imani kwa wananchi.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Spika, pili nampongeza Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Dkt. John Magufuli na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kwa kuwasilisha hotuba nzuri ya Bajeti. Pia nawapongeza Wizara ya Ujenzi kwa kusimamia vizuri miradi yote ya barabara nchini.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2010/2011 Serikali ikamilishe ujenzi wa barabara ya *Old Shinyanga*/Nyasamba ambayo ni njia mbadala ya kuelekea Mwanza kupitia Jeshi la 82KJ. Kuhusu ujenzi wa mtandao wa barabara za Manispaa ya Shinyanga kwa kiwango cha lami kupitia mfuko wa barabara, nawashukuru kwa kuwa mmetenga fedha katika Bajeti ya mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, nawatakia utendaji mwema.

**MHE. GOODLUCK J. OLE-MEDEYE:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Mbunge wa Chato na Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe Mbunge wa Kyela kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuongoza Wizara hii muhimu kwa ustawi na maendeleo ya Taifa letu.

Niwapongeze pia Katibu Mkuu Balozi Herbert Mrango na Naibu Katibu Mkuu Dkt. John Ndunguru kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa watendaji wakuu wa Wizara hii. Vilevile nawapongeza Wakurugenzi na watendaji wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara kwa kuwasaidia viongozi wakuu wa Wizara kupanga na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria na kanuni za ujenzi nchini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa barabara, nimeisoma hotuba ya Waziri pamoja na mpango wa maendeleo wa miaka mitano (2011/2012 – 2015/2016). Mipango ya barabara imeainishwa iliyotekelezwa mwaka 2010/2011 na itakayotekelezwa kuanzia mwaka 2011/2012 – 2015/2016. Kwa kuzingatia idadi ya miradi iliyopangwa kutekelezwa na kiasi cha fedha zilizotengwa, naomba Wizara itoe maelezo juu ya vigezo vinavyotumika kuteua miradi itakayotekelezwa na kupanga fedha za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuchambua hotuba ya Waziri na ziara nilizofanya maeneo mbalimbali nchini nimebaini kuwa hakuna uwiano kwenye mgawanyo wa rasilimali. Yapo maeneo ya nchi ambayo yamepata zaidi na yanaendelea kupata kuliko mengine. Naomba Serikali irekebishe kasoro hizi ili kuwepo uwiano wa maendeleo hususan miundombinu nchini.

Mheshimiwa Spika, barabara Mkoani Arusha imetajwa kwenye hotuba ya Waziri, hata hivyo sijaona mpango mahsusi ule kujenga barabara za mkoa huo. Uk. 223 ramani inaonesha kuwa ni kilomita 28 tu za barabara za mkoa ndizo zenye lami. Kukosekana kwa miundombinu ya barabara mkoani Arusha kumekwamisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Wilaya za Arumeru, Monduli, Longido na Karatu hazina kiwanda hata kimoja kwa sababu wawekezaji wanaogopa adha itakayowapata kwa kuwekeza pasipo na barabara kwani hawataweza kusafirisha bidhaa watakazotengeneza.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itueleze mipango yake ya kuingiza barabara za Mkoa wa Arusha kwenye mpango na kutenga fedha kwa ajili ya utekelezaji. Barabara zifuatazo zipewe kipaumbele:-

(i) Oldonyasambu – Ngarenanyuki;

(ii) Arusha – Losinyai;

(iii) Arusha - Simanjiro kupitia Oljoro;

(iv) Arusha – Themi ya Simba (kupitia Bwawani – Karangai kwenye *Nelson Mandela main Campus – (proposed);* na

(v) *Kilimamoto jet* – Monduli.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utekelezaji wa ahadi ya Rais, Mheshimiwa Rais alipotembelea Halmashauri ya Arusha tarehe 19/9/2010 aliahidi kuwa atasaidia ujenzi wa barabara ya Ngaramtoni – Sambasha kwa kiwango cha lami. Aidha, aliahidi kuwa barabara zote za wilaya zitaimarishwa ili zipitike mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara itusaidie kutekeleza ahadi hii. Kero kubwa kwa barabara za wilaya ni Mianzini – Tinubolo; *Moshi Road jet – Olgilai Masama Spring* - Ng'iresi; Ngulelo – Bangeta – Njoranga; Kilimamoto – Musa – Nengung'u; Kijenge - Nduruma – Bwawani na Mbauda – Losinyai.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Babati – Dodoma, barabara hii ni muhimu sana kwa sababu inaunganisha Makao Makuu ya nchi na Makao Makuu ya Afrika Mashariki. Kiasi cha fedha kilichotengwa shilingi bilioni 10 ni kidogo sana hivyo kwamba kwa mtu mwenye uelewa wa ujenzi ataona kuwa Serikali haina *commitment* ya kutosha ya kukamilisha ujenzi wa barabara hii. Barabara hii ni ya siku nyingi ambayo niliitumia wakati nikiwa mwanafunzi wa *Iyunga School.* Naomba Serikali itenge fedha za kutosha ili ikamilishe barabara hii.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Arusha – Moshi – Holili. Nashukuru, Serikali kwa uamuzi wa kupanua barabara hii ili kuharakisha maendeleo. Naomba mpango wa awali wa kupitisha barabara hiyo Kilimamoto – Musa – Kisongo na kwenda Usa irejewe kwani itafungua milango ya uwekezaji kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya viwanda eneo la Musa na Kisongo.

**MHE. *ENG.* ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, ninapongeza Wizara kuanza ujenzi wa barabara kilomita 85 Tabora – Nyahua kwa shilingi milioni 7,000.64 sehemu kubwa ya

barabara hii iko jimboni Igalula, ombi langu, kutoka Nyahua mpaka Chaya mpakani mwa Singida Wilaya ya Manyoni mwaka ujao itengewe fedha ili lami iungane na sehemu ya Itigi – Chaya ambayo inawekwa lami. Pia kifusi kinachowekwa kutoka kwa Alex njia panda ya Malongwe kuelekea Chaya ni vumbi hivyo magari ambayo siyo *four wheel* yanazama wakati wa kiangazi. Ikinyesha mvua tope litakwamisha magari *borrowed pit* iwe na ubora na siyo kuchukua pembeni mwa barabara.

Mheshimiwa Spika, Meneja *TANROADS* na Mhandisi Mshauri wawasimamie wakandarasi hawa ili kifusi bora kipatikane na kushindiliwa vizuri. *Quarry* nzuri zipo katika barabara hii tuachane na vumbi ili mwaka mzima ipitike tukisubiri lami. Itigi – Tabora sasa magari mengi yanaitumia ukilinganisha na kutumia Itigi – Ziba – Mwisi – Ndala – Puge – Tabora. Muda, mafuta na uharibifu wa magari *(tear and wear)* unapungua kwa kupita njia hii fupi na ya mkato. Uchumi wa vijiji inapopita barabara ya Itigi – Tabora pia utaimarika, hususan vijiji vya Karangasi, Tura, kwa Alex, Mpumbuli, Kigwa, mpaka Tabora unaimarika na kupata wanunuzi wa asali, mahindi, karanga na tumbaku. Ni kiungo kwa barabara za Kata na Vijiji vya pembezoni. Biashara za akinamama lishe na nyumba za wageni zinapata wateja.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Goweko – Darajani Kandama kiwango cha changarawe, Nyahua kwenye lami. Ninaomba *road fund* ili kuwe na barabara ya mkato badala ya kupitia Kigwa – Utundu Ukulu kuja Goweko unapotokea Itigi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe pongezi kubwa kwa Wizara chini ya Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kuwasilisha hotuba nzuri yenye mvuto mkubwa kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, niipongeze Serikali kwa kuweza kuanza kwa mradi wa barabara inayojengwa kwa lami barabara ya Tunduma – Sumbawanga, Sumbawanga – Nkasi, Kibaoni – Mpanda.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iweze kuangalia barabara ya Sumbawanga – Mpanda, ujenzi wake unaenda kwa kusuasua, hivyo naomba ujenzi wa barabara hii iongezewe fungu ili iweze kukamilika kwa wakati muafaka. Na ikumbuke maeneo haya yaliyosahauliwa kwa muda mrefu na hata Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete alitoa ahadi ya kutengeneza barabara za Mkoa wa Rukwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mpanda – Kigoma, barabara hii ni ya vumbi lakini ndio inayounganisha Mkoa wa Rukwa na Kigoma. Niombe Serikali inajenga barabara hii kwani kiungo muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa mikoa ya Rukwa na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mpanda – Mwese, barabara hii ni muhimu sana. Kwa wananchi wa Wilaya ya Mpanda A na Tarafa ya Mwese ambako kuna shughuli muhimu za kiuchumi na kilimo. Kwani huku kuna mazao ya kahawa nzuri inayozalishwa maeneo hayo pia zao la migomba na maharage.

Naiomba Serikali iweke kipaumbele kwa barabara hii kwa kuipanua na kuhakikisha inafika Ziwa Tanganyika na kukutana na barabara ya Ilagala Mkoani Kigoma ambayo naamini itawasaidia sana wananchi wa maeneo hayo hasa kuboresha mazao yanayozalishwa huko pamoja na mazao yanayovunwa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mpanda – Karema, barabara hii ni muhimu sana kwa maendeleo ya wananchi wa Ziwa Tanganyika ambao wanaishi mpakani mwa nchi hii. Ni vizuri sana kukafanyika matengenezo ya kudumu ili kuwasaidia wananchi wanaoishi pembezoni mwa nchi hii. Naishauri Serikali watenge fungu la kutosha kwa ajili ya kuhudumia barabara hii.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali iangalie barabara ya Mpanda – Tabora ijengwe kwa kiwango cha lami kwani ikiimarishwa barabara hii tutakuwa tumewasaidia sana wananch hawa wa maeneo ya mipakani katika kujenga uchumi wao na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya naunga mkono hoja hii.

**MHE. CHRISTOWAJA G. MTINDA:** Mheshimwa Spika, naomba kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, miundombinu na ahadi za viongozi, katika kutekeleza majukumu ya viongozi mbalimbali za Kiserikali inapokuwa kwenye ziara hutoa ahadi mbalimbali kwa wananchi hususan za ujenzi wa miundombinu ikiwemo shule na barabara. Mfano mzuri ni aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Lowassa, alipotembelea Kijiji cha Utaho, Tarafa ya Ihanjo, lililokuwa Jimbo la Singida Kusini wakati huo mwaka 2006 na sasa Jimbo la Singida Magharibi alitoa ahadi akimwelekeza Waziri wa Miundombinu kwamba Kijiji cha Utaho kijengewe shule mpya ya msingi baada ya kuwauliza wananchi wanachokitaka na hiyo ilikuwa kufidia Mlima wa Mawe (Utaho) ambao ulibomolewa kwa ajili ya kupata mawe na kokoto ili kujengea barabara ya Manyoni – Singida ambayo imeshakamilika.

Kwa nini ahadi hii mpaka sasa haijatekelezwa na hakuna hata lolote linazungumzwa kuhusiana na suala hilo? Kwa kuwa ofisi ya Serikali si mtu binafsi bali ni taasisi na hivyo hata baada ya mtoa ahadi kujiuzuru ningetegemea kwamba ofisi/Wizara ya Miundombinu/Ujenzi ingelifanya kazi suala hili. Naomba majibu kwa suala hili.

Mheshimiwa Spika, uhujumu wa mali za vijiji, barabara ya Manyoni – Singida ilishakamilika na kufunguliwa rasmi mwaka 2010 na nafahamu kwamba mkandarasi *(SIETCO –China)* anapewa muda wa kati ya mwaka mmoja hadi mitatu ili kuendelea kuangalia na kurekebisha barabara pindi kutatokea tatizo na hivyo anaweza kutumia *material* yaliyopo kwa kazi hiyo. Je, kwa nini mkandarasi huyu ameendelea kuuza kokoto zilizopo katika eneo (kijiji cha Utaho) – Puma (Singida Magharibi) kwa wakandarasi wengine wa Kichina? Kwa nini badala ya kutekeleza masharti ya kazi yeye anafanya biashara ya kokoto malori kwa malori tena bila kulipa kodi wala ushuru wa Kijiji husika? Naomba majibu ya kuridhisha kwa swala hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wakandarasi walio chini ya kiwango, kutoka ujenzi wa miundombinu ya barabara, kuna ujenzi ambao hufanywa chini ya kiwango ambao unazifanya barabara zianze kutiwa viraka hata kabla ya kumaliza mwaka. Barabara zinabonyea na kuna kuwa na matuta, tena *highways,* ajali kadhaa zimekuwa zikisababishwa na ujenzi huo ulio chini ya kiwango ambao haukubaliki. Mfano, tatizo hili linajionesha zaidi katika barabara ya Morogoro – Mbeya hasa katika Mlima Kitonga ambako kuna kuwa kukifanyika matengenezo ya mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, ukarabati unaofanyika mara kwa mara kwenye barabara nyingi kila baada ya kipindi kidogo unadhihirisha kwamba barabara hizo zinajengwa chini ya kiwango. Kwa hili wa kulaumiwa ni wale wanaowapatia kandarasi wakandarasi walio chini ya kiwango kuona wao ndio wanaokuwa wamejiridhisha na utendaji wao wa kazi unaogeuka mzigo kwa Taifa. Nataka kujua watu hao wanaotoa kandarasi wanachukuliwa hatua gani baada ya barabara au hata majengo kuharibika au kuporomoka kwa muda mfupi baada ya kazi kwisha?

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara kwa hotuba nzuri na nampongeza Waziri kwa uchapakazi wake na uwazi katika kazi yake na kwa kuanza nachangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya lami toka Tunduma Sumbawanga, kasi ya barabara hii ni nzuri ingawa inatofautiana kutoka kwa mkandarasi mmoja na mwingine yupo wanaenda kwa *speed* nzuri na wengine wawili hawaendi kwa *speed,* ninashaka kama kweli barabara itamalizika mwaka 2012 Disemba. Naomba msukumo uongezwe kwa wakandarasi wawili wanaoanzia kutoka Tunduma wote wawili wale wana-*speed* isiyoleta matumaini kuimaliza kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, barabara za lami Mkoani Rukwa ni mkoa uliochelewa kuwekeza barabara za lami na nashukuru Mheshimiwa Waziri kutenga fedha za kutosha kwa mkoa kwa ajili ya kutengeneza lami Mkoani kwetu, ni mwanzo mzuri na kwa moyo wake Ndugu Magufuli ataendeleza hiyo nia njema aliyonayo.

Mheshimiwa Spika, Wilaya/Jimbo Nkasi Kusini, barabara ya Nkana – Kala kilomita 67, barabara hii iliombewa na Mkoa iwe ya *TANROAD* baada ya kuzidiwa Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi, barabara hii imekuwa na mchango wa vifo vingi vya akinamama na watoto kwani si rahisi kunusuru maisha ya mjamzito aliye na shida ya kujifungua, tumepoteza wengi. Pia barabara hii nimesema sana sana nikiwa Mbunge wa eneo hilo. Naomba Wizara ikubali maombi ya mkoa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kitosi – Wampembe kilomita 68, barabara hii haina tofauti na barabara ya Nkana – Kala barabara zote zilishaishinda halmashauri kutokana na jiografia tata ya eneo la Bonde la Ufa Ziwa Tanganyika. Naiomba Wizara ikubali iwe ya *TANROADS* kama ilivyokwishaombewa na halmashauri lakini pia mkoa.

Mheshimiwa Spika, ziara ya Mheshimiwa Rais tarehe 29/08/2010 alielezwa matatizo wanayoyapata wananchi wa maeneo haya na alikubali kushughulikia ziwe katika ubora unaotakiwa kumbe kukubali kuwa chini ya *TANROAD* ni ukombozi wa kutosha kwani halmashauri/wilaya imeshindwa kwa sababu inaenda ziwani kwenye miteremko ya Bonde la ufa la Ziwa Tanganyika, kumbe barabara hizi mbili zikitengenezwa zitakuwa ni jibu la ahadi za mpendwa Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete.

Mheshimiwa Spika, maombi maalum, naiomba Wizara iendelee kuwabana na kuwasimamia wakandarasi wa Kichina wanaojenga barabara ya lami toka Sumbawanga kwenda Namanyere yaani Sumbawanga – Kanazi kilomita 78 na ile ya Kanazi – Kibaoni kilomita 75 zijengwe kwa *speed* inayotakiwa, vilevile barabara ya Sumbawanga – Kasanga nayo. Naomba isimamiwe iende kwa kasi inayofanana na Waziri Magufuli.

Mheshimiwa Spika, mwisho nazidi kumuomba kaka Magufuli kuwa barabara ya Namanyere - Kirando siku moja iwe ya lami itasaidia kulifungua Ziwa Tanganyika na wananchi. Wanawezaji kuwekeza katika uvunaji, usindikaji wa samaki na hivyo kuboresha uchumi wa wananchi.

Mheshimiwa Spika, nampa hongera Mheshimiwa Waziri, unachapakazi! Naunga mkono hoja.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kabla ya kusahau nianze kwa kusema bayana naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza Wizara ya Ujenzi kwa hotuba nzuri sana na pia kwa kazi nzuri inayofanywa na Waziri Mheshimiwa Dkt. John Magufuli na Naibu Waziri Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, nawapongeza sana. Nianze kwa kusema mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii ya Miundombinu lakini hii hainizuii kuchangia Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mkomazi – Ndungu – Kisiwani mpaka Same, barabara hii inapitia katikati ya Jimbo la Same Mashariki, Jimbo ambalo limesheheni uchumi mkubwa sana upande wa mazao. Kuanzia Kata ya Bendera, Kihurio, Ndungu, Maore ndizo kata zinazolima mpunga mwingi unaolisha wananchi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Tanga. Barabara hii inapita kwenye jimbo pekee lililojenga Kiwanda cha Kusindika Tangawizi na kuiuza nje ya nchi na kuingizia Taifa fedha za kigeni. Jimbo la Same Mashariki limesheheni mazao mengi katika Mkoa wa Kilimanjaro, Kata yangu ya Maore ndiyo inayolima nazi za kutosheleza mkoa wote wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete ambavyo aliitoa ahadi ya kujenga barabara hii kwa lami ili kuboresha uchumi wa wananchi wa Same Mashariki na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naipongeza *TANROADS* kwa kuanza ujenzi wa barabara hii kwa kilomita tano kuanzia Kata ya Maore.

Mheshimwa Spika, tatizo kilomita tano zimekamilika lakini kama kilomita tano hizi hazitaendelezwa hata hizi kilomita tano zilizowekwa lami zitakufa. Rais alipokuja kuomba kura mwaka 2010 aliahidi kilomita kumi katika Bajeti hii ili ifikapo mwaka 2015 barabara hii ikamilike.

Mheshimiwa Spika, haina maana yoyote kutumia fedha za Serikali kujenga kilomita tano halafu kuziacha bila ya kuendeleza. Hizi kilomita tano zitakufa na ni matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itafute njia ya kuendeleza barabara hii kipindi hiki hiki.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARY P. CHATANDA**: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara hii kwa kuandaa na kuwasilisha Bajeti nzuri inayoweza kutekelezeka endapo itasimamiwa vizuri lakini kwa umahiri mkubwa wa Mheshimiwa Magufuli, Waziri na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Mwakyembe.

Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Serikali ya CCM kwa kazi kubwa iliyofanyika kama utekelezaji wa Ilani ya CCM ambayo kila aliye na macho haambiwi tazama hususan barabara za lami, ujenzi wa nyumba za Serikali zikiwemo za hapa Dodoma zinazoitwa nyumba za Magufuli.

Mheshimiwa Spika, aidha katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 imeonyesha wazi namna ambavyo Serikali imedhamiria kuendelea kukamilisha na kujenga barabara nyingine katika kila mkoa. Ni matumaini yangu kwamba watendaji na wakandarasi watafanya kazi zao kwa umakini na ubora ili kuweza kutumika na wananchi waweze kupata urahisi wa kusafiri na kusafirisha mazao yao na kujiinua kiuchumi kwa mtu mmoja mmoja na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ujenzi wa barabara hizi Mheshimiwa Waziri azungumze na makandarasi badala ya kupenda maeneo wanayofanyia kazi na vibarua ni vema wakatumika vijana au wanawake waliopo kwenye maeneo hayo ili kuwasaidia kujipatia riziki na kujiinua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu matuta ya barabarani, ni kweli wananchi wamekuwa wakiathirika kwa kugongwa kutokana na kutoitumia vizuri kwa kuwa makini kuvuka katika barabara hizo, bado Serikali iendelee kutoa elimu kwa njia ya semina/waelewe matumizi ya barabara hizo za lami vinginevyo kuendelea kuweka matuta ni uharibifu wa barabara hizo, haiwezekani nchi yetu ikaendelea na utaratibu wa kujenga matuta ambayo kwa upande mwingine yanaharibu vyombo vya usafiri hususan magari, pikipiki/bajaji na kadhalika. Ni vema Serikali ikapunguza ukubwa wa matuta kwani maeneo mengine yamezidi kipimo.

Mheshimiwa Spika, suala la alama za barabarani zinazoashiria au kuelekeza madereva tahadhari wakati wa kuendesha magari baadhi ya wananchi wasio waaminifu wamekuwa wakizitoa alama hizo kwa maslahi yao na kuuza kama vyuma chakavu. Hivyo jukumu letu viongozi wa vitongoji/vijiji katika maeneo ya barabara za lami wakapewa maelekezo ya utunzaji wa alama hizo, kwani wanaotoa/kuiba ni vijana au wananchi wao wanao waongoza katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, suala la mizani, naomba Mheshimwa Waziri wa Ujenzi kwa ujasiri alionao afuatilie kwa karibu maeneo yenye mizani kwani watendaji waliopo katika maeneo hayo baadhi yao sio waaminifu, hupitisha magari yenye mizigo iliyozidisha uzito kutokana na kupewa kitu kidogo, bila kujali kwamba Serikali inapata hasara ya uharibifu wa barabara hizo na kuiongezea mzigo Serikali badala ya kuendelea kujenga barabara nyingine, inatengwa Bajeti mara kwa mara kwa ajili ya ku-*repair.*

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa nyumba za watumishi/viongozi ni jambo jema lakini nyumba ambazo zipo zinakaliwa na watendaji au viongozi wanapopata uhamisho au kustaafu

wasiendelee kung'ang'ania kuwemo kwenye nyumba hizo, kwani kwa kufanya hivyo kunawasababishia watumishi/viongozi wengine kupata taabu pale ambapo wanatakiwa kuingia katika nyumba hizo. Kwa mfano nyumba zinazokaliwa na Wabunge, uwepo utaratibu wa mkataba unaoishia muda wake wa Ubunge ili kutoa nafasi ya nyumba hizo kwa wengine waliobahatika badala ya hivi ilivyo sasa wachache wao wamepangisha hali Serikali imempangisha yeye kwa bei ndogo na yeye anachuma kwa kuiibia Serikali.

Mheshimiwa Spika, nyumba za Serikali nyingi ziliuzwa huko nyuma kwa bei ya kutupwa huku zikiwa hazilingani na thamani ya gharama ya ujenzi huku ni kuiibia Serikali. Naiomba Serikali ikumbuke fedha zinazotumika ni kodi ya wananchi hivyo uwepo utaratibu mzuri wa kuuza nyumba hizo.

**MHE. DKT. CYRIL A. CHAMI:** Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ahadi ya Mheshimiwa Rais barabara ya Kiborloni – Kikarara – Tsuduni – Kidiana kuingia *Forest Kilimanjaro* (18 kilimita), nawaomba msiisahau. Ipo Moshi Vijijini eneo la *Old Moshi.*

Mheshimiwa Spika, pongezi tena.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi. Wizara ya Ujenzi ndiyo Wizara yenye jukumu la msingi na roho ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, nchi yetu tumeshuhudia uchumi wa nchi yetu umekuwa ukikua kwa kasi sana pale dhamira ya Serikali ilipojielekeza katika kujenga barabara za lami na zingine kwa kiwango cha changarawe nchi nzima.

Katika mgawanyo wa barabara zile za Kitaifa, Kimkoa na za Halmashauri pamoja na zile za vijiji. Wilaya ya Bukombe na Mbogwe tunayo barabara ya lami inayotoka Isaka kwenda Lusahunga, tunaishukuru Serikali kwa mpango wa kuifanyia matengenezo kwa kiwango cha lami kila wakati pindi inapoharibika barabara hii ya lami kwetu imekuwa chachu ya maendeleo kwa wananchi wa Wilaya yetu ya Bukombe na Jimbo letu la Mbogwe ambapo wananchi wamepata manufaa makubwa kwa kukua uchumi kwa kuboresha thamani ya mazo ya wakulima bei za mazao kama mpunga, mahindi na kadhalika zimekuwa zikipanda muda wote pindi wanunuzi wa mazao haya wa kutoka ndani ya nchi hata wale toka nchi jirani za Rwanda, Uganda na *DRC* wamekuwa wakichangia kuboresha bei za mazao tajwa na mazao ya bustani kama nyanya zimekuwa na bei nzuri na kuboresha maisha ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, barabara ni uhai, barabara ni afya, barabara ni usalama na kama nilivyosema hapo juu barabara ni uchumi. Kwa uchumi na ujenzi wa wilaya yetu mpya na jimbo letu la Mbogwe tunaiomba Wizara ya Ujenzi kwa kutupatia uwezekano sasa wa barabara zaidi kwa ajili ya kuhudumiwa na Wakala wa Barabara *(TANROADS).* Barabara ambazo nitamwomba Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kupandisha hadhi barabara zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, Masumbwe, Lugunga, Nyasato, Bwelwa, Ilolangulu, Bugalagala, Kashelo, Lulembela, Nyikonga, Ipalamasa, Butobela (Mwendakulima), Bitengo Lumasa (barabara hii itaziunganisha barabara kuu za lami za Geita – Buzilayombo na barabara na Isaka – Lusahunga nayo ya lami). Niiombe Serikali ifanye kila linalowezekana kuipandisha daraja kuwa *TANROADS* na kisha ijengwe kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Geita - Gengetatu – Gengetano - Gengesaba – Kashishi, Nyarugusu, Nyaruyeye – Wigo – Ivumwa – Nyitundu Bwendamwizo – Iboya, Bwelwa, Nanda Kisumo, Nyanholongo, Katome hadi Ushirombo Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri niombe kushauri kuwa Wizara kuanzisha Wakala wa Barabara Vijijini. Chombo hiki kitasaidia sana kuboresha barabara nyingi zaidi za vijijini ziweze

kulisha barabara – *TANROADS* na barabara kuu ya Kitaifa na Kimataifa itokayo Isaka Lusahunga kwenda Rwanda, Burundi na Uganda.

Mheshimiwa Spika, barabara nyingi vijijini katika Jimbo la Mbogwe ziko katika hali mbaya naomba chombo hiki cha Wakala wa Barabara Vijijini utasaidia ujenzi wa barabara ngazi za vijijini, kata, tarafa hadi wilayani ili kujenga uimara wa Wakala wa Barabara wa Taifa *(TANROADS).*

**MHE. DKT. MILTON M. MAHANGA**: Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja hii na kumpongeza Waziri na watendaji wote wa Wizara. Ningependa, hata hivyo kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, miaka mitatu iliyopita Serikali ilianzisha mradi mkubwa wa kujenga barabara muhimu za Jiji la Dar es Salaam kwa lami ili kupunguza msongamano jijini hapo na kwa kuanzia shillingi bilioni 20 zilitengwa. Hata hivyo baada ya mradi huo kuanza, kila mwaka Serikali imekuwa ikisisitiza umuhimu wa mradi lakini kwa miaka miwili hii, Serikali imeshindwa kutenga fedha ya maana kwenye Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ili kuendeleza mradi huu kwa kazi inayostahili. Hii imepelekea mradi huu si tu kulimbikiza madeni ya mabilioni ya shilingi, lakini barabara muhimu zilizolengwa kama Tabata Dampo – Kigogo, Ubungo Maziwa – *External,* Kimara – Kilungule – *External* na *Jet Corner* – Vituka – *Davis Corner* hazijaanza kujengwa na hata mwaka huu zimetengewa tu fedha ambazo hata fidia huenda zisitoshe. Serikali inasemaje kuhusu kutenga fedha za kutosha kila mwaka kwa ajili ya mradi huu?

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Kimara – Mavurunza – Bonyokwa – Segerea kwa lami ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Aidha, Bodi ya Barabara Mkoa wa Dar es Salaam, ilishaidhinisha barasbara hiyo iombewe kupandishwa hadhi kuwa barabara ya mkoa kwani inaunganisha maeneo muhimu ya Wilaya ya Kinondoni na Ilala. Hata hivyo barabara hiyo haijawekwa kwenye mpango wala Bajeti ya Serikali. Je, Wizara sasa itakubali kuanza ujenzi wa barabara hiyo hata kama fedha za *road fund?* Kwa vyovyote vile ningeshauri kwa mwaka 2011/2012 upembuzi yakinifu na usanifu ungefanyika ili mwaka 2012/2013 barabara hiyo ianze kujengwa kwa lami.

Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kuahidi kujenga barabara muhimu ya *ring road* ya kutoka Tanki Bovu – Goba na Tegeta Kibaoni – *Wazo Hill* – Goba – Mbezi – Malambamawili – Kinyerezi – Banana na baada ya usanifu kukamilika zaidi ya miaka miwili iliyopita, juhudi thabiti za Serikali kutafuta fedha za ujenzi hazionekani sana! Nashauri Serikali iweke juhudi madhubuti kupata fedha za ujenzi wa barabara hii muhimu.

Mheshimiwa Spika, ili kupata suluhisho la muda mrefu na la uhakika wa kuondoa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam, ukiacha barabara zinazojengwa sasa na ahadi ya kujenga *fly-overs*, nashauri mipango miwili ifuatayo iangaliwe na kutekelezwa na Serikali kwa:-

(a) Kujenga kwa lami barabara zote muhimu za michepuo ndani ya jiji ili kuwezesha magari kuchepuka kutoka barabara kuu kila inapowezekana. Barabara hizi za michepuo zipo maeneo ya Kariakoo, Jangwani, Tabata, Kimara, Mabibo, Sinza, Mikocheni na Kinandoni.

(b) Kujenga *highway* ya *six-lane* inayoweza kuitwa *Dar es Salaam by-pass* kutoka maeneo ya Bagamoyo kupitia Wilaya ya Kibaha, Wilaya ya Kisarawe, Msongola/Mkuranga – Kongowe hadi Kigamboni. *Highway* hii itatumika kwa magari makubwa yatokayo bandarini kwenda nje ya Dar es Salaam na pia kuwezesha kuunganisha vizuri barabara kuu za Bagamoyo, Morogoro, Pugu na Kilwa. Aidha, pembeni mwa barabara hii itengwe *industrial corridor* ili viwanda sasa vijengwe nje ya jiji kwenye *corridor* hii. Kwa kuanzia katika miaka mitano ijayo, *corridor* hii itwaliwe na fidia ilipwe ili mpango wa maendeleo 2016/2021 ujenzi ufanyike.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja ya mambo yanayochangia kuongezeka haraka kwa maendeleo katika nchi ni mtandao mzuri wa mawasiliano kama barabara, kuwepo kwa ajira za uhakika za usafiri ndani ya nchi kunarahisisha sana usafirishaji wa idadi kubwa ya watu na kiasi kikubwa cha bidhaa toka pande moja ya nchi hadi nyingine. Hili mbali ya kuokoa muda, lina mchango mkubwa katika shughuli na gharama za kibiashara na hatimaye bei ya bidhaa. Kwa kifupi mtandao mzuri wa mawasiliano unaongeza tija kwa kiwango cha juu iwe ni kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Tanzania ina tatizo kubwa la mawasiliano ya ardhini kwa maana ya usafiri na usafirishaji, sehemu kubwa ya mtandao wa barabara upo katika hali mbaya kabisa. Kielelezo cha ubovu wa barabara zetu si kigeni kabisa kwa wakazi wa miji yetu. Barabara takriban zote alizoziacha mkoloni zikiwa na lami hivi sasa ni vumbi na makorongo matupu.

Mheshimiwa Spika, kweli Serikali inajitahidi ujenzi unaendelea lakini kama ilivyo kawaida ya jambo lolote ambalo halifanyiki kwa dhati kuna ushahidi kuwa barabara takribani zote zinazojenga chini ya miradi hii zina ubora ambao upo chini ya viwango vinavyotakiwa. Katika baadhi ya miradi hii makandarasi wamekimbia baada ya kushindwa kuhimili vitendo vya rushwa na ufisadi walivyohitajiwa kushiriki.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie suala la kwetu Tanga kwa wananchi/wakazi wa Tanga – Horohoro. Wananchi waliokuwa katika Vijiji vya Tanga – Horohoro waliokuwepo katika vijiji hivyo kabla ya sheria za *TANROADS* kuingizwa kwani vijiji vilikuwepo kuanzia miaka ya 1920 chini ya uongozi wa vijiji husika. Mheshimiwa Waziri tarehe 28/05/2010 katika uzinduzi wa ujenzi wa barabara hiyo ya Tanga – Horohoro, Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete alitoa agizo la kulipwa fidia wananchi hawa mara moja. Wananchi wote waliopewa *(notice* mwaka 2003) na *TANROADS* kuvunja nyumba zao na wakavunja kwa kutii amri hiyo.

Mheshimiwa Spika, wananchi wameingiwa na wasiwasi kwa sababu Mheshimiwa Rais alifanya ziara tarehe 28/05/2010 Wizara ya Miundombinu ilituma wataalamu wake tarehe 23/10/2010 kuja kuonana na wananchi waliobomoa nyumba zao na kufanya makubaliano jinsi ya fidia itakavyolipwa, tathimini hiyo ilifanyika lakini wananchi hawajafahamishwa lini watalipwa fidia hiyo na ni kiasi gani?

Mheshimiwa Spika, tarehe 18/11/2010 Kamati maalum imepokea barua kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa yenye Kumb.Na.FA.7/23/01/3 inayotaka Kamati Maalum kwa niaba ya wananchi kuwa na subira Serikali inashughulikia madai yetu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mbunge wa Jimbo, wananchi hawa pia walifanya jitihada, walifikisha suala lao hili tarehe 15/01/2011 na tarehe 07/03/2011 walikutana na Mbunge wa Jimbo lakini hakukuwa na jibu lililowapa matumaini.

Mheshimiwa Spika, ninakuomba wewe Waziri binafsi kuingilia kati suala zima la malipo ya fidia ya nyumba za wananchi waliovunja na kubomoa nyumba zao kupisha ujenzi wa barabara Tanga – Horohoro kwa sababu wananchi hawajui hatua yao na wanahitaji fidia hiyo kwa ajili ya ujenzi wa makazi yao. Kwa sasa macho, masikio, mawazo yapo mikononi kwako. Tafadhali Mheshimiwa Waziri naomba ulitolee kauli wananchi hawa wakusikie.

Naomba kutoa ushauri/mapendekezo kuwa Serikali ihakikishe kuwa ushuru wote wa barabara unaelekezwa kwenye ujenzi wa barabara mpya na kurekebisha zile zilizoharibika, asilimia 50 ya fedha za ushuru wa barabara zielekezwe kwenye ujenzi wa barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kipindi hiki cha mwaka 2011 – 2015 ihakikishe kuwa maeneo yote ambayo hivi sasa yanatumia vivuko katika barabara kuu na mabarabara zinazounganisha mikoa, yawe na madaraja ya uhakika na utumiaji wa vivuko kusitishwa. Na naomba kabla ya kufikia hayo uvushaji katika vivuko vyote uwe bila malipo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukarabati barabara zilizopo Serikali ihakikishe majengo kilomita 500 za barabara kuu mpya za lami kila mwaka katika kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Spika, sanjari na kuthamini makandarasi wazalendo, suala la kuharakisha ujenzi wa miundombinu ili kukuza uchumi wa Taifa ni jambo linalohitaji kupewa msukumo wa kipekee. Serikali ihakikishe miradi mikubwa ya ujenzi ipewe makampuni yenye uwezo mkubwa kifedha, kiutendaji (vifaa vya kutosha na vya kisasa), uzoefu na utaalamu wa hali ya juu. Makampuni hayo yapewe kazi hizo na kuweka utaratibu wa kuwashirikisha wazalendo *(sub-contractors)* katika kutekeleza kazi za mradi husika, lengo likiwa ni kuondokana na ucheleweshaji wa miradi ya barabara ambayo tumeshuhudia kutokana na mapungufu ya kiutendaji.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupatia uzima.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Ujenzi sambamba na hilo naomba pia nimpongeze Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Naibu Waziri wa Ujenzi Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Katibu Mkuu pamoja na wataalam wote wa Wizara kwa kazi nzuri inayofanywa na uongozi wa Wizara kwa ujumla wake. Pamoja na kwamba fedha mnazopata sio nyingi lakini mnajitahidi sana kwamba barabara zinajengwa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mbeya kunajengwa kiwanja kikubwa cha ndege na kwa kuwa Mbeya pamoja na mikoa jirani kuna maeneo mengi ya utalii je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kujenga barabara za lami hususani barabara Isyonje kwenda Makete barabara ya Mbalizi hadi Mkwajuni, Mbalizi – Isongole? Barabara hizo zitatoa fursa kwa kusafirisha mazao na aina zingine za bidhaa zitakazoweza kusafirishwa hadi nje kwa kutumia uwanja wa ndege wa Songwe; sambamba na hilo bado itawapa fursa watalii wengi kutembelea maeneo ya utalii kwa urahisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo naomba kuchangia ni kuhusu malalamiko ya makandarasi wengi kwamba fedha za malipo kwa ajili ya kazi ambazo zinafanyika zinachelewa kiasi kwamba hata kazi zao inakuwa vigumu kuzikamilisha kwa wakati. Je, ni kwa nini Serikali isiwe makini kwa suala hili?

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika nchi yetu kuna ongezeko kubwa la magari na kusababisha msongamano mkubwa wa magari katika barabara zetu bila kutaja kuwa ni Dar es Salaam lakini hata mikoa mingine kama Mbeya, Arusha, Mwanza na kadhalika, je, ni kwa nini tusijifunze kutoka nchi zilizoendelea kama *South Africa* ambako katika kila barabara wamejenga *inter-change* zinazo saidia kuondoa msongamano mkubwa wa magari?

Mheshimwa Spika, pamoja na mchango wangu katika hoja hii naomba kuunga mkono hajo hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni foleni kubwa sana katika mkoa wetu wa Dar es Salaam na kwa kuwa vivuko vinavyosimamiwa na Wizara ya Ujenzi wasafiri huwa wanalipia, je, Wizara haioni kuna umuhimu wa kuanzisha usafiri wa majini ili kupunguza foleni kwa wakazi hasa wale wanaotoka maeneo ya Kigamboni, Kawe, Kunduchi, Msasani, Tegeta na Bagamoyo njia hii itapunguza foleni kubwa katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimwa Spika, kwa kuwa Serikali imeweka mizani ili kulinda barabara zake, je, Serikali haioni kuna upotevu mkubwa wa fedha unaotokana na uharibifu wa magari unaosababishwa na matuta katika barabara zetu kwa kisingizio cha kuzuia ajali wakati ajali bado zinaendelea kupoteza maisha ya watu na matuta yamejaa katika barabara zetu zote nchini na ukizingatia hayo matuta ndio yanayochangia kuwepo kwa ajali, kwa hiyo, naishauri Serikali kuondoa matuta katika barabara zote kuu na kubakisha zile za katikati ya mji, lakini pia naishauri Serikali kutafuta njia mbadala ya utaratibu ili kuweza kutenga sehemu kwa wale wanaotumia kwa miguu na kwa wale wenye kutumia barabara wakiwa na mikokoteni na maguta hasa katika Jiji la Dar es Salaam utakuta mwenye guta au mkokoteni anakaa katikati ya barabara kuzuia magari kupita na husababisha foleni kubwa, naishauri Serikali iwe na utaratibu kwa hao wanaotumia vyombo hivyo

kwani hawana leseni ya barabara wala bima na wao ndio watumiaji barabara wakubwa kuliko wenye gari.

Mheshimiwa Spika, rushwa katika mizani ni kubwa sana na ndio maana watu hawajali kuzidisha uzito kwa kuwa hutoa rushwa na kuachiwa, magari huwa yanasheheni mizigo mingi sana, nakuomba Waziri uwaambie watu wa *TANROADS* wangapi wamekamatwa na wameshtakiwa na hili nakuomba unijibu katika majumuisho.

Mheshimiwa Spika, nimefarajika sana kusikia Serikali imejenga nyumba kwa kuwapangisha watu na wengi wanakipato kikubwa ndio mnawapangisha, naishauri Serikali pia wawapangishe na watu wa kawaida, kama vile walimu au madaktari na wasijenge maeneo tu ya kifahari bali wajenge Magomeni, Temeke na Tabata na mikoani. Bodi ya Usajili wa Wabunifu Majengo na wakadiriaji majengi *(AGRB).*

Mheshimiwa Spika, siku zote tunashuhudia majengo yanaanguka ovyo na yanauwa watu hasa yale yanayojengwa siku hizi, zamani mambo haya ya kuanguka nyumba yalikuwa hakuna ingawa taaluma ilikuwa ndogo, hii inatokana na kuwaajiri wakandarasi waliokuwa hawana sifa wanaojali zaidi fedha kuliko ubora wa kazi zao na maisha ya watu, naishauri Serikali iwe makini sana katika kuwaajiri hawa wakandarasi.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza hotuba ya Waziri Mheshimiwa Magufuli, nampongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwa kuwakumbuka wananchi wa Mkoa wa Rukwa kuanza kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Barabara zifuatazo za Tunduma – Sumbawanga, Sumbawanga – Kibaoni, Sumbawanga – Kasanga, nasema tunashukuru sana.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukrani hizo tunaomba Serikali iendelee kujenga barabara kwenda katika maeneo ya uzalishaji, kwenye tarafa, kata na vijiji kwani huo ndio wajibu wa Serikali. Wananchi wa Mkoa wa Rukwa ni wavumilivu, watulivu na ni wasikivu. Wamevumilia vya kutosha, wamepambana vya kutosha ni kweli subira yavuta heri.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha wananchi wa Mkoa wa Rukwa kukaa miaka 34 toka uundwe Mkoa wa Rukwa bila kuwa na barabara ya lami na leo hii ndio wanataka kushuhudia barabara ya lami ni ukombozi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kilyamatundu – Muze Muze – Mfinga na Mfinga – Kibaoni. Baranbara hiyo ilikuwa imesahaulika toka wakati mkoloni alipoondoka nchini maana ndiyo aliyekuwa akiitengeneza barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuweka msukumo kwa kuanza barabara hiyo. Tunaomba Serikali itengeneze kwa kiwango cha changarawe barabara yote.

Mheshimiwa Spika, madaraja yajengwe kwa kiwango kinachotakiwa, yasijengwe kama madaraja yaliyojengwa mwanzoni. Madaraja hayo yalilipuliwa sana, yatatakiwa kurudiwa maana kwa sasa yanabomoka sana hata likipita lori la tani saba tu yanabomoka.

Mheshimiwa Spika, umuhimu wa barabara hiyo ni maeneo ya uzalishaji mazao ya kila aina kama samaki toka Ziwa Rukwa, pia kwa huduma mbalimbali za kijamii kama vile elimu, afya, shughuli za kiuchumi na kisiasa.

Mheshimiwa Spika, daraja la Mto Momba linalounganisha vijiji vya Kilyamatundu, Jimbo la Kwela na Kijiji cha Kamsamba kilichopo Jimbo la Mbozi Magharibi, shida na madhara yanayowakumba wananchi wa maeneo hayo kushindwa kusafirisha mazao, shida ya kwenda kupata huduma za afya, kutozwa fedha kwa wananchi kwa kupitia kivuko cha miguu kilichotengenezwa na mzungu wa Ki-*missionary*, kivuko hicho kinachotumika hadi sasa ambacho wananchi hulipia shilingi 500/= hadi 1000/=.

Mheshimiwa Spika, madhara ya kukosa fedha za kulipia ushuru wa kulipa kivuko, baadhi yao hulazimika kuvuka chini na hatimaye kukamatwa na mamba. Akinamama wajawazito hupoteza maisha na shughuli za uchumi kuathirika.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itambue ahadi alizotoa Mheshimiwa Rais wakati wa uchaguzi. Kuweka lami barabara zifuatavo za Kalambanzite – Ilemba, Miangalua – Chombe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Ujenzi kwa kazi nzuri anayofanya. Pamoja na pongezi hizo nashauri mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ahadi ya Rais, nashukuru Wizara kwa kuanza kujenga barabara ya lami Kawawa kwenda Nduoni (kilomita 19) na baadae Marangu Mtoni kwenda Soko la Kilema (kilomita 5) kwa gharama ya shilingi bilioni 10. Haya ni matengenezo ya awamu ya kwanza. Awamu ya pili itahusu utengenezaji wa kilomita 15. Ombi langu ni kwa Wizara kuendelea na matengenezo haya hasa ikizingatiwa ni ahadi ya Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mizani ya Njia Panda, ninaomba Wizara itafute namna ya kushughulikia mizani iliyopo Njia Panda imekuwa kero. Mzani wenyewe ni mdogo na huchukua muda mrefu kupima uzito magari. Matokeo yake kunakuwa na mlolongo wa magari kuanzia Njia Panda hadi Chekereni.

Mheshimiwa Spika, aidha magari yakipima uzito katika mizani zinazoanzia Dar es Salaam yakifikia Njia Panda uzito huwa umeongezeka. Ningependa kujua Wizara inatatuaje tatizo hilo.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kubomoa nyumba zinazowekewa alama ya X, barabara ya Himo - Marangu na Marangu - Mtoni kwenda *KINAPA*, nyumba zilizojengwa pembeni zimewekewa alama X ikionyesha zitabomolewa baadae. Ningeomba kujua mpango wa kuwafidia watu hao utafanyika lini. Hii itasaidia wahusika kujiandaa kuhama maeneo hayo. Aidha, fidia zao zitalipwa lini?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Halmashauri ya Moshi, imetengeneza barabara zifuatazo; Kilema Pofo – Kilema -Hospitali, Uchira – Kisomachi- Kwalarie, Marangu – Komela - Kiraracha, Kilacha – Matala Msae. Lole – Kiteore – Marera, Kilema – Sokoni – Maua, Himo – Makuyuni – Lotima, Kahe – Soko – Kiomu, Kawawa – Yanur – Nduoni, Mabungo – Ngunjoni, Marangu – Sembeti na Pakula – Kilema.

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA:** Mheshimiwa Spika, na mimi nachukua fursa hii kuchangia hotuba ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la ujenzi wa maghorofa ya Kariakoo Dar es Salaam. Suala hili limekuwa tatizo sugu na kero kwa wafanyabiashara hasa kipindi cha mvua. Majengo haya hayapo katika ramani nzuri na hata mengine yanajengwa hayana ubora na hata kuhatarisha maisha ya watu. Majengo haya yamejengwa kwa msongamano usio wa kawaida bila hata kuacha nafasi na cha kushangaza maghorofa haya yanajengwa bila hata kuachwa miundombinu kama mitaro ya kupitisha maji taka. Hata ajali ya moto ikitokea kwa msongamanoo huu wa maghorofa haya ni rahisi kuungua kwa majumba mengi kwa sababu nyumba moja ikishika moto ni rahisi na nyingine kuwaka kwa sababu ya msongamano. Vilevile mvua zikinyesha panakuwa hapapitiki. Je, watu hawa wanaojenga maghorofa haya Kariakoo vibali hivi wanavitoa wapi?

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la fidia kwa wananchi wanaobomolewa nyumba zao, suala hili limekuwa linawaathiri wananchi wengi. Katika kutekeleza miradi mbalimbali ya ujenzi wa barabara hapa nchini. Nyumba nyingi za wananchi zimekuwa zikivunjwa na kusababisha wananchi hawa kuishi bila makazi ya uhakika na kusababisha malalamiko mengi miongoni mwa wananchi wetu. Pamoja na umuhimu wa kuwa na barabara kwa ajili ya kuweza kuharakisha upatikanaji wa maendeleo ya Taifa letu, Serikali sasa inapoamua kuwalipa watu hawa fidia

waliobomolewa nyumba zao watu hawa wamekuwa hawalipwi fidia zinazoweza kukidhi mahitaji yao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la wazee wa Tanzania wasiojiweza pamoja na wanawake wajane wasiojiweza, wazee wa Tanzania nao wapewe kipaumbele na Serikali kujengewa nyumba za kuishi. Wazee hawa wamekuwa wakihangaika sana kuhusu makazi ya kuishi pamoja na akinamama wajane wasiojiweza wamekuwa wakiombaomba barabarani na kulala katika vituo vya mabasi na kwenye mitaro. Tumewashuhudia wanawake hawa wajane wasiojiweza wakilala barabarani na watoto wao na hata wengine kufanyiwa vitendo vya kikatili kama kubakwa.

Nilikuwa naiomba Serikali itenge fungu la kutosha kwa ajili ya wazee hawa wasiojiweza na wanawake hawa wajane wasiojiweza waweze kujengewa nyumba za kuishi na hata kama nyumba zipo basi ziboreshwe ili watu hawa waweze kupata makazi bora kama wanavyofanya wenzetu wa Ulaya na Marekani wanawadhamini wazee. Kwa hiyo, inabidi na sisi Watanzania tuige kuwadhamini wazee.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la msongamano wa magari Dar es Salaam, msongamano huu wa magari katika Jiji la Dar es Salaam umekuwa ni tatizo kubwa sana. Watu wengi wamekuwa wakipoteza muda wao katika foleni ya magari na hii inasababisha kuathirika kwa uchumi wa Taifa letu. Mfuko wa Bodi ya Barabara kwa kushirikiana na halmashauri uweke utaratibu wa kufungua barabara za pembezoni mwa miji ili kuhakikisha kuwa tatizo la foleni linamalizika na kupunguza muda mwingi unaopotea kwa wanyafakazi na wanafunzi wa maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la matuta barabarani, wananchi wengi wamekuwa wakilalamika kuhusu matuta haya yanayojengwa barabarani. Hakuna kipimo wala aina maalum ya matuta kiasi kwamba mengine ni makubwa mno. Matuta haya yamekuwa yakisababishwa ajali hasa nyakati za usiku, madereva wengi wanakuwa hawaweki ishara yoyote ya kujulisha kwamba kuna matuta barabarani na matuta haya yanasababisha hata abiria wengine kutenguka viuno na akinamama wajawazito kupata mshituko na kujifungulia barabarani kabla ya kufikishwa hospitali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala zima la wakandarasi wa barabara. Wakandarasi wengi wamekuwa sio waadilifu, wamekuwa wakichukua *cotract* za mabarabara kwa muda mrefu na hawazimalizi kwa muda muafaka. Nilikuwa naiomba Serikali na Wizara iangalie jambo hilo kwa uangalifu mkubwa sana. Pamoja na nia njema ya kujenga barabara nyingi nchini naishauri Serikali isiingie mikataba ya ujenzi na wakandarasi kabla ya kupata fedha za kugharamia miradi husika kwani kufanya hivyo kunaiongezea Serikali gharama zisizo za lazima kwa kulipa faini na riba zinazotokana na ucheleweshwaji wa malipo baada ya kazi kufanyika.

Mheshimiwa Spika, nitaunga hoja mkono hoja endapo nitapatiwa majibu kwa yote niliyoyachangia hapo juu.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinozofanywa na Serikali katika kuhakikisha barabara ya Dodoma – Kondoa – Babati inajengwa kwa kiwango cha lami, naiomba Serikali iendeleze juhudi zake za kuhakikisha barabara hii inakamilika.

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010 – 2015 Ukurasa wa 28 inasema wazi kuwa barabara ya Handeni – Kiberashi – Kibaya – Mrinjo – Chamba - Densee – Farkwa – Kwamtoro – Singida inafanyiwa upembuzi yakinifu ili ijengwe kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, katika jambo la kustaajabisha kabisa ukurasa wa 152 wa kitabu cha Waziri inaonyesha hiyo barabara inabadilishwa kinyume na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala.

Mheshimiwa Spika, leo katika kitabu chako Mheshimiwa Waziri nashangaa kuona barabara hiyo imebadilishwa badala ya kutoka Mrinjo Chini – Soya Chambalo – Chemba – Densee – Kwamtoro hadi Singida, leo inatakiwa kwenda Dalai hadi Bicha, nani kabadilisha Ilani ya Uchaguzi iliyoiweka madarakani CCM?

Mheshimiwa Spika, Ilani iliyoiweka CCM madarakani imeonyesha maeneo ambayo barabara hii itapita na wananchi wanajua iweje sasa barabara hiyo iende Bicha ambako karibu kilomita 8 ni pori tu?

Mheshimiwa Spika, naomba sana mradi huu ubaki kama ulivyoonyeshwa kwenye Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2010 – 2015 ukurasa wa 28. Ahsante.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Spika, kazi kubwa iliyofanywa na Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi toka Uhuru inapaswa kupongezwa na kila mzalendo. Ni kwa maana hii nachukua nafasi hii kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu wake kwa kazi nzuri sana inayofanywa na Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Rombo, nataka kuchukua pia nafasi hii kuishukuru kwa dhati Serikali kwa uamuzi wake wa ujenzi wa barbara ya Tarakea – Rongai – Kamwanga, Tarakea – Rombo Mkuu, Marangu – Rombo Mkuu na Kilacha – Mwika. Barabara hii ambayo karibu itamalizika ni ukombozi mkubwa sana kiuchumi na kijamii kwa wananchi wa eneo hili. Hata hivyo bado kuna matatizo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi umesimama kati ya Mamsera na Rombo Mkuu kama kiloomita 15. Wananchi wameanza kupata wasiwasi, tunaomba kipande hicho kikamilishwe.

Mheshimiwa Spika, matengenezo ya *access roads* maeneo mengi yameachwa. Ombi letu ni kwamba barabara hizo ambazo nyingi ni za vijiji tunaomba zitengenezwe.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingi ambazo kifusi kilichukuliwa zimeachwa bila kufukiwa na uharibifu mkubwa wa mazingira umefanyika. Ombi maeneo hayo alazimishwe mkandarasi kufukia.

Mheshimiwa Spika, mikataba mingi kati ya mkandarasi na wananchi haijalipwa na mkandarasi ana kiburi kuwalipa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ilipoamua kuuza baadhi ya nyumba zake, kwa bahati mbaya iliuza nyumba za baadhi ya vijiji katika Jimbo la Rombo. Mfano mzuri ni nyumba za Kijiji cha Makiidi Kata ya Makudi Rombo. Nyumba hizi zilijengwa na wananchi kwa michango yao kwa ajili ya kuwahudumia maofisa ambao wanatumwa katika kijiji chao.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuuzwa kwa makosa wananchi kupitia Serikali yao ya kijiji, Diwani pamoja na viongozi wengine wameshaleta malalamiko ambayo hadi sasa hayajatolewa maamuzi. Napenda kutoa taarifa kwamba huu ni mgogoro ambao kama hautatolewa kauli utaendelea kuwafanya walionunua nyumba hizo waishi kwa mashaka. Wananchi katika Wilaya ya Rombo tunaomba wananchi warejeshewe nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, umaliziaji wa Ujenzi wa barabara za Sam Nujoma na Kilwa unatia shaka na unachafua *record* nzuri na utendaji wa Wizara. Ni vema ufuatiliaji ufanywe kwa kina ili mkandarasi awajibishwe.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo napenda kwa dhati kuunga mkono hoja hii na kuendelea kuwapongeza sana kwa kazi nzuri.

**MHE. AZZA HILLAL HAMAD:** Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja ya Bajeti hii kwa 100%, lakini nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri Mheshimiwa John Pombe Magufuli na Naibu wake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, sasa niingie katika hotuba hii pamoja na mazuri yote yaliyopo katika Wizara ya Ujenzi namuomba sana Mheshimiwa Waziri aiangalie kwa huruma barabara ya Solwa – Mwakitolyo na Didia – Solwa.

Mheshimiwa Spika, nazitaja barabara hizi kwa sababu ndiyo kitega uchumi kikubwa kwa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga kwani mchele tunaosema unatoka Shinyanga unatoka katika maeneo haya sasa barabara hizi sehemu kubwa ni mbuga ambayo maji yanasimama wakati wa masika, tunawasaidiaje wananchi wa Halmashauri ya Shinyanga ambao wanauza mazao yao kwa bei ndogo kutokana na miundombinu mibovu ya barabara hizi?

Mheshimiwa Spika, kutokana na ubovu wa barabara hizi unapelekea hata kuwa na vifo vingi vya akinamama wajawazito wanaotakiwa kwenda hospitali kubwa kwani magari yanahangaika sana kupita katika barabara hizi hasa wakati wa masika.

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali itusaidie wananchi wa Halmashauri ya Shinyanga katika barabara hizi angalau ziwe za mkoa na ziwe za changarawe kwani zikiwa nzuri pia zitaunganisha na Wilaya ya Kahama – Jimbo la Msalala na Wilaya ya Geita.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii lakini naomba nipewe majibu ya barabara ya Kolandoto – Kishapu – Mwanhunzi Ilani ya CCM 2005-2010, inasema itaweka lami naomba Waziri atakapokuwa anajumuisha anipe jibu kuhusu barabara hii, itaanza lini kwani sijaona fungu lolote katika barabara hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya Bajeti hii. Ahsante.

**MHE. JUMA A. NJWAYO**: Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kuunga mkono hoja. Aidha nawapongeza Waziri wa Ujenzi, Naibu wake, watendaji wote na wahandisi wote walioko chini ya Wizara hii kwa majukumu yao ya kila siku. Pia napenda kumshukuru na kumpongeza kipekee *Engineer* Omari Mataka – Mhandisi wa Mkoa wa Mtwara kwa kazi nzuri anayowafanyia Watanzania na hasa wana Mtwara. Mhandisi huyu ni mchapakazi, msikivu na mshauri mzuri, aongeze tu bidii zaidi ili Watanzania tuneemeke kwa kazi zake.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo ni kama ifuatavyo, Serikali ni lazima itazame upya utaratibu wa usimamizi wa barabara zinazojengwa nchini. Hivi ni kwa nini tunasubiri mkandarasi amemaliza kazi ndipo tumwambie haipokelewi, hajakidhi viwango na sio mapema anapojenga? Kusubiri kutoipokea haina tija badala yake tunasababisha usumbufu mkubwa usio wa lazima. Tuanze sasa kuwasimamia wakandarasi wetu tangu wanapoanza kazi na kila kwenye mapungufu yarekebishwe mapema badala ya kusubiri mwishoni.

Mheshimiwa Spika, usumbufu uliopo sasa kati ya Nangurukuru na Mbwemkulu kupita na kuchepuka nje pembeni mwa barabara iliyoanza kuzoeleka ni adha na ususmbufu usio kifani.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa Bajeti ya awali ya upembuzi yakinifu wa barabara kati ya Mtwara – Tandahimba – Newala hadi Masasi tuliambiwa gharama zake ni kama shilingi bilioni 2.3, lakini kwenye Bajeti ya Waziri ni takribani shilingi milioni 350 tu zimetengwa. Je, kuna uhakika wa kumaliza kwa fedha hizo. Nisingependa kusikia umaliziaji wa kazi hiyo umeshindikana kwa ufinyu wa fedha. Aidha, Mheshimiwa Rais wetu mpendwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete wiki iliyopita amewaahidi wananchi kwenye barabara hiyo kukamilika, hivyo ikitokea vinginevyo itakuwa kumbebesha Rais wetu uwongo usiokuwepo. Cha maana hapa ni kuwa Bajeti tengwa iendane na kazi tarajiwa kwenye barabara hii.

Mheshimiwa Spila wilaya zote za Mkoa wa Mtwara barabara zipitazo wilayani zina lami isipokuwa Tandahimba jambo ambalo inaonekana kana kwamba Wizara hii inaitenga Tandahimba. Naomba kwenye Bajeti ijayo angalau kilomita tano pale mjini papatiwe lami.

Mheshimiwa Spika, wananchi wamechoka na ahadi zisizoisha kwa eneo la Ndundu – Somanga. Ni vyema basi ahadi iliyopo kwenye hotuba hii kuwa mwezi Novemba, 2011, barabara hiyo itakamilika ikamilishwe.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawapongeza kwa ujenzi unaoendelea wa kipande cha lami cha kilomita tano kati ya Mtama na Mkwiti eneo la Kinolombepo, kwani naamini kukamilika kwake ni kumaliza vifo na upotefu wa mali za wananchi.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE**: Mheshimwa Spika, naanza kwa kuunga mkono hoja iliyoletwa mbele yetu na Wizara ya Ujenzi, pamoja na kuunga mkono hoja naomba nitoe ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara kuna baadhi ya maeneo yanayohitaji kufanyiwa marekebisho makubwa.

Mheshimiwa Spika, mizani za mpaka zimekuwa zikilalamikiwa na wananchi wengi kwamba zimejengwa kama miradi ya wakubwa fulani Wizarani kwani inakuwaje lori lipime katika mizani kubwa zilizojengwa barabarani ipime na kuonekana kutokuzidi lakini zinapoenda kupima mizani ya mpaka huonekana kuzidi kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba kwa kipindi hiki mikoa ya Rukwa na Katavi imepata miradi mingi ya barabara lakini pia ni ukweli usiopingika kwamba mikoa hii ilisahaulika kwa muda mrefu hivyo ni haki yake kupata miradi ambayo kwa sasa inaweza kuonekana na mingi lakini kimsingi si mingi ukilinganisha na miaka 50 tangu nchi hii ipate Uhuru.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee barabara ambayo ni *short cut (critical path)* kutoka Tunduma eneo la Isanga na Ndarambo kupitia Chonga Legeza – Mwendo Mwimbi, Kamawe, Tatanda Komkokwe hadi Kasanga bila ya kulazimika kupita Sumbawanga. Barabara hii maarufu kama barabara ya zamani ya Nyerumani inayounganisha nchi ya Tanzania na Burundi, na Zambia eneo la Mpulungu pamoja na *Congo DRC.*

Mheshimiwa Spika, barabara hii ni muhimu sana kwa nchi kwani itaunganisha nchi hizo nilizozitaja.

Mheshsimiwa Spika, kimsingi barabara hizi kwa upande wa Jimbo la Kalambo inahudumiwa na *TANROADS* ila upande wa Jimbo la Mbozi Magharibi inahudumiwa na Halmashauri ambayo hali yake ni mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, barabara hii niliyoitaja kwa upande wa Jimbo la Kalambo tatizo linalotukabili ni ujenzi wa daraja la Mto Kalambo, mto ambao ni mpana tangu lilivyojengwa na mkoloni wa Kijerumani.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SALEH A. PAMBA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. Napenda kukupongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri. Nawapongeza pia *TANROADS* na wadau wote wa sekta ya ujenzi kwa hotuba nzuri yenye kuleta matumaini ya kuifungua nchi yetu kwa barabara. Maeneo ambayo nayagusia katika mchango wangu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kivuko cha Pangani. Tunaishukuru Serikali kwa kutupatia Mv. Pangani II ambayo ni mkombozi kwa wakazi/wananchi wa Pangani. Katika Bajeti ya mwaka 2011/2012 zimetengwa fedha kwa ajili ya Pangani I, tunashukuru. Tunaiomba Serikali iharakishe ukarabati wa Pangani I. Hali ya kivuko cha Pangani I kimeharibika mno. Nadhani ni bora kununua kipya.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tanga – Pangani – Saadani – Makunze. Tunashukuru kwa Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hiyo. Ni matumaini yangu kwamba kazi hiyo itakamilishwa mapema na kwamba tutaisukuma katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili fedha zipatikane na barabara ijengwe haraka. Sisi Wanapangani barabara hiyo ni ukombozi wetu.

Mheshimiwa Spika, wakati wa utekelezaji wa *feasibility study* na *detailed design* wafikirie daraja ya Mto Pangani nayo iwe sehemu ya barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, thamani ya barabara zinazojengwa kwa gharama kubwa sana. Hizo ni fedha za umma za wananchi maskini, hivyo Serikali isimamie kuhakikisha kwamba barabara zinajengwa kiwango *(quality of roads).*

Mheshimiwa Spika, barabara ya Tanga – Pangani na Pangani – Muheza. Barabara hizi ni za changarawe *(gravel road).* Wakati wa masika barabara hizi hazipitiki kabisa. Mkandarasi chini ya *PMMR Programme* ameshindwa kabisa. Apatikane mkandarasi mwingine mwenye uwezo na utaalam ili barabara hizi ziweze kupitika wakati wote.

**MHE. SYLVERSTER MASSELE MABUMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na wataendaji wote wa Wizara hii muhimu kwa hotuba yao nzuri na kwa kazi nzuri kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, dira na dhamira ya Wizara ni nzuri sana kwa maendeleo ya sekta ya ujenzi. Hata hivyo ushauri wangu ni kwamba Wizara ihakikishe kwamba dira hii ijulikane na watendaji wote na wakala walio chini ya Wizara hii. Naamini Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wapo Wizarani kuhakikisha kwamba Ilani ya CCM inatekelezwa kwa vitendo.

Hoja yangu ni kwamba baadhi ya watendaji na hasa wahandisi wameshindwa kuwa wazalendo. Baadhi ya wahandisi wa Serikali wameshindwa kusimamia makampuni yanayopewa *tender* za kujenga barabara zetu na madaraja hawasimamiwi iapasavyo matokeo yake barabara zinajenga chini ya viwango na havina ubora kabisa. Mifano ipo mingi mojawapo barabara ya Kilwa – Dar es Salaam na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali ielekeze nguvu zake kwenye ujenzi wa barabara zetu kwa sababu uchumi wetu kwa sehemu kubwa utakuzwa kwa kuwa na barabara nzuri.

Mheshimiwa Spika, ni aibu kwamba kuna maeneo ndani ya nchi yetu yana mavuno mazuri ya vyakula, vilevile kuna maeneo yana upungufu mkubwa wa chakula. Hali hii imesababishwa na miundombinu mibovu ya barabara kwamba watu ambao maeneo yao yana mavuno mazuri wameshindwa kusafirisha mazao kwenda kuuza kwenye maeneo ambayo hayana chakula. Nashauri Bajeti hii mara tu itakaporidhiwa na Bunge lako Tukufu itumike kama Wizara ilivyoomba.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ninalopenda kulizungumza ni vivuko katika maeneo ambayo hayawezi kupitika bila ya vivuko. Umuhimu wa vivuko hivi unaeleweka hasa katika suala zima la kuokoa maisha ya watu wetu, pia katika kuinua hali za maisha ya watu wa maeneo husika kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, nashauri vivuko vyote viwe vinakaguliwa mara kwa mara ili kuvihakiki ubora wake. Pindi ikibainika kuwa vina kasoro, nashauri visiruhusiwe kubeba watu ili kuepuka maafa yasiyotarajiwa.

Mheshimwa Spika, kuhusu ubomoaji wa makazi ambayo yamejengwa ndani ya hifadhi ya barabara, Serikali Kuu na za Mitaa lazima washirikiane kuhakikisha kwamba wananchi hawafanyi ujenzi wa aina yoyote bila ya kibali kinachoidhinisha ujenzi huo. Kuanzia sasa napenda kushauri iwe mwisho ujenzi wowote kufanywa pasipo kibali kutoka mamlaka husika. Sheria hii ikizingatiwa italisaidia Taifa kuokoa fedha nyingi zinazotumika kuwalipa fidia wananchi. Pia itapunguza lawama na manung'uniko kutoka kwa wananchi wanaovunjiwa nyumba zao.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu mizani za kupima magari. Niseme tu kwamba baadhi ya watendaji si waadilifu, Serikali inapoteza fedha nyingi kutokana na malipo hafifu yanayofanywa na wenye magari ya mizigo bila kujali magari hayo yana uzito mkubwa ambao unaathari ya moja kwa moja kwenye barabara zetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie kuhusu msongamano wa magari katika miji mikubwa yakiwemo Majiji, Manispaa na Halmashauri ya miji hapa nchini. Naishauri Serikali iandae utaratibu wa usafiri maalum ndani ya miji yote mikubwa ili magari ya watu binafsi yasiruhusiwe kuingia ndani ya miji mikubwa, hii itasaidia kupunguza msongamano wa magari. Pia nashauri

pawekwe utaratibu mahsusi wa maegesho ya magari ili kupunguza ajali zinazotokana na uegeshaji mbovu wa magari katika miji mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ijenge maegesho mahsusi ya magari kama ilivyo katika miji mingine huko ughaibuni. Serikali ikijenga maegesho ya magari yaliyojengwa kwa utaratibu wenye kueleweka, Serikali itaweza kuongeza mapato yake kwa njia ya kodi ya kuegesha magari.

Mheshimiwa Spika, mwisho naunga mkono hoja.

**MHE. ABUU H. JUMAA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata fursa ya kuchangia Bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka 2011/2012. Nachukua pia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kazi kubwa ya kusimamia na kuendeleza sekta ya ujenzi wa barabara, mfuko wa barabara, Wakala wa Barabara, Wakala wa Majengo ya Serikali, Wakala wa Ufundi Umeme pamoja na kuratibu shughuli za Baraza la Taifa la Ujenzi. Bodi za Usajili wa Makandarasi, Wahandisi, Wasanifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi na Usimamizi wa vifaa na mitambo ya Serikali. Majukumu haya ni mazito kwani yanahitaji utaalamu mkubwa na umakini katika utendaji kuhakikisha rasilimali zinazotumika kuendeleza sekta hii zinaleta ufanisi na kutoa huduma bora na nafuu kwa wananchi.

Bajeti hii imelenga kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambayo inatoa msisitizo wa kuendeleza sekta ya ujenzi ili iwe endelevu na yenye ufanisi kwa maana ya kuwarahisishia wakulima kusafirisha mazao yao na pembejeo kuwafikia kwa urahisi kwa kutumia barabara zinazopitika kila msimu na kwamba sekta hii itafungua mianya ya huduma na maendeleo ya jamii na kiuchumi katika maeneo mengi hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kujenga na kukarabati barabara kuu kwa kiwango cha lami ni kazi ambazo wananchi wanaelewa zinatumia rasilimali na fedha nyingi za ndani na nje ya nchi. Inasikitisha kuona kwamba barabara hizo zinajengwa lakini baada ya muda mfupi sana zinakuwa na mashimo na mabonde na hii inawapa wananchi wasiwasi kwamba hakukuwa na usimamizi mzuri wa makandarasi wanaofanya kazi hizo na kutilia mashaka utendaji wa Maofisa wa Wizara. Aidha, udhibiti hafifu wa uzito wa magari na matumizi bora ya barabara zetu inachangia kwa kiasi kikubwa kubomoka haraka au kuwepo na mmomonyoko wa matuta katika kingo za barabara. Tatizo hili pia linaonekana katika ujenzi wa nyumba za Serikali ambapo nyumba nyingi zilizojengwa miaka ya karibuni na Wakala wa Majengo zina nyufa na nyingine zinahitaji ukarabati mkubwa. Mfano ni nyumba ya *DC* wa Siha Mkoani Kilimanjaro na naamini zipo nyingi sana za aina hiyo ambazo zinahitaji ukarabati.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki kama sitampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa kutambua mchango mkubwa unaotolewa na sekta binafsi katika kukuza na kuimarisha uendelezaji wa sekta ya ujenzi hapa nchini. Kwa kutambua umuhimu huo Wizara imeweka mazingira mazuri ya kushirikisha sekta binafsi katika ujenzi wa miradi ya barabara na majengo ya Serikali, madaraja na pia kuwezesha upatikanaji wa mitambo ya ujenzi na kuhamasisha watu binafsi kuanzisha kampuni za kukodisha mitambo. Mipango ya ujenzi wa Daraja la Kigamboni ni moja kati ya mipango ya Wizara ambayo wananchi wanongojea kwani wanaamini kushirikishwa kwa sekta binafsi katika mpango huu utawezesha daraja hilo kujengwa na kukamilika katika muda mfupi.

Pamoja na mipango hii mizuri, bado kuna malalamiko katika ushirikishwaji na uajiri wa makandarasi katika miradi ya ujenzi wa barabara na nyumba za Serikali. Makandarasi wengi wanalalamikia masharti magumu yaliyowekwa ili waweze kupata kazi hizo. Masharti hayo ni pamoja na kuwa na dhamana *(security bond)* ya fedha nyingi ambazo makandarasi hawa hawana. Japo wana utaalamu wa kufanya kazi, hawana dhamana za kuwapa uwezo wa kukopesheka, mitaji yao ni midogo sana hivyo kukosa nguvu ya kuweza kununua/kukodisha mitambo mikubwa ya kurahisisha kazi, pia hawana uwezo wa kuajiri wafanyakazi wengi ili kazi ikamilike haraka.

Serikali ingeweka mikakati au sheria za kuwawezesha makandarasi wananchi waweze kupata unafuu katika ushindani wa kupata kazi kama kuweka sheria za kuwataka makandarasi

wenye kampuni za kigeni kushirikiana na kampuni za wananchi vinginevyo sheria hii isiruhusu wastahili kupata kazi. Sheria hii itawasaidia sana makandarasi wetu kuwajengea uwezo wa kuongeza uzoefu wa kazi na ujuzi kwa kampuni za wananchi.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni kumekuwapo na wimbi la watendaji wa Wizara kupiga X kubwa kwa rangi nyekundu nyumba za wenyeji hasa vijijini ambazo wamejenga kabla ya barabara kupitishwa katika maeneo hayo. Hii imewasikitisha sana wananchi na wanaona kama ni fedheha kwani barabara zilifuata watu majumba na si watu walifuata barabara. Serikali katika zoezi la kutambua mipaka na maeneo ya barabara *(Road Reserve)* na hasa maeneo ya vijijini, ingewashirikisha wananchi na kuwaandaa kwa zoezi hilo. Pia Serikali ingetafuta kwanza pesa ya fidia na baada ya kukubaliana na wananchi wenye nyumba hizo waweze kuwalipa mara moja ili waweze kusogeza nyumba zao kutoka katika maeneo hayo badala ya kuwavamia na kuwawekea alama nyekundu za X bila maandalizi ya awali.

Mheshimiwa Spika, kilio cha wananchi wa Kibaha Vijijini kuhusu barabara ni kikubwa sana kwani kuna kata nyingine ukiingia lazima utokee barabara kuu na urudi barabara kuu ndipo uende katika kata nyingine. Naomba Serikali iwawezeshe vijana wa Jimbo la Kibaha Vijijini waweze kuhudhuria katika Chuo cha Teknolojia ya kujenga barabara za vijijini kilichoko Mbeya ili wawe chachu ya kushirikisha wananchi kuendeleza ujenzi wa barabara, kufungua maeneo yao kwa njia ya nguvu kazi.

Katika maombi ya kuhakikisha barabara zinapitika na kusaidia wananchi wa Jimbo hili kusafirisha mazao na mifugo yao, wananchi wana matarajio makubwa katika Bajeti ya mwaka huu na wanaiomba sana Wizara itekeleze mipango ya ujenzi wa barabara ya Makofia hadi Mzenga inayotoka Bagamoyo kupitia Kibaha Mjini hadi Kibaha Vijijini, Kisarawe na kuishia Mkuranga. Pili barabara ya kutoka Kongowe hadi Bagamoyo kuelekea Kibaha Mjini, Kisarawe hadi Mkuranga na mwisho barabara ya Chalinze hadi Magindu kuelekea Morogoro Vijijini. Naunga mkono hoja.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Spika, niruhusu nitoe pongezi zangu kwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya hasa ujenzi wa barabara. Kazi ya Wizara hii inaonekana kwa macho na tunaipongeza. Tanzania yenye barabara nzuri inawezekana. Pamoja pongezi hizo naomba nichangie yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kyaka Bugeni kilomita 59.1 kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Karagwe niruhusu nitoe shukrani zangu kwa Serikali hasa Wizara ya Ujenzi kwa kukubali kutekeleza ahadi ya Rais ya kujenga barabara ya Kyaka – Bugene kilomita 59.1. Wananchi wa Karagwe wanashukuru sana na tunamuomba Waziri afikishe shukrani hizi kwa Mheshimiwa Rais. Ombi letu ni kwamba Serikali ihakikishe kuwa kampuni iliyopewa kazi hiyo inafanya ujenzi huo kwa kiwango cha hali ya juu sana na kwa muda uliokubaliwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Bugene – Kasulo, kipande cha barabara ya hii ndicho kipande kitakachokamilisha na kuunganisha barabara ya Kyaka – Bugene kwa maana ya barabara ya kuunganisha barabara ya lami inayounga nchi za Uganda na Rwanda. Ni barabara muhimu sana hasa kwa kuwa inatumika kusafirisha mizigo toka bandari ya nchi kavu ya Isaka.

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Serikali Bungeni kwamba upembuzi yakinifu ungeanza Julai, 2011. Sina uhakika kama upembuzi yakinifu huo umeanza. Kama bado naomba uanze haraka na *tender* zitangazwe ili mkandarasi aingie *site* aanze kazi mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Gakorongo – Murongo, Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2005 imeelezea kuifanyia upembuzi yakinifu barabara hii katika mwaka wa fedha wa 2011/2012. Napenda kujua kama kazi hii imeanza na kama haijaanza naomba ianze haraka, *tender* zitangazwe na barabara hii ijengwe kiwango cha lami. Ahadi ya Serikali ni kuikamilisha barabara hii ndani ya miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, fidia kwa wananchi watakaovunjiwa nyumba zao na mali zao. Katika ujenzi wa barabara ya lami ya Kyaka – Bugene itapita katika maeneo ya makazi ya watu na hivyo

wengi wao watapoteza nyumba na mali zao hasa migomba na kahawa. Natambua sheria za nchi kuhusu fidia katika hili napenda niseme kuwa tulishapitisha shilingi bilioni tano (5,000,000,000,/=) kwa ajili ya fidia. Wananchi wengi wamekuwepo miaka mingi enzi za mkoloni na kabla ya Uhuru. Hivyo hawajavunja sheria yoyote ya nchi na hawakuwahi kuvamia eneo la barabara hiyo, hivyo wanahitaji kupewa fidia bila kuzungushwa. Ninaomba na kuisihi Serikali isifanye vinginevyo kuwanyima wanannchi hawa fidia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, natanguliza kuunga mkono hotuba ya Waziri wa Ujenzi. Kazi iliyofanyika ni wazi kwani barabara zote zilizojengwa zinaonekana kwa watu wanaosema hakuna kilichofanyika wanakosea. Barabara za lami zimejengwa, barabara za changarawe zimejengwa ni wazi kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwenye halmashauri zetu zote zinapata fedha toka mfuko wa barabara na hakika kwamba sehemu kubwa barabara zimefanyika hata wenzetu wa Vyama vingine wanajua kwani wanapitisha fedha kwenye Halmashauri zao.

Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo zimejengwa kwenye hifadhi za barabara na sasa zimewekwa X kwa ajili ya kubomolewa, ni kweli kwamba kuna majengo katika hifadhi za barabara na ni haki kubomolewa kinacho stahili ni malipo kwa kiwango kinachostahili na kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Spika, kuna wananchi wa Kamwanga ambao wamevunjiwa nyumba zao na hawakulipwa. Kuna baadhi wamelipwa na wengine hawakulipwa. Kinachoshangaza ni kulipwa wananchi wa Kamwanga Juu ambayo ni Rombo na Kamwanga Chini ni Longido bado malipo hayajafanyika.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya Arusha - Namanga. Barabara hiyo kuna sehemu ambayo imejengwa chini ya kiwango, nashukuru Waziri amekuja kuona kasoro hii na kutoa tamko ijengwe tena mpaka sasa bado mkandarasi hajafumua lami na kujenga tena naomba ufuatiliaji ili kazi hiyo iboreke.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali kwa kukubali kujenga barabara ya Kamwanga – Sanya Juu nimelia kwa muda mrefu ili kuunganisha barabara anmbayo imejengwa na kuishia Kamwanga sasa inaunganishwa nashukuru sana. Kilichobaki ni kufidia nyumba za wananchi zilizobomolewa.

Mheshimiwa Spika, kuunganisha Wilaya ya Siha na Wilaya ya Longido, niliomba barabara hiyo iwe ya mkoa kwa kuwa kwanza inaunganisha Mkoa wa Kilimanjaro na Mkoa wa Arusha pia inaunganisha Wilaya ya Siha na Longido. Barabara hiyo ikimalizika hakutakuwa na sababu ya kutoka Namanga kwenda Moshi kupita Arusha kwani kutoka Longido Siha ni kilomita 56. Naomba kwa kuwa Waziri ametuma watu waliokwenda kuangalia barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, upanuzi wa barabara ni muhimu, kwani wembamba unasababisha ajali nyingi ambazo zinatokea mara kwa mara.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Awali ya yote napenda kumpongeza Waziri wa Ujenzi - Mheshimiwa Dkt. John Pombe (Kingoni Mnyakaya) Magufuli pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe kwa kazi nzuri na ya uwazi na *speed* tunayotaka. Makandarasi pia wanawapongeza. Pia nachukua nafasi hii kumpongeza Katibu Mkuu kaka yangu Balozi Herbert E. Mrango, na Naibu wake Dr. Eng. John Ndunguru kwa kuanza na kasi zaidi, ari zaidi na nguvu zaidi hasa katika maeneo ya Mikoa iliyokuwa pembezoni na kwa kweli zilisahaulika. Nawapongeza wote kwa ujumla akiwemo Mr. Kilowoko, Eng. Kissimbo na kwa kweli na dada Ngimbwa Mwenyekiti wa *Board* ya Makandarasi mwanamke.

Mheshimiwa Spika, mimi sikuridhishwa kabisa na hoja ya Mbunge mwezetu yenye fitna na ubinafsi ya kuhoji maeneo viongozi kama Rukwa au Mwanza kupata ujenzi wa barabara. Hivi anataka vitu vyote, kazi zote ziende kaskazini tu? Chuo cha Maendeleo kipo wapi? *KIA* ipo wapi?

Mahakama ya Haki za Binadamu ipo wapi? Makao Makuu ya *EA* yako wapi? Mbona sisi wa Kusini hatujalalamika? Hizo barabara anazolalamikia ni zipi? Si ndizo hizo kuu ambazo wao wanazo zaidi ya miaka 30 au 20 iliyopita? Ukiwa kiongozi ndiyo wananchi wanaotoka eneo hili wateseke? Huo ni ubinafsi, na haufai kuendelezwa. Kabla hajasema, atembelee kwanza maeneo hayo na ndipo apime. Tunamheshimu sana, aunge mkono bajeti hii kama sisi tulivyounga mkono wakati anafuatilia umeme wa Ngadu na vijiji vingine. Nawatia moyo Wizara, msitubague.

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Ruvuma umepata mvua nyingi na wakati mwingine ni kipindi cha mvua. Nashauri pesa zilizotengwa zipelekwe mapema ili kuwezesha kufanya kazi kabla ya mvua kuanza.

Nashukuru na kupongeza barabara za eneo la Kitanda, Ifinga na ile ya kutuunganisha na Mkoa wa Morogoro, kwa kweli barabara hizi ni muhimu sana. Mkoa wa Ruvuma una mbuga kubwa ya *Selous*, lakini Mkoa huu umekuwa haufaidiki kabisa na fursa hii kutokana na watalii kushindwa kupitia Mkoa wa Ruvuma. Barabara hizi zitengewe pesa angalau moja iwekwe *Otta seal* ili kuwezesha utalii.

Mheshimiwa Spika, napongeza sana barabara ya Dodoma – Iringa, Masasi - Tunduru – Namtumbo – Songea (Peramiho) – Mbinga – Mbambabay. Angalau watu wataelewa maana ya *Mtwara corridor*, na kwa kweli itawezesha pia kupunguza bei ya chakula.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hakuna meli wala reli, mazao yote hupitia barabara kuu ya Songea – Njombe – Dar es Salaam na kadhalika, ni vyema barabara hizo zitengewe pesa za kutosha kwa ajili ya maboresho.

Nampongeza Mkandarasi wa Luhekoi, ni Mtanzania na anafanya kazi nzuri. Nashauri wawezeshwe na wapate bei nzuri kulingana na kazi, kwa tabia ya kuwanyonya sana *local contractors,* ndio maana hawakui.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa bajeti ya Liuli – Lituhi sehemu hii ilioza kabisa, lakini pia ungaliwe utaratibu wa kipande cha *Mbamba Bay* – Liuli na eneo la Mto Lwika, Lundo, mto unafurika na kuna mradi wa kilimo cha mpunga, ni vyema kuishirikisha Wizara ya Kilimo na Chakula – umwagiliaji ili kuchangia pesa katika eneo la mradi, kwani gharama ni kubwa.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunisikiliza, kilio changu barabara ya Nyoni – Maguu-Kipape – Chemeni – Matuta – Mango – Njombe. Barabara hii ni muhimu sana kiuchumi na inawezesha kupunguza umbali wa safari. Isitoshe eneo hili la barabara ndilo eneo kuu wa zao la kahawa nchini.

Mheshimiwa Spika, naungana na Mheshimiwa Komba kuhusu kuboresha stendi ya Songea mjini.

Mheshimiwa Spika, napongeza barabara ya Mbinga – Litembo – Mkili, ni muhimu sana la msingi pesa itolewe kwa wakati. Naipongeza Wizara kwa kuboresha barabara za Tabora kwani niliwahi kuchangia humu Bungeni juu ya hali mbaya ya barabara za Tabora, lakini pia Rukwa, mlishangaa kuona lami zipo mita 50 kushoto na kulia mwa daraja, ni vyema mmefanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, nashauri *TBA* iruhusu pia kujenga nyumba kwa ajili ya kuuza hasa katika Mji wa Dodoma ili kukuza Mji.

Mheshimiwa Spika, kuna kijumba kidogo kilichokuwa kinatumia na *Comworks* wakati wa ujenzi wa barabara ya *Mbamba Bay* Lituli (Kihagara) kijiji nilichotoka mimi, hakitumiki na kinaharibika tu, kwani hakina mlinzi na milango ilibomolewa. Mzee yule aliyekuwa analinda mwanzo wala hakupewa chochote. Naomba afutwe machozi hata kama ni Sh. 100,000/= tu, na kijumba hicho tuwape wananchi wakitumie kwa ajili ya vikundi vya barabara vijijini ambavyo tumeanzisha. Hivyo itawezesha kutunza eneo hilo pamoja na jengo. Aidha, Wizara itoe pesa kidogo na jengo. Aidha, Wizara itoe pesa kidogo kukarabati jengo hilo. Naamini kuwa milioni motu tu itarekebisha vizuri jengo hilo badala ya kutuwekea gofu, kwani nasi vijijini tumechoka magofu.

Mheshimiwa Spika, mwaka huu hatuwezi kudai zaidi, kwani pesa hazitoshi, lakini mwanzo mzuri. Tunashauri tu kwenda na *schedule* ili mwaka kesho barabara hizi ziwe zimekwisha, tupeleke huduma maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali iwezeshe makandarasi kutoa mizigo yao mapema bandarini. Utaratibu uliopo ni mbaya na unaongeza gharama za mradi. Isitoshe gharama ya *demurrage* inayochajiwa haisaidii nchi, kwani inakwenda kwa *shipping lines*, lakini mzigo wote unabebwa na Watanzania. Ni vyema kuangalia vizuri suala hilo ili kuondoa tatizo hasa kwa *local contractors.* Wizara iongee na Wizara ya Fedha juu ya suala hilo.

Aidha, Wizara iandae eneo maalum linalowezesha mizigo inayolenga kujenga barabara zake kutolewa na kuwekwa hapo wakati mambo ya malipo ya kodi yanandaliwa ili kumpunguzia mzigo *contractor* au *supplier*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kutoa mchango wangu katika Wizara hii muhimu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nina mambo machache ambayo ningependa kuyazungumzia katika bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, wakala wa ufundi na umeme *(TAMESA)* moja ya majukumu ya kitengo hiki pia ni kutengeneza magari ya Serikali lakini cha ajabu tumeshuhudia magari ya Serikali yakienda kutengezwa kwenye *garage* za watu binafsi au makampuni na kuacha kitengo hiki cha Serikali ambacho naamini kina uwezo. Ninaomba zichukuliwe hatua za haraka kuhakikisha Wizara zote za Serikali zinalazimishwa kupeleka magari na vifaa vyote vya Serikali kutengenezwa katika kitengo hicho.

Mheshimiwa Spika, kila Wizara imetenga bajeti ya matengenezo ya magari na vifaa vingine kwa ajili ya Wizara zao, hivyo ni vizuri fedha hizi zikapelekwa katika kitengo hiki. Kama Wizara hazitalazimishwa kupeleka magari, lakini naamini hawatafanya kwa sababu huko hakuna 10% wanazozipata kwenye makampuni au *garage* za watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, Makampuni haya yana bei za ajabu sana kwa sababu ya kuweka hizo 10% za wakubwa wanaowapelekea magari ya kutengeneza. Kama kweli tunataka kuokoa fedha hizi lazima tuwe wakali katika hili.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhusu magari ya Serikali na matumizi yake. Tumeona magari ya Serikali yakitumika kwenye shughuli ambazo siyo za kiserikali, mfano, kupeleka wake wa wakubwa sokoni, *salon* na mengi baada ya saa za kazi yanaonekana maeneo ya starehe. Naamini hii siyo sahihi. Naungana na maoni ya Kamati ya Miundombinu ya kutaka Maafisa wa Serikali wanaostahili kutumia magari ya Serikali wakopeshwe magari na kupewa posho maalum kwa ajili ya kununulia mafuta ya kuendeshea magari hayo badala ya kutumia magari ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia naomba baada ya kazi, magari haya yaegeshwe kwenye maeneo mahsusi yaliyotengwa na Wizara husika maana tunayaona yanaegeshwa huko Mitaani. Naamini huu siyo utaratibu wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na malalamiko kwa wasafirishaji kuwa mizani zimezidi na hii inawacheleweshwa sana njiani. Wanaomba kuwe na utaratibu mzuri wa kupunguza vituo hivyo ili kupunguza usumbufu wanaoupata. Suala lingine kuhusu mizani, wanadai mizani hizo zinatoa uzito tofauti. Unaweza kupima mizani ya Kibaha ukaambiwa uzito uko sawa, lakini ukifika Chalinze unaambiwa umezidisha uzito. Ni kwa nini kunakuwa na tofauti hizo? Tunaomba Wizara iifuatilie tatizo hili kwa karibu ili tuweze kuondoa kero hizi kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru. Hayo ndiyo machache niliyokuwa nayo, mengi nilichangia katika Kamati yetu ya Miundombinu kwa kuwa mimi ni Mjumbe.

**MHE. ALBERT OBAMA NTABALIBA:** Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Wizara ya Ujenzi kwa kazi nzuri inayofanywa na Waziri - Mheshimiwa Dkt. John Magufuli na Naibu wake – Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe pamoja na Watendaji wa Wizara. Nchi inayo imani na utendaji wao, na ndiyo maana wameaminiwa kwa kupewa bajeti kubwa kuliko Wizara nyingine.

Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuwashukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa juhudi zake za kutafuta fedha na kuzindua barabara ya Manyovu – Mwandika, barabara ya Uvinza na Daraja la Maragarasi. Napongeza kuweka mipango ya ujenzi wa barabara ya Kidahwe hadi Nyakanazi.

Mheshimiwa Spika, nina ombi maalum kwamba ujenzi wa barabara toka Manyovu hadi Kasulu (km 42) iwe kwa kiwango cha lami. Sababu ya ombi hili ni:-

(a) Kuunganisha nchi ya Burundi kupitia Manyovu hadi Kasulu kuelekea Bukoba, Mwanza na Dar es salaam, kwa sababu kuna mabasi yanayotoka Burundi – Bujumbura hadi Dar es Salaam.

(b) Wananchi wameienzi Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Naomba tuwape ushirikiano huo huo, kwani walituchagua vya kutosha kwa imani hiyo ya barabara.

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri alisemee kwenye majumuisho yake.

Mheshimiwa Spika, ningeomba barabara za Mkoa nazo zipewe lami, kwani Mkoa wa Kigoma zimeonyesha hazitajengwa kama Mikoa mingine nilivyoona na Wizara iliyowasilisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mizani, naomba mtindo wa faini upunguzwe, kwani wenye magari hawapunguzi uhalifu huo. Ombi ni kushusha mzigo huo na ndiyo itakuwa dawa ya kuzidisha mizigo.

Mheshimiwa Spika, nimempa Waziri wa Ujenzi - Mheshimiwa Dkt. John Magufuli madai ya wanananchi wa Mnanila juu ya fidia ya maduka 120. Ombi langu kwa Waziri ni kuliangalia jambo hilo kwa moyo wa huruma sana, kwani walipoteza nguvu zao na mitaji kwa kujenga maduka ya kudumu kwa maagizo ya Halmashauri ya Wilaya iliyodhani barabara ingepitia pembeni. Mheshimiwa Magufuli, tupe faraja yako.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawatakia maisha mema ya usimamizi mzuri sana wa Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LETICIA NYERERE:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kwa jitihada zake kubwa kwa kuchapa kazi na Watanzania wote wanalifahamu hili.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo unalenga kukumbushia ahadi ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete ya mwaka 2005 aliyoitoa hapo Ngudu Kwimba. Mheshimiwa Rais aliahidi barabara ya lami kutoka Mabuki – Ngudu – Malya, vilevile kutoka Ngudu kwenda Magu.

Kwa kuwa Mheshimiwa Rais alisimikwa Uchifu baada ya ahadi hiyo, na kupewa Jina la “Nh’umbu Banh’u” kwa maana ya kumbukumbu ya watu. Katika mila za Wasukuma, unapotoa ahadi hii unatarajiwa kutekeleza ahadi hiyo haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa ni miaka sita tangu Mheshimiwa Rais atoe ahadi hiyo, na kwa kuwa tungependa kulinda heshima ya Mheshimiwa Rais Usukumani, namwomba Mheshimiwa Waziri atumie uzoefu na ubunifu wake kutekeleza ahadi hii haraka iwezekanavyo.

Kwa kufanya hivyo, tutaendelea kulinda heshima ya Rais wetu mbele ya macho ya Wasukuma hasa wale wa Wilaya ya Kwimba.

Mheshimiwa Spika, sina sababu ya kutokuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri, hasa ikizingatiwa kuwa Waziri wa Ujenzi amekuwa ni mfano wa kuigwa na viongozi wetu nchini.

**MHE. AMINA N. MAKILLAGI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika hoja iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia moja moja.

Mheshimiwa Spika, nianze kumpongeza Waziri wa Ujenzi - Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Naibu Waziri - Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe, Katibu Mkuu na wale wote walioshiriki kwa namna moja au nyingine kuandaa bajeti hii. Baada ya pongezi, natoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nikianza na suala la ujenzi wa barabara, naipongeza Serikali kwa kazi kubwa na nzuri inayofanywa ya kuhakikisha nchi yetu inafungua barabara kwa lengo la kuunganisha nchi yetu na nchi za jirani, Mkoa kwa Mkoa, Wilaya kwa Wilaya, Vijiji kwa Vijiji kazi ambayo inasaidia kuimarisha uchumi wa Taifa. Pamoja na kuipongeza Serikali, naomba kuishauri katika maeneo machache yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na tatizo kubwa la ujenzi wa barabara na Madaraja yasizokidhi kiwango na kusababisha Serikali kuingia hasara ya matengenezo ya mara kwa mara, hivyo kuongeza matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kuwa Serikali iwe makini wakati wa kuchagua Mkandarasi wa ujenzi wa barabara na madaraja. Pia sheria inayombana Mkandarasi, lazima isimamiwe vyema, ili yule aliyehusika katika ujenzi wa barabara mbovu ikitokea kuharibika kabla ya muda uliowekwa Mkandarasi na mshauri husika wawajibishwe kwa kujenga barabara au daraja hilo kwa gharama zake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara za kuunganisha Mikoa kwa Mikoa, Wilaya na Wilaya, katika baadhi ya Mikoa na Wilaya, bado lipo tatizo la mawasiliano ya barabara kati ya Mkoa na Mkoa, Wilaya na Wilaya, mfano, Mkoa wa Pwani, Mara, Kigoma na Tabora barabara za kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa na Wilaya za Mkoa bado hazijafunguka na zilizofunguka ni kiwango cha changarawe. Naishauri Serikali sasa ifanye uamuzi wa kuunganisha Mkoa na Wilaya zake kwa kufungua barabara.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ukarabati wa barabara kwa changarawe, naishauri Serikali itenge fedha kila mwaka kujenga barabara moja katika kila Mkoa kwa kiwango cha lami badala ya ujenzi wa changarawe, ujenzi ambao kila mwaka unagharimu fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali itafute mkopo kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami katika Mikoa ya Nyanda za juu Kusini, Kanda ya *Ziwa Victoria*, Kanda ya Kati ili kuweza kufungua milango ya uchumi katika Mikoa hiyo yenye raslimali nyingi ambazo zinachangia kukua kwa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, uharibifu wa barabara kutokana na tatizo la magari yanayobeba abiria na mizigo kuzidi uzito limekuwa ni tatizo kubwa sana. Naishauri Serikali itazame utaratibu wa kuwatoza wahalifu fedha kama adhabu ya kubeba mizigo kuliko uwezo wa gari na barabara. Badala ya kulipa fedha kama adhabu, wapewe adhabu kali ya kuteremsha mizigo yote na kuitaifisha na kupiga mnada ili fedha itakayopatikana iwekwe kwenye mfuko wa barabara na kusaidia maeneo husika ya ujenzi wa barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba Mheshimiwa Waziri atakapohitimisha hoja yake anipe maelezo ya kina ni lini:-

(a) Barabara ya Musoma – Busekera – Musoma vijijini itajengwa kwa kiwango cha lami?

(b) Nini kauli ya Serikali katika kutenga fedha katika mwaka wa fedha 2012/2013 ili barabara zifuatazo zijengwe katika kiwango cha lami?

(c) Barabara ya Musoma – Busekera, barabara ya Makutano, Butiama, Mugumu, Loliondo, Kibaha, Bagamoyo, Kibaha, Kisarawe, Daraja la Rufiji Utete, barabara ya kuunganisha Tabora na wilaya zake?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru sana Serikali kwa kuendelea kuboresha barabara za Mkoa zilizoko Mkoani Njombe, hususan barabara za Njombe – Makete, Ndulamo – Kitulo – Mfumbi; Makete – Bulongwa – Kikondo na kuipandisha hadi barabara ya Ikonda – Lupila – Mlangali kuwa barabara ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya Njombe - Makete kilometa 109. Barabara hii ni miongoni mwa barabara ambazo zimeahidiwa na Serikali ya Awamu ya Nne kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 – 2015 na pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyotoa kwa wananchi wa Makete.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kuwa hakuna fedha zilizotengwa hata kidogo kwa ajili ya kuanza ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami. Naomba maelezo ya Serikali, ni lini utekelezaji wa ahadi hii utaanza, hasa ukizingatia kwamba muda wa kufanya kazi Makete ni miezi minne tu kwa mwaka kwani miezi mingine yote huwa ni kipindi cha mvua.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kikondo – Makete ndiyo inayounganisha Mkoa mpya wa Njombe na Mbeya kwa kupitia Makete. Hii ndiyo barabara inayopita kwenye vitega uchumi vya Taifa vya Hifadhi ya Taifa ya Kitulo, shamba la ng'ombe wa maziwa Kitulo na mradi wa kufua umeme wa Bulongwa kwenye maporomoko ya Mto Rumakalya/Ruvanyina. Hakuna mpango wowote wa Serikali kuijenga kwa kiwango cha lami. Serikali itoe maelezo ina mpango gani wa kutengeneza barabara kwa kiwango cha lami? Hivi kweli Serikali inajali vitega uchumi hivi vilivyopo Makete?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Ikonda – Lupila – Ludewa imepandishwa hadhi na kuwa ya Mkoa, lakini cha kushangaza katika mwaka huu wa fedha 2011/2012 hakuna fedha yoyote iliyotengwa kuhusu matengenezo ya barabara hii. Naomba Serikali itoe maelezo kuhusu mpango mkakati wa barabara hii kutengenezwa. Barabara hii inaunganisha Mikoa mitatu ya Mbeya, Njombe na Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana wizara kwa kuweka mkazo katika matumizi ya nguvu kwa kutumia *labour based technology*. Naishauri kazi zote za barabara za vijijini ambazo bajeti yake huwa ni ndogo, basi zitekelezwe kwa kutumia mfumo huu kwa sababu hii itasaidia kuongeza kipato kwa wananchi na pia kuongeza ubora wa barabara zenyewe kwani wanaotumia wakishiriki kutengeneza watakuwa na uchungu wa kusimamia katika miradi hii ya barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalamu wake kwa kuandaa hotuba hii na kuleta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, tunaishukuru sana Serikali kwa dhamira na nia nzuri ya kuangalia na kuanza mchakato wa kuanza kufungua Mkoa wa Tabora na kuunganisha na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali kupita *TANROADS* kuingia Mkataba na Makandarasi kwa ujenzi wa lami barabara za Nzega – Tabora (km 115), Manyoni – Itigi (km. 264), Tabora – Urambo (km. 94) tangu tarehe 30 Julai, 2010 lakini bado miradi yote inasuasua.

Mheshimiwa Spika, tangu tumeingia Mkataba na Wakandarasi hao ni mwaka sasa unakaribia kwisha na kazi bado haijaonekana angalau kwa robo yake.

Mheshimiwa Spika, tulichoshughulikia na kilichopo ni makandarasi kuandaa maeneo na kuletea vifaa vya *site*. Zaidi ya hili, hakuna kingine kilichofanyika.

Mheshimiwa Spika, wataalam na wakandarasi wale hawajapewa fedha za kuanza ujenzi wa barabara zote tano za Mkoa wa Tabora. Tunaitaka Serikali ifafanue hapa Bungeni, ni kwa nini hili limetokea wakati ahadi ya Serikali ilikuwa ifikapo 2011 angalao ½ ya kazi uwe imekamilika?

Mheshimiwa Spika, mwaka huu 2011/2012 fedha zimetengwa kwa ajili ya barabara zote za Tabora. Tunaiomba sana Serikali fedha hizo zitoke kwa wakati ili ujenzi uende kwa wakati na kuepuka kuongezeka kwa gharama kwa mipango ambayo tayari ilishapitishwa.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa la ubora wa barabara zetu zinazotegenezwa kwa *Road Fund* na baadhi ya wakandarasi maeneo mbalimbali. Hili linasababishwa na kukosekana kwa *(follow–up)* ufuatiliaji kuanzia hatua za mwanzo wa miradi. Serikali inakabidhi kazi kwa mkandarasi inamwachia bila kumpa nini anatakiwa kukabidhi kwa Serikali. Naye anafanya anavyopenda.

Mheshimiwa Spika, tunatakiwa kama nchi kuwa na viwango vya ubora wa barabara tunazozihitaji. Kwenye mikataba ya ujenzi wa barabara ilelezwe wazi ili wanaopewa kazi hizo wakienda kinyume wawajibishwe.

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo kubwa la msongamano wa magari kwenye mizani zetu. Muda mwingi sana unapotea pale Wizarani matokeo yake *drivers* wakitoka pale wanaendesha *speed* kubwa ili kufidia muda, nalo linasababisha ajali barabarani. Serikali iangalie jinsi ya kuweka utaratibu utakaosaidia kupima magari (hasa ya abiria) haraka na kuokoa muda, lakini pia kuepusha abiria kusafiri usiku na kupunguza ajali. Mizani ya Mikumi, Mikese na Kibaha inatisha kwa foleni.

Mheshimiwa Spika, matuta ya barabarani hayana viwango, hakuna *standards* za aina ya matuta kwenye barabara zetu. Mengine yapo kama vichuguu (yana ncha) inayoharibu magari na vyombo vingine vya barabarani. Matuta ni muhimu yawepo kwa kuwa yanadhibiti mwendo lakini yawe na viwango na *standard* zinazokubalika. Yasiwe kero kwa watumiaji.

Mheshimiwa Spika, alama za barabarani zinaondolewa sana kwa ajili ya vyuma chakavu. Hili ni tatizo, baadhi ya ajali zinatokea kwa sababu hakuna alama yoyote ya kuonyesha *speed limit*, au kona, daraja na kadhalika. Serikali ilete sheria hapa Bungeni ya kuthibiti wizi wa alama za barabarani.

Mheshimiwa Spika, naomba Waziri atueleze, ni adhabu gani inatolewa kwa madereva wanaogonga alama za barabarani, mfano, kingo za mito, madaraja, kona na kadhalika? Limekuwa ni jambo la kawaida dereva akishagonga anaondoka na hakuna hatua yoyote wala kurudishia eneo lililoharibiwa.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kahira – kilomita 60 Kakonko kwenda Mpanda (Wilaya ya Urambo)ilipandishwa hadhi kuwa ya *TANROADS* tangu mwaka 2008. Hadi leo haijawahi kupata matengenezo makubwa angalau kwa kiwango cha changarawe. Mwaka 2009 ilipitishwa greda kwa ajili ya kusafisha tu. Hakuna mifereji iliyowekwa kutolea maji ya mvua. Matokeo yake mvua zikinyesha, haipitiki kabisa. Naiomba Serikali iangalie pia eneo hili.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Urambo – Ulyankulu ni muhimu sana kwa kusafirisha mazao yanayolimwa Ulyankulu kulisha Mkoa mzima na Mikoa mingine. Tunaiomba Serikali ihakikishe barabara hii muhimu inapandishwa hadhi, isimamiwe na Serikali kuu.

Mheshimiwa Spika, nina imani kubwa sana na Mheshimiwa Waziri Magufuli na Naibu wake katika utendaji wao kwenye Wizara hii. Tunatumaini tarehe 23 June, 2012 barabara zetu za Tabora zitakabidhiwa rasmi zikiwa zimekamilika kwa viwango na ubora.

**MHE. DUSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuiunga mkono hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Ujenzi kutokana na ukweli kwamba Wizara hii ina jukumu kubwa la kujenga misingi endelevu ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu na vile vile kujenga *image* ya Serikali ya CCM kwa kuhakikisha kuwa miradi ya barabara inakamilika na barabara zinapitika katika vipindi vyote vya mwaka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuunga mkono hoja hii, ni ukweli usiopingika kuwa hali ya barabara zetu hususan za vijijini ni mbaya sana, na kwa bahati mbaya sana huku ndiko waliko Watanzania wengi takriban asilimia 80 na ndiko ambako uzalishaji wa nchi hii imejikita. Kwa hali hii, siyo ajabu kuwa umaskini unazidi kujikita vijijini maana wazalishaji wa nchi hii hawana miundombinu inayowawezesha kutumia vyema fursa za kiuchumi zilizopo.

Mheshimiwa Spika, ubovu wa barabara za vijijini kwa kiasi kikubwa unakwamisha uzalishaji mazao vijijini, unaongeza gharama za usafirishaji na hivyo kuongeza gharama za maisha na kufanya bidhaa zetu kushindwa kushindana. Miundombinu mibovu ni kikwazo siyo tu kwa biashara kati ya Wilaya kwa Wilaya, Mkoa kwa Mkoa, bali ni kikwazo kibiashara kati yetu na nchi nyingine. Hali hii inatukosesha kama Taifa fursa nyingi za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, lazima tuweke mkakati madhubuti wa kuboresha barabara zetu husan za vijijini kupitika katika vipindi vyote vya mwaka. Hili ni jambo muhimu sana kwa ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Lazima tuwe na mfumo bora wa kifedha utakaotuwezesha na kutuhakikishia kufanyika kwa kandarasi za barabara kwa uhakika. Wakati umefika sasa wa kuibua miradi ya *PPP* hata kwa barabara za vijijini.

Mheshimiwa Spika, tunashuhudia ukuaji wa kasi wa gharama za ujenzi wa barabara; wakati hali ikiwa hivyo ni muhimu sasa kuhakikisha kuwa viwango vya ubora wa kandarasi zetu nazo zinapanda. Wajenzi wabanwe ili kandarasi hizi zitupatie barabara za viwango vinavyolingana na fedha nyingi tunazotumia na tuhakikishe barabara hizi zinadumu kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu tukijipanga na kuchukua hatua madhubuti za kuwa na *performance based maintenance contracts*. Kwa kufanya hivi, itasaidia kuwafanya wakandarasi kulazimika kuboresha viwango vya utendaji kazi wao na kuondokana na kuingia gharama zisizo na ulazima wowote.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Mkinga, tunaishukuru Serikali kwa kazi kubwa iliyoifanya ya kuhakikisha Wilaya ya Mkinga inapata barabara za uhakika. Barabara ya Tanga - Horohoro inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunashukuru kwa fidia zilizotolewa kwa wananchi. Hata hivyo, wapo wananchi ambao walibomoa nyumba zao kwa hiari yao wenyewe na kutolipwa wakati wa zoezi la ulipaji fidia. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuahidi kuwa Serikali itahakikisha inawalipa wananchi hawa. Naomba kauli ya Serikali, ni lini ahadi hii ya Mheshimiwa Rais itatekelezwa?

Mheshimiwa Spika, barabara ya kuunganisha Tarafa ya Marimba na Makao Makuu ya Wilaya (Kasera) hai sasa haijafunguka. Ahadi ya Serikali ilikuwa barabara hii ingekuwa imefunguka mwezi Juni, 2010. Nini kimesababisha barabara hii isifunguke kama ilivyopangwa?

Tunashukuru kuwa kwa mwaka huu barabara za Muheza – Maramba – Kasera; Mbaramo, Misonzwe – Maramba – Kasera zimetengewa kwa jumla ya Shilingi milioni 183.25. Hofu yetu ni: Je, barabara hizi sitakamilika katika mwaka huu? Hofu yetu juu ya kukamilika kwa barabara hii inatokana na ukweli kwamba mwaka 2010 barabara hizi zilitengewa jumla ya Shilingi milioni 190 ili kukamilisha ujenzi wake Juni, 2010 jambo ambalo halikutekelezwa. Naomba kauli ya Serikali juu ya suala hili.

Mheshimiwa Spika, majaribio ya matengenezo ya barabara kwa kutumia teknolojia ya *TerraZyme* katika barabara ya Muheza - Amani yanaonyesha matokeo mazuri. Nashauri tuanze kutumia teknolojia hii hususan katika barabara zetu za vijijini kama ile ya Mbuyuni - Kasera ni kutokna na ukweli kuwa teknolojia hii imetumika kwa mafanikio katika nchi mbalimbali ikiwemo India.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. JOHN J. MNYIKA:** Mheshimiwa Spika, mkakati wa kuifungua nchi kupitia kuweka kipaumbele ujenzi wa miundombinu ikiwemo barabara ni wa msingi kwa kuwezesha Taifa kutumia vizuri raslimali kwa maendeleo ya uchumi wa Tanzania na mabadiliko ya maisha ya wananchi. Hata hivyo, ukilinganisha mtandao wa barabara nchini wenye jumla ya kilometa 86,472 huku za lami zikiwa kilometa 6,500 tu, ambayo ni chini ya asilimia 10 miaka 50 baada ya uhuru, kasi ni ndogo sana. Hivyo, kuna umuhimu wa Serikali kuongeza wigo wa mapato ya Serikali na kuleta bajeti ya nyongeza *(supplementary budget).* Ukiondoa tozo za mafuta ni lazima kuwe na mkakati maalum wa kuchukua sehemu ya mapato kutoka kwenye raslimali na maliasili kuwekeza katika barabara ili kuvifungua nchi mapema zaidi. Hii iambatane na kuweka mkazo kwenye barabara za vijijini ili kupunguza wimbi la watu wengi hususan vijana kuhamia mijini ikiwemo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa kupunguza foleni ya magari katika jiji la Dar es Salaam, bado Serikali haijaweka kipaumbele cha kutosha pamoja na kupoteza mapato, Shilingi bilioni nne kwa siku kuondokana na foleni. Ikumbukwe kuwa mradi huu ulipaswa kutekelezwa kwa ukamilifu toka mwaka 2009 kutokana na mpango mkakati wa kuboresha miundombinu ya Jiji. Aidha, kuna umuhimu wa kujenga njia za ziada barabara ya Morogoro kwenye kifungu 2005 kasma 4138 kiwango cha Shilingi bilioni tano ni kidogo sana. Matokeo yake kazi itakayoendelea pekee ni kukamilisha barabara ambazo zilipaswa kukamilishwa kwenye mwaka wa fedha 2010/2011.

Barabara nyingine zimewekewa fedha za matengenezo pekee. Ni muhimu kwa kuwa upembuzi yakinifu umeshafanyika, tathmini ya fidia ifanyike katika mwaka wa fedha 2011/2012 ili ujenzi uanze mapema kama nilivyoshauri kupitia Bodi ya Barabara na kuptia barua zangu kwa *TANROADS* pamoja na Wizara ya ZUjenzi. Kasma 4161 kuhusu ujenzi wa daraja ya juu *(fly –over)* kiasi cha Shilingi bilioni 20 ni kidogo ambacho kitahusisha ujenzi wa *flyover* Tazara pekee, ni muhimu fedha zikaongezwa ili ujenzi wa *fly over* ya Ubungo uweze kufanyika kutokana na umuhimu wa eneo hilo kwa biashara ya kimataifa ya usafirishaji wa mizigo tokea bandarini na pia kupunguzwa foleni kwa wananchi. Hata hivyo, ikiwa wabia wa maendeleo wako tayari, kipaumbele kiwe kwenye kujenga barabara za kuchuja foleni *(filter ring roads)* za ardhini kabla ya hewani kama zilivyotajwa kwenye kasma 4138.

Pia ili kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara, pawepo mamlaka moja ya kusimamia ujenzi na uendeshaji wa miundombinu ya Dar es Salaam. Mradi wa mabasi ya utawala *(DIARY)* ukamilishe kulipa fidia kwa kushughulikia malalamiko ya wananchi, na kuweka mfumo thabiti wa usafiri wa halaiki wa umma *(mass transit system)* kwa kutumia pia miundombinu ya kampuni ya *UDA* na Manispaa za Jiji la Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, aya ya 55 na 56 (ukurasa 30 na 31) ziongezwe, barabara za Mpiji Maoha Bunju (iliyotolewa ahadi bungeni 2007) na Kimara – Mkuranga – Bonyokwa na Segerea iliyotolewa ahadi na Rais Kikwete kujengwa kiwangto cha lami Mei, 2010. Aidha, kiungo cha fedha kwa barabara nyingi za Jimbo la Ubungo ukurasa 187, 188, 202, 203, 217 ni kidogo ukilinganisha na mahitaji na mchango wa Dar es Salaam katika mapato kutokana na tozo za mafuta na kodi nyingine zinazohudumia barabara. Kiambatisho 5 (c) ukurasa 178 iongezwe barabara ya Sam Nuyoma (hasa kujaa maji eneo la Mlimani *City* ambapo maji hujaa).

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ieleze hatua ilizochukua kupandisha hadhi orodha ya barabara ya Dar es Salaam tulizoomba pamoja na kuweka vigezo maalum ya kupandisha hadhi barabara za Dar es Salaam.

**MHE. AL-SHAYMAA J. KWEGYIR:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia kuhusu barabara ya Muheza – Amani, kuhusu majaribio ya kutumia lami nyepesi, kitaalamu inaitwa *Terra Zyme* mwezi Julai, 2010 – July, 2011 na Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Harrison Mwakyembe ameridhia Aprili, 2010. Naomba *TANROADS* watoe taarifa kuhusu barabara hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza lami hiyo nyepesi ikiwekwa hapatakuwa na matengenezo kwa wastani wa miaka minne. Zitaokoa fedha za matengenezo ya kila mara, ili ziweze kutengeneza barabara nyingine.

Mheshimiwa Spika, tutengeneze barabara moja kwa moja, kwa miaka saba kwa barabara zenye urefu wa kilometa 100 tupate jumla ya kilometa 700.

Mheshimiwa Spika, je, katika bajeti hii 2011/2012 tunatenga kilomita ngapi kwa kuweka lami nyepesi?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ROSWEETER KASIKILA:** Mheshimiwa Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na afya njema aliyonitunuku. Namshukuru Spika kwa nafasi hii ya kuchangia Wizara ya ujenzi ambayo mimi ni mwanakamati katika Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Ujenzi, Naibu wake, Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Ujenzi kwa taarifa nzuri waliyoiandaa, lakini kwa kazi nzuri ya ujenzi wa barabara nchini kote na hasa barabara ya kutoka Tunduma hadi Sumbawanga, Sumbawanga hadi Mpanda, Sumbawanga hadi Kasesya na Kasanga kupitia Matai.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa barabara hiyo, lakini naendelea kuomba barabara ambazo zipo chini ya Halmashauri zitazamwe na zihudumiwe na *TANROADS* kwani Halmashauri zetu ni masikini, hazina uwezo. Barabara hizo ni Kalambazite mpaka Ilemba, Laela – Mwimbi - Katazi - Mwazye mpaka Matai, Matai – Kasanga, Ntendo – Kate, Namanyere – Kirando, Kala – Ninde na Kitosi – Wampembe mpaka Kirongwe – Kabwe.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara hizi *(feeder roads)* zitakapojengwa zitakuwa ni ukombozi mkubwa kwa wajawazito na watoto. Akina mama wajawazito mara nyingi wanajifungulia njiani, wengine wanaponea chupuchupu, wengine wanajifungua watoto wafu na wazazi wengine wanafia njiani aidha kwa kutokwa damu nyingi sana, lakini watoto wachanga wanafariki kwa degedege linalotokana na kukawia kufika hospitali baada ya kupata rufaa kutoka Zahanati au Kituo cha Afya.

Mheshimiwa Spika, mipango mingi ya ujenzi wa barabara imepangwa, pesa nyingi zimepangwa kwa ajili ya barabara, lakini kazi hufanyika baada ya muda mfupi, barabara hufumka baada ya muda mfupi, barabara zinakuwa *sub-standard*.

Mheshimiwa Spika, barabara ni *Sub-standard* kwa sababu ya wizi wa vifaa kama nondo, mafuta, *cement* na kadhalika. Wizi huu umekithiri na unafanyika na wajenzi wakishirikiana na wenyeji wa mahali ambapo barabara inapita au madaraja yanajengwa.

Mheshimiwa Spika, natoa rai yangu kuwa Waziri wa Ujenzi pamoja na kuwa anagawa kazi kwa Makandarasi, awe anafanya ufuatiliaji wa karibu, lakini pia ushirikishwaji wa wananchi kwenye maeneo husika kwenye ulinzi (ulinzi shirikishi) ili malighafi zinazotumika kwenye ujenzi wa barabara na daraja husika zilindwe, zisiibiwe na hatimaye wakandarasi waweze kukabidhi barabara zenye ubora kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali kwa juhudi kubwa inayofanya ya kujenga barabara nchini. Nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa usimamizi mzuri. Naomba waendelee na moto huo huo kwa ujenzi wa utunzaji wa barabara zetu.

Naishauri Serikali iendelee kuvunja nyumba na *structures* zilizoko katika *reserve* za barabara. Ni haki wafichwe wale ambao wako kwenye eneo ambalo Serikali inataka kujenga barabara, lakini wengine wote walioko kwenye *reserve*, Serikali ivunje. Ni vyema wananchi wajifunze kufuata sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, liko tatizo la mizani nchini, kwa magari makubwa kama mabasi kuiibia Serikali. Mabasi haya yanazidisha uzito na wakifika katika mizani wanaomba abiria waliokaa nyuma wasogee mbele ili kupunguza uzito.

Mheshimiwa Spika, nilishuhudia wiki iliyopita, *bus* likitoka Dodoma kwenda Dar es Salaam. Wizi huu uko nchi nzima. Nashauri uwepo utaratibu mzuri wa kuzuia wizi huu katika mizani, Maofisa waingie pia katika magari haya. Abiria wengine wanaambiwa wachuchumae.

Mheshimiwa Spika, Mkoani Kilimanjaro kuna mahali kunaitwa Njia panda (Makutano ya barabara itokayo Dar es Salaam na iendayo Moshi na iendayo Holili). Hapa *Traffic* ya magari yanayopima mizigo ni kubwa na iko masaa 24. Iko mizani ya upande mmoja, ambayo magari yote yanazunguka kupima mzigo na kurudi walikotoka.

Mheshimiwa Spika, ni hatari sana kwa maisha ya wananchi, inawezekana ajali kubwa ikafanyika. Nashauri Serikali ijenge mizani nyingine upande wa kushoto ambao utatumiwa na magari yaingiayo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kupitia Wizara zake husika kujenga Kituo cha Polisi katika eneo lililotajwa hapo juu. *Traffic* ni kubwa, inawezekana mizani inakusanya fedha nyingi, na benki ya karibu itakuwa Moshi Mjini ambapo ni takribani ya kilometa 20 kutoka Njia panda.

Mheshimiwa Spika, iko barabara inayojengwa kwa kiwango cha lami kutoka Mkuu Rombo mpaka Marangu. Barabara hii imejengwa muda mrefu na ningeomba Serikali iangalie kiwango *(quality)* cha ujenzi ule. Sina hakika kama katika kilometa 261.9 zilizotengwa kujengwa Kilimanjaro ni pamoja na fedha ya kumalizia barabara hiyo. Ningeshauri Serikali ikamilishe barabara hii ili pia kusaidia wananchi wa Taifa hili kutangamana vizuri katika harakati za Soko la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, nashauri pia Idara ya Nyumba *(TBA)* itunze nyumba zake. Ipokee kodi ya pango, lakini pia ifanye *repair* nyumba zinapomaliza muda fulani. Kuacha tu wateja waishi katika nyumba bila *serious restructions* na matengenezo, itazifanya nyumba zichakae. Nashauri Serikali itunze nyumba zake na zikodishwe kwa gharama kwa kutegemea maeneo mfano, ziko *flats* ziko Masaki/*Oysterbay* zamani zilitumiwa na *UN* zilikuwa nzuri na safi, leo ni tofauti.

Mheshimiwa Spika, Wilayani Kasulu *UNHCR* walitoa fedha zaidi ya Shilingi milioni 160 za kujenga nyumba ya *DC* tangu mwaka 2006 (kwa sababu wakati wakimbizi wa Burundi wanaingia nchini, Serikali iligawa nyumba ile kwa *UNHCR* kutumika kama Ofisi). Fedha hii ililipwa kama pango la nyumba *UNHCR* wanayoitumia. *TBA* wamepokea fedha hiyo na nyumba ya *DC* haijajengwa na hata *TBA* Kigoma wakiulizwa wanasema ni *TBA* Makao Makuu.

Mheshimiwa Spika, nashauri Serikali ivalie njuga hili. *DC* Kasulu anahangaika katika Ma-*guest house* hana nyumba, ingawa *UNHCR* walitoa fedha.

Mheshimiwa Spika, foleni za Dar es Salaam zinamfanya mtu wa kawaida awe na mashaka kama Serikali inajali watu wake. Raia wanaamka saa kumi za usiku kwenda maofisini. Familia, wazazi hawajui watoto wao wamekwendaje shule na wala wamekula nini, kwa sababu muda wa kurudi kazini ni usiku na muda wa kwenda kazini ni usiku. Yote hayo ili kuwahi foleni. Yumkini *performance* ya utendaji kazi maofisini imepungua kwa sababu watu wanafika wamechoka. Foleni za Dar es Salaam hazina siku ya kazi wala siku ya mapumziko.

Mheshimiwa Spika, nina imani Serikali inaweza kuondoa kabisa/kupunguza foleni hizo. Naiomba Serikali itafute mbinu zote kuondoa foleni hizo.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara hii ya Dodoma – Babati umuhimu wake ni wa Kitaifa, na kwa kuwa barabara hii imepuuzwa kwa muda mrefu, naomba nipate ufafanuzi wa kina toka kwa Waziri, ni kwanini/au kuna ugumu gani kwa Serikali kutenga fedha za kutosha kukamilisha barabara hii badala ya kutenga fedha nusu nusu? Mfano, kusema Serikali imetenga fedha toka Mayamaya na Bonga wakati sehemu kubwa ya barabara hii imeachwa Shilingi bilioni tatu kwa kilomita zaidi ya 150 ni za changarawe au lami? Hivi kwanini Serikali isikamilishe ujenzi wa barabara hii? Mfano, badala ya viongozi wa Serikali wanakwenda Arusha kupitia Dar es Salaam ndiyo wapande ndege. Kwanini isiweke lami barabara hii ambayo kufika mpaka Arusha ni kama masaa matano tu badala ya kutumia siku nzima kupitia Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, naishauri tu Serikali ichukulie hii barabara kwa umuhimu wa pekee kuokoa gharama nyingi zinazopotea za safari katika mafuta na muda.

Mheshimiwa Spika, Wizara ifuatilie fidia zinazolipwa wananchi ambao nyumba zao zimebomolewa kwa ajili ya barabara, wengi wamepunjwa fidia zao zinachakachuliwa mfano *along the road from Minjigu to Babati Singida*, wananchi wengi wanalalamika. Nawaomba Mawaziri wawili mtembelee maeneo hayo na mkutane na wananchi moja kwa moja na siyo kuongea na viongozi watawadanganya, kaeni chini na wananchi wenyewe mjionee hayo mapungufu.

**MHE. MWIGULU L. N. MADELU:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kukupongeza Mheshimiwa Waziri Dkt. John Magufuli na Naibu Waziri wako Dkt. Harrison Mwakyembe kwa umakini na utendaji wenu wa kazi. Kazi zenu tunaziona na Watanzania wenye mapenzi mema wanaiona.

Mheshimiwa Spika, naipongeza bajeti ya Serikali kwa bajeti nzuri yenye kutia matumaini na iliyoandaliwa kitaalamu. Mfano, bajeti ya mwaka 2010/2011, Shilingi bilioni 275.9 za ndani Shilingi bilioni 246 zilitoka hadi kufikia Mei. Kwa mwaka wa fedha huu tunashukuru kuwa Shilingi bilioni 245.4 jumla ya Shilingi bilioni 221.6 kuwekwa kwenye mfuko wa barabara.

Mheshimiwa Spika, Wizara ina utaratibu mzuri, iendelee na tabia ya kufuatilia kwa karibu matumizi ya fedha za mfuko wa barabara zinazopelekwa Mkoani na Wilayani na kuwabana wadau wote wanaohusika na ujenzi ili ujenzi ulingane na thamani ya pesa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili Serikali ilifanye kwa uangalifu zoezi la bomoa bomoa hususan wale ambao barabara imewafuata, malipo yawiane na makazi wanayohamishwa.

Kuna umuhimu wa wakazi kupewa semina na kuelimishwa ili wasiwe wanapatwa na mshituko wanapoona X kwenye makazi yao. Ni vyema vilevile kufanya maandalizi ya kubomoa bomoa kabla ya kuweka alama za X.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara iangalie kwa jicho la huruma barabara ya Kiomboi – Kisiriri kwenda Kidavu na Tyulia kwa kuwa zinapita milima hatari sana. Zitengenezwe kwa kiwango ambacho magari ya abiria yatapita bila matatizo. Naomba pia barabara ya kutokea Shelui kwenda Sekenke hadi Tyulia Kidavu na ile ya kwenda Shelui II.

Nitashukuru sana pia kama barabara ya kutokea Shelui Mtoa – Mtekente- Urughu hadi Kibaya. Hii itasaidia kukuza uchumi.

Bila kusahau naomba daraja la Mbulu lijengwe ili litoe huduma Kata ya Mbulu, Igurubii, Mwamashimba, Kining'inila, Itunduru, Vunungi na Igunga Mjini.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha fedha zinaleta tija, naomba Wizara ni vyema sana zikatumika kujenga barabara kufuata vipaumbele ili fedha ziweze kuwa na *Impact.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Viongozi wote wa Taasisi zilizopo chini ya Wizara kwa kazi nzuri na hotuba ya Kisayansi yenye takwimu nzuri na nyepesi kufuatilia na kuelewa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo hayo, naomba maelezo na kutoa mapendekezo katika maeneo yafuatayo:-

(a) Mradi wa *PMMR – TANGA EAST* kwa Wilaya ya Muheza unagusa barabara mbili. Boza (Pangani) – Mkuzi – Muheza na Muheza – Amani. Kitabu cha Hotuba ya Waziri ukurasa wa 90 unataja tu kilomita 1092 ndani ya mradi huo bila kuainisha barabara na mpangilio wa fedha zilizotengwa. Tunaomba maelezo.

(b) Wakati nilipohoji utendaji wa Mkandarasi aliyepewa jukumu la barabara za *Tanga East,* Wizara iliridhia kwamba *Y. N. Investment* na *Lucky Contractors* (Wakandarasi) wameshindwa kutekeleza wajibu wao na ndani ya miaka miwili utendaji wake hauridhishi. Katika Semina ya Wabunge Mkoa wa Tanga iliyoendeshwa na Mwekezaji *COWI* kiwango cha utendaji wa Mkandarasi huyo kwa barabara hiyo ilikuwa ni *0% (Zero)* lakini alishalipwa fedha zaidi ya Sh. 800,000,000/=. Baraza la Maendeleo ya Mkoa wa Tanga *(RCC)* mbele ya Mkuu wa Mkoa walimkataa Mkandarasi huyo na hata msimamizi mshauri *Consultant* hakuwa na imani naye. Je, kwa udhaifu huo anaendelea na kazi hadi lini? Hata sasa August 1, 2011 licha ya kwenda eneo la kazi bado utendaji haujaridhisha.

(c) Wakandarasi wote wawili *Y. N. Investment* na *Lucky Contractors* hawana viwango vya ukandarasi daraja la kwanza wala la pili: Je, *Registrar* wa Bodi ya Wakandarasi anaweza kutuelezea viwango vyao na: Je, chini ya Mpango wa *PMMR* Sheria imewaruhusu kupandishwa daraja kwa kuwa Wakandarasi hao wameungana *(Joint Venture)*? Je, Bodi hiyo imeangalia usajili wa Kampuni hizo mbili ili kuona kama ni kweli kwamba wana hisa wa kampuni hizo mbili wanafanana na hivyo kutoa shaka kuwa chini ya mmiliki mmoja kama walivyoingia katika tenda ya ujenzi wa barabara za Raskazoni Tanga chini ya Jiji mwaka 2008/2009/2010?

Mheshimiwa Spika, hii ni barabara muhimu kwa wakulima wakubwa wa chai, utalii na kuchangia uchumi wa Taifa. Lakini inapita katika maeneo magumu sana ya milima, mabonde na maporomoko ya hatari kwa maisha ya watu, bidhaa, watalii na wananchi. Barabara hii imetolewa ahadi na Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete mwaka 2010 wakati wa Kampeni kujengwa kwa kiwango cha lami. Je, mpango wa *PMMR* ndiyo mpito wa kuelekea kutekelezwa kwa ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais? Nini mkakati rasmi wa kutekelezwa kwa ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais kabla ya mwaka 2012/2015?

Mheshimiwa Spika, *TANROADS* imeshapokea kwa kupandishwa barabara kadhaa Mikoa mbalimbali. Hii ina maana ya kuendelea kuongeza ukubwa wa mtandao wa barabara za Taifa na za Mkoa sasa kufikia kilomita 33,000 wakati Wilaya ikiwa na kilomita 52,000 (wastani). Ili kuwezesha *TANROADS* kumudu majukumu hayo ya ziada lazima *TANROADS* iendelezwe na kuimarishwa kama ifuatavyo:-

(a) Kuongeza wataalamu na uwezo wa wataalamu;

(b) Kuongeza vitendea kazi vya kisasa na vya kutosheleza;

(c) Kuongeza fedha kuwezesha *TANROADS* kumudu utekelezaji wa majukumu na miradi inayoendelea kuongezwa kwao; na

(d) Kuongeza na kuboresha vituo vya kazi ili kuwezesha *TANROADS* kusimamia kazi ngumu ya kupunguza msongamano wa magari Jiji la Dar es Salaam na Mwanza kwa kuanzia. *TANROADS* iwe na ofisi maalum za kusimamia mpango huo katika Wilaya za Ilala, Temeke, Kinondoni na Mwanza. Halmashauri za Jiji Ilala, Temeke na Kinondoni hazitamudu utekelezaji wa mpango huo maalum kutokana na mchanganyiko mkubwa wa majukumu yao na mahitaji ya fedha.

Mheshimiwa Spika, mradi wa majaribio ya matengenezo ya barabara kwa kutumia *Terra Zyme*, shabaha ya majaribio hayo ni kupunguza gharama za matengenezo ya barabara za udongo/changarawe ili kuwezesha kuongeza mtandao wa barabara kwa kasi kubwa zaidi. Ni eneo la urefu wa kilometa nne limetengenezwa katika Wilaya ya Muheza Barabara ya Muheza – Amani mwaka 2010 na pia upo mpango unaofanana na huo katika Wilaya ya Same.

Wahisani waliojitolea kufanya majaribio hayo walitoa muda wa mwaka mmoja kuwezesha Tanzania kufanya tathmini ya kazi iliyofanyika na kuona kama imekidhi haja na kudumu kwa mwaka mmoja wa awali 2010 – 2011. Baada ya ujenzi huo kwa gharama za wahisani chini ya *TANROADS* ufuatiliaji sasa umekamilika na jibu lazima lipatikane.

Mheshimiwa Spika, nilitoa nafasi wakati wa ziara ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi alipotembelea barabara ya Muheza – Amani mwezi Aprili, 2011 aone na kushuhudia eneo hilo la barabara iliyojengwa kwa *Terra Zyme* na kuongea na wananchi wa eneo husika na akadhihirishiwa kuridhika kwa wananchi hao na pia kuona tofauti ya eneo hilo la kilometa nne kulinganisha na eneo la barabara iliyojengwa kwa mfumo wetu wa kawaida lilikuwa limeharibika na linafanyiwa ukarabati upya na kwa gharama kubwa. Barabara ilipojengwa, Sementi haikutumika. Barabara ikishajengwa inadumu kwa wastani wa miaka mitatu. Hivyo, fedha Taifa inazookoa kwa miaka mitatu ni nyingi na ndiyo mchango wa hazina yetu ya kuongeza mtandao wa barabara nchini.

Mheshimiwa Spika, makadirio ya fedha zinazookolewa ni:-

(i) TShs.5,000,000 kwa Km 01 kwa miaka 3 =
TShs.5,000,000 x 1 x 3 = TShs.15,000,000/=

(ii) Je, tukitenga 600 Km?
= 5,000,000 x 600 x 3 = TSh. 9,000,000,000/=

Je, wataalamu wa *TANROADS* wamefanya makadirio na tathmini ya faida ya matumizi ya teknolojia hii na athari za mazingira kama zipo kwa kiwango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MUSTAPHA B. AKUNAAY:** Mheshimiwa Spika, mimi ni mdau mkubwa wa Sekta ya Barabara kwa sababu ninahusika na wakulima, wafugaji, watalii aidha, mimi ni Mjumbe wa Mfuko wa Barabara. Kwa misingi hiyo, naomba nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa vile kati ya mtandao wa kilometa 86,472 ni kilometa 6320 tu (7.6%) ndiyo lami hii, ina maana kuwa fedha nyingi inatumika kwa matengenezo ya mara kwa mara katika barabara za udongo ambayo mara baada ya kutengenezwa huharibiwa na mvua.

Mheshimiwa Spika, nashauri kwamba kwa vile barabara hizi ndizo zinatumika katika kusafirisha mazao ya shamba na mifugo, Serikali itafute mkopo ili barabara zote nchini ziwekwe lami.

Mheshimiwa Spika, kwa vile Serikali inatumia fedha nyingi katika kuboresha barabara, kazi mojawapo ya *Police Traffic* iwe kulinda barabara. Aidha, jamii ihamasishwe kulinda barabara.

Mheshimiwa Spika, kwa vile *Road humps* nyingi zimejengwa bila utaalamu wa *"Engineers"* Serikali iamue kwamba *TANROADS* tu ndiyo pekee itakuwa inaweka *Road Humps.*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba barabara nyingi zinajengwa chini ya kiwango lakini vyeti vinatolewa kwamba kazi ni sawa. Nashauri kwamba kazi yoyote isilipwe bila kuhakikishwa na *Road Consultants* na *Employer* ili kupata *"Value of money"*

Mheshimiwa Spika, siku nyingi tuliongea barabara inayounganisha Katesh – Haydom – Elamillay – Bashay – Mbulu na Babati – Kuta - Mbulu. Tunaomba Mheshimiwa Waziri wakati wa

kujumuisha hoja, atoe maelezo, imekuwaje katika bajeti hii amesahau barabara hii au ni makosa ya uchapishaji?

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha, nashauri kwa kuzingatia mahitaji makubwa ya ukarabati wa barabara, Mfuko wa Barabara *(RF)* uongozewe bajeti angalau trillioni mbili.

Mheshimiwa Spika, nashukuru.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa barabara ni muhimu sana katika kuinua uchumi wa Taifa letu, Tanzania, tunajua Watanzania wote kuwa Wizara hii ya ujenzi imefanya kazi kubwa katika ujenzi wa barabara, hongera sana Rais wetu pamoja na Waziri na Naibu Waziri kwa mipango mizuri ya ujenzi wa barabara katika nchi yetu. Ukweli barabara za Mikoani na Wilayani ni nzuri sana ingawa kuna changamoto ambazo zinaweza kutatuliwa.

Mheshimiwa Spika, katika Jimbo la Mufindi Kusini kuna barabara inayotoka Nyololo – Igowole – Kibao – Mtwango – Kiwanda cha Mgololo. Ni barabara muhimu sana katika kuinua uchumi wa Taifa letu. Kuna viwanda ambavyo vinachangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa. Wananchi walio wengi wapo katika barabara hii, tatizo kubwa la barabara hii bado haijajengwa kwa kiwango cha lami. Naiomba Serikali kuingiza kwenye mpango wa kujenga kiwango cha lami barabara ya Nyololo – Igowole – Kibao – Mtwango – hadi Kiwanda cha Karatasi Mgololo.

Katika vikao vyetu vya Mkoa wa Iringa vya *Road Board,* tumepitisha na kukubaliana kwa sauti moja kuwa barabara hii ni muhimu kwa uchumi wa Taifa letu. Kuna Kiwanda cha Chai, Kiwanda cha Mbao, Kiwanda cha Upandaji miti, Mgololo, kuna kilimo cha mpunga cha umwagiliaji, pia itakuwa msaada mkubwa sana kwa wananchi wa Wilaya ya Mufindi kwa ujumla, gharama kubwa sana inatumika katika ukarabati wa barabara hii. Mimi sijaelewa kwanini isijengwe kwa kiwango la lami? Ni kama kilometa 94 tu.

Mheshimiwa Spika, nitashukuru sana kama ombi langu litakubaliwa. Ahsante.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza naipongeza sana Wizara hii kwa mchanganuo mzuri kwenye ujenzi wa barabara na ujenzi wa nyumba. Katika Wizara kero kubwa ni Mameneja wa Mkoa, naomba wapewe ushirikiano wa kuachiwa mipango ya barabara kwani mara nyingi wanakuwa hawana maamuzi wakidai kila kitu kinafanyika Wizarani. Hii ni kosa kubwa. Hawa Mameneja wapewe madaraka ya kusimamia kazi hii. Hii ni kwa sababu wanapewa Makandarasi ambao hawana uwezo wa kuwafukuza, inashindikana kuwafukuza mpaka itoke Wizarani. Huu siyo uungwana.

Mheshimiwa Spika, kuharibika kwa barabara ni kwa sababu hakuna reli. Naomba usafiri wa reli ufufuliwe, kwani kuwepo magari makubwa kwenye barabara huharibu barabara kwa sababu ya uzito – matuta ya barabarani hayajengwi kwa kiwango kinachohitajika. Barabara ya kutoka Segera kupitia Korogwe hadi Mkomazi tungeomba Serikali ianze mara moja kutengenezwa kwani magari mengi huharibika kwa ajili ya mashimo.

Mheshimiwa Spika, naomba mizani ya Mketa ifutwe kwani imejaa rushwa mno kiasi toka wameanza kukamata magari sijawahi kuona mizigo iliyozidi imeshushwa. Kama siyo rushwa ni nini? Kumekuwepo na shida kwenye nyumba za Serikali, wanaokaa, wafanyakazi waki-*retire* nyumba hawarudishi. Ni kwanini wakati nyumba hizo siyo zao, ni za Serikali?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono Bajeti hii ambayo ni safi sana kwa asilimia mia moja.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuwashukuru Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu, Wadau wa barabara pamoja na Wafadhili wote wa barabara zetu kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali yangu ya CCM kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa ilani yake katika sekta ya barabara.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mambo mazuri yalifanywa na Serikali, lakini kuna changamoto nyingi zinazoikabili Wizara hiyo zikiwemo zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, ufinyu wa bajeti kwa barabara za Dar es Salaam fungu lililowekwa na Serikali kwa lengo la kupunguza msongamano, haitawezekana. Hivyo naiomba Serikali iangalie kwa jicho la huruma Dar es Salaam. Hali ya msongamano inaendelea kuwa mbaya na bajeti hii naona tatizo litaendelea kuwa palepale.

Mheshimiwa Spika, napenda niishukuru Serikali yangu kwa kuendeleza barabara zilizo pembezoni mwa mji ambazo ni zile za Mbezi – Maramba 2 – Kinyerezi – Majumba Sita, *Jet – Devis Corner,* lakini pia kwa kuona umuhimu wa kujengwa kwa daraja la Kigamboni. Naomba Serikali yangu ujenzi wa daraja sasa uanze, kwani imekuwa ni historia tu.

Mheshimiwa Spika, naomba niingie katika suala zima la mlundikano wa magari katika eneo la Rangi Tatu Mbagala na Ukonga Majumba Sita na Gongolamboto Mwisho. Miji hii inakua kwa haraka sana, hivyo tunavyopanga mipango yetu tuangalie kwa upana mkubwa zaidi. Nasema hivyo kwa sababu pale Majumba Sita, Kituo cha Mabasi kilichopo ni kidogo sana ukilinganisha na idadi kubwa ya mabasi yanayosimama pale. Hali hiyo imejitokeza tena katika Stendi ya Mabasi ya Gongolamboto Mwisho.

Mheshimiwa Spika, sasa nachangia kuhusu ubora na viwango vya barabara. Kwa kweli barabara ya Kilwa haikufikia viwango kabisa. Je, Serikali ina mikakati gani na jambo hilo, lakini pia katika suala zima la fidia kwa wakazi wa barabara ya Kilwa? Ni tatizo.

Mheshimiwa Spika, kwa mawazo yangu na walio wengi ni kwamba mradi wowote unapokuja sehemu ya wananchi ni muhimu wahusishwe na waeleze umuhimu wa mradi na waukubali. Lakini kwa wananchi wa barabara ya Kilwa hawakulipwa fidia zao, basi hata mradi ule umeanguka imeshindikana kufanikiwa.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa Serikali yangu sikivu ya Chama cha Mapinduzi iwaridhishe kwa kuwaangalia kwa jicho la huruma wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa maslahi ya Chama changu na Serikali yangu iliyo makini.

**MHE. JASSON RWEIKIZA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Wizara ya Ujenzi kwa kazi kubwa inayofanyika katika kuboresha barabara, madaraja, vivuko na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, naomba kusema kuwa ile barabara ya Bukoba hadi Rubafu (km 42) imesahaulika. Mchakato ulianza mwaka 2007. Mkataba ulisainiwa mwaka 2009, lakini hadi leo hakuna hata km 1 iliyojengwa. Barabara hii inajumuisha pia kivuko ili Tanzania na Uganda ziwe na mawasiliano mazuri. Fursa nyingi sana zitafunguliwa iwapo barabara hii itaboreshwa na kivuko kuwekwa na kuanza kazi. Watanzania wataweza kusafiri kwa urahisi zaidi kuelekea Uganda na kupeleka bidhaa mbalimbali za kibiashara kama maharage, ndizi, mbogamboga na kadhalika.

Pia barabara na kivuko chake ni muhimu kwa usalama. Mwaka 1978 Idd Amini alibomoa daraja la Kagera tukakwama sana. Tukiwa na barabara mbadala, tunakuwa salama zaidi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2009 Makamu wa Rais alitembelea eneo la barabara hii na akasisitiza kuwa barabara hii itajengwa haraka, lakini hadi leo hakuna chochote.

Mheshimiwa Spika, naomba barabara hii iingizwe katika bajeti na kazi ianze mara moja.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kutoa mchango wangu kuhusu hotuba ya Waziri wa Ujenzi - Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli aliyewasilisha Bungeni Mpango wa Maendeleo na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2011/2012.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu wananchi wanaoishi Kigamboni, Dar es Salaam wamepata taabu na matatizo makubwa juu ya usafiri salama. Ajali kadhaa zimetokea na baadhi ya wananchi wamepoteza maisha yao kwa kuzama baharini.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi tumesikia katika vyombo vya habari kwamba kivuko cha Kigamboni kitajengwa katika ubora wa ngazi ya kimataifa. Katika kitabu cha hotuba ya Waziri ukurasa wa 120, kasma ya 4167, fedha ya ndani iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa daraja la Kigamboni ni Shilingi milioni 316.60 na ujenzi kufanywa na Serikali/*NSSF*. Sina uhakika kama kiasi hicho cha fedha kitatosha kujenga kivuko chenye ubora wa kimataifa kama inavyosemekana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ni lini kivuko cha Kigamboni kitaanza kujengwa?

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, katika hotuba yake juu ya miradi ya kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, ukurasa wa 29, usanifu wa *Flyover* ya Tazara umeanza Juni, 2011 kwa ufadhili wa *JICA*. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imesema kwamba kwa upande wa ujenzi wa *Flyover* ya Ubungo, Serikali imepeleka maombi kwa Serikali ya Japan kupitia *JICA* ili kusaidia ujenzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwuliza Waziri wa Ujenzi, ni kiasi gani cha fedha kimeombwa ili kukamilisha ujenzi huo? Pia naomba kufahamu, ni kwanini hakuna kiasi chochote cha fedha kilichotengwa kujenga *Flyover* nne zilizoonyeshwa katika Kasma ya 4161, ukurasa 119 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kwamba zitajengwa Dar es Salaam na zitajengwa katika maeneo yapi?

Mheshimiwa Spika, ni vyema wananchi wakapata taarifa sahihi ya kwamba kazi inaanza lini ili wapate matumaini kwamba tatizo la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam linafanyiwa kazi na litatatuliwa lini?

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. FATUMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, hongera kwa bajeti nzuri inayounganisha wananchi. Nampa hongera Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya nchini. Safi sana. Hongera kwa *Manager* Maico Kulaya wa Lindi kwa kuendeleza barabara za Lindi kwa lami hasa kuanzia Masaninga hadi Lindi, ameweza kuendeleza mtandao wote wa barabara Mkoani. Shukrani sana.

Mheshimiwa Spika, hoja yangu ni kwamba, Kivuko kutoka Lindi Mjini kwenda katika Vijiji vya Kitunda – Lindi ni kivuko muhimu sana, kwani upande wa pili ndiyo upande tunaopata mboga zote na matunda. Watu wengi wanaishi Kitunda. Watu wanavuka kwa taabu sana kuja Lindi Mjini kiasi kwamba, watu wanapoteza maisha kutokana na vyombo vya usafiri wanavyotumia huwa hafifu. Tunaomba kivuko tafadhali.

Mheshimiwa Spika, mwisho ninaunga mkono kwa asilimia mia moja.

**MHE. ASHA MUHAMED OMAR:** Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu 2011/12 Wizara ya Ujenzi imepanga kusajili bodi ya Wakandarasi kwa ajili ya kukagua miradi ya ujenzi hivyo namuomba Waziri wakati wa kufanya zoezi hilo la kusajili hao makandarasi wa ujenzi kutafuta makandarasi ambao wana ubora na wanaokubali, wawezao fanya kitu na kumalizika kwa wakati anaopangiwa kukamilika wakati wanapofunga mikataba na Wizara na Serikali.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali pamoja na Wizara ya Ujenzi izidi kuendelea na kusimamia utekelezaji wa ahadi kisheria kwa wabunifu hao wakati wa kufanya mchakato wa

kutafuta wabunifu hao wa ujenzi ambao ndiyo wanaoangaliwa wakati wanapokuwa wakifanya shughuli hiyo ili kuweza kuondokana na matatizo ambayo yanaweza kutokea wakati wa kazi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka huu wa fedha wa 2011/2012 Serikali pamoja na Wizara imeandaa kuendeleza ujenzi wa jengo jipya la madarasa ya ufundi stadi, hivyo naiomba Wizara ya Ujenzi ikiboreshe Chuo hicho ili kuweza kutoa mafundi wazuri watakaoiletea faida nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imetenga kiasi cha fedha kwa ajili ya kuvifanyia ukarabati vivuko ambavyo ni vibovu, havitumiki pamoja na kuvifanyia ukarabati mapema ambayo hayafanyi tena kazi. Hivyo naiomba Wizara ya Ujenzi kuchukua juhudi ili suala hili liweze kufanyika mara moja ili wananchi waweze kuvitumia vitu hivi na kuondokana na usumbufu ambao umekuwa ni wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Ujenzi pamoja na Serikali kuyapima uzito magari barabarani, kwani kuna umuhimu mkubwa wa kufanya hivyo na upimaji huo ufanyike kwa njia ya teknolojia ambayo itakuwa inatoka Makao Makuu ya Ofisi ya *TANROADS* jambo ambalo litaweza kupunguza na kudhibiti vitendo vya wizi wakati wa kufanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Spika, tatizo la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, limekuwa ni tatizo kubwa mno jambo ambalo linafanya watu wengi wanapokuwa wanakwenda kazini na kurudi wananchi hao huchelewa. Hivyo, naiomba Wizara hii kuliangalia tatizo hili na kulipa uzito na kulipatia ufumbuzi unaofaa.

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Spika, napenda awali ya yote kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete – Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jitihada zake za kujenga barabara nyingi za lami hapa nchini. Shukrani za dhati nazitoa kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli - Waziri wa Ujenzi kwa jitihada na juhudi anazoonyesha katika kutimiza wajibu wake kama kiongozi katika Taifa hili. Shukrani nyingine nazitoa kwa Mheshimiwa Dkt. Harrison G. Mwakyembe - Naibu Waziri wa Ujenzi kwa uongozi wake makini. Pia shukrani nyingine ziwafikie Katibu wa Wizara pamoja na wataalamu wa Wizara kwa juhudi zao za pamoja za kuitumikia nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utagawanyika katika baadhi ya vipengele vifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa jitihada hizo za upanuzi wa barabara za Mitaa ya Jiji la Dar es Salaam na Vitongoji vyake. Kwa hakika barabara zinazopanuliwa kwa kiasi kikubwa zimesaidia kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam. Pia vibarabara vinavyoongezwa katika baadhi ya maeneo katika Jiji la Dar es Salaam kama vile Tabata Dampo – Kigogo - Ubungo Maziwa, Ubungo Maziwa – Mabibo – Kigogo, Kimara Baruti – Msewe – Changanyikeni na kadhalika vitasaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la foleni. Lakini hata hivyo bado tatizo la msongamano katika Jiji la Dar es Salaam ni kubwa na linakatisha tamaa.

Naishauri Wizara ya Ujenzi badala ya kuendelea kung'ang'ania kujenga majengo ya Serikali katikati ya Jiji la Dar es Salaam ihakikishe kuwa majengo yote mapya ya Serikali yanayojengwa Jijini Dar es Salaam yajengwe nje kidogo ya Posta/katikati ya Jiji. Pia ihakikishe kuwa baadhi ya Wizara na taasisi mbalimbali zinahamishwa toka *City Centre* ili zihamie kwenye majengo hayo mapya. Hii itasaidia kwa kiasi fulani kupunguza msongamano wa magari katika *City Centre* ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, jambo la mabasi yaendayo kasi limekuwa la kufikirika zaidi kuliko uhalisia. Hata hivyo, nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa jitihada za mwanzo ambazo zimeanza kuonekana. Ikiwa mfadhili amepatikana ambaye ni Benki ya Dunia, naishauri Wizara pamoja na Serikali ihakikishe kuwa inafanya kila iwezalo kufanikisha zoezi hili. Mradi huu ukikamilika ni dhahiri kuwa utapunguza tatizo la usafiri katika Jiji la Dar es Salaam na hali kadhalika utapunguza sana tatizo la foleni katika Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zote zinazofanywa na Wizara, chini ya Mheshimiwa Dkt. Magufuli na Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe bado kumejionyesha dhahiri kwamba kuna udhaifu mkubwa juu ya mgawanyo wa railimali usiowiana. Kuna baadhi ya Mikoa kama vile Kilimanjaro, Morogoro, Pwani, Mbeya na kadhalika imepewa miradi ya barabara nyingi za lami unapolinganisha na Mikoa mingine kama vile Mara, hususan katika Wilaya ya Tarime ambayo haina hata barabara moja ya lami licha ya kuwa na msimu wa mvua mara mbili kwa mwaka ambao hupelekea barabara karibu zote kuharibika na hivyo kuleta kero ya usafiri kwa wananchi wa Tarime. Ushauri wangu kwa Wizara na Serikali ni kwamba iangalie kwa makini suala la mgawanyo wa raslimali katika nchi hii uwiane. Serikali isipendeleze eneo fulani na kusahau eneo fulani. Hali hii itasaidia kwa kiasi fulani kupunguza malalamiko yasiyo ya lazima katika suala hili la maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali ihakikishe kuwa inalipa fidia halali kwa wananchi wanaobomolewa nyumba zao au ambao viwanja vyao huathiriwa na ujenzi wa barabara. Napendekeza kuwa kabla ya kubomoa nyumba hizo ni vizuri wananchi hao wakapewa fidia zao halali. Mathalan katika Wilaya ya Tarime katika Mji mdogo wa Sirari, naishauri Serikali/Wizara husika kutoa fidia halali kwa waliobomolewa nyumba zao mwanzoni mwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, nasikitika sana kuielezea historia ya Wilaya ya Tarime mbele ya Bunge lako Tukufu kuwa ni Wilaya ya zamani sana katika nchi hii ya Tanzania, lakini ni wilaya iliyosahaulika sana kimaendeleo. Ni Wilaya ambayo inazalisha kila aina ya mazao, lakini haina miundombinu imara. Wakulima wanataabika, wafanyakazi wanataabika, wanafunzi wanataabika, hata wafanyabiashara wanataabika! Wanataabika kwa kukosa huduma ya barabara. Hali ya hewa ya Tarime hususan mvua ya misimu miwili kwa mwaka husababisha usafiri kuwa mgumu sana Wilayani Tarime. Chonde chonde, namwomba Mheshimiwa Magufuli/Mheshimiwa Mwakyembe na watendaji wote wa Wizara kuhakikisha kuwa angalau kutokana na hali halisi ya Tarime wanaziwekea lami barabra mbili za *Nyamwaga Road* – Mto Mara inayopitia Mogabiri, Nyamwigura, Rozana, Kemakorere, Nyarero, Nyamwaga, Nyangoto, Kerende hadi Mto Mara. Hii barabara iko chini ya *TANROADS*. Hii barabara ni muhimu sana kwa uchumi wa Taifa/Wilaya.

Barabara ya pili ni ile *Security Road* inayoanzia Rorya – Susun – Kubiterere – Sirari – Gwitiryo-Nyabisaga – Borega – Ganyange – Kimusi – Nyantira – Muriba – Kobori – Itiryo – Nyamombara – Mangucha hadi Kegonga. Hii barabara iko mpakani mwa Kenya na Tanzania. Upande wa Kenya una lami hadi vijijini. Upande wa Tanzania una matope ambayo husababisha magari kukwama pindi mvua inyeshapo. Binafsi naamini kuwa tukiamua tunaweza. Sasa tuamue.

Mheshimiwa Spika, naiomba vile vile Wizara itusaidie kupandisha barabara ya Komaswa – Manga – Kibasuka – Nyamongo yenye urefu takribani Kilometa 40 iwe chini ya *TANROADS* kwani Halmashauri ya Wilaya ya Tarime haina uwezo wa kuihudumia. Hali kadhalika barabara ya Mangucha – Masanga – Masurura – Gibaso – Kirende yenye urefu takribani Kilometa 30 na yenyewe iwe chini ya *TANROADS*. Mwisho, barabara ya Nyamwaga – Keisangura – Tagare – Muriba yenye umbali kwa takribani Kilometa 10 iwe chini ya *TANROADS*. Hali hii kwa kiasi kikubwa itasaidia kupunguza tatizo la usafiri katika Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Spika, msisitizo nauweka kwamba naomba barabara mbili ziwekewe lami na Barabara tatu zipandishwe hadhi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto nyingi tulizonazo Wilayani Tarime, pia kuna tatizo la madaraja mawili ambayo tangu enzi na enzi yamekuwa kero kubwa sana hapa Wilayani. Kusema ukweli Halmashauri ya Wilaya ya Tarime haina uwezo wa kuyajenga madaraja hayo. Hivyo, naishauri Wizara husika iangalie kwa jicho la huruma tatizo hili na kulitafutia ufumbuzi haraka iwezekanavyo. Madaraja hayo ni yale ya Daraja la *Kyoruba* (Kata ya Pemba) na lile la Daraja la Mto Mori (Kata ya Nyatondo linaunganisha Wilaya ya Tarime na Wilaya ya Rorya). Madaraja haya yakijengwa yatasaidia kuimarisha uchumi wa wananchi wa maeneo husika na hivyo kuharakisha suala la maendeleo ya mtu binafsi, familia na hata Taifa zima.

Mheshimiwa Spika, naiomba Wizara ya Ujenzi ijenge nyumba za watumishi wa Serikali Wilayani Tarime kwani mazingira ya Tarime yanawafanya watumishi wengi wa Serikali kukataa kwenda kufanya kazi Tarime kwa visingizio kuwa hakuna amani. Hali hii imesababisha Wilaya kukosa watumishi wa kutosha na hivyo kukwamisha ufanisi bora wa huduma za jamii. Naiomba Serikali ilifikirie suala hili kwa jicho la uyakinifu. Naamini tukiamua tutaweza. Sasa tuamue.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nasisitiza Tarime ni Wilaya ya zamani sana katika nchi yetu ya Tanzania. Ni aibu kwa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi kuisahau Wilaya ya Tarime. Namwomba Mheshimiwa Magufuli pamoja na Mheshimiwa Mwakyembe waisaidie Tarime hasa waipatie barabara za lami angalau mbili tu pamoja na hayo madaraja mawili sugu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara ya Msana Bukumi kwa kiwango cha lami, ukizingatia ni barabara muhimu ya kihistoria, ambayo Baba wa Taifa alikuwa akiitumia katika harakati za kutafuta uhuru wa nchi yetu? Lakini barabara hiyo ni muhimu kwa ajili ya kuunganisha Wilaya nyingine. Hivyo pia kujengwa kwa barabara hiyo itasaidia wananchi wa Mkoa wa Mara kushiriki vyema katika kuchangia pato la Taifa kupitia zao la Samaki, pia kwa wananchi wa Mkoa wa Mara kuweza kuwasiliana na Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika hotuba ya Waziri imeeleza kuwa barabara ya Makutano Butiama, Nyamswa, Msama na Loliondo ipo kwenye upembuzi yakinifu: Je, Serikali inatoa tamko gani kwa ajili ya kutenga fedha katika mwaka ujao wa fedha ili ujenzi wa barabara hiyo uanze?

**MHE. KOMBO K. KOMBO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu Muumba mbingu na ardhi pamoja na vilivyomo katika mbingu na ardhi kunifikisha katika mwezi huu wa Ramadhani hali nikiwa naweza kuvuta pumzi kwa rehema zake, uweza wake na vile vile baraka za Mtume wake kipenzi chake na mwombezi wa *Ummat Muhammad (S.A.W).*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo mafupi, sasa nataka na mimi nitoe mchango wangu wa maandishi kwa Wizara hii ya Ujenzi ambayo hotuba yake imesomwa na Waziri husika wa Wizara - Mheshimiwa John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Spika, katika kuwasilisha hotuba yake, Mheshimiwa Waziri aliwasilisha katika mfumo wa kipekee, mfumo ambao unakubalika zaidi katika mfumo wa kileo wa Sayansi na Teknolojia na ni mfumo ambao utawavutia Watanzania wengi licha ya kutokuwa na uhakika wa uhalisia juu ya uwasilishwaji wake.

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri kwamba bajeti iliyopangiwa ya Ujenzi ni kubwa kuliko bajeti zote. Hata hivyo na mimi nimeshangazwa na kauli ya Waziri alipotaka Bunge limuidhinishie jumla ya Sh. 7,974,670,219/= kwa matumizi mengineyo ambayo hayakuainishwa.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kwa heshima zote kwamba lugha ya matumizi mengineyo itolewe ufafanuzi, kwani inatia shaka nafsi za Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli usiopingika kwamba umefika wakati Serikali ikubali na ipunguze matumizi mabaya ya fedha za umma. Haiwezekani kumnunulia Afisa mmoja wa Wizara gari la Shilingi milioni 220 au zaidi wakati kuna wananchi hawana hata fusi katika barabara zao na wengine hawajui barabara ni kitu gani.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana kabisa na baadhi ya wachangiaji kwamba ujenzi wa matuta unaofanyika katika barabara zetu ni miongoni mwa mambo yanayosababisha ajali kutokana na kutofanyika kwa utafiti wa kina katika kujengwa kwake.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba Jiji la Dar es Salaam lilikosa miundombinu katika ujenzi wa barabara zake. Hata hivyo, Serikali ina wajibu wa kutafuta wataalamu watakaoweza kuleta mabadiliko na kuondoa idhilali zilizopo zinazotokana na msongamano wa magari.

Mheshimiwa Spika, imefika wakati sasa mtu anayetoka Temeke kwenda Posta anachukua masaa mawili mpaka matatu akiwa na gari. Hivyo, Serikali itawapa lawama gani wafanyakazi wakati miundombinu ya barabra ni mibovu?

Mheshimiwa Spika, kuna tabia ambazo zimeshajengeka za kutolewa ahadi ambazo hazitekelezwi ipasavyo. Mfano, kunaweza kutolewa kauli ya kwamba barabara iliyojengwa kutoka eneo fulani hadi mahali fulani itamalizika muda fulani, lakini kumalizika kwake ikawa ni kwa maneno tu, sio kwa vitendo.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Waziri wa Ujenzi alizungumzia vivuko kufanyiwa ukarabati. Katika hili, kumetengewa fedha nyingi kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati vivuko hivyo. Hili linatia wasiwasi wa pili kuona kwamba kuna ubadhirifu wa fedha za umma kutokana na fedha zilizoelezwa kuwa ni za matumizi mengineyo na hazikutolewa ufafanuzi na hizi za vivuko. Kwanini Serikali isiangalie ununuaji wa vivuko vipya na ing'ang'anie kukarabati vivuko ambavyo kuna uhakika vitagharimu fedha nyingi katika kukarabatiwa kwake na havina muda endelevu wa kudumu kuhudumia Watanzania walio katika maeneo yenye vivuko?

Mheshimiwa Spika, Serikali ina wajibu wa kuliangalia hili kwa kina kwani kunaonekana kuwepo kwa harufu ya ubadhirifu katika hili. Kwa vyovyote kutafutwe vivuko vipya na pale ambapo pataamuliwa kukarabatiwa kivuko, basi kiwe ni kile tu ambacho hakitakuwa na gharama kubwa katika kukarabatiwa kwake.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nilimsikia Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi wakati akijibu swali la mmoja wa Wabunge akisema kwamba Serikali haitawalipa fidia wale wote waliojenga karibu na barabara na wakavunjiwa. Swali ni: Je, hao ambao hawatalipwa fidia walikwishapewa taarifa na Serikali kwamba eneo hilo litapita barabara au kulikuwa na kiashiria chochote kilichoonyesha kwamba eneo hilo litapitiwa na barabara? Kwa wale ambao walijenga kabla ya taarifa ya Serikali au kuelewa viashiria wameshalipwa? Kama hawajalipwa, watalipwa lini na Serikali?

Mheshimiwa Spika, ni vyema kauli ikaandamana na matendo na matendo ya kauli ya Serikali ni kuwafidia wananchi ambao walivunjiwa nyumba zao, walipotezewa vipande vyao na hata maeneo yao ya mashamba ambayo walikuwa wakijipatia mahitaji yao ya lazima. Kuna wale ambapo baada ya bomoabomoa waliweza kupoteza maisha yao kwa presha au kwa kupata ugonjwa mwingine baada ya kuvunjiwa aidha nyumba au sehemu yake ya biashara. Serikali ina wajibu wa kuwafidia wahusika na Marehemu hao angalau kuwapa moyo, kwani ni ukweli usiopingika kwamba kuna familia zimepoteza watu wao kutokana na vitendo vya kuvunjiwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina wajibu wa kukaa na kulitafakari hili kwa kina, kwani siyo vyema hata kidogo kutofikiria kwanza tuanze vipi kabla ya kuwavunjia wananchi ambao wao ndio walioiweka Serikali madarakani, lakini leo ikaamua kuwavunjia katika hali ambayo walikuwa hawajajitayarisha pa kwenda kuishi. Serikali ilikuwa na haki na wajibu wa kuwatafutia makazi ndiyo wakaendelea na bomoabomoa zao wakihakikisha kwamba wananchi wameshawapa haki zao na wanaendelea kujiwekea majengo mengine kwa ajili ya makazi yao.

**MHE. REV. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa jitihada za kutengeneza barabara mpya kwa kiwango cha lami na changarawe. Bado nasisitiza kasi zaidi kwa kazi hiyo na kwa uwiano mzuri na siyo suala la "kila mwamba ngozi kuvutia kwake", hali ambayo nashawishika kuamini kwamba ndivyo inavyofanyika sasa.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo nilihoji hapa Bungeni bado nasisitiza umuhimu wa barabara toka njia panda ya Karatu – Mang'ola – Matala hadi Falago iwekwe katika mpango wa

Wizara kwa ujenzi wa kiwango cha lami. Barabara hii ni muhimu sana kwa Mikoa ya Arusha, Singida na Shinyanga kwa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano - Mheshimiwa Jakaya M. Kikwete alipokuja Karatu kwenye Kampeni mwisho mwa mwaka jana aliahidi kujenga barabara za viungo katika Mji wa Karatu kwa umbali wa kilometa mbili, sijaona ahadi hii ya Rais katika kitabu cha bajeti. Naomba kupata majibu kwamba ahadi hii ya Rais itatekelezwa lini? Muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, naomba *TANROADS* isimamie vizuri Wakandarasi kwani barabara zinajengwa chini ya viwango. Haya ni malalamiko kwa maeneo mengi. Je, uhusiano kati ya *TANROADS* na Mhandisi wa Ujenzi wa Wilaya ukoje katika kuhakikisha kwamba barabara zote ndani ya Halmashauri zinajengwa kwa viwango? Hapa kuna tatizo kubwa sana, Halmashauri ikihoji ubovu wa barabara jibu linatolewa kwamba hii ni *TANROADS,* sisi hatuhusiki. Sasa tukubali tu kujengewa barabara mbovu?

Mheshimiwa Spika, tatizo sugu la daraja la Baran – Bonde la Eyasi mahali ambapo kilimo cha umwagiliaji huendeshwa kwa ufanisi mkubwa, sasa imekuwa vigumu kupita upande wa pili. Daraja hili ni tatizo kubwa na uwezo wa Halmashauri ni mdogo. Naomba Wizara ipate kuwasaidia wananchi hawa.

Mheshimiwa Spika, moja ya mpango wa Serikali ni kuondoa matuta barabarani. Je, ni nini mbadala wake? Kwani watu wengi hufa kwa ajali. Moja ya eneo hatari na wengi wamekufa ni eneo la Rhotia – Karatu na jana tarehe 1 Agosti, 20211 wamezika tena mtu kwa kugongwa na gari. Wananchi wanataka kuwekwe matuta ili kupunguza mwendo kasi.

Je, Mheshimiwa Waziri nini ufumbuzi wa kudumu katika kuokoa maisha ya wananchi wetu?

**MHE. SUBIRA K. MGALU**: Mheshimiwa Spika, nachukua fursa hii kuendelea kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunijalia afya njema inayoniwezesha kuchangia bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya inayopelekea maandalizi mazuri ya hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu utajielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Ndundu - Somanga ya kipande cha Kilometa 60 imechelewa sana kukamilika tangu ilipoanza kujengwa Julai, 2008 kwa ahadi ya kukamilisha ndani ya miezi 18.

Mheshimiwa Spika, kutokamilika kwa kipande hiki kwa muda uliowekwa kina athari kubwa sana kwa wakazi wa Mikoa ya Kusini hasa kipindi cha masika ambapo magari mengi yanakwama. Pamoja na magari mengi kukwama kipindi cha masika, wananchi wa maeneo hayo hasa wa Kata za Chumbi, Muhoro, na maeneo ya Nyamwage yenyewe wanapata taabu sana.

Mheshimiwa Spika, kuchelewa ukamilishaji wa kipande hiki pamoja na mambo mengine inasemekana kunasababishwa na mkandarasi kuchelewa kulipwa pesa. Kuchelewa kwa malipo ya mkandarasi kunaweza kusababisha Serikali kuingia gharama zaidi kwa malipo ya tozo kwa ucheleweshaji huo.

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itakamilisha kipande kilichobaki cha kilometa 60, ni wazi itafungua njia/fursa za uchumi katika Mikoa ya Kusini (Pwani, Lindi na Mtwara) ambapo Mikoa hii ipo nyuma sana kimaendeleo katika nyanja zote.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya Wizara ya Ujenzi ya mwaka 2011/2012, Wizara haijatenga kiasi chochote cha kuwezesha maeneo ya *Delta* kufikika kwa urahisi kupitia ujenzi wa daraja linalounganisha Kata ya Mbwera. Kata za Mbwera, Kongoroni, Mbuchi na Maparoni ni

visiwa na usafiri unaotumika ni boti za kienyeji. Kwa kipindi cha miaka 45 iliyopita, Kata ya Mbwera ilikuwa inafikiwa na magari kutokea Muhoro, lakini leo daraja hilo limeharibika na kwa pesa za *Road Fund* Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji haiwezi kutengeneza daraja hilo kwa kuwa linategemewa kugharimu zaidi ya Shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali kutupia jicho la huruma wananchi wanaokaa maeneo ya *Delta* kwa kuchukua hatua za makusudi za kusaidia uwezekano wa ujenzi wa daraja hili ili maeneo hayo yaweze kufikika na kuokoa vifo vya akina mama wajawazito wanapopata matatizo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu vivuko na magari, naishukuru sana Serikali kwa kutimiza ahadi ya ununuzi wa kivuko kipya cha Utete. Pamoja na maegesho ya kivuko cha Utete kukamilishwa na kivuko kuanza kazi, kuna changamoto kubwa ya fedha za mafuta ili kukiwezesha kivuko kufanya kazi iliyokusudiwa ya kuwavusha wananchi hususan wagonjwa na wakulima. Hivyo, naiomba Wizara itenge fedha za kutosha kwa ajili ya kununua mafuta ili kivuko hicho kifanye kazi vizuri kwani hivi sasa kivuko hicho hakifanyi kazi.

Mheshimiwa Spika, katika barabara za Mkoa Ukurasa wa 201 wa Kitabu cha hotuba ya Waziri wa Ujenzi, barabara ya Ikwiriri - Mloka ambayo imo katika orodha ya ahadi za Rais, haimo katika orodha hiyo na haijatengewa pesa zozote. Barabara hii ni muhimu sana kwa vile inaunganisha pamoja na mbuga wa wanyama *Selous*. Barabara hii ina hali mbaya sana. Iwapo itafanyiwa matengenezo ni wazi idadi ya watalii wanaokwenda mbuga ya *Selous* itaongezeka, hivyo kuongeza pato la Halmashari ya Wilaya ya Kisarawe.

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kushukuru kwa kazi ya usanifu inayoendelea katika miradi ya Makurunge – Saadani – Pangani – Tanga (km.178), Makofia – Mlandizi – Ukumburu (km.148), na Kibaha – Mapinga (km.23). Naomba pia ahadi ya Mheshimiwa Rais ya kujenga barabara za Makao Makuu ya Mkoa wa Pwani (Kibaha) kiwango cha lami itimizwe.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SAIDI R. BWANAMDOGO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Wizara kwa uwasilishaji mzuri wa bajeti, nina maeneo yafuatayo ambayo naomba yafanyiwe kazi:-

Mheshimiwa Spika, fidia kwa wananchi waliopo kwenye barabara ya Msata – Bagamoyo. Ujenzi katika barabara hiyo unaendelea vizuri. Hata hivyo, baadhi ya watu waliokutwa na barabara baada ya upanuzi wa mita 30 kila upande wa barabara bado hawajalipwa fidia. Hili ni kero kubwa na naomba lifanyiwe kazi haraka.

Mheshimiwa Spika, pamoja na taarifa kwamba barabara ya Makurunge – Saadani – Pangani – Tanga ipo kwenye upembuzi yakinifu kwa sasa, naomba liwekwe daraja la chuma kwenye mto Wami hata kabla ya ujenzi wa barabara kuanza. Wananchi wengi na hata watoto wanauawa sana na mamba wanapojaribu kuvuka mto huu kutoka upande mmoja wa mto kwenda upande wa pili ambako ndiko kwenye Kijiji cha Matipwili.

Mheshimiwa Spika, kipande cha Kilometa 60 cha barabara kati ya Ikwiriri na Somanga – Lindi, kinaleta adha kubwa sana kwa watu tunaotumia njia hizo, ukiachilia mbali ubaya/ubovu wa eneo hilo pia eneo hilo lina ujambazi mkubwa kwa abiria na mali zao. Hivyo, naomba kimaliziwe.

Mheshimiwa Spika, Wizara inadaiwa fedha nyingi sana na wakandarasi. Kwahiyo, kiasi kinachoombwa na Wizara kwenye bajeti hii sina uhakika kama kitafanya kazi iliyokusudiwa kwani wakandarasi wengi watakaohusika na ujenzi wa miradi ya 2011/2012 ndio hao hao wanaoidai Serikali. Hivyo hawawezi kufanya kazi hii mpya kwa moyo wakati wanaendelea kuidai Serikali.

Mheshimiwa Spika, inachukua muda mrefu sana kuanzia kuweka X nyumba, kufanya tathmini hadi kulipwa. Kwa kuwa zoezi la kuweka nyumba X kwa mwaka 2010/2011 limewaathiri watu wengi, ni vyema Serikali isichukue muda mrefu sana kulipa fidia kwa watu hawa. Vinginevyo, hili ni bomu kubwa na likianza kulipuka litaleta madhara makubwa sana.

**MHE. SAID NKUMBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu na Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi. Katika mchango wangu, naomba niipongeze Wizara ya Ujenzi na Serikali kwa ujumla kwa kuziwekea umuhimu wa pekee barabara za Mikoa ya Rukwa, Tabora na Kigoma katika kuhakikisha kwamba ujenzi wa barabara kuu katika Mikoa hiyo inaanza kujengwa kwa kiwango cha lami. Kwa namna ya pekee naipongeza kwa dhati Wizara kwa kuamua kuanza kujenga barabara ya Tabora – Sikonge kilometa 70 kwa kutenga kiasi cha Shilingi milioni 590.31 kwa ajili ya maandalizi ya ujenzi huo. Ni matumaini ya wananchi wa Sikonge kwamba jitihada hizi zitafanyika kila mwaka ili kukamilisha barabara hii mapema iwezekanavyo kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Spika, pili napenda kuiomba Wizara kutenga fedha kwa ajili ya barabara iliyopandishwa hadhi miaka miwili iliyopita, lakini kipande cha mibono-kipiri hakina fedha. Nashukuru kwa kuitengea fedha barabara ya Tutuo – Izimbili – Usoke kwa mwaka wa pili mfululizo, imekuwa ikipata fedha kwa matengenezo baada ya kupata hadhi ya Mkoa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawashukuru Waziri na Naibu Waziri, toka wateuliwe wameamua kutoka na kwenda kuziangalia barabara na utendaji wa kazi unaoendelea wakisisitiza ubora wa kazi kwa waliopewa kazi ya utengenezaji barabara. Ziara hizo zimewasaidia kuzijua barabara hizo, matatizo yake na namna ya kuzisaidia ziweze kupitika vizuri wakati wa masika na kiangazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Spika, nami napenda kuchukua fursa hii kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nashauri Serikali iongeze muda wa kuangalia barabara kutoka mwaka mmoja mpaka mitano ili idhibiti uchakachuaji na matengenezo ya mara kwa mara.

Pili, kwa kuwa *Road Fund* inakuwa inapatikana kwa ku-*charge*, *over loading, transit charges* na kadhalika: Je, Serikali haioni kuwa kwa ku-*charge overloading* wanaziathiri barabara zetu?

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa katika Mkoa wa Kigoma Kata ya Kagoa kuna mto unaopita katikati ya Kata hiyo na maeneo ya Kabogo Mgumile na Nyauboza ujulikanao kama mto Lwiche, na wakazi wengi wamekuwa wakipoteza maisha kutokana na ukosefu wa muundo mbinu kama daraja ambalo lingeweza kunusuru maisha ya wakazi hawa wa Kata ya Kagera. Kama bajeti hii ndogo, tunaomba Waziri mwakani au bajeti ijayo wananchi hawa wawekewe daraja ili kupunguza vifo hivi.

Mheshimiwa Spika, nawasilisha.

**MHE. PROF. PETER MSOLLA:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa hotuba nzuri yenye vielelezo vizuri vya takwimu na ramani ambavyo vinafanya taarifa hiyo kueleweka vizuri.

Mheshimiwa Spika, kero kubwa zote katika Jiji la Dar es Salaam ni msongamano wa magari ambao kila siku unazidi kuongezeka na hali kuwa mbaya zaidi kutokana na uwingi wa Mikokoteni na Bajaji. Je, Serikali ina mpango gani kabambe kuondoa kero hii kwa njia ya kudumu?

Mheshimiwa Spika, Serikali ilitamka wazi kwamba barabara kwenda Makao Makuu ya Wilaya zitajengwa kwa kiwango cha lami: Je, ni lini sasa barabara ya kutoka Iringa kwenda Kilolo (Makao Makuu) na ya kutoka Ilula – Mlafu – Isagwa – Kisinga hadi Kilolo (Makao Makuu) zitajengwa kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, barabara zote hizi ni za *TANROADS*.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri na kubwa wanayoifanya.

Pili, nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kuwasilisha bajeti yake vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, hoja zangu pamoja na bajeti ya Wizara hii kuwa kubwa kuliko Wizara zote, naomba Serikali iiongezee zaidi kutokana na umuhimu hasa wa barabara za lami. Pia urasimu wa kupandisha daraja barabara za changarawe upunguzwe ili barabara sasa zijengwe na *(TANROAD)* Mkoa badala ya Halmashauri za Wilaya ambazo hazina pesa za kutosha, huku mkizitazama kwa jicho la huruma barabara za Jimbo la Mtera.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**MHE. NAOMI M. KAIHULA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa na afya njema na kuweza kuchangia katika Wizara hii muhimu kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitagusia mambo matatu ninayofikiri hayaendi vyema katika Wizara hii, hata kama kwa wakati huu yanaonekana kuwa ni shwari, lakini muda siyo mrefu yatakuwa ni tatizo katika nchi yetu. Mojawapo, ni makazi ya Kata za Upanga. Mimi ninayeandika hoja hii ni mkazi wa eneo hilo tangu mwaka 1982.

Mheshimiwa Spika, Baba wa Taifa kwa hekima zake, ili kuleta usawa na kuondoa upendeleo wa kikoloni, alitaifisha majengo mengi ya Upanga ambayo yalikuwa ni ya Wahindi au watu wenye asili ya Kihindi. Wazalendo wenye asili ya Tanzania wakapangishwa na Mawizara yao. Kwa mkakati huu mwelekeo wa matabaka ukawa umefanikiwa sana.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kifupi wakaaji wengi wazalendo kwa ajili ya umasikini wao wakaingia katika mtego wa ufisadi wa kuwauzia Waasia hawa ambao nafikiri kwamba wamejipanga kukomboa eneo hilo na kulifanya liwe la Waasia watupu ili waendelee kufanya mambo yao. Hadi sasa ninaposema kasi ni kubwa mno, kwani sasa wakishirikiana na Shirika la Nyumba wananunua majengo na kujenga maghorofa makubwa rosheni zaidi ya ghorofa 10, lakini inasemekana wanapangisha wageni tu au wanapangishana wenyewe.

Mtanzania mzalendo akienda kupanga wanamwondoa kwa kumtajia kodi kubwa mno ambayo inamkimbiza, lakini wao kwa wao hujipangia bei poa. Lakini angalizo hasa ni kwa ujenzi huu una matatizo ya miundombinu ya uondoaji wa maji machafu na upatikanaji wa maji safi. Kutokana na ongezeko kubwa la watu katika makazi ambayo yalikuwa ni ya watu wachache kabisa: Je, hii siyo hatari ya kuleta magonjwa ya mlipuko katika eneo hilo?

Mheshimiwa Spika, jambo hili siyo dogo, ndiyo maana nikasema muda siyo mrefu matatizo haya yatakuwa makubwa. Ushauri wangu ni kuitaka Wizara hii ikishirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Makazi kuangalia jinsi ya kuzuia utabakalishaji wa eneo hili na kuona kuwa wazalendo ambao siyo matajiri, wa asili ya Watanzania weusi, wanalindwa na kupewa upendeleo wa makusudi kuwawezesha kupata hati za kununua flati wanazozimiliki ili kusawazisha matabaka ya Upanga.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, hili pia ni muhimu sana, nalo ni nyumba za Serikali zilizouziwa wafanyakazi wa Serikali wastaafu kwa kisingizio kwamba ni masikini, wasaidiwe hifadhi. Lakini ukweli ni kwamba hawa ndugu zetu wame-*mis-use*, wametumia vibaya upendeleo huu, kinyume chake wameziuza hizo nyumba kwa matajiri sana na kujengwa majumba ya ajabu, huwezi kuamini. Wengine wao wamejenga wenyewe kwa fedha zao. Kwahiyo, kwa kusema kweli wale walikuwa wanategemea viwanja/*site* tu ndizo walizokuwa wanategeshea.

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi, hili suala bado linawauma sana wananchi hasa pale majengo haya yamewanyima viongozi wengi nafasi ya kuishi katika nyumba za Serikali na kuishi mahotelini ambapo kunagharimu Serikali fedha nyingi ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, ushauri ni kuona kuwa Serikali inarudisha nyumba zake kwa Serikali na kuwapatia nyumba nyingine kule kwao, yaani wastaafu wapewe nyumba au wajengewe nyumba kule kwao *(Home of domicile)* badala ya kung'ang'ania nyumba za Serikali badala ya kuwaacha kwenye *site* zile ambazo kila mtu anatamani angekaa wakati fulani anapofikia madaraka fulani ama anapokumbwa na uhamisho. Pia wafanyiwe tathmini iwapo kweli walikuwa hawana uwezo na sasa je, wakoje?

Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini siyo kwa uthamani, ni suala la matuta yasiyokuwa na mpangilio. Kumezuka mtindo wa kuweka matuta kiholela. Sasa mfano Jiji la Dar es Salaam bila hata ya matuta tayari mwendo umeshadhibitiwa na msongamano wa magari, hivyo hakuna hata uhitaji wa matuta ya kuharibu magari ya walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, ushauri ni kwamba iwapo ni lazima kuwepo na tuta, basi kazi hiyo ifanywe na wataalamu na wala siyo kwa mapenzi ya kila mtu. Wenye magari wanahitaji kutendewa vyema kuhakikisha kuwa magari yao hayaharibiwi na matuta yasiyokuwa na kiwango. *TANROAD* kama vile wanavyodai kodi kubwa za barabara hata kutumia Polisi kuhakikisha kuwa kodi ya barabara inalipwa, basi fanyeni hivyo hivyo kuona magari yao yanapita kwenye barabara safi.

Mheshimiwa Spika, ahsante, naomba kuwasilisha.

**MHE. NASSIB S. OMAR:** Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia fedha nyingi sana katika kununua magari ya *Toyota VX* kwa ajili ya matumizi ya Maofisa wake. Gari moja VX ni zaidi ya Shilingi milioni 260. Fedha hizi ni nyingi mno. Hivyo, napendekeza kuwa Maofisa wa Serikali wapewe mikopo ili waweze kununua gari. Magari yaliyopo sasa yawekwe katika *"Pool"* ili ziweze kutumika kwa wageni au hata kukodishwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali inadaiwa pesa nyingi na Makandarasi. Madeni haya yanatozwa riba na kwa hiyo, fedha nyingi za ziada huhitajika nje ya bajeti. Hivyo, Serikali lazima itekeleze miradi kutokana na fedha ilizokuwa nazo ili kuepuka madeni na hiyo riba.

Mheshimiwa Spika, kwa muda mrefu sana Wizara imekuwa ikizungumzia daraja la Kigamboni. Ni wakati muafaka sasa kwa daraja hilo kujengwa kwa azma ya kupunguza msongamano wa magari.

**MHE. JOSEPHINE GENZABUKE:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naunga mkono hoja asilimia mia moja. Napenda kumpongeza Waziri wa Ujenzi - Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Naibu Waziri - Mheshimiwa Harrison Mwakyembe, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Ujenzi kwa utendaji wao mzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuishukuru Serikali ya CCM kwa kutekeleza ilani yake kwa kuufunga Mkoa wa Kigoma kwa kuanza kujenga miundombinu ya barabara. Barabara ya Mwandiga - Manyovu imekamilika, Kidawe - Uvinza - Malagasi inaendelea kujengwa. Nilikuwa naomba sasa Serikali iweze kutusaidia ili barabara zilizosalia ziweze kujengwa. Barabara hizo ni Kidawe – Kasulu - Kibondo – Nyakanazi, Kasulu - Mnanila na Kasulu - Kanyani - Uvinza.

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi Wizara ilivyoanza, ninaamini kabisa barabara hizo zitaweza kujengwa ili wananchi wa Mkoa wa Kigoma nao waweze kuwa na maisha bora, kwa kusafiri na kusafirisha mazao yao kuyapeleka kwenye masoko na bila matatizo na hatimaye kujiinua kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali iweze kujenga Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kwa kiwango cha lami. Kwa sababu sasa hivi Kigoma hakuna ndege inayokwenda kwa sababu uwanja wa ndege ni wa vumbi tupu na wenye ndege wameacha kupeleka ndege zao. Wananchi wanapata shida sana ukizingatia kuwa usafiri wa reli unasuasua na barabara hazijakamilika kujengwa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maeleo hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Ujenzi – Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa taarifa nzuri na uwasilishaji wa hoja yake. Nawapongeza wasaidizi wake wote akiwamo Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Idara na Wakala zote zilizopo chini ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja hii katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ichukue hatua maalumu ya kukopa pesa ili iweze kugharamia ujenzi wa barabara ambazo zimo katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano. Serikali ikope na isiogope kukopa na ijitahidi kadri iwezekanavyo kutotumia fedha za ndani katika ujenzi wa miundombinu. Huu ni uwekezaji mkubwa na hivyo ni busara ukafanyika kwa fedha za kuazima. Tusiogope kukopa kwa vile sasa nchi yetu inayo sifa ya kukopesheka. Madeni ya *TANROADS* yalipwe ili kuwajengea imani Wakandarasi wanaofanya kazi hizi.

Mheshimiwa Spika, naishukuru sana Serikali kwa kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa kivuko cha *MV Geita* na pia kwa kutenga fedha kwa kununua kivuko kipya kwa ajili ya Kisiwa cha Maisome na kahunda. Naomba sana Serikali iwe makini wakati wa ukarabati na ujenzi wa vivuko hivi ili viweze kuwa na kivuli *(shade)* na vyeo kwa ajili ya abiria.

Sambamba na vyoo, Wizara ihakikishe katika maeneo vivuko vinapoegesha kujengwe nyumba za abiria kusubiria. Sasa hivi wananchi wanateseka sana hasa wakati wa masika. Pia vivuko vilale Visiwani na siyo ng'ambo yake. Jambo hili nimekwishaandika barua kwa Waziri wa Ujenzi kuhusu kivuko cha *MV Kome II* kulala Kisiwani Kome na siyo Nyakaliro. Hadi sasa sijapewa jibu na bado kivuko kinalala Nyakaliro na siyo Kome. Naomba leo nipate jibu, lini wataanza kulala Kome?

Mheshimiwa Spika, tatu, ili kusimamia vizuri kazi za ujenzi wa barabara, Wizara ianzishe utaratibu wa kupitia usanifu mara mbili *(design audit)* na baada ya ujenzi kuwe na utaratibu wa kawaida wa *"Post Construction technical audit"* ili kama thamani ya fedha itakuwa haifanani na kazi iliyofanyika, basi Mkandarasi na Mhandisi mshauri wawajibike.

Mheshimiwa Spika, Wizara iombe Bunge liweke kipengele katika Sheria ya Manunuzi ya Umma, kitakachokuwa kinawalazimisha wakandarasi wakubwa kuwajengea uwezo wa kifundi *(Technical Apprenticeship)* mafundi na waajiriwa wa muda, kutokana na sehemu ya fedha za mkataba wao na Serikali kama itampendeza Waziri, niko tayari kutoa ufafanuzi zaidi wa namna jambo hili lilivyo katika nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, Kampuni za ndani nchini zitafutiwe nafuu ya ushindani katika zabuni za Serikali ambazo Kampuni za kigeni zinashiriki. Kampuni za kigeni, hasa za kichina zinapata nafuu kubwa ya kodi na riba za Benki, hususan kwenye vifaa vya ujenzi, na hivyo kuwapa uwezo mkubwa wa kushinda zabuni karibu zote ambazo wanashiriki. Jambo hili siyo tu kwamba linachangia kuzidi kutorosha fedha zetu za mtaji, bali linachochea kushuka kwa thamani ya fedha yetu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. BETTY E. MACHANGU:** Mheshimiwa Spika, Idara ya *TEMESA* utendaji kazi wake Mikoani hauridhishi. Utengenezaji wa magari ya Serikali ni hafifu sana kiasi kwamba magari mengi ya Serikali yanapelekwa *garage* za binafsi. Mfano, Tabora, Kigoma, magari yanapelekwa Mwanza.

Mheshimiwa Spika, kuna tetesi pia za mafundi wa *TEMESA* kwamba huondoa *spare* nzuri katika magari ya Serikali yanapopelekwa *TEMESA* na ku-*replace spare* mbovu. Wakati huo huo *invoice* wanazopeleka katika Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya ni za gharama kubwa ambayo hailingani na kazi wanazofanya. Nashauri Serikali ipitie gereji hizi na vyema wakawapitia

*RAS* na *DAS* ili kusikia kutoka kwao, na hivyo kuweza kunusuru fedha nyingi za Serikali zinazolipwa gereji za binafsi.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. AMOS G. MAKALLA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Ujenzi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nashukuru Serikali imetenga fedha kwa ajili ya barabara ya Magole – Turiani (Km 48) imetengewa fedha Sh. 4,339.96 na ujenzi utakamilika Juni, 2012.

Mheshimiwa Spika, nataka kupata maelezo wakati Mheshimiwa Waziri akihitimisha hotuba yake: Je, fedha za ujenzi wa barabara Turiani – Mziha mbona mwaka huu hazijatengwa? Ni kwanini kuna wakati Waziri aliwahi kujibu kuwa fedha kwa ajili ya barabara ya Magole –Turiani – Mziha zipo na kasi ya ujenzi itaongezeka? Naomba majibu wakati wa kuhitimisha hotuba, kinyume cha hapo nitaondoa shilingi.

Mheshimiwa Spika, Dakawa – Dihombo ni barabara ya *Short cut* ambayo itaungana na Magole – Turiani. Naomba barabara hii ipandishwe hadhi na itengewe fedha mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Mhonda – Ubiri – Pemba ni muhimu na itasaidia wananchi wa Pemba - Kibati kufika Turiani kwa urahisi kuunganisha na barabara kuu ya Magole – Turiani.

Mheshimiwa Spika, naomba barabara ya Sangasanga – Mzumbe – Mlali – Nyandura ipandishwe hadhi iwe ya Mkoa, ifike Nyandika. Hivi sasa imefika Langali na haitengewi fedha za kutosha. Naomba itengewe fedha ijengwe kwa kiwango cha lami toka Mzumbe – Nyandika.

Mheshimiwa Spika, barabara ya Sanga Sanga – Mzumbe kwa kukosa matuta au vidhibiti mwendo imesababisha vifo vya watu tisa katika Kijiji cha Vikenge na Changarawe. Nimeshaomba kwa kuongea na Waziri lakini pia niliongea katika hotuba ya Waziri Mkuu. *TANROAD* Mkoa wamekuwa wakisingizia fedha hawana. Inakuwaje watu wanaendelea kufa na Serikali haichukui hatua za kudhibiti magari kwa kuweka alama na matuta?

Mheshimiwa Spika, naomba majibu kabla sijaunga mkono hoja. Naomba wakati Waziri anajumuisha hotuba, naomba majibu ya hoja hizo tatu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. DAVID H. MWAKYUSA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja na timu nzima ya Wizara kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, kuna barabara mbili ambazo ningependa kuzungumzia kwa nia ya kutaka kujua mpango wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Barabara Kyimo – Ikuti – Luswisi (Ileje) – Itumba inaunganisha Wilaya za Rungwe na Ileje na iko katika hali mbaya kutokana na kutofanyiwa matengenezo ya mara kwa mara. Kuna mpango gani wa kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami?

Mheshimiwa Spika, barabara ya Kyela – Ipande – Masukulu – Pakati ikijengwa itakuwa kiungo muhimu kati ya Wilaya za Rungwe na Kyela na itachochea maendeleo katika *Corridor* ya kati ambapo barabara itapita. Sehemu inayohitaji kujengwa ni chini ya kilomita nne inayounganisha Ipande na Masukulu.

Je, ni lini Serikali itajenga barabara kuviunganisha Vijiji vilivyotajwa?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DK. WILLIAM A. MGIMWA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nachukua nafasi hii kumpongeza Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayofanya kwenye Wizara ya Ujenzi. Baada ya pongezi hizo naomba sasa nichangie kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna umuhimu wa bajeti ya Wizara kwa kiwango kikubwa ioanishwe na matarajio ya Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano unaoanza mwaka kesho. Hoja kuu hapa ni kwamba *Capital projects,* kawaida ni endelevu, yaani huchukua zaidi ya mwaka mmoja. Maana yake miradi yote au mingi itamalizika mwaka 2012/2013 hasa barabara na nyumba wakati tutakuwa tayari tunaanza mpango mpya wa maendeleo wenye miradi ambayo tumekwishapitisha tayari. Jambo la kujiuliza hapa ni: Je, kwa kiwango gani tunaweza kujikuta tuna miradi kiporo ambayo italeta *financial burden to the new financial year 2012/13?* Kama ni kweli: Je, Wizara ifanye nini? Au ina mkakati gani kulikabili tatizo hili tutakapoanza *New Strategic Plan ya 2012/2013?*

Mheshimiwa Spika, katika kikao cha *RCC* – Iringa kilichofanyika mwezi Machi, 2011 kilipitisha barabara muhimu kwa ukarabati au kuzipandisha hadhi ili zihudumiwe na *TANROADS*. Hata hivyo, katika kitabu cha hotuba yako barabara zifuatazo hazimo:-

(1) Iringa – Kilolo;

(2) Iringa – Kalenga - *Ruaha National Game Reserve;*

(3) Kalenga – Kiponzelo – Wasa - Lugoda kuwa ya Mkoa na hivyo ipate kukarabatiwa vizuri.

Je, nitarajie barabara hizi zitatengenezwa lini?

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini wamenipigia simu kuwa katika Mpango wa mwaka 2011/2012 barabara ya Nyololo- Igowole – Kibao – Mtwango – Mgololo ijengwe kwa kiwango cha lami imepita katika Viwanda vya Chai, Mbao, Kiwanda cha Karatasi Mgololo. Ni barabara muhimu sana katika uchumi wa Taifa pia katika vikao vya *Road Board* ya Mkoa wa Iringa walipitisha. Waliwahi kupeleka *proposal* ya barabara hii tangu miaka ya 2004.

Mheshimiwa Spika, naomba katika majumuisho Mheshimiwa Waziri aitolee majibu. Ahsante.

**MHE. BENEDICT N. O. NANGORO:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na wataalam kwa kuandaa hotuba hii.

Mheshimiwa Spika, *Structure* ya Bajeti ya Wizara iendane na *structure* ya barabara asilimia za barabara zilizo katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri na Kijiji – *Percentage za structure* ya bajeti zi-*match percentage* za kiasi cha barabara iliyopo katika kila fungu.

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa baadhi ya kazi za *TANROADS* uboreshwe ili kuboresha *quality* ya baadhi ya barabara.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kujenga Kilometa saba za lami Kibaya Mjini, utekelezwe sasa.

Mheshimiwa Spika, *priority areas* ziwe ni kukamilisha *Strategic Roads* ikiwemo barabara ya Babati, Kondoa – Dodoma hadi Iringa.

Mheshimiwa Spika, Katika *Resource allocation* jitihada ifanyike ili barabara za lami ziwe *fairly distributed throughout the country*.

**SPIKA:** Watu wamesahau kuja? Sasa namwita Naibu Waziri wa Ujenzi aweze kutoa mchango wake katika kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili nami niweze kuchangia hoja ya Makadirio ya Wizara yetu ya Ujenzi iliyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi hapa Bungeni jana asubuhi.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kutoa shukrani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania - Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, kwa heshima aliyonipa kwa kuniamini na kuniteua katika kipindi hiki cha pili wa Awamu ya Nne kutumikia kwa wadhifa wa Naibu Waziri wa Ujenzi. Kwa unyenyekevu mkubwa, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa imani aliyoonyesha kwangu na wapiga kura wa Jimbo la Kyela.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda kwa uongozi wake mahiri na maelekezo yake kwangu juu ya utekelezaji wa majukumu yangu ya kazi. Naomba nimshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli - Mbunge wa Chato, kwa jinsi anavyonishirikisha kwa karibu katika majukumu ya kuiongoza Wizara ya Ujenzi. Nimefarijika pia kwa ushirikiano nilioupata kutoka kwa watumishi wote wa Wizara pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu - Balozi Herbert Mrango, akisaidiwa na Engineer John Ndunguru - Naibu Katibu Mkuu. Nawashukuru sana watumishi wote wa Wizara ya Ujenzi na Taasisi za Wizara walioko Dar es Salaam, na Mikoani.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe mwenyewe na uongozi mzima wa Bunge, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge kwa kuonyesha uwezo mkubwa wa kuliongoza Bunge letu katika kipindi kifupi. Naomba nimalizie kwa kuwashukuru wapigakura wa Jimbo la Kyela kwa msimamo wao imara na adhimu wa kukataa kurubuniwa na pesa ndogo ndogo za msimu na kunitunuku ushindi wa kishindo kwa mara ya pili mfululizo tangu mwaka 2005. Naomba ushirikiano wao, maana bado tunazo changamoto nyingi mbele yetu katika kuliletea Jimbo letu maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya utangulizi huo, naomba nianze kujibu baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge kama ifuatavyo:-

Naomba nianze kwa mchango wangu kwa kutamka kwamba naunga mkono na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote tuunge mkono hoja hii ili mipango ya miradi mbalimbali iliyoombewa fedha iweze kutekelezwa.

Pili nieleze tu kwamba, kwa ujumla, hoja za Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na wale waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni kwa kupitia ya Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Hotuba ya Waziri wa Fedha na Hotuba ya Waziri wa Ujenzi, tutazitolea majibu kwa maandishi kabla ya kumalizika kwa Mkutano wa Bunge hili. Kama ilivyo kawaida, mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi atawatambua Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maandishi na kwa kuzungumza kwa kuwataja.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuanza kujibu hoja mbalimbali, naomba nipokee kwa mikono miwili shukrani nyingi na pongezi ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge wengi kwa kazi nzuri iliyofanywa na Wizara yetu na Serikali kwa ujumla katika kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, sasa nipitie baadhi ya hoja kama ifuatavyo: Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, kwa Sekta ya Ujenzi, Mheshimiwa Salvatory Machemli, alikuwa na mengi ya kuiambia Serikali, nitagusia machache tu kutokana na muda na Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi atagusia mengine. Kwanza ameuliza kwamba Wizara imechukua hatua gani kutekeleza ushauri wa *CAG* uliotokana na ukaguzi wa ufanisi wa kazi za Wizara na *TANROADS*.

Mheshimiwa Spika, kwanza ifahamike kwamba kwa *TANROADS* kama ilivyo kwa taasisi nyingine za umma, inafanyiwa ukaguzi na *CAG* mara kwa mara na ukaguzi anaouongelea Mheshimiwa Machemli, ulihusisha miradi iliyotekelezwa kufikia mwaka 2006 na naomba nimhakikishie Mheshimiwa Machemli kwamba hatua kadhaa zimeshachukuliwa na Wizara na *TANROADS* kurekebisha mapungufu yaliyojitokeza. Uamuzi kwa mfano wa Wizara kukataa

kupokea barabara ya Kilwa kutoka kwa mkandarasi au hatua ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, miezi miwili iliyopita kutaka *value for money, audit* ifanyike kwa miradi yote ya ujenzi katika Halmashauri, ni sehemu ya kutengeneza ushauri wa *CAG*.

Mheshimiwa Spika, pili, Mheshimiwa Machemli alidai kuwa utakuwa muujiza mkubwa kwake kama Wizara itajenga barabara za lami zaidi ya kilomita 11. Nimekuwa najiuliza ni kitu gani hasa kinamfanya Mheshimiwa Machemli ashangae sasa, ashindwe kuamini wakati miujiza mingi ameishaiona chini ya Serikali ya awamu ya nne? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulikuwa na Vyuo Vikuu vitatu tu, leo tunavyo 37, huo ni muujiza! Tulikuwa na sekondari 1,200 tu mwaka 2005, leo zipo 4,266. Muujiza! Tulikuwa na wanafunzi 41,000 tu mwaka 2005 wa Vyuo vikuu, leo wapo 140,000. Huu ni muujiza! Tulikuwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, chuo kikubwa kupita vyote na tulijivuna kwamba tulikuwa na wanafunzi wengi 5,000, leo *UDOM* ina wanafunzi zaidi ya 20,000 na inaelekea muda siyo mrefu kwenye *pick* yake ya kuwa na wanafunzi 40,000. Huo nao ni muujiza! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi tulivyojipanga kwa ushirikiano wenu Waheshimiwa Wabunge na kwa kutumia utaratibu mpya wa *PPP* badala ya kutegemea fedha ya Serikali peke yake na wafadhili, nina uhakika tutafika na tutaweza.

Mheshimiwa Abia Nyabakari, amelalamika sana kuhusu barabara za Rukwa. Anataka barabara toka Kalambazite hadi Ilemba yenye urefu wa kilomita 24, kama ambavyo Mheshimiwa Malocha, vilevile Mbunge wa Kwela alivyoomba, alitaka ipandishwe hadhi. Mheshimiwa Nyabakari, anataka vilevile barabara ya Mkuti kwenda Lwampembe ipandishwe hadhi na ihudumiwe na *TANROADS* na kujengwa kwa lami au zege.

Mheshimiwa Spika, hizi ni hoja nzuri, ila napenda tu kuwafahamisha Waheshimiwa Wabunge kuwa maombi ya kupandishwa hadhi hasa kwa barabara ya Kalambazite yamepokewa Wizarani na yanafanyiwa kazi. Aidha, kuhusu kupandishwa hadhi kwa barabara ya Mkuti kwenda Wampembe, namwomba Mheshimiwa Nyabakari afuate tu taratibu kama zilivyoainishwa katika Sheria ya Barabara Na. 13 ya mwaka 2007 na kanuni zake za mwaka 2009.

Vilevile niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge wa Rukwa na Wabunge wengine wote kuwa bado wana nafasi kubwa kuleta mabadiliko makubwa Mkoani mwao kwa kutumia fedha ya Mfuko wa Barabara. Mkoa wa Rukwa kwa mfano, utakuwa na zaidi ya shilingi bilioni 2.9 kwa barabara za Halmashauri ambazo zikisimamiwa vizuri na Waheshimiwa Wabunge, zinaweza kuleta mabadiliko makubwa katika Sekta ya Ujenzi kwenye Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Spika, kwa Mkoa huo huo wa Rukwa, Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac, katika mchango wake wa maandishi alitaka kujua kiasi cha pesa kilichotengwa kwa barabara mbalimbali za Mpanda. Mimi namshauri tu aangalie kitabu cha hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, kiambatanisho namba tano, ataona kila kitu kimeainishwa pale. Aidha, ombi lake la Wilaya ya Mpanda Vijijini la kuiongezea Halmashauri yake fedha kwa ajili ya barabara za vijijini, nina uhakika ombi hilo limepokewa na TAMISEMI.

Mheshimiwa Desderius John Mipata – Mbunge wa Nkasi Kusini alileta maombi ya kupandishwa hadhi barabara ya Nkana - Kala yenye urefu wa kilomita 72 na Kitosi - Wampembe ya kilomita 68. Maombi yamepokelewa na Wizara ya Ujenzi, yanafanyiwa kazi. Mheshimiwa Josephat Kandege - Mbunge wa Kalambo, alitoa hoja kwamba mizani za mikeka zinalalamikiwa sana, tumeipokea kwa lengo la kulifanyia kazi suala hili.

Mheshimiwa Spika, naongelea hoja moja moja tu za Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ni nyingi kupita kiasi. Inabidi kuchambua moja moja kwa kuweza kufiti katika muda mfupi tu niliopewa.

Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia - Mbunge wa Mtwara Mjini naye amekuwa na swali lake la msingi hapa akisema anataka kujua hatua iliyofikiwa na ununuzi wa kivuko cha Kilambo ambacho tenda yake ilitangazwa mwezi Juni, 2010. Ningependa tu kumweleza kwamba

kivuko cha Kilambo kinaendelea kutengenezwa nchini Uholanzi na mkandarasi aliyeshinda zabuni *M/S Dutchment.* Kivuko hiki kitakamilika kufikia mwishoni mwa Desemba, 2011.

Mheshimiwa Spika, pia ukurasa wa 33 wa hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kuna makosa kidogo ya uchapaji, kivuko kilichopaswa kutajwa ni Kilambo na siyo Ilagala, kwa hiyo, marekebisho yatafanyika ili isomeke Kilambo. Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi - Mbunge wa Mbozi Mashariki, anauliza ni lini *TANROADS* au Wizara ya Ujenzi kupitia *TANROADS* itaweka matuta eneo la Kijiji cha Ihanda na Lumbila Ruanda kwenye barabara ya *TANZAM*?

Mheshimiwa Spika, ombi la kujenga matuta eneo la Ihanda Wilaya ya Mbozi kwenye barabara hiyo, tumelipokea na linafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria. Mheshimiwa Charles Kitwanga (Mawe Matatu) - Mbunge wa Misungwi, ametaka kujua tu kwamba maombi ya kupandisha daraja na kujenga kwa lami barabara ya Buhingo - Ilele yenye urefu wa kilomita 30 kuwa ya Mkoa yamefika wapi? Nataka kumweleza ndugu yangu Mheshimiwa Kitwanga (Mawe Matatu) kuwa Serikali inazingatia na kutambua umuhimu wa barabara hii yenye urefu wa kilomita 30. Hata hivyo, Wizara imesitisha kwa muda zoezi la kupandishwa daraja barabara za Wilaya kuwa za Mkoa ili kuimarisha kwanza barabara za Wilaya zilizopandishwa daraja mwaka 2009.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya – Mbunge wa Viti Maalum, ameongea mengi lakini moja tu ambalo naweza kulisema sasa hivi ni kuhusu *TEMESA,* alisema imetelekezwa. Kwa kweli, siyo kweli kwamba *TEMESA* imetelekezwa. Wizara ya Ujenzi imeanza mkakati wa kuboresha karakana zake hatua kwa hatua na kuzifanyia ukarabati na kuziongezea vitendea kazi. Aidha, Serikali inaandaa mwongozo sasa hivi utakaotumika kwenye Wizara na taasisi zote za Serikali katika kutumia karakana za Wakala wa Ufundi Umeme *(TEMESA)* kutengeneza magari yao. Pia napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa *TEMESA* inao mafundi wengi waajiriwa ambao wana uzoefu na uwezo wa kufanya kazi za matengenezo ya magari.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Ruhwanya alitaka kujua vilevile ujenzi wa daraja la Kingamboni utaanza lini? Jibu letu ni kwamba usanifu wa daraja hili unaendelea, na ujenzi rasmi tunategemea utaanza mwanzoni mwa mwaka 2012.

Mheshimiwa Amour Abu Juma, Mbunge wa Kibaha Kijiji anasema barabara za lami zinajengwa chini ya viwango. Ameongea mambo mengi, lakini hilo moja ni kubwa. Mimi nataka tu kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba hili tumeliona na tunaimarisha usimamizi na udhibiti wa ubora wa barabara.

Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda - Mbunge wa Handeni, naye katika mchango wake wa maandishi anaomba uharakishaji wa ulipaji wa fidia kwa barabara ya Nkata kwenda Handeni kwa maeneo ya *SUA*, Amani, Mazingara na Mkata kwa vile wengine tayari wameshalipwa fidia ili kuweza kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara hiyo. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa fidia zitalipwa kwa mujibu wa sheria na kwa wale wanaostahili kulipwa.

Mheshimiwa Lucy Philemon Owenya – Mbunge wa Viti Maalum, ameongea mengi lakini moja ambalo linajitokeza ni kwamba daraja lililoko kwenye barabara ya *Old Bagamoyo*, karibu ya Hospitali ya *TMJ* huwa linajaa maji mvua ikinyesha, ili kuzuia lisisababishe ajali lijengwe upya. Ni kweli daraja hilo hujaa maji wakati wa mvua nyingi kwa sababu upande wa chini wa mto kumejengwa na kuziba njia ya asili ya maji. Kwa hiyo, daraja hilo litajengwa upya wakati barabara itakapojengwa upya ikiwa ni pamoja na kuboresha njia za maji. Usanifu wa kuijengea barabara hii kuwa njia mbili unaendelea.

Mheshimiwa Spika, kuna hoja nyingi zinajirudia. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, anataka tutumie teknolojia mpya za ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kwa haraka, kwa mfano nchini Malaysia, wanajenga nyumba kwa kutumia takataka za mashambani, vyuma kidogo na ambazo ni madhubuti na kwa muda mfupi. Anataka sheria zetu ziangaliwe ili teknolojia hizi upya ziweze kukubalika.

Mheshimiwa Spika, ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tumeupokea na Wakala wa Majengo kwa kushirikiana na *National Housing Building Research Agency*, wanaendelea na utafiti kwa lengo la kutumia teknolojia mpya na kupunguza gharama.

Mheshimiwa Dkt. Rashid - Mbunge wa Rufiji, anaulizia kuhusu barabara ya Muhoro - Mbwera anasema inatengenezwa kila mwaka lakini chini ya kiwango, hivyo haipitiki, hivyo huu ni ufujaji wa fedha. Lakini nimkumbushe tu kuwa barabara ya Muhoro - Mbwera inasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji na Mheshimiwa Mbunge ana nafasi kubwa ya kudhibiti hali hiyo katika Halmashauri ya Rufiji.

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa - Mbunge wa Lupa anasema *invoice* ya zaidi ya Shilingi bilioni 20 iliyopelekwa *TANROADS* kutoka Kampuni ya Sogea, ina utata na hivyo ichunguzwe. Tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba *invoice* anayoizungumzia bado haijapokelewa na *TANROADS* na ikipokelewa uchunguzi wa kina utafanyika.

Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo - Mbunge Viti Maalum, anasema zimetengwa fedha kiasi gani na ujenzi utaanza lini kwa kiwango cha lami katika barabara ya Mkiwa – Itigi – Rugwa kuunganisha Mikoa ya Singida na Mbeya? Kwa kweli upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unaendelea. Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 924.489 kwa ajili ya matengenezo ya kawaida na matengenezo maalum.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Paul Lwanji - Mbunge wa Manyoni Magharibi, alisema barabara ya Manyoni – Itigi – Chaya imeanza kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini matengenezo ya kawaida kwa barabara ya zamani yametekelezwa. Kwa kweli nataka kumweleza Mheshimiwa Mbunge kwamba hili ni kosa, tutakaa na mkandarasi kumweleza ajirekebishe kwenye hilo suala.

Pengine kwa sababu imebakia sijui dakika moja au mbili, niongelee kuhusu ndugu yangu na rafiki yangu wa karibu sana Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka - Mbunge wa Simanjiro. Nadhani bado analalamika kuhusu ujenzi wa barabara ya *KIA* - Mererani na kudai kuwa pengine imeachwa kuwa kuna upendeleo kwa viongozi wa juu wa nchi. Kwa kuwa Mheshimiwa Ole-Sendeka ni rafiki yangu na rafiki, lazima nimweleze ukweli, tu kwamba hakuna barabara hata moja ambayo tumeipendelea hapa inayoelekea nyumbani kwa kiongozi yeyote yule mwandamizi nchini. Ipi?

Mheshimiwa Spika, miradi yote ina maelezo makini ya umuhimu kiuchumi na kijamii. Mimi nilijiuliza: pengine hii barabara ya Singida – Katesh – Dareda – Babati – Minjingu inamfuata kiongozi gani? Mheshimiwa Chambiri, huyu Mbunge wa Babati Mjini? Au barabara ya Dodoma – Babati inamfuata nani? Mheshimiwa Zabein Mhita? Au barabara ya Kidahwe – Uvinza, inamfuata Mheshimiwa gani pale? Mheshimiwa Kafulila au Mheshimiwa Zitto? Kwa hiyo, mimi nilikuwa nasema hakuna ukweli kabisa kwenye hilo. Tumejitahidi ku-*balance* haya masuala.

Mheshimiwa Spika, mimi nina barabara ambayo ni barabara ya Mkoa kuanzia mwaka 1961, Rais ameitolea ahadi mwaka 2005, lakini siwezi nikaanza kuipigania leo ijengwe kwa kiwango cha lami, wakati barabara za Mikoa, barabara za Tabora – Nzega – Punge; Tabora – Ndono – Urambo, barabara za bado ni changarawe, nitakuwa niko *very unfair* na sisi ni viongozi.

Barabara anayoiongelea Mheshimiwa Christopher Ole-Sendeka ya KIA – Majengo – Mererani hadi Orkesmet, haikuwa kwenye orodha ya barabara zinazohudumiwa na Wizara ya Ujenzi hadi zilipopandishwa hadhi na kuwa barabara za Mkoa mwezi Julai, 2009. Barabara hii ilikuwa ya Wilaya kabla ya hapo na tuliipandisha kwa kuheshimu kwamba Rais alipopita pale mwaka 2005 alisema: "hii barabara nataka ijengwe kwa kiwango cha lami." Ndiyo maana tumekwenda polepole na ujenzi wake. Barabara ni mchakato na ndiyo maana katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara ilitoa jumla ya Shilingi milioni 197 kwa ajili ya usanifu wa kiwango cha lami ili kutekeleza ahadi hiyo ya Mheshimiwa Rais na tulikamilisha hilo mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda umepita, nilitaka niseme kwamba kwa mwaka 2011/2012 barabara ya Majengo – Mererani – Orkesmet ina jumla ya kilomita 125.9 na

imetengewa jumla ya shilingi milioni 603.180 na shilingi milioni 157.02. Naomba aangalie kiambatanisho Na. 2 ukurasa wa 140 na vilevile kiambatanisho Na. 5(a) ukurasa wa 176.

*(Hapa Kengele iligonga kuashiria muda wa mzungumzaji kwisha)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mtoa hoja, dakika za kutaja majina hatutazihesabu.

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kujibu baadhi ya hoja ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge kwa umahiri mzuri sana. Lakini kwa bahati mbaya sana michango ni mingi kweli, makaratasi haya yote yana majibu na mengine nimeyaacha katika meza yangu pale.

Mheshimiwa Spika, hoja yetu imechangiwa na Waheshimiwa Wabunge wengi sana, lakini nianze kwa kusema kwamba waliochangia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu walikuwa 57. Waliochangia kwa hoja ya Waziri wa Fedha walikuwa 36, waliochangia kwa maandishi ni 178, waliochangia kwa kusema hapa Bungeni ni 27, na wote waliokuwa wanachangia hata kwa maandishi walikuwa wanaleta karatasi tano au sita. Kwa hiyo, kuzijibu kwa dakika hizi chache ambazo umenipa, inawezekana itahitaji miujiza pia.

Mheshimiwa Spika, naomba niwataje tu waliochangia kwenye hotuba ya Wizara yangu kwa kuandika nao ni Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi, Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mheshimiwa Charles Muhangwa Kitwanga, Mheshimiwa Mhonga Said Ibrahim Ruhwanya, Mheshimiwa Abuu Hamoud Jumaa, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Rashid Ali Omar, Mheshimiwa Dkt. Seif Seleman Rashidi, Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, Mheshimiwa Diana M. Chilolo, Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri, Mheshimiwa Abdulkarim Esmail Hassan Shah na Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Fakharia Khamis Shomar. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa David Zacharia Kafulila, Mheshimiwa Josephine Tabitha Chagulla, Mheshimiwa Selemani Said Bungara, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mheshimiwa Jerome Dismas Bwanausi, Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac, Mheshimiwa Dkt. Festus B. Limbu, Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mheshimiwa Hamad Ali Hamad, Mheshimiwa Deo Kasenyenda Sanga, Mheshimiwa Ali Khamis Seif, Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mheshimiwa Stephen Julius Masele, Mheshimiwa Goodluck Joseph Ole-Medeye, Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mheshimiwa Athumani Rashid Mfutakamba, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Christowaja Gerson Mtinda, Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na Mheshimiwa Mary Pius Chatanda. *(Makofi)*

Pia Mheshimiwa Dkt. Cyril August Chami, Mheshimiwa Halima James Mdee, Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, Mheshimiwa Dkt. Milton Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Aina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Mchungaji Luckson Ndaga Mwanjale, Mheshimiwa Amina Abdallah Amour, Mheshimiwa Ignas Aloyce Malocha, Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema, Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mheshimiwa Juma Selemani Nkamia, Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, Mheshimiwa Azza Hillal Hamad, Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mheshimiwa Saleh Ahmed Pamba, Mheshimiwa Sylvester Massele Mabumba na Mheshimiwa Gosbert Begumisa Blandes. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mheshimiwa Godfrey Weston Zambi tena, Mheshimiwa Al-Shaymaa John Kwegyir, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mheshimiwa Rosweeter Faustin Kasikila, Mheshimiwa Paulina Philipo Gekul, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Mustapha Boay Akunaay, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mheshimiwa Stephen Hilary Ngonyani, Mheshimiwa

Mariam Nasoro Kisangi, Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mheshimiwa Rebecca Michael Mngodo, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa Asha Mohamed Omari, Mheshimiwa Nyambari Chacha Mariba Nyangwine, Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mheshimiwa Kombo Khamis Kombo, Mheshimiwa Mchungaji Israel Yohana Natse, Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mheshimiwa Saidi Ramadhani Mwanamdogo,

**SPIKA:** Ni Bwanamdogo.

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Saidi Ramadhani Bwanamdogo. Unajua majina mengine ni magumu kwa watu tunaotoka Kanda ya Ziwa. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Wewe endelea tu hivyo hivyo.

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Sabreena Hamza Sungura, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Naomi Amy Mwakyoma Kaihula, Mheshimiwa Suleiman Nassib Omar, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mheshimiwa Dkt. Charles John Tizeba, Mheshimiwa Betty Eliezer Machangu, Mheshimiwa Amos Gabriel Makalla, Mheshimiwa Prof. David Homeli Mwakyusa, Mheshimiwa William Augustao Mgimwa, Mheshimiwa Prof. Peter Mahamudu Msolla, Mheshimiwa Benedict Ngalama Ole-Nangoro na Mheshimiwa Henry Daffa Shekifu. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Mheshimiwa Pudenciana Wilfred Kikwembe, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mheshimiwa Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mheshimiwa James Daudi Lembeli, Mheshimiwa Deogratias Aloyce Ntukamazina, Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mheshimiwa Yussuf Haji Khamis, Mheshimiwa George Gregory Teu na Mheshimiwa Anthony Gervase Mbassa. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Angellah Jasmine Kairuki, Mheshimiwa Abas Zuberi Mtemvu, Mheshimiwa Mussa Zungu Azzan, Mheshimiwa Benardetha Kasabago Mushashu, Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mheshimiwa Susan Anselm Jerome Lyimo, Mheshimiwa Maria Ibeshi Hewa, Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mheshimiwa Esther Lukago Minza Midimu, Mheshimiwa Philipa Geofrey Mturano, Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mheshimiwa Eugen Elishininga Mwaiposa, Mheshimiwa Moses Joseph Machali, Mheshimiwa Abdallah Sharia Ameir, Mheshimiwa Alphaxard Kangi Ndege Lugola, Mheshimiwa Zarina Shamte Madabida. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Christopher Olonyokie Ole-Sendeka, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe, Mheshimiwa Salome Daudi Mwambu, Mheshimiwa Chritina Lissu Mughwai, Mheshimiwa Zaynabu Matitu Vullu, Mheshimiwa Shukuru Jumanne Kawambwa, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mheshimiwa Modestus Dickson Kilufi na Mheshimiwa Nimrod Elirehema Mkono. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Regia E. Mtema, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mheshimiwa Ester Nicholas Matiko, Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mheshimiwa Kuruthum Jumanne Mchuchuli, Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa, Mheshimiwa Susan Limbweni Aloyce Kiwanga, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mheshimiwa Ramadhani Haji Saleh, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mheshimiwa Amina Andrew Clement na Mheshimiwa Anastazia James Wambura. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Haroub Muhammed Shamis, Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni, Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, Mheshimiwa Yusuph Abdallah Nassir, Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki, Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mheshimiwa Ezekiel Magolyo Maige, Mheshimiwa Kheri Khatib Ameir, Mheshimiwa Elizabeth Nkunda Batenga, Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mheshimiwa Lolesia Jeremiah Maselle Bukwimba, Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile na Mheshimiwa Eng. Stella Martin Manyanya. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Albert Obama Ntabaliba, Mheshimiwa Leticia Mageni Nyerere, Mheshimiwa Amina Nassoro Makilagi, Mheshimiwa Dkt. Binilith

Satano Mahenge, Mheshimiwa Magdalena Hamis Sakaya, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mheshimiwa John John Mnyika, Mheshimiwa John Zefania Chiligati, Mheshimiwa Assumpter Nshunju Mshama, Mheshimiwa Moza Abedi Saidy na Mheshimiwa Agripina Zaituni Buyogera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wale waliochangia kwa kuzungumza hapa ni hawa wafuatao; kwanza ni Mheshimiwa Dkt. Harrison George Mwakyembe ambaye ni Naibu Waziri, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Eng. Salvatory Naluyaga Machemli, Mheshimiwa Abia Muhama Nyabakari, Mheshimiwa Zabein Muhaji Mhita, Mheshimiwa Andrew John Chenge, Mheshimiwa Rosemary Kasimbi Kirigini, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga na Mheshimiwa Mariam Salum Mfaki. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Mariam Nasoro Kisangi, Mheshimiwa Wiliam A. Mgimwa, Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba, Mheshimiwa Fatuma Abdallah Mikidadi, Mheshimiwa AnnaMaryStella John Mallac, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Mwigulu Lameck Nchemba Madelu, Mheshimiwa Abdul Rajab Mteketa, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura na Mheshimiwa Augustino Lyatonga Mrema. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Ramo Matala Makani, Mheshimiwa Capt. John Damiano Komba, Mheshimiwa Ismail Aden Rage, Mheshimiwa John Zefania Chiligati, Mheshimiwa Eustace Osler Katagira, Mheshimiwa Pindi Hazara Chana na Mheshimiwa Iddi Mohamed Azzan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja zilizohusu Wizara ya Ujenzi na kwa ukweli kabisa maoni mengi yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge wa Vyama vyote, yaani CCM, CHADEMA, *CUF* na wengine wote wamechangia vizuri sana katika hotuba hii na ninaamini kabisa kwamba ushauri wao mwingi tumeuzingatia kikamilifu sana.

Mheshimiwa Spika, lakini ni ukweli pia kwamba kazi nyingi zimefanyika katika suala zima la barabara. Tunapozungumza kwamba tangu tupate uhuru, barabara za lami ambazo zimejengwa ni kilomita 6,500 na kwa sasa hivi kilomita zaidi ya 11,154.34 zipo kwenye mtandao wa kujengwa kwa kiwango cha lami. Hii siyo miujiza na huu ni ukweli usiofichika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninafahamu na Watanzania wote wanafahamu, lakini hata wenzetu wa Vyama vya Upinzani wanafahamu kwa sababu barabara hizo wanazipita wanapokwenda kuzitembelea hata wakati wa maandamano huwa wanazipitia hizo barabara zikiwa zinatengenezwa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, labda nianze tu kwa kuzungumza, ukichukua kwa mfano sasa hivi barabara ya kutoka Mtwara uje Dar es Salaam, uje Dodoma, uende Singida, uende Mwanza, uende Geita, uende Sengerema, uende Kagoma, uende mpaka Bukoba na Mtukula barabara yote ile ni lami *except* kilomita 60 zilizobaki kati ya Ndundu na Somanga na pale kuna Mkandarasi ameshamaliza zaidi ya kilomita tano, ameshaweka *Prime* zaidi ya kilomita 20 na tuna uhakika kabla ya mwezi wa 11, 2011 lami inakamilika kwa kiwango cha lami zile kilomita 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tuli-*guess* kwamba tunaweza tukatumia *Tax,* lakini ni uhakika sasa watu watakuwa wanatembea hata kwa Bajaji kutoka Mtwara mpaka Bukoba wakipita kwenye barabara ya lami. *(Makofi)*

Lakini chukua barabara nyingine, amua labda uchukue barabara ya kutoka Singida ukiwa unaelekea Arusha. Ukitoka Singida mpaka Babati ni zaidi ya kilomita 223 kuna Wakandarasi watatu wanatengeneza kwa kiwango cha lami. Lakini utoke Babati uende Minjingu, utoke Minjingu mpaka Arusha tunajua kuna lami ya kilomita 104, lakini pale napo zimepatikana fedha kutoka Benki ya Dunia Shilingi bilioni 74 kwa kuanza kuweka *re-ceiling* nyingine. Kwa hiyo, kwa maana nyingine mtu atatoka Singida mpaka Arusha na inawezekana atoke Arusha aende Namanga kwa sababu nako kuna Mkandarasi anatengeneza kwa kiwango cha lami kilomita zote 105.

Ukiacha hilo, umeamua labda sasa uchukue barabara nyingine tu mahali popote hata kuanzia kwa akina Mheshimiwa Kabwe Zubeir Zitto, ukitoka Mwandiga hadi Manyovu kilomita 60 barabara ile imeshamalizwa kutengenezwa kwa kiwango cha lami na fedha zile zimetolewa kwa asilimia mia moja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete - Mwenyekiti wa CCM. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia ukiamua utoke Kigoma uje Mwandiga zile kilomita 36 zimeshamalizwa kwa kiwango cha lami. Utoke pale uende sasa kuelekea Uvinza kuanzia Kidawe huko kote kilomita 76.6 kuna fedha na Mkandarasi yuko pale na jiwe la msingi limeshawekwa, Shilingi bilioni 80 zinatengeneza kwa kiwango cha lami.

Uamue basi upite mpaka kwa Mheshimiwa David Zacharia Kafulila ukipitia kwenye daraja la Malagarasi, kuna Shilingi bilioni 80 na kilomita 48 zinatengenezwa kwa kiwango cha lami.

Utoke pale uende mpaka Urambo Kaliua, kilomita 146 kuna fedha tumeweka mwaka huu zaidi ya Shilingi bilioni 1.4 kwa ajili ya kutengeneza barabara ile kwa kiwango cha lami na *design* imeshamalizika.

Mheshimiwa Spika, lakini ukitoka Urambo, utaamua wewe mwenyewe ukishafika Tabora ambapo kuna kilomita 90, kuna Wakandarasi wawili wanatengeneza kwa kiwango cha lami. Utoke Tabora unaweza ukaamua kuja mpaka Nzega kilomita 115 au uamue uje mpaka Manyoni ukiunganisha zile kilomita 89 kwa kupitia Itigi, pale kuna Wakandarasi watano wanatengeneza kwa kiwango cha lami, shilingi bilioni 424.4 zinatumika pale. Kwa hiyo, tunapozungumza kwamba barabara za lami zinatengenezwa wala siyo miujiza, huo ndiyo ukweli na Wakandarasi wako kwenye *sight*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, unaweza ukaamua kwamba sasa sitaki kutumia hiyo barabara, umemua sasa kutoka labda Mingoyo ukipitia Masasi mpaka Mangaka, pale pote kilomita ni za lami kutoka Masasi hadi Mangaka ni kilomita 54. Ukishatoka pale Mangaka hadi Tunduru ambapo pale *Mission* ya *World Bank* imepita tarehe 26 na ilikuja ikamwona Mheshimiwa Waziri Mkuu na fedha zitatolewa *design* imeshamalizika. Ukitoka Tunduru mpaka Namtumbo kilomita 197 kuna Wakandarasi watatu wanatengeneza kwa kiwango cha lami. Toka Namtumbo nenda Songea kuna Wakandarasi chini ya mradi wa *MCC*. Toka Songea hadi *Mbamba Bay* kilomita 76 kuna Wakandarasi. Kwa hiyo, imebaki *section* ya kilomita 65 kutoka *Mbamba Bay* kwenda mpakani kwenye Ziwa Liuli ili kusudi tuje tuunganishe mpaka *Nkata Bay* kule Malawi. Kwa maana nyingine, Malawi watakuwa wanasafirisha bidhaa zao kutoka Malawi kuja mpaka kwenye bandari ya Mtwara na hapa tutakuwa tume-*create* vizuri ile *Mtwara Development Corridor* iliyosainiwa. Hiyo ni lami! *(Makofi)*

Sasa tunapozungumza, hii siyo miujiza? Ni miujiza kweli! Tunataka tutengeneze lami kila mahali ili wenzetu watakapokuwa wanaandamana wawe wanaandamana kwenye barabara za lami na huu ndiyo utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, unaweza ukaamua kuchagua mahali popote, labda uanzie hapa Dodoma, kutoka hapa Dodoma hadi Iringa kilomita 260 kuna Wakandarasi watatu tumewaganya katika *section* tatu. Wakandarasi wapo na wanafanya kazi. *(Makofi)*

Unaweza ukaamua kwamba sasa nataka nianzie Dodoma kwenda Babati, ukitoka hapa Dodoma mpaka Babati zile kilomita 43, kwanza mpaka Mayamaya kuna Wakandarasi wanatengeneza pale, kuna kampuni ya *Syno Hydro* na kazi imeshaanza na wanaotaka ku-*prove* waende wakaangalie hata leo au kesho au baada ya Bunge hili. Ukitoka pale Mayamaya hadi Bonga kilomita 188 tumeweka kwenye bajeti hii shilingi bilioni 3.3 lakini *mission* ya *African Bank* na *JICA* nayo imefika hapa ikamwona na Waziri Mkuu, wanatoa pesa nyingine. Ile nayo itatwangwa kwa kiwango cha lami. *(Kicheko/Makofi)*

Ukitoka Bonga kwenda Babati zile kilomita 19.2 kuna Mkandarasi anatengeneza kwa kiwango cha lami. Sasa chagua mahali popote, lakini unaweza basi kutoka Bagamoyo kwenda

Msata zile kilomita 64 napo kuna Mkandarasi anatengeneza kwa kiwango cha lami, Shilingi bilioni 64 zinatumika pale.

Unaweza ukaamua sasa labda tuanzie Tanga Horohoro kule nako kuna Mkandarasi anatengeneza chini ya mradi wa *MCC*. Unaweza ukaamua kutoka Tunduma kuja Mpanda ukitoka pale Tunduma uje Sumbawanga kilomita 230, kuna Wakandarasi watatu wamegawanywa chini ya mradi wa *MCC*, Shilingi bilioni za fedha zinatoka pale.

Mheshimiwa Spika, lakini amua pia uteremke chini utoke Sumbawanga uende *Kasanga Port* ili kusudi watu wa kutoka *DRC* wawe wanasafiri kuja huku, kilomita 112. Kuna Wakandarasi wanafanya kazi pale kwa kiwango cha lami. Utoke Sumbawanga uje Kibaoni na Kizi pale kilomita 150, kuna Wakandarasi wawili, fedha zote zimetolewa na Serikali ya *CCM* inayoongozwa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka huu tumeweka fedha kutoka Kibaoni – Kizi – Mpanda lakini kutoka Mpanda – Mishambo nako tumeweka fedha. Lengo letu ni kuunganisha barabara ya kutoka Tunduma – Mpanda – Kigoma – Kidawe – Nyakanazi mpaka hata kule Uganda kwa kiwango cha lami ili watu wawe wanapita. Haya yanayofanywa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi, siyo madogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri, wala hata hatujabagua. Hata ukitoka Siha ukazunguka Mlima Kilimanjaro ile barabara kuna kandarasi tunatangaza mwaka huu, kwani tumeshamaliza kufanya *design*. Kwa hiyo, chagua mahali popote, nenda Bariadi, Mwigumbi, Lamadi, kuna wakandarasi. Yaani chagua popote, kushoto, kulia, nyuma, mbele, wapi, kote kuna wakandarasi. Kwa hiyo, hii ni kazi kubwa inayofanywa na Serikali. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania wanafahamu na nafikiri Wabunge wote kwa pamoja wakiwepo hata hawa wenzetu wanaotupinga pinga mnatakiwa kutu-*support* kwa sababu barabara hizi hazina ubaguzi, watapita wote, hata wa CHADEMA watapita, wa *CUF* watapita, wa *UDP*, hata wale ambao hawana Chama watapita kwenye babarabara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua mambo yanayohitaji kujibiwa ni mengi, lakini kuna masuala ya jumla yalikuwa yanazungumzwa hapa kuhusu barabara zetu katika nchi hii. Nilipotoa kitabu hiki nilifanya makusudi kutoa ramani za kuanzia Arusha mpaka Tanga ili Waheshimiwa Wabunge wajue kwamba ni Mkoa upi una kilomita nyingi za lami na Mkoa upi hauna lami. Kwa mfano, ukienda Mkoa wa Arusha, au uamue kwenda Mkoa wa Rukwa, *network* za Mkoa wa Rukwa ni kilomita 2,180 na *trunk road* (barabara kuu zinazohudumiwa na Wizara) ni kilomita 887, lakini wana kilomita 14.4 tu za barabara za lami na zile ni madaraja yaliyojengwa chini ya mradi wa *World Bank*.

Mheshimiwa Spika, unapomwona mtu analalamika hapa, anazungumza kwamba barabara hizi zinapendelea wakubwa, mimi natamani kulia, kwa sababu kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa ana kilomita 14 tu. Wafipa hawajui hata rangi ya lami. Hawajui! Watani zangu hawa, ni kilomita 14 tu kwenye *net work* ya kilomita 2,180. Sasa tunapoamua kupeleka shilingi bilioni 600 kutengeneza barabara za lami kule Wabunge wasilalamike. Ukichukua kwa mfano Mkoa wa Ruvuma wana kilomita 1,960 za *network* ya barabara zote zinazohudumiwa na Wizara yangu. Kilomita za lami walizonazo ni 192, nyingine zote ni changarawe. Ukiamua kupeleka barabara kule unafanya jambo la maana katika kutandaza maendeleo katika nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Singida wana kilomita 1,689, barabara za lami ni kilomita 288 tu. Unapoamua kupeleka barabara katika Mkoa wa Singida huwapendelei.

Mheshimiwa Spika, Unapoamua kupeleka barabara za lami mkoa wa Mara hujawapendelea. Ukipeleka barabara za lami Mkoa wa Mbeya ambao wana *network* ya kilomita 2,261, lakini barabara zenye lami ni kilomita 360 tu ambazo hazifikii hata nusu ya *network* nzima, huwapendelei. Ukiwapelekea lami kule ukatengeneza barabara ya Mbeya - Lwanjali -

Makongorosi, hujafanya makosa. Najaribu kuzungumza hapa ili kusudi Watanzania wote tuwe na haki na haya tunayoyazungumza hapa tutambue kwamba wananchi wanatusikia.

Mheshimiwa Spika, hebu tuchukue Mkoa wa Dar es Salaam. Dar es Salaam wana kilomita 560.6 zinazohudumiwa na Wizara yangu. Kati ya hizo, barabara kuu ni kilomita 120.4 na zote ni lami. Sasa unataka nikatengeneze barabara za Halmashauri ambazo wanapelekewa fedha za *Road Fund* lakini wanashindwa kuzitengeneza? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunafanya yale yanayoihusu Wizara yangu. Hata hivyo, ninafahamu changamoto za Dar es Salaam na ndiyo maana siku zote nimekuwa nikizungumza kwamba, Halmashauri za Dar es Salaam zisiposhirikiana na Wizara na Wadau mbalimbali, suala la msongamano Dar es Salaam haliwezi kudhibitiwa. Utatengeneza barabara, wao watakwenda kugawa vibanda mle; utatengeneza barabara, wao watapeleka vituo vya mafuta; utatengeneza barabara, wao watakwenda kupimia watu viwanja, hakuna! Utatengeneza barabara, wao watakwenda kuvunja kifungu cha 29 cha Sheria Na. 13 ya Mabango. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusiposimamia sheria na bahati nzuri Ibara ya Katiba Na. 26 kifungu cha (1) na (2) inatutaka kila Mtanzania asimamie sheria pamoja na Katiba. Sasa ndiyo maana nimezungumza katika hotuba yangu kwamba, suala zima la kuondoa msongamano katika Jiji la Dar es Salaam inawezekana hata siyo kujenga *fly overs* tu. Unaweza ukajenga *fly overs* baadaye wakajenga mlemle kwenye *fly overs,* wakagawa viwanja. Utafanyaje? *(Makofi/Kicheko)*

Tumejaribu kubuni mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia maji, feri kutoka kule Bagamoyo, kupanua barabara ya kutoka Mwenge ambapo zinatumika shilingi bilioni 88 ili iwe njia nne pamoja na njia nyingine za *service road*, ingawaje Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam wanasema tumetenga Shilingi bilioni tano. Shilingi bilioni 88 zinazotumika kupanua barabara ya kutoka Mwenge - Tegeta, hizo haziko Dar es Salaam? Shilingi bilioni 38 zinazotumika kutengeneza barabara ya Mandela, haziko Dar es Salaam? *These are the challenges.*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme na kwa dhati kabisa kwa Waheshimiwa Wabunge wa Dar es Salaam kwamba, wazisaidie Manispaa za Dar es Salaam zizingatie sheria ili Dar es Salaam pawe mahali pazuri pa kuishi. Bila kusimamia Sheria, Dar es Salaam unaweza ukapaki gari mahali popote. Vituo vya Mafuta vinagawiwa hata katika umbali wa mita mbili wakati kwa mujibu wa sheria umbali wa vituo vya mafuta unatakiwa uwe kilomita kumi. Tulikuwa tunahangaika na suala la kupunguza msongamano wa Dar es Salaam, tuna vituo saba vya kujenga ambavyo fedha zimetolewa na *World Bank*, vituo vile hatujakabidhiwa.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Urafiki ambacho tulitakiwa tukijenge pale tayari ameshagaiwa mtu ana kituo cha mafuta. Nataka niwaeleze ukweli na ninajua na watu wa Manispaa za Dar es Salaam wanafahamu. Kituo cha *Fire* ambapo tumetangaza na mwezi huu *contractor* anamaliza kazi, bado hajakabidhiwa Kituo cha *Fire*. Kariakoo ndiyo usiseme, kesi nyingi sana zimefunguliwa. Kwa hiyo, Dar es Salaam ni tatizo na ndiyo maana mimi nakubaliana kabisa na Kamati zilizozungumza kwamba inawezekana wakati umefika wa kuivunja vunja Kamati ya Dar es Salaam pawepo na watu *special* kwa ajili ya kusimamia barabara za Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukibembelezana, suala la msongamano Dar es Salaam halitakwisha. Jiji la Nairobi wameanza kazi. Kwa sasa hivi wanatengeneza barabara za *fly overs* na *inter-chain* za kilomita 50.4 ambazo zinawa-*cost* Shilingi bilioni 445, na wamebomoa mpaka ghorofa 12 wamezilaza chini. Sisi ukitaka kugusa kitu, hiyo inakuwa kazi, na ndiyo maana nataka niwaeleze ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge kwamba Tanzania nzima tusipotekeleza sheria hakuna barabara itakayokuwa *solved. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sheria hizi tumezipitisha sisi wenyewe na bahati nzuri nimekuja nazo hapa. Sheria hii ni ya tangu mwaka 1932 na *Orders* zimetolewa Na. 40 ya mwaka 1932, Na. 44 ya mwaka 1939, Na. 17 ya mwaka 1942 na Na. 27 ya mwaka 1959 wakaanza kufanyia nyingine *amendments*. Na. 40 ya mwaka 1969, Na. 92, 93 mpaka sheria Na. 13 ya mwaka 2007. Sasa tufike mahali tuheshimu sheria. Kama hamtaki upana wa barabara huu uliopo, tuamue hapa kwamba

upana wa barabara za Tanzania uwe ni rula moja ili kusudi hata Bajaji isipite. Kupanga ni kuchagua. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nataka niwaeleze kwamba kwa kweli kazi za Uwaziri ni ngumu, ni mateso. Msiwaone hawa watu, ndiyo maana wanasemwa, inabidi ukae kimya tu ukiwa mnyonge. Ningefurahi sana mimi niwe huko nyuma.

**WAHESHIMIWA WABUNGE:** Njoo! *(Kicheko)*

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Lakini lazima pawepo na mtu wa kufanya, nikiwepo na mimi wa kutekeleza hizi sheria. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ukichukua kwa mfano Mkoa wa Kilimanjaro, wao barabara zao zina *network* ya kilomita 974, barabara kuu ni kilomita 295 na zote ni lami. Lakini pia hata barabara za Mkoa ambazo ni kilomita 120 zote ni lami, lakini unafanyaje kama mradi unaukuta pale? Unauzuia usiendelee? Maana yake ni lazima tuumalize, ndiyo kazi nzuri! Ndiyo wajibu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nenda Mkoa wa Manyara ambao wana *network* ya kilomita 1,688 kati ya hizo *trunk road* ni kilomita 217 na ni kwa sababu moja tu kwamba Manyara ni Mkoa mpya. Barabara aliyokuwa anaizungumzia Mheshimiwa Christopher Ole - Sendeka, imepandishwa hadhi mwaka 2009 na ni ya Mkoa. Sasa huwezi ukaweka lami barabara iliyopandishwa hadhi mwaka 2009 ukaacha ile iliyopandishwa hadhi mwaka 1961. Huo ndiyo ukweli na msema kweli ni mpenzi wa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia Mheshimiwa Naibu Waziri alikuwa anazungumza hapa kwamba, kuna fedha ambazo zimetengwa kwenye barabara hii yenye kilomita 125.9 ambazo ni shilingi milioni 603.18. Imetengewa fedha nyingine kiasi cha Shilingi milioni 157.02 na haya yote yako kwenye kiambatanisho Na. 2 ambacho kiko ukurasa wa 140, kiambatanisho Na.5 'A' ambacho kiko ukurasa wa 176. Kiambatanisho Na. 5 'C' ambacho kiko katika ukurasa wa 191, Kimbatanisho Na. 5 'D' ambacho kiko ukurasa wa 205.

Mheshimiwa Spika, aidha, barabara ya Rosinyoi - Njoro imetengewa shilingi milioni 830.2. Barabara ya Rokisare – Sukuro, imetengewa shilingi milioni 112. Barabara ya Singe - Kimotoroki na Berera imetengewa Shilingi milioni 591 kwa ajili ya matengenezo na Sshilingi milioni 261 nyingine, iko katika ukurasa wa 139 na hizo zote ziko kwenye Jimbo la Simanjiro. Lakini mbali na hivyo, hii barabara ya lami inayojengwa ya Kateshi - Derega - Babati - Minjingu, imetengewa Shilingi bilioni 149. Barabara ya Babati - Bonga imetengewa Shilingi bilioni 19.68 na ziko Manyara. Sasa nilisikitika sana Mheshimiwa Mbunge alipoanza kuzungumza katika mtazamo unaoonyesha kwamba Serikali sasa imeanza safari ya kuelekea kwenye kifo chake.

Serikali haiendi kwenye kifo, Serikali ya CCM haifi. *Actually* kwa kutengeneza barabara katika maeneo yote, Rukwa, Ruvuma, Morogoro, Serikali ya CCM ndipo inafufuka na inasimama vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka niseme ukweli na bahati nzuri *Hansard* ninayo hapa, tutajenga barabara zote, lakini kupanga ni kuchagua. Huwezi ukaanza kujenga *regional road* kabla hujatengeneza *trunk road*. Huwezi ukaacha barabara ya Manyara inayotoka Babati - Singida ambayo ni *trunk road*, ukaacha barabara ya Dodoma - Babati, ukaacha barabara ya Dodoma - Iringa, ukaacha barabara ya Tunduru - Namtumbo, eti kwa sababu unataka kutengeneza barabara ya Zolizoli, hii ya nanii, haiwezekani! Mimi nasema ukweli na ukweli utabaki kuwa ukweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeendelea kutenga fedha kwa ajili ya barabara zote kulingana na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi.

**MHE. CHRISTOPHER OLE - SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, siruhusu taarifa yoyote. Leo tuko *constrained with time*. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Spika, Wizara yetu ya Ujenzi kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi, tutaendelea kusimamia ujenzi wa barabara zote nchini ili ziweze kupitika. Zile barabara za Mikoa tutazitengea fedha kupitia Mfuko wa Barabara *(road fund)* ambao kwa bahati nzuri kwa mwaka huu fedha zimeongezeka na katika viambatanisho Na. 2 mpaka kiambatanisho Na. 5 (f) vimefafanua vizuri. Nilitaka niyazungumze haya kidogo ili kusudi niweze kutoa ufafanuzi mzuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *compensation* kwa watu wa Dar es Salaam, tumetoa *compensation* kwa watu 111 ambao tumewalipa jumla ya Shilingi bilioni 3.479 na walilipwa tarehe 16 Desemba, 2010 na sahihi zao ziko hapa.

Hii ni baada ya kupelekwa Mahakamani na wale waliokuwa wanalalamika na wakatushinda kwenye kesi Na. 31 ya mwaka 2004. Lakini wapo wengine ambao tuliwafuata sisi wenyewe ambao walikuwa nje ya *road reserve*, ambao walilipwa Shilingi milioni 1,315 na walipokea fedha zao tarehe 24 Desemba, 2002. Wapo wengine ambao wameshalipwa tena fedha jumla ya Sh. 464,000,631/= na walipokea fedha zao tarehe 17 Aprili, 2008. Nitamwomba Mheshimiwa Mbunge, mtani wangu pale nitampa hizi *documents* ili kusudi akaone orodha ya watu wote ambao walilipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, wapo wengine ambao tumewalipa fidia kwa barabara za *Jets Corner* na kadhalika. Ule mradi *cost* yake ni shilingi bilioni 34, lakini tumelipa fidia kwa Shilingi bilioni 17 ambazo ni karibu na nusu ya gharama ya mradi ule. Tunawalipa wale wanaostahili fidia, wale ambao hawastahili fidia hakuna fidia. Watanzania ni lazima waelewe kwamba kufuata barabara unafuata umasikini. Ni lazima uiache barabara mita 22.5 na kwa Sheria ya sasa hivi Na. 13 ya mwaka 2007 unaacha mita 30.

Waheshimiwa Wabunge ni mashahidi, nenda hapo nje ya barabara kuna mtu anajenga pale, na ni Dodoma watu wote tunapita pale. Ni mbishi na ameshachimba msingi. Ikanibidi nimwambie *Regional Manager* wa Dodoma kwamba kaweke alama pale. Ni jeuri ya pesa!

**MBUNGE FULANI:** Ndiyo!

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni lazima tufike mahali tusimamie sheria zetu. Ndiyo maana watu wanavamia maeneo ya shule, *open spaces*. Tusiposimamia Sheria hakuna barabara itakayojengwa.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wamechangia hoja, sasa sifahamu kama nitaweza kuzijibu zote. Lakini ngoja nijitahidi kujibu haraka haraka. Mnataka nimalizie hapa hapa?

**WABUNGE FULANI:** Ndiyooo!

**WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Eeh! Niliteee kakaratasi kangu! *(Kicheko)*

Mheshimiwa Anne Malecela, ambaye amezungumza kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, mambo yote yaliyozungumzwa hapa tunakubaliana nayo. Ushauri wake ni mzuri sana na nataka niseme tu kwamba ushauri huu ambao tumekuwa tukipewa na Kamati ya Miundombinu, kwetu sisi umetusaidia sana katika kufanya kazi vizuri. Naipongeza sana Kamati hii na kwa kweli imekuwa kichocheo kikubwa katika kufanya kazi zetu, na Waheshimiwa Wabunge wote walioko kwenye Kamati hii nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Salvatory Machemli amezungumzia mambo mengi, mengine yamejibiwa na Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nataka nizungumze machache tu. Ametoa *comparison* ya barabara zinazojengwa Tanzania kwamba sisi ni asilimia ndogo sana

ukilinganisha na nchi kama Malawi, Msumbiji, Zambia na kadhalika. Ninamwomba Mheshiwa Machemli akapige hesabu vizuri kwa sababu *network* ya barabara zinazosimamiwa na *TANROADS*, *trunk road* ni kilomita 12,700. Ukizi-*assume* zile kwamba ni *one hundred percent* ukachukua zile kilomita 6,500 maana yake ni *almost fifty percent.*

Mheshimiwa Spika, ukichukua pamoja na *regional roads* ambazo ni *almost* kilomita 33,000.6 unazungumzia juu ya *seventeen percent*. Lakini ukichukua *network* ya barabara za Tanzania ambayo ina kilomita za mraba 949,000 sawa na kukusanya nchi zote za Afrika Mashariki, Kenya, Rwanda, Burundi, na Uganda, bado hazijafikia *network.* Kwa hiyo, kama tungeamua kutengeneza barabara za lami ukazipeleka Rwanda, wangekosa hata mahali pa kulima. Kwa sababu kila mahali pangekuwa ni lami. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, huwezi ukalinganisha ukubwa wa Tanzania wa kilomita 949,000 na nchi kama Malawi. Mimi nimefika Malawi, Msumbiji, kwa hiyo, nilitaka nimweleze Ndugu Salvatory Machemli, jirani yangu kwa maji kwamba hii ni *calculation* ambayo si ya kweli na kwamba hapa hapahitajiki miujiza, kama huu ni muujiza kwa CHADEMA basi muujiza umeshaanza kutokea wa kutengeneza barabara nyingi ambazo zimeanza kuonekana.

Mheshimiwa Spika, amezungumzia juu ya sekta ya barabara ina matatizo mengi, amezungumzia Tanzania imezungukwa na nchi nyingi, nimetoa mifano hapa karibu kila nchi nane (8) zinazotuzunguka sisi zimeunganishwa na barabara ya lami. Mheshimiza Zitto na Mheshimiwa Obama Ntabaliba, ukitoka Mwandiga hadi Manyovu, ukitoka pale Manyovu kwenda Burundi hakuna lami. Ukienda Rwanda na Burundi pale Kobelo Nyakasanza ukiwa unakuja Isaka ni lami Tanzania na bahati nzuri inawekewa *re-ceiling* nyingine kilomita zote 242 na kuna shilingi bilioni 200 na kitu zimetolewa na *European Union* na Wakandarasi wako kule Straberg na Tchiko fedha zinatengenezwa.

Mheshimiwa Spika, nenda Uganda kule Mutukula, rafiki yangu Waziri wa Ujenzi wa Uganda Ndugu Nasasila alikuja kujifunza baada ya kutengeneza barabara ya kutoka Kagoma kwenda Mutukula. Nenda Sirari kwenye bajeti hii tumetenga fedha kilomita 85.5, tunaipanua ile barabara ya kutoka Sirari kuja kwenye mpaka wa Mkoa wa Mara utengenezwe kwa kiwango cha lami na kandarasi yuko kule. Sasa hivi tunafanya *design* kutoka Tanga, Horohoro kuja mpaka Saadan kilomita 178 katika mradi wa *East African Community*. Kwa hiyo, kila mahali ndiyo maana tumetengeneza hata mpaka wa Kasanga Port. Kwa hiyo, Tanzania inajitahidi katika kutumia hii *geographical conditions* ambazo zilizungumzwa na Mheshimiwa Rais wetu katika kuhakikisha tunaunganisha nchi yetu na barabara za lami kila mahali.

Mheshimiwa Mbunge amezungumza mengi, sasa kwa sababu ya muda sifahamu kama naweza nikamjibu yote lakini mengine yalikuwa ni michango mizuri tu ambayo hata kama ni mchango unaotolewa wa Upinzani mingine ni ya kuishukuru. Kwa sababu ukiwa na mtoto anakufuatafuata kule anajua babu unayofanya nayo ni mazuri.

Mheshimiwa Spika, amezungumzia juu ya daraja la Kigamboni. Mwaka jana tumepitisha hapa mambo ya *PPP*. Tanzania sasa hivi tuna-*operate* juu ya *Design Build Operate and Own and Transfer,* ndio maana tumeingia mkataba na wenzetu wa *NSSF*. Serikali itachangia asilimia 40, *NSSF* watatoa asilimia 60 na ndiyo maana katika mwanzo huu na bahati nzuri *design* imeshamalizika na siku ya kwanza ya kutangaza ile *pre-qualification* ilitangazwa tarehe 1 Aprili, waliosoma kwenye magazeti, *compensation* ya watu wote wa eneo hilo wameshalipwa na *NSSF* wameshasema wana zaidi ya shilingi bilioni 100. Kwa hiyo, nina uhakika katika kipindi hiki wataanza kutangaza tenda kwa ajili ya kuanza kutengeneza daraja na litakuwa daraja ambalo ni *special,* la aina yake.

Mheshimiwa Spika, hizi ni kazi zinafanywa, tusingeweza kuleta mabilioni hapa wakati *NSSF* wanatengeneza fedha na *NSSF* ni ya Tanzania na ndio maana tunajitahidi kuwakaribisha wawekezaji wengine pia watakaoweza kufanya kazi kwa njia ya *PPP*. Hata wawe wa CHADEMA, tengenezeni barabara yenu muiite CHADEMA na sisi CCM tutaanza kuandamana mlemle. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, pamezungumziwa kuhusu kulipa madeni. Watu waliokuwa wanafuatilia Marekani, Marekani ilikuwa na madeni mpaka wameyasuluhisha jana. Sasa kama Marekani ina madeni sembuse Serikali ya Tanzania! Ukishamuweka kandarasi kwenye barabara ni lazima pawepo na madeni na kandarasi hawezi akalipwa fedha mpaka a-*produce certificate.* Huwezi ukamweka pale halafu unaanza kumpa fedha, *no!* Lazima a-*produce certificate* na akifanya kazi mbaya tunamfukuza na wapo ambao tumekuwa tunawafukuza, mpaka sasa tumeshafukuza makandarasi 2,008, katika orodha yote ya makandarasi 7,000 ambao wamesajiliwa, ni kazi ngumu. Kwa hiyo, madeni lazima yawepo, lakini tunaendelea kuyalipa na jana Mheshimiwa Waziri Mkuu ametoa kibali tumelipa shilingi bilioni 100 na sasa tunaendelea kufanya kazi.

Mheshimiwa Abia Nyabakari amezungumza mengi, amezungumzia kuhusu barabara za Rukwa. Nakubaliana naye sasa hivi ni wajibu wetu tuifungue pia Rukwa, barabara zipitike, watu wafanye biashara, tuna njaa, vyakula vitatoka Rukwa na mahali pengine.

Mheshimiwa Zabein Mhita amezungumzia kuhusu barabara ya Mayamaya kwenda Bonga kama tumeiwekea fedha. Nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara ile tunaitengeneza kwa lami na makandarasi wapo, hakuna mchezo tena, Kikwete hana mchezo tena, CCM haina mchezo tena. Tunatengeneza barabara na wanaotaka kushuhudia wakaangalie sasa hivi, wazunguke kwenye maeneo yote niliyoyazunguka mpaka hata barabara ya kutoka Kagoma kwenda Biharamulo, Lusahunga kwa Mheshimiwa Dkt. Mbassa tunatengeneza na sisi hatuangalii barabara inapita kwa CHADEMA, CUF, sisi ni barabara tu na ndio uzuri wa CCM. (*Makofi)*

Mheshimiwa Andrew Chenge amezungumzia kuhusu barabara zile, nampongeza sana kwa ushauri wake, lakini nataka kuzungumzia ile barabara ya Kolandoto kupitia Sibiti mpaka kwa Mheshimiwa Mkono, *feasibility study* ilifanyika mwaka 2008 na imepandishwa hadhi sasa kuwa *trunk road*. Tutaendelea kuifanyia *detailed design* ili barabara ile nayo iweze kupitika kwa baadaye tutakapopata fedha ikiwa pia ni pamoja na barabara ya Mheshimiwa Mkono ya kutoka Makutano hadi Fort Ikoma. Kwa mwaka huu tumeiwekea fedha kwa kuanza kujenga kwa kiwango cha lami. Tumeshamaliza kufanya *design* lakini tunaanza na kilomita 50 lakini pia Nato, Makutano mpaka tukazunguke kule Loliondo mpaka Mto wa Mbu tunafanya *design* nayo tutaijenga kwa kiwango cha lami ila hatutapita mle ndani ya Serengeti. Lengo Watanzania hawa wote wawe wanapita kwenye barabara za lami, ndio lengo la Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, nakubaliana sana na ushauri wa Mheshimiwa Andrew Chenge, kaka yangu na hasa ku-*involve* pia *PPP* na kadhalika, haya yote ni masuala muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rosemary Kirigini naye amezungumzia mengi, ameunga mkono, lakini nataka kumhakikishia kwamba ile barabara ya kutoka Bunda, Kisorya kupita kwa Mheshimiwa Lugola na bahati nzuri Mheshimiwa Lugola ni mwanafunzi wangu, nimemfundisha Sengerema Sekondari, inawezekana hiyo siri hamuijui, pamoja na kwamba yeye anaonekana mzee kuliko mimi kwa sababu anakula vizuri, tumeanza kuitengeneza kwa *design.* Nataka niwaeleze ukweli Waheshimiwa, nina wanafunzi wengi humu, Mheshimiwa Nkamia ni mwanafunzi wangu, kwa hiyo shikamoo ninazipata hata kwa Wabunge humu. Kwa hiyo, ile barabara nayo tunaitengeneza. Tunafanya *design* na watu wako kule wanafanya *design,* ile barabara tunaitengeneza kwa kiwango cha lami. Ni ukweli Mkoa wa Mara hauna barabara nyingi za lami nao. Nao ni lazima tuufungue kwa kutengeneza barabara za kutosha za lami. Kwa hiyo, nakubaliana na ushauri wa Ndugu Rosemary Kirigini.

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, muda wangu sijui umebaki kiasi gani? Wahandisi Washauri (*Consultants)...*

**SPIKA:** Tutakugongea kengele ya kwanza na ya pili.

**WAZIRI WA UJENZI**: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa ngoja nizungumze kwa raha zaidi.

Mheshimiwa Spika, Ma-*Consultants* na Ma-*Contractor,* kuna Sheria ya *Contractors Registration Board,* Na. 17 ya mwaka 1997, kuna Sheria ya *Engineers Registration Board,* Na. 15 ya

mwaka 1997 na kuna Sheria ya Ma-*Architecture and Quantity Surveyor Board,* Na. 16, tumeanza kuzitumia hizi sheria katika kuwabana Ma-*Consultants* ili kusudi wanapopelekwa kwenda kusimamia kazi wakasimamie kweli kazi kwa niaba ya *client*. Kwa hiyo, tutaanza kuwabana kweli pamoja na makandarasi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mwambalaswa ushauri wako ni mzuri kwamba ni lazima sasa Washauri tuanze pia kuwalipa vizuri. Tunapotangaza tenda zetu watakapokuwa wana-*apply* tutawalipa vizuri na madeni yao ambayo tumeanza kuyalipa nao wamekuwa *included* katika kuwalipa madeni. Pia tumetoa maagizo kwa *TANROADS* mradi ukiwa unashughulikiwa katika Mkoa ule isilazimike tu watu wa ku-*supervise* ule mradi watoke Makao Makuu lazima hata yule wa Mkoani kule akasimamie barabara na ile barabara ikifeli yule *Regional Manager* wa Mkoa atakuwa *answerable,* anaondoka. Lazima tufike mahali tuanze kubanana sasa hivi ili kusudi barabara zetu zianze kwenda kwa utaratibu unaotakiwa. Kwa hiyo Mheshimiwa Victor Mwambalaswa nakubaliana na wewe.

Mheshimiwa Mkiwa Kimwanga anaipongeza Wizara kwa kazi nzuri, anazungumzia juu ya Nyerere Road kutoka Mwanza hadi Musoma eneo la Mabatini pale kuna umuhimu wa kujengwa *flyover.* Nakubaliana na yeye kabisa na hili pia limezungumzwa na Mama Hewa. Mama yetu tutaliangalia ni kwa namna gani tutaanza kufanya *design* katika masuala ya kupunguza msongamano katika Majiji yetu Mwanza napo tutaliangalia, Dodoma napo tutaliangalia, Arusha tutaliangalia pamoja na Dar es Salaam, ili tuangalie ni namna gani tunaweza tukafanya *design* za kutosha katika kuhakikisha kwamba tunapunguza msongamano katika Majiji yetu.

Mheshimiwa Spika, nimeshagongewa kengele ya kwanza, Mheshimiwa Mariam Mfaki pongezi kwa Wizara, anawashangaa wale wanaosema Serikali haijafanya lolote na mimi ninawashangaa kama wewe Mama. Ni vyema wakatema mate chini na kweli nafikiri wameshatema. Mama Mfaki kwa sababu ni Mama yetu yale maneno ni mazito sana, kwa hiyo, nina uhakika wenzetu wataelewa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, anazungumzia kuhusu barabara za Dodoma kwamba hakuna barabara kwa ajili ya kupita magari makubwa. Hili kwa kweli Mama Mfaki tutaliangalia ni namna gani ya kufanya *design* na hasa kwa kuzingatia kwamba hapa ni Makao Makuu.

Mheshimiwa Mariam Kisangi anasema yeye ni muathirika wa bomoabomoa, nakubaliana naye mtani wangu. Ninakueleza dada yangu mtani wangu nitakupa hiyo orodha ya watu ambao wamelipwa *compensation* ili kusudi tuweze kufuatilia kwa pamoja lakini nataka niseme kwa dhati watani zangu Wazaramo, Wakwere walioko Dar es Salaam kama wako ndani ya *Road Reserve* hakuna fidia. Wale ambao wako nje ya *Road Reserve* lazima wafidiwe, wale waliofuatwa na barabara lazima wafidiwe na bahati nzuri tuna orodha ya watu wengi waliofidiwa hapa na nitampa Mama Kisangi ili kusudi aweze kuangalia wasije wakawa watu wengine walichukua hiyo fidia kumbe ilikuwa yake na bahati nzuri Mama Kisangi ni mtani wangu tunaelewana sana. (*Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa pongezi kwa Rais na Wizara ya Ujenzi, lami inaletwa katika Wilaya na mengi amezungumza. Amezungumzia kuhusu Mpanda, amezungumzia barabara zake kwamba barabara ya Mkoa ijengwe kwa lami. Mheshimiwa Peter Serukamba naye ametoa pongezi na ametoa ushauri mwingi tu. Mheshimiwa Fatma Mikidadi ametoa pongezi kwa Rais, pongezi kwa Wizara. Amezungumzia ahadi ya Rais zilizoahidiwa katika Mkoa wa Lindi, nataka niseme kwamba ahadi zote zilizotolewa na Mheshimiwa Rais tunazo. Zimeorodheshwa zote tunazo na tutakuwa tunazipanga, katika kipindi cha miaka mitano (5), nina uhakika tutakuwa tumezimaliza ikiwa ni pamoja na ahadi ya barabara ya Mheshimiwa Ole-Sendeka ambayo nayo ilitolewa ahadi na Mheshimiwa Rais lakini kwa mwaka huu tunaikarabati kwa kiwango cha changarawe, mwaka kesho tukifanikiwa kupata fedha tutatengeneza.

Mheshimiwa AnnaMaryStella Mallac barabara za Vijijini ziwe zinahusika sana. Amezungumzia barabara zingine ambazo zinahusika na TAMISEMI ambazo nao huwa wanatumia fedha za *Road Fund*. Wito wangu ambao napenda niutoe kwa Wakurugenzi ambao huwa wanachukua fedha za Mfuko wa Barabara wazitumie vizuri kwa mujibu wa sheria. Sheria ya mwaka 1998, kifungu Na.2 kinasema "*That money should be used for road maintenance only"* sio vinginevyo lakini ni ukweli fedha za *Road Fund* zimekuwa zikitumika kwa matumizi mengine

mabaya. Nitamwomba Meneja wa *Road Fund* ikiwezekana kila Mkoa fedha zitakapokuwa zinatolewa za *Road Fund* katika Wilaya Waheshimiwa Wabunge wawe wanapata nakala ya fedha hizo ili kusudi muweze kuzifuatilia kule wasizichakachue Wakurugenzi na wale watakaozitumia vibaya tukishapata orodha yao tutampelekea Mheshimiwa Waziri Mkuu ili a-*deal* nao. Ni lazima tufike mahali tuanze kushikana mashati kwa ajili ya fedha za *Road Fund* ili zilete manufaa kwa wananchi kulingana na malengo yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Herbert Mntangi ametoa pongezi na ameeleza mengi tu. Mheshimiwa Mwigulu Madelu amezungumzia kuhusu hili daraja la Mbutu. Nataka kumuahidi daraja la Mbutu tumeshalimaliza kulifanyia *design* na katika mwaka huu tutaanza kulijenga mapema sana. Kwa hiyo, wananchi wa Igunga hilo daraja tutaanza kulijenga na huu ni utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa sababu Chama cha Mapinduzi hakisemi uongo na ndio maana hata ninayewakilisha bajeti hapa mimi ni Waziri wa CCM, kwa hiyo, wasiwadanganye wengine wakaja huko wakasema kwamba wanatengeneza hilo daraja, hawana fedha mwenye fedha ni CCM, Rais Jakaya Mrisho Kikwete. Naona Mheshimiwa Mbowe ananiangalia, ndio, hiyo *message sent and delivered*. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Abdul Mteketa amezungumzia Jimbo la Kilombero na umuhimu wa barabara zake. Daraja la Kilombero tumeweka fedha shilingi bilioni moja pointi kadhaa na barabara zake tutazizingatia. Morogoro nayo ni moja Mikoa ambayo haina barabara nyingi za lami. Tutaliangalia hili ili kufuungua Mkoa wa Morogoro ambao ni *very productive.*

Mheshimiwa Richard Ndassa amezungumza na ameomba niende nikaliangalie lile daraja. Nimekubali tutaenda kwenye hilo daraja la Malijisu.

Mheshimiwa Mtutura amezungumzia kuhusu barabara yake ya Tunduru na ile barabara nyingine ya kutoka Tunduru kwenda Mangaka, ile itajengwa kwa fedha za *African Development Bank* na *JICA*.

Mheshimiwa Augustino Mrema, nimempongeza sana kwa barabara zake na maneno yake mazuri ya kumpongeza sana Mheshimiwa Rais. Unajua ni wachache wanaosema ukweli na Mheshimiwa Mrema Mungu akubariki sana na ndio maana ulishinda kule, kwa sababu wewe huwa hufichi ukweli. Unampongeza Rais wa CCM kwa sababu amefanya kazi nzuri. Mheshimiwa Mrema nakupongeza sana na Mungu akubariki sana na ndio maana wananchi wa Vunjo hawakufanya makosa, endelea kushirikiana na CCM katika kutatua matatizo ya wananchi wa Vunjo kwa sababu Sera zinazotekelezwa sasa hivi ni Sera za Chama cha Mapinduzi, ndicho kilichochaguliwa na wananchi katika ridhaa ya miaka mitano (5). *(Makofi)*

Mheshimiwa Eng. Ramo Makani ametoa ushauri mzuri na mimi nakubaliana naye sana. Mheshimiwa John Komba amezungumza maneno mengi kuhusu barabara zake. Nataka kukuthibitishia, tutaendelea kuhakikisha zile barabara zinazojengwa hata zile ulizozileta kwa ajili ya mapendekezo zinazounganisha mpaka Wilaya ya Kyela na maeneo mengine kwenda mpaka kwa Mheshimiwa Jenista Mhagama, tutaziangalia na kwa sababu tunajua hizo ni barabara za ulinzi ni namna gani tunaweza tukazi-*include* hata kwa kutumia fedha za *Road Fund.*

Mheshimiwa Ismail Aden Rage amezungumza mazuri tu yote. Kuna shilingi bilioni 424.25 katika miradi ya barabara zile na tumeongeza pia nyingine ya kutoka Urambo kwenda Kaliua nayo ianze kutengenezwa. Kwa hiyo, hii ni kazi nzuri ya Chama cha Mapinduzi katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi. Makandarasi wote sasa hakuna kusimama kufanya kazi kwa sababu wamepewa *site* kazi yao ni kufanya kazi na Serikali italipa na nina uhakika Waheshimiwa Wabunge wa vyama vyote mtapitisha hii bajeti ya shilingi trilioni 1.49 ili kusudi barabara hizo zikatengenezwe. Hata Mheshimiwa Freeman Mbowe, pitisha fedha hiyo. Hata Mheshimiwa Zitto, usipopitisha maana yake barabara ya Kidahwe - Uvinza itakwama kwenda kwa Mheshimiwa Kafulila na daraja lake la Malagarasi. Kwa hiyo, nawaomba wote mpitishe bajeti hii ili kusudi barabara hizi zitengenezwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Chilligati maombi yake nimeyapokea, tutayazingatia katika kuhakikisha zile barabara zake alizoziomba na madaraja yake yaweze kutengenezwa.

Mheshimiwa Eustace Katagira naye amezungumza kuhusu barabara ya Kyaka na Mheshimiwa Pindi Chana amezungumza mambo mengi ikiwa ni pamoja na barabara zako Mheshimiwa Spika, tutazingatia ikiwa pamoja na barabara ya kilomita 109 kutoka kwako kule kwenda Makete Njombe kwa watani zangu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, napenda sana kujibu hoja zote zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Muda ni mdogo, haya yote ambayo nimeyajibu hapa na wale wote 178 waliochangia kwa maandishi, tutajibu kwa maandishi na bahati nzuri yote tumeshayaandaa tutawagawia majibu haya kwa Waheshimiwa Wabunge wote na naomba *Hansard* irekodi hivyo, kwa hiyo ni matumaini yangu kwamba wakati wa vifungu hawatasimama sana kuuliza maelekezo ili kusudi bajeti hii iweze kupita, tuweze kwenda kutekeleza yale ambayo tunatakiwa kuyatekeleza.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, naomba kutoa hoja.

*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NCHI ZA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA**: Mheshimiwa Spika, naafiki.

**TAARIFA**

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, Taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ole-Sendeka, tunachokisema, leo tunalo tatizo kweli la muda kwa sababu hatuna hata dakika za Spika za kuongeza, tukifika kwenye vifungu utapata nafasi.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA**: Mheshimiwa Spika, ni fupi tu.

**SPIKA:** Utaingia kwenye vifungu.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA**: Mheshimiwa Spika, haya.

**SPIKA:** Katibu!

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nimeshasema *Sergeant-At-Arms* anapoweka Siwa hamtakiwi kuongea, hapa nimekuta mnaongea hapa, wakirudia nawatoa. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyosema, leo ni ngumu sana na zile saa tumepewa basi saa kumi na mbili na nusu inabidi tuwe tumeahirisha. Kwa hiyo, saa kumi na mbili na dakika ishirini tutapitisha kwa *guillotine* kwa sababu tumeshakubaliana.

**Fungu 98 - Wizara ya Ujenzi**

**Matumizi ya Kawaida**

Kif. 1001- *Administration and General* … … …Tshs 2,209,019,359/=

**MWENYEKITI:** Atakayekuwa anarudia lililojibiwa simpi nafasi na tumekubaliana ni masuala ya Sera na sio kibarabara changu na njia fulaji. Mheshimiwa Rajab Mbarouk Mohamed

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. *Vote 98, subvote 1001…*

**MWENYEKITI:** Endelea tu mshahara wa Waziri.

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naanza *item* 210100 ambacho knahusiana na mshahara. Hapa naona msahahara umepungua ambapo kwa mwaka huu ni shilingi milioni 534/- lakini posho zimeongezeka hadi kufikia kiasi cha shilingi milioni 305 tofauti na mwaka jana na mwaka juzi, naomba maelezo ya Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika maelezo yangu nilieleza kwamba Wizara ya Ujenzi iliundwa mwaka jana baada ya kutenganishwa kutoka kwenye Wizara ya Miundombinu. Kwa hiyo, wafanyakazi wengine wapo Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Kwa hiyo, mishahara imepungua kwa sababu wafanyakazi wengine wameenda kwenye Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ataikuta huko kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu posho ni kwa sababu Idara imeundwa upya, kwa hiyo, imeongezeka zaidi.

**MHE. JUMA S. NKAMIA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwenye kitabu cha Waziri, ukurasa wa 152. Nadhani amekiuka Kanuni ama Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, ukurasa wa 28 iliyokiweka Chama cha Mapinduzi madarakani. Kwenye Ilani inasema kwamba barabara ya kutoka Handeni – Kiberashi –Mrijo Chini –Soya –Chambalo – Chemba –Donse –Farqwa – Kwa Mtoro hadi Singida itajengwa, kwa sasa itafanyiwa upembuzi yakinifu lakini kwenye kitabu inaonyesha kwamba hiyo barabara inatoka Handeni –Kiberashi – Kijungu –Kibaya –Njoro –Oldoroti –Mrijo Chini –Dalai –Bicha –Chambalo –Chemba –Kwa Mtoro – Singida. Napenda kufahamu Kanuni hii ama Ilani ya Chama cha Mapinduzi iliyotuweka madarakani kwa nini imekwenda kinyume na hiki kitabu cha Mheshimiwa Waziri na aposema barabara hii inakwenda Chambalo inakwenda mbele halafu inarudi nyuma? Inawezekana Mwalimu wangu hajui hii barabara inakopita.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi imezungumza kuanzia ukurasa wa 72 mpaka 82, kwa hiyo kuyashika yote yale na kujua wapi kinaenda nini, inawezekana hili ni tatizo la uchapishaji tu na yeye alikuwa anakoseaga siku nyingine nilipokuwa nikimfundisha. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashakuru sana. Niliuliza swali la kisera kwenye mchango wangu wa maandishi kwamba wakati wa kujenga barabara ya Nyakanazi mpaka Kigoma ni vizuri tukawa tunaunganisha. Kwa mfano, unapofika Kibondo ni kilomita chache sana kuingia Burundi ili kuiweka barabara hiyo iwe ya kimataifa. Sasa Waziri hili atalichukua kwa umuhimu wake?

**WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara anayoizungumzia kutoka Nyakanazi –Kibondo - Kasulu hadi Kigoma ina kilomita 300 lakini ni kweli pia kutoka Kasulu kwenda Manyovu kuna kilomita 42 ambazo zinaunganisha na Burundi. Kazi tuliyofanya sisi Wizara ya Ujenzi ni kufanya *design* ya kilomita zote 300 na tulitumia mwaka jana shilingi bilioni 1.8. Sasa ni mahali gani itaanzia, hilo ni suala la kisera na bahati nzuri tunaweza tukaweka wakandarasi hata watatu wakaanzia hata Kasulu, wakaanzia hata kwa Mheshimiwa Zitto, wakaanzia hata Nyakanazi. Lengo letu kubwa ni barabara ile yote kilomita 300 imalizike kwa kiwango cha lami. Hicho ndicho tunachokitaka lakini pia katika miaka inayokuja tutaanza kufanya mpango wa kuanza kufanya *design* kwa barabara ya Kasulu kwenda kwa Mheshimiwa Obama zile kilomita 42 ili ziunganishe kwenda Burundi.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuhitaji maelezo ya barabara ya KIA –Mererani ambayo mwaka jana ilitengewa shilingi bilioni mbili kwa kujenga kwa kiwango cha lami na mwaka huu ilitengewa shilingi milioni 157 na si vinginevyo, msome kwenye ukurasa wa 140 lakini bado kuna haja na itahitaji maelezo ya hiyo kwamba ni kwa nini imetoka shilingi bilioni mbili ambayo haikutolewa hata mwaka jana ikaja shilingi milioni 157 kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nilitaka niweke bayana jambo moja kwamba mimi kamwe haiwezi kuingia akilini mwangu kuhoji barabara zinazounganisha Mikoa ya nchi hii na

haswa ikizingatiwa Mikoa mingine iko pembezoni kama Katavi, Rukwa, Mtwara, Lindi nikahoji, siwezi kamwe. Bahati mbaya sana, kaka zangu Madaktari wote wawili walipotosha maudhui mazima ya hoja yangu bila kusoma maelezo yangu wakijibu hoja ya mwongozo nilioomba kwa Spika. Kwa hiyo, napenda tu kutoa maelezo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kwamba na kwa sababu siruhusiwi kuuliza swali la pili ieleweke kwamba barabara nilizokuwa nazilenga ni zile za Mwika –Kiraracha, Kwa Sadala – Mashama - Kibosho Shine –Kwa Rafael, nikasema barabara hizi sio *trunk road*, hizi ni barabara za vijijini zinazounganisha Vijiji na Vijiji sio Wilaya na Wilaya. Ndiyo nikasema ni upendeleo na bado nabaki kwenye hoja yangu, upendeleo ni mkubwa usahihisheni. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namfahamu sana Mheshimiwa Ole-Sendeka. Katika barabara ambazo huwa zinajengwa hakuna Sheria inayozuia barabara za Vijijini kujengwa kwa lami. Tunapopeleka fedha kwenye Halmashauri za Wilaya kutoka *Road Fund* zipo Halmashauri ambazo huwa zinaamua kutengeneza barabara zao kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, huwezi ukazizuia Halmashauri zinazoamua kutengeneza barabara zao kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa barabara zingine ambazo anazizungumzia kule Kilimanjaro zingine ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi ambazo alizitoa kule na miradi ile ilikwishaanza. Kwa hiyo, isingekuwa busara katika bajeti ya mwaka huu mradi ambao umeshaanza kuusitisha ili kusudi usiendelee kuzitengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa yale niliyoyazungumza nimeyanukuu kutoka kwenye *Hansard* ambayo ninayo hapa. *(Makofi)*

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilikuwa nimeomba maelezo kuhusu barabara ya Shelui –Sekenke –Ntwike –Dolomoni mpaka Ibaga. Barabara hiyo inatengenezwa na *TANROAD* kilomita 21 tu, barabara yote inaachwa nikauliza hivi kweli unaweza ukamvisha mtoto suruali ukaacha shati, inawezekana kweli barabara inaishia katikati? Naomba barabara hiyo yote ichukuliwe na *TANROAD*.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zote za Mikoa ambazo zinahudumiwa na *TANROAD* katika Mikoa yote 25 ikiwemo na ile Mikoa mipya iliyoanzishwa zimetengewa shilingi bilioni 27 na fedha hizo zitatumika kupitia Mfuko wa Barabara. Kwa hiyo, ilikuwa ni vigumu kwa baadhi ya barabara zingine kuziorodhesha katika kitabu hiki lakini nimthibitishie kama ni barabara iko chini ya *TANROAD* tutaihudumia kwa kutengenezwa ili kusudi iweze kupitika katika sehemu zote.

**MHE. DEO H. FILIKUNJOMBE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza nakushukuru kwa kuniona lakini pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu walau Ludewa tangu tumepata uhuru sasa tutakuwa na kilomita moja na nusu ya lami kwa mara ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la msingi ni kwamba kikubwa kwetu sisi ni kuona tunakuwa na barabara ya lami kutoka Njombe hadi Ludewa ili tuweze kuwa na fursa nyingi na miradi ya Liganga na Mchuchuma iweze kuendelea. Naomba kauli yake thabiti kuhusu barabara ya lami kutoka Njombe hadi Ludewa kwa ajili ya kuendeleza Wanaludewa wote na Watanzania kwa ujumla.

**WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua umuhimu wa barabara ya Njombe hadi Ludewa yenye jumla ya kilomita 109 kujengwa kwa kiwango cha lami na bahati nzuri...

**MWENYEKITI:** Kilomita 109 ni Makete.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni Makete na ile pia ni ahadi ya Mheshimiwa Rais. Sasa Njombe ni Mkoa mpya kama ulivyo Simiyu, kama ulivyo Geita, kwa hiyo, tutaangalia katika kupanga mikakati ambayo itaanza kuhakikisha barabara hizo na kulingana na ahadi ya Mheshimiwa Rais zinatengenezwa kwa kiwango cha lami katika muda muafaka. Nimthibitishie

kwamba hilo suala lake tunalizingatia na tumeanza kujipanga ni namna gani tumeanza hata kufanya *feasibility study* na *detail design*.

**MHE. ASSUMPTER N. MSHAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Sera ya Ujenzi wa Barabara ni pamoja na ujenzi wa madaraja, wakati Mheshimiwa Rais alipokuwa akieleza Sera ya Barabara alipotembelea Mkoa wetu wa Kagera hususani Jimbo la Nkenge alieleza kwamba tutajengewa daraja la Kabingo lakini nikiangalia sijaona kifungu kinachoonesha suala hilo. Naomba tu kuelewa kama je, hilo daraja litajengwa?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu Mheshimiwa Mshama kwamba hili daraja sifahamu kama lipo chini ya Wizara ya Ujenzi au ni TAMISEMI. Kwa sababu ni ahadi ya Rais, ahadi ya Rais haiwezi ikapingwa, kama itakuwa ni TAMISEMI watatekeleza, kama ipo *TANROAD*, basi *TANROAD* itatekeleza, kwa hiyo, tutafuatilia ipo kwenye Wizara gani.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nimpongeze Waziri lakini katika mchango wangu nilizungumzia barabara ya Rujewa – Madibira kujengwa kwa kiwango cha lami, lakini barabara hiyo imekuwa kwenye ahadi na kwenye Ilani mara nyingi bila utekelezaji na mwaka huu inasemekana itakuwa ni madaraja tu, nilitaka wananchi wa Mbarari wajiridhishe kwamba madaraja ndiyo itakuwa ni kujenga lami au inakuwaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile daraja la Manienga bado halijatamkwa kwenye utaratibu wa ujenzi nilitaka kujua hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kumueleza Mheshimiwa Mbunge kwamba kupanga ni kuchagua na tumeanza ujenzi wa madaraja kwa sababu madaraja ni sehemu muhimu sana ya barabara.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Mimi nitaenda *TBA*, sitaenda kwenye barabara kwa sababu nina shilingi bilioni 88. Kwenye suala la *TBA* ambalo pia Naibu Waziri anayo taarifa, baada ya Shirika la Saruji kubinafsishwa na kupewa Kiwanda cha Twiga, kulikuwa na makubaliano kwamba zile mali za Shirika zingerudi Serikalini na baadaye walikabidhiwa *TBA*, lakini kuna mchakato ambao unaendelea ambao unatia hofu sana wale wapangaji wa hizo nyumba, kwa sababu Kampuni ya Twiga inasema kwamba ilipewa hizo nyumba wakati kuna mchakato ambao maelekezo ya aliyekuwa Waziri Mkuu aliyatoa kwamba hati husika zigawanywe mara mbili, mali ya Serikali ibaki Serikalini na mali ya kampuni ibaki kwenye kampuni. Nataka Naibu Waziri *specifically* anisaidie kwa sababu nilishatoa hii taarifa miezi minne iliyopita kwenye ofisi yake.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali la Mheshimiwa Mdee na kwa kufuatilia kwa karibu suala hilo, napenda kumtaarifu tu kwamba suala hilo limeundiwa Kamati na Kamati itakapokamilisha uchunguzi wake kwa sababu kuna nyaraka nyingi za kuzipitia, tutamfahamisha Mbunge na wananchi wanaohusika.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Katika mchango wangu nilihoji kwamba katika nchi zinazochimba mafuta ziliwahi kufadhili Mikoa mitano Tanzania ya Lindi, Mtwara, Singida, Rukwa, Kagera na Kigoma. Katika Mkoa wa Lindi walifadhili kilomita 200, tenda zilichelewa kufunguliwa bei za vifaa zikapanda, sasa hivi wametengeneza takribani kilomita 114 bado zingine hazijaisha, je, Serikali itatengeneza barabara hizo?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sijaelewa ni barabara zipi zile zinazofadhiliwa na *OPEC* kwa Mkoa wa Lindi, labda azitaje halafu tunaweza kufafanua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunge fafanua kidogo.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *OPEC* Mkoa wa Lindi walifadhili kilomita 200, zilizotengenezwa ni kilomita 114, barabara hizo ilikuwa Kilwa – Tingi - Kipatimo kwa Wilaya ya Kilwa, Nachingwea zilikuwa Nachingwea – Kilimarondo, bado kilometa 30, Liwale ilikuwa

ni kutoka Liwale - Nachingwea bado kilomita kumi na saba na Ruangwa ilikuwa Nanganga - Ruangwa.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, unasema ni *OPEC* ndiyo waliofadhili?

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zinazochimba mafuta *(OPEC)* walifadhili katika Mkoa wa Lindi pamoja na Mikoa mingine minne.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti barabara hizi inawezekana haziko chini ya *TANROAD* lakini nitawasiliana na wenzangu wa TAMISEMI ili tujue ni barabara zipi hizo ili tuweze kumjibu Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona. Katika mchango wangu wa maandishi niliomba ufafanuzi kwamba kwa kuwa barabara ya Nzega - Tabora iko kwenye matengenezo sasa hivi na kwa sababu hiyo *traffic* yote ya magari imehamia barabara ya Nzega – Itobo – Bukene -Mwamali - Tabora, sasa hivi barabara hiyo inapitiwa na magari mengi na yenye uzito mkubwa zaidi ya mara kumi ya ilivyo kawaida yake. Kutokana na sababu hii, barabara hii ya Nzega – Itobo - Bukene - Mwamali - Tabora inaharibika kwa haraka na kwa kiwango kikubwa kwa sababu inapitiwa na magari mengi na yenye uzito mkubwa zaidi ya hata mara kumi ya kawaida yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliuliza kwamba je, Wizara ina mpango wowote wa dharura wa kuiongezea bajeti *TANROAD* Tabora ili barabara hii iweze kuwa *maintained* kwa kipindi hiki ambacho barabara ya Nzega -Tabora inatengenezwa na *traffic* yote imehamia huku kwa sababu bila hatua hiyo ya dharura barabara hii pia itaharibika kabisa na kutakuwa hakuna tena njia mbadala.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi anapopewa kazi ikiwa ni pamoja na hao Makandarasi wanaotengeneza barabara kutoka Nzega hadi Tabora kilomita 115, huwa wanalazimika kutengeneza pia *diversion* na hizo *diversion* huwa ziko ndani ya mkataba. Kwa hiyo, nitakachosema ni kwamba ninamuagiza Meneja wa *TANROAD* Tabora ahakikishe magari yote yanapita kwenye barabara ya Tabora – Nzega badala ya kupita kwenye barabara ya *Region Road* ambayo madaraja yake hayawezi yakahimili uzito huo lakini kama ile barabara pia inamhusu nayo ahakikishe pia inatengenezwa na kurudishwa katika hali nzuri kama alivyopendekeza Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mpango wa Serikali wa kupunguza msongamano Dar es Salaam, ni mpango ambao unazungumzia sana barabara ambazo ziko nje kabisa na Mji na barabara hizi na magari haya yakiwa hayapati msongamano nje ya Mji sijui yataingiaje Mjini. Nikisema hivyo nazungumzia barabara ya Uhuru ambayo michoro yake na pesa zake zimeshakadiriwa ambazo ni shilingi bilioni 14, nilitaka kujua tu kwamba barabara hii ndiyo barabara ambayo ilipokea Uhuru mwaka 1961 na barabara hii ndio tunasherehekea Uhuru wa nchi yetu miaka 50 mwaka huu. Nilitaka kujua Serikali ina mpango gani kuhusu barabara hii ya Uhuru?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezingatia ushauri wa Mheshimiwa Zungu na kwa sababu lengo kubwa pia ni kuhakikisha kwamba tunapunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam tutaangalia uwezekano wa kutumia fedha za *Road Fund* katika kufanya *rehabilitation* ya barabara hii ya Uhuru ili maana ya Uhuru iweze kuleta maana katika Jiji la Dar es Salaam.

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mwaka 2005 Rais alipotembelea Ngudu-Kwimba, alitoa ahadi ya kujenga barabara za lami kutoka Mabuki - Ngudu mpaka Malya na nyingine kutoka Ngudu-Magu. Baada ya kutoa ahadi hiyo, Rais alisimikwa kuwa Chifu na akaitwa jina la *'Khombu ya Vantu'***,** maana yake kumbukumbu ya watu. Kwa kuwa suala hili lilichanganya mambo ya kimila, Waziri haoni kwamba kuna haja sasa asimamie ile ahadi ya Rais alete hizo barabara za lami ambazo ziliahidiwa na Rais bila kusubiri bajeti yoyote ile? *(Kicheko)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumjibu dada yangu Mheshimiwa Leticia Nyerere kwamba barabara ya Mabuki-Malya-Nangudu-Magu zote zile ni barabara za *Region Roads*. Kupanga ni kuchagua, tunaanza kwanza na *trunk roads*, lakini ahadi ya Rais inabaki palepale na kwa sababu ahadi ni ya kipindi cha miaka mitano, tutaangalia katika kipindi cha miaka mitano tunafanya nini katika barabara alizozitaja ikiwa ni pamoja na kuanza kufanya *feasibility study* ili Mheshimiwa Rais aendelee kuwa *'Khombu ya Vantu'*.

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufahamu tu kwa sababu kuna barabara ambayo ilikuwa itoke Itende - Kilindoni yenye urefu wa kilomita 14.3 na ambayo tayari ilikuwa imeshatangazwa kwa Wakandarasi ili ije kutengenezwa lakini kwa bahati mbaya walio-*bid,* wali-*bid* tenda kwa pesa nyingi ambazo hata Waziri alisema kwamba kweli kiwango kilikuwa kikubwa lakini katika Kitabu inaonekana ni milioni 1.9. Nataka kufahamu kweli ujenzi wa barabara hii utakuwepo au kuna taratibu zingine ambazo labda Serikali imeweka pesa upande mwingine kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa barabara hii kwa kilomita 14.3?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumjibu Mheshimiwa Shah kwamba ujenzi wa barabara hii upo kwa sababu upo ndani ya makubaliano na wenzetu na *MCC* ambao wanajenga uwanja wa ndege. Ni kweli kabisa kama alivyozungumza mwaka jana tulipotangaza tenda waliotenda hawaku-*meet* zile *condition* zilizokuwa zimewekwa na ndiyo maana tumeamua kutangaza mwaka huu ili Wakandarasi waanze ujenzi kwa kiwango cha lami hizo kilomita ambazo amezitaja Mbunge.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri na Naibu Waziri kwa kuanza kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami barabara ya kutoka Sikonge kuja Tabora kilomita 70.

Hoja yangu ipo pale Igunga, kwa niaba ya wananchi wa Igunga, kila Viongozi wa Kitaifa wanapokwenda pale wamekuwa wakilalamikiwa sana na wananchi wa Igunga juu ya daraja linaloitwa daraja la Mbutu, sijaridhika sana na maelezo kwamba tutajenga. Nilitaka nione kwa usahihi zaidi Serikali ikitoa maelezo hapa ya kuwaridhisha wananchi wa Igunga kwamba imepanga pesa kiasi gani kwa ajili ya kuanza ujenzi mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa maelezo kwa Mheshimiwa Nkumba kama ifuatavyo. Serikali imeliona tatizo hili kwa muda mrefu la daraja la Mbutu na tukaona busara mwaka huu tutenge fedha. Namwomba Mbunge afungue ukurasa wa 113 wa kitabu cha hotuba ya Waziri atakuta pesa tumetenga kwa ajili ya mwaka huu wa fedha na kwa sababu tumedhamiria kulitatua tatizo hilo kutokana na matatizo ya muda mrefu yaliyopo hapo, Wizara ipo tayari kuongezea pesa pale ambapo kutatokea upungufu.

**MHE. DKT. FAUSTINE E. NDUGULILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wa eneo la Mbagala ambao nyumba zao zilibomolewa mwaka 2002 kupisha ujenzi wa barabara, baadhi yao walienda Mahakamani wakashinda kesi na kulipwa fidia, lakini mwaka jana kuna barua tatu ambazo zimeandikwa na Serikali, moja ya mwezi wa tano ambayo iliandikwa na Waziri wa wakati huo Mheshimiwa Kawambwa na mbili ambazo ziliandikwa na Katibu Mkuu wakati huo akiwa Chambo, zote zikithibitisha kwamba Serikali itawalipa fidia wananchi hao. Kumekuwa na kauli ambazo siyo rasmi kwamba wananchi hawa hawatalipwa, naomba tupate tamko la Serikali kwamba wananchi waliopisha barabara Mbagala watalipwa fidia na Waziri anaweza akathibitisha hilo kwa barua?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Sheria ni kitu kibaya sana, nimeeleza hapa kwamba ni kweli tumeshalipa fidia ya watu 111, shilingi bilioni tatu na mia nne sabini na tisa elfu na mia tano kumi na moja na mia nne tisini na tatu na senti sabini lakini pia tumekwishalipa fidia kwa wale ambao barabara iliwafuata, tulilipa tarehe 24 mwezi wa kumi na mbili mwaka 2002, shilingi bilioni moja na mia tatu kumi na tano na mia mbili arobaini elfu lakini tukalipa tena tarehe 17 mwezi wa tisa mwaka 2008, shilingi milioni mia nne sitini na nne na mia sita thelathini na moja elfu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa siwezi nikatamka hapa nitawalipa watu waliovunja sheria, kama umevunja sheria na mimi siwezi nikavunja sheria hapa. Kwa hiyo, ukweli ndiyo unabaki hivyo, lakini kama wapo watu wengine ambao barabara iliwafuata na orodha yao anayo Mheshimiwa Mbunge na bahati nzuri Mheshimiwa Dkt. Ndungulile huwa tunawasiliana naye ayalete halafu tutatuma Tume ya Wahandisi kwenda kuangalia na kama kweli barabara itakuwa imewafuata tutawalipa tu fidia.

**MHE. DKT. AUGUSTINO L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa naangalia kitabu hiki cha Waziri, ukurasa wa 110 barabara ya Arusha – Moshi – Himo - Holili na Arusha halafu kuna *bypass and* Himo *Weighbridge*. Mimi sikuelewa kama maana yake ni ile mizani iliyopo hapo Njia Panda mnatuwekea kubwa na mpya ambayo imekuwa ni kero, naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo la Himo, kuna Mzani wa Wizara, panakuwa na msongomano mkubwa sana wa magari na inakuwa ni tatizo. Kwa hiyo, tumetenga kiasi hiki cha fedha ili kusudi tutengeneze *bypass* lakini pia kuwalipa fidia wale ambao watafuatwa na barabara ambao watakuwa nje ya *road reserve* kwa Sheria Na.13 ya mwaka 2007.

**MHE. ANNE M. KILANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ukiangalia katika Ilani za Uchaguzi zote utakuta kwamba Ilani za Uchaguzi zinasisitiza kuhamia Makao Makuu ya Serikali Dodoma, lakini ukiangalia nyumba za Serikali zinazojengwa, niliongea wakati natoa maoni ya Kamati kwamba nyumba karibu zote za viongozi wa Serikali zinajengwa Dar es Salaam na nyumba mbili tu ndiyo zinajengwa Dodoma. Ni vema Waziri akajibu kwa ujumla kwamba Serikali mna dhamiria kweli kuhamia Dodoma au ni danganya toto?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, bila kutaja Malecela halijakamilika vizuri unajua Wagogo watani zangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhamia Dodoma na ndiyo maana hata sasa tupo Dodoma, ndiyo maana hata tunatengeneza barabara ya kutoka Dodoma kwenda Iringa, tunatengeneza barabara ya kutoka Dodoma kwenda Babati, lakini ndiyo maana tulijenga nyumba mia tatu pale Kisasa, lakini pia katika bajeti ya mwaka huu, kutokana na ushauri wa Kamati ya Miundombinu tumepanga na utaona katika hotuba yangu nimezungumza kwamba tutaanza kujenga nyumba elfu kumi Dar es Salaam na Dodoma, kwa ku-*involve* watu binafsi na tumeziandika hapa. Kwa hiyo, lengo kubwa wawekezaji wazuri wajitokeze tushirikiane na *TBA* tujenge nyumba nyingi hapa Dodoma na kila mmoja anapapenda Dodoma, hata mimi napapenda Dodoma kwa sababu ni kwa watani zangu Wagogo.

**WAZIRI WA NCHI OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Waziri, nilitaka kuongeza kwamba Serikali imeamua kuimarisha miundombinu kama sehemu muhimu ya kuhamia Dodoma. Hata kwa mwaka huu, Serikali itatumia siyo chini ya shilingi bilioni 32 kwa ajili ya miundombinu ya Dodoma Mjini kwa lengo hilohilo la kuharakisha uhamiaji Makao Makuu.

**MHE. SUZAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ajali nyingi hapa Tanzania zimekuwa zikitokana na kutokuwepo kwa alama za barabarani hususan sehemu za matuta na sehemu za kona kali lakini siku za hivi karibuni kumekuwa na utaratibu mtu anapogongwa tu wananchi wanaandamana au wanalala barabarani wakidai matuta na baadaye Serikali inajenga matuta. Nilitaka kujua je, matuta ni suluhu ya ajali na Serikali inasemaje kuhusu hilo?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza matuta si suluhu ya ajali kama ilivyo maandamano si suluhu lakini katika Sheria Na.13 ya mwaka 2007 kwenye *highway* zote kujenga matuta ni kuvunja Sheria. Kwa hiyo, tutaendelea kuzingatia hili kwa kuweka alama za barabarani. Wito wangu ninatoa kwa watumiaji wa barabara waheshimu Sheria za Barabara ikiwa ni pamoja na Sheria Na.30 ya mwaka 1973 lakini pia watumiaji wengine wakiwepo hata ndugu zangu Wasukuma wasing'oe alama za barabarani kwa ajili ya kutengenezea matela ya ng'ombe pamoja na Wagogo.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa maandishi nilielezea kuhusu kudhoofika kwa shughuli za uchumi na kijamii na ongezeko la akinamama wajawazito na wananchi kukamatwa na mamba, yapata wananchi 28 kutoka mwaka 2001 mpaka sasa kutokana na ukosefu wa Daraja la Mto Momba linalounganisha Wilaya ya Mbozi na Sumbawanga Vijijini kupitia Vijiji vya Kinyamatundu na Kamsamba, je, Serikali inasema nini kuhusu hili? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitolee maelezo suala la Mheshimiwa Malacho kama ifuatavyo. Usanifu wa Daraja la Mto Momba unaogharimiwa na Serikali ya Denmark na unaendelea kwa taarifa ya Mheshimiwa Mbunge na baada ya kazi ya usanifu kukamilika Serikali sasa itaingia kwenye mchakato wa kutafuta fedha za kujenga Daraja la Mto Momba.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa inaonekana Halmashauri nyingi zinashindwa kujenga barabara na kwa kuwa barabara za pembezoni ambazo zinaunganisha Kondoa na Mikoa ya Singida, Arusha na Manyara, kwa kuwa bajeti inayopangwa katika Halmashauri haitoshelezi na si rahisi kujenga barabara hizo muhimu…

**MWENYEKITI:** Hakuna kusoma.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mfano wa barabara ambazo ziko pembezoni ni za Singida, Manyara na Dodoma. Kwa kuwa bajeti hii inayopangwa haikidhi mahitaji ya kujenga barabara hizo katika Halmashauri ambazo ni muhimu na haunganisha Mikoa ambayo iko jirani na Mkoa wa Dodoma. Je, Mheshimiwa Waziri sasa si wakati muafaka kwa Wizara yake kuchukua barabara hizo?

**MWENYEKITI:** Hilo tu?

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moza kama ifuatavyo:-

Jukumu la kuhamisha barabara kutoka barabara ya *feeder roads* au ya Halmashauri ya Wilaya kwenda *Regional roads* kwenda *trunk roads,* ni suala la kisheria kupitia Sheria Na.13 ya mwaka 2007 na kanuni zake za mwaka 2009, barabara inayokidhi viwango vile ndio inapandishwa daraja. Barabara ambayo haikidhi viwango hivyo hata kama ni *trunk road* inaweza ikarudishwa kwenye Halmashauri. Wito wangu kwa Halmashauri husika na kwa sababu sasa hivi tunahusika na mambo ya *D by D* wahakikishe fedha zinazopelekwa kwenye Halmashauri zinatumika kulingana na matumizi na ndio maana nimesema fedha za *road fund* zote zinazotolewa kwenye Halmashauri za Wilaya zitumike kwa ajili ya matengenezo ya barabara tu na si kulipana posho.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAMISEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hela zilizopangwa kwenye Halmashauri kwa maana ya *Road Fund* kwa mwaka huu ni shilingi bilioni 91. Shilingi bilioni 3.3 ni hela ambazo zimetumika kwa ajili ya kufuatilia, jumla ya hela zote zilizotengwa kwa ajili ya *Road Fund* ni bilioni 95. Sasa kwa maana ya kwamba hela hizi hazitoshelezi kama Mheshimiwa Mbunge anavyozungumza hapa kinachotakiwa kufanyika hapa ni kwamba Halmashauri zote tunatakiwa ku-*rearrange priorities* zetu*. It is true* kama *Member of Parliament* anavyosema kwamba hela hizi ni kidogo sana. Sheria ile ambayo Mheshimiwa Waziri anaizungumzia hapa inazungumzia asilimia 30 na asilimia 70 kwa ajili ya kwao wao. Hii asilimia 30 na asilimia 70, ni asilimia 90 kwa maana asilimia 10 ya hela zote za *Road Fund* ni zile zinazokwenda katika *development*. Kwa hiyo, anachosema Mheshimiwa Mbunge ni sahihi lakini tunachofanya Mheshimiwa Magufuli alipokuwa anajibu swali hapa juzi alizungumza habari ya kwenda kupeleka maombi maalum ili iweze kuwa *considered just in case* inatokea kwamba hizi hazitoshi lakini sasa uwezo wetu ndio unaotufikisha hapa tulipo.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina tatizo na Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya kuweka *assurance* tu ya wananchi wetu kule Mtwara. Iko barabara ya Mtwara – Tandahimba - Newala hadi Masasi inayotakiwa kufanyiwa *feasibility study,* kwenye mchakato wa bajeti, barabara hii wataalam wali-*estimate* kama shilingi bilioni 2.3 hivi lakini kwenye bajeti hapa imepitishwa shilingi milioni 289 ambayo ni kidogo sana. Pia Mheshimiwa Rais alipofanya ziara ya

Mkoa wa Mtwara wiki iliyopita amewaahidi wananchi wa maeneo yale kwamba katika mwaka huu wa fedha *feasibility study* ya barabara itakamilika ikiwa ni pamoja na daraja ambalo nimelisahau jina lake, lakini linalopitia eneo lile. Sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri atuhakikishie jambo hili maana kwenda vinginevyo ni kumwangusha Rais, anatuhakikishiaje kwamba tunamaliza *feasibility study* kama maneno ya Mheshimiwa Rais wetu mpendwa yalivyokuwa? (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Njwayo kwamba barabara ya kutoka Mtwara - Newala hadi Masasi itafanyiwa *feasibility study* kama ilivyoahidiwa na Mheshimiwa Rais pamoja na lile Daraja la Mwiti. Ndio maana katika bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha kwa ajili ya kutangaza tenda ili ianze kufanyiwa *feasibility study* na *detail design* kwa ajili ya kutengenezwa kwa kiwango cha lami kwa sababu maeneo hayo ni ya uzalishaji sana na hasa korosho. *(Makofi)*

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna barabara moja katika Jimbo la Mufindi Kusini inayotoka Nyololo - Kibao - Mtwango mpaka Mgololo na hii barabara imepita kwenye viwanda nane (8) hata vile viwanda vinafanya uzalishaji mkubwa sana katika Taifa letu la Tanzania. Sasa cha ajabu kutoka mwaka 1932, kiwanda cha chai kilipoanza kule, hakuna barabara ya lami inayopita kule. Sasa Mheshimiwa Waziri naomba utamke na wananchi wa Mufindi kule wasikie mna mpango gani na barabara hii ambayo inatoa manufaa kwa taifa letu la Tanzania? (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Nyololo - Mgololo kule kwenye kiwanda inatoa manufaa sana kwenye nchi hii kama ilivyo barabara ya kutoka Geita kwenda Nyulugusu, barabara ya kutoka Kilimanjaro kwenda Simanjiro, kwa hiyo, tutakachofanya tunaanza kwanza na barabara za *trunk road* ya kutoka Dodoma kwenda Iringa, tukishamaliza *trunk road* zote tutaingia na barabara zingine za *regional road* katika kuziwekea *consideration* katika kuzitengeneza kwa kiwango alichopendekeza Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. DKT. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sera ya nchi yetu kuunganisha Makao Makuu ya Mkoa na Mikoa mingine. Katika swali langu la maandishi niliulizia kuhusu kuunganishwa kwa Mkoa Mpya wa Simiyu yaani Bariadi na Mji wa Mwanza. Katika maelezo ya Mheshimiwa Waziri, nilisikia kama anazungumzia kwamba usanifu umeanza wa barabara, sikuelewa vizuri kwamba ni barabara ipi, sijasikia mahali popote kwamba usanifu umeanza na ni barabara ipi hiyo. Naomba ufafanuzi wa suala hili na atamke wananchi wa Mkoa wa Simiyu na Mwanza wajue ni lini hasa Serikali itaanza kujenga barabara ya kuunganisha Mwanza na Bariadi? Ahsante.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichozungumza hapa ni kwamba katika Mikoa mipya minne ya Njombe, Simiyu, Geita na Katavi, tumepata maelekezo kutoka Mheshimiwa Rais kwamba Makao Makuu ya Mikoa hii tuanze *feasibility study* na *detail design* kwa ajili ya kuunganisha Mikoa hii kwa barabara za lami. Sasa sijajua ni barabara ipi itakayounganisha Mkoa wa Mwanza na sijajua hata mpaka wa Mkoa Mpya wa Simiyu hata Mkoa wa Geita, sijui mpaka wake ukoje na wala hata Wakuu wa Mikoa hawajatangazwa na ndio maana na sisi hatujateua ma-*Regional Manager*. Mambo haya yakishakamilika, tutayafanya haya yote ili kusudi tuweze kufanya kadri Mheshimiwa Dkt. Limbu anavyozungumza.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hoja yangu ya msingi nilisema barabara ya kutoka Makutano kwenda Natta siyo kilometa 50 bali ni kilometa 90. Nilitaka kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, barabara kutoka Makutano kwenda Butiama itaanza kujengwa kwa lami lini maana wananchi wa Butiama wamekuwa wakisubiri kwa mika 50 tangu tupate Uhuru, ni miaka 11 tangu Mwalimu atuache. Tunataka tupate kauli ya Serikali, barabara kutoka Makutano kwenda Nata mpaka huko inakokwenda kupitia Butiama itaanza kujengwa mwaka huu kabla ya sherehe ya miaka 50 ama laa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mkono kama ifuatavyo:-

Akifunua ukurasa wa 117 wa Hotuba yangu, tumezungumzia pale barabara ya Makutano –Natta - Mugumu tukaweka kwenye *bracket* Makutano - Natta *Section*. Nafahamu kabisa kutoka Makutano - Natta hadi Fotikoma kuna karibu kilometa 100 *feasibility study* imeshamalizika, *details design* imeshamalizika kwa hiyo katika bajeti ya mwaka huu tumetenga hizi fedha kwa kuanza kutangaza tenda na kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami.
Tunaanza na Makutano - Natta. Tukimaliza pale tunaendelea tena Natta – Fotikoma lakini tukimaliza hivyo tena tunazungusha Mugumu - Loliondo mpaka Mto wa Mbu. Butiama kuna lami mpaka pale kwenye *junction* kilometa 12 zilizotengenezwa kwa *water-seal* na kufunguliwa na Mheshimiwa Mkapa.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji mzuri.

**MWENYEKITI:** Usiwapongeze muda hautoshi.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Barabara Kuu zinajengwa kwa lami maeneo mengine barabara zilizokuwa za lami za zamani huachwa. Mfano mzuri ni barabara inayotoka kuanzia Kibaha Tumbi mpaka Mlandizi. Katika maeneo haya wananchi walikuwa wamekwishawekeza na shughuli mbalimbali za kiuchumi huwa zinafanyika lakini barabara hizi za zamani zinasaidia sana wakati wa matatizo kama ajali na zinakuwa ni *alternative road* kwa kufanya magari yaendelee kupita bila kukwamisha usafiri katika maeneo hayo. Sasa barabara hizi zimekuwa zikiachwa, hazijafanyiwa matengenezo yoyote na hata ile lami sasa inapotea. Napenda kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, Serikali ina mpango gani kuendelea kuzitunza barabara hizi ili ziendelee kustawisha sehemu hizi na kukuza Miji hii katika maeneo hayo? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na wazo hili zuri la Mheshimiwa Koka, tutalizingatia katika utekelezaji wetu.

**MHE. AGRIPINA Z. BUYOGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naungana kabisa na juhudi za Mheshimiwa Waziri katika kusimamia shughuli za ujenzi wa barabara lakini ili barabara zetu ziwe salama na kwa kuwa sasa Mkoa wa Kigoma tuko kwenye furaha za kuwa kwenye mkakati wa kupata barabara za lami, naomba tamko la Serikali ni mkakati gani wa makusudi wa kuharakisha kutengeneza Reli ya Kati ili barabara zetu za lami zitakapokuwa zimekamilika zisiharibike haraka? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Hiyo itasomwa kesho Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naheshimu kanuni zetu, baba yangu ameshamaliza, ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DKT. CHARLES J. TIZEBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nina ombi kwamba vile vivuko ambavyo viko kwa ajili ya kuhudumia wananchi walioko Visiwani ingekuwa vizuri kama vingekuwa vinalala huko huko Visiwani ambako vinahitajika wakati wa dharura. Je, Mheshimiwa Waziri anaweza kutusaidia katika hili? *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni wazo zuri la Mheshimiwa Dkt. Tizeba na kwa vile Katibu Mkuu na Mkurugenzi wa *TAMESA* yuko hapa basi nawaagiza kile kivuko cha Nyakalila kwenda huko kwenye Jimbo lake kiwe kinalala kule ili pakitokea matatizo wawe wanabebwa watu vizuri kupelekwa hospitali.

**MHE. CAPT. JOHN D. KOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu kuhusu *Mtwara Corridor,* kitabu kinasema kuna Makandarasi kutoka Tunduru, Namtumbo, Songea, Peramiho Mbinga lakini nimeona kutoka Mbinga mpaka Mbamba Bay lakini haijaeleza kama kuna Mkandarasi pale. Nilikuwa nataka kujua na nilimuomba Waziri aniambie barabara hii ingawa fedha nimeziona ni lini hasa barabara ile itaanza kupelekewa Mkandarasi na kuanza na kujengwa rasmi kwa kiwango cha lami? Ahsante.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumhakikishia kwamba barabara yote ya kutoka Tunduru, Namtumbo, Songea, hadi Mbinga Mbamba Bay tumejipanga itengenezwe kwa kiwango cha lami. Ndio maana katika bajeti ya mwaka huu tumeziweka hizo fedha ili tutangaze tenda. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Komba, apitishe bajeti yangu ili baadaye kuanzia kesho tuanze hata kutangaza *tender* Makandarasi wakaanze kufanya kazi. *(Makofi)*

**MHE. ISMAIL A. RAGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jana katika *television* ya *TBCI*, ilitolewa taarifa kwamba Wakandarasi wamegoma katika Mkoa wa Tabora. Naomba tamko la Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri eti waligoma?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa maelezo kwa Mheshimiwa Rage Mbunge wa Tabora kama ifuatavyo:-

Hata mimi nilipata bahati kuona hilo tangazo kwenye *TBCI,* ilikuwa ni taarifa inasema Makandarasi wamesimama kufanya kazi lakini kilichonistua ni kwamba taarifa hiyo ilikuwa inamnukuu hata Meneja wa *TANROAD* wa Mkoa wa Tabora ambaye yuko hapa kwa wiki nzima lakini baada ya kuhoji tukagundua kwamba hiyo taarifa ilikuwa *cut and paste* kwa sababu sehemu ya mahojiano ilifanyika mwezi wa tano. Kwa hiyo, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Rage na wananchi wa Tabora kwamba Wizara ilishapitia hapo na Makandarasi wote wako kazini na Mkurugenzi Mtendaji siyo wa *TANROAD* alipita hivi majuzi tu na kusisitiza kwamba kazi lazima ifanyike na mimi mwenyewe nilitoa agizo pale kwamba ni sehemu ya mkataba kwa Makandarasi wote kuhakikisha kwamba barabara zile za zamani zinakuwa *maintained* na mimi navyosema sasa hivi wananchi wa Tabora watathibitisha kwamba barabara hizo zinapitika. Kwa hiyo, taarifa siyo sahihi na napenda tu kuwaomba wenzetu wa *TBC,* wao ni chombo cha Taifa wasianze kuiga mambo ya vyombo vingine kuanza kuchakachua taarifa na kuweka *image* ya Serikali vibaya. *(Makofi)*

**MHE. REGIA E. MTEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mitandao yote ya barabara nchini hutakuta popote alama za barabarani zinazowasaidia watu wenye ulemavu matokeo yake mpaka leo tukitaka kuvuka barabara mpaka tupewe msaada au huruma ya Dereva anayeendesha gari, ndipo upite na ni miaka 50 sasa walemavu tumechoka kuhurumiwa, tumechoka kusaidiwa, ningependa kusikia kauli yako Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tutalizingatia hili katika barabara tutakazoanza sasa kuzijenga ili kusudi masuala haya ya walemavu yaweze kuzingatiwa.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya marekebisho yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, dakika 10 zimebaki tunaingia kwenye *guillotine*.

Kif. 1002 - *Finance and Accounts Unit*…… Tshs. 718,193,800/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning Division*........ Tshs. 719,562,800/=
Kif. 1004 -*Information, Education and Communication Unit*.......................... Tshs. 316,430,500/=
Kif. 1005 - *Procurement Management Unit*.......Tshs.264,299,200/=
Kif. 1006 - *Internal Audit Unit*..................................Tshs. 217,254,100/=
Kif. 1007 - *Legal Services Unit*................................ Tshs.149,656,400/=
Kif. 1008 - *Management Information System Unit*........................ Tshs. 188,886,700/=
Kif. 2002 - *Technical Services Division*……… Tshs.8, 123,919,086/=
Kif. 2005 -*Transport Infrastructure Division*..Tshs.231, 889,106,255/=
Kif.2006 - *Transport Service Division* …………………… Tshs. 0/=
Kif.5002 - *Safety and Enviribment Division* …….Tshs.643,965,800/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**FUNGU 98 – WIZARA YA UJENZI**

Kif. 1001- *Administration and General*………………… Tshs. 0/=
Kif. 1003- *Policy and Planning Division*…… Tshs.1, 792,473,000/=
Kif. 2002- *Technical Services Division*………Tshs. 9,055,393,000/=
Kif. 2005- *Transport InfrastructureDivision* ………………...................Tshs.1,237,140,693,000/=
Kif. 2006 - *Transport Service Division*……………………Tshs. 0/=
Kif. 5002- *Safety and Environment Division*…Tshs.2,988,380,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila Marekebisho yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu limekaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia Makadirio ya Wizara ya Ujenzi, kwa mwaka wa fedha wa 2011/2012, Kifungu kwa Kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko. Hivyo naomba kutoa hoja kwamba makadirio hayo sasa yakubaliwe rasmi na Bunge lako.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Ujenzi yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA**: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kwa uamuzi huu ni kwamba hoja ya Waziri wa Ujenzi imepitishwa na Bunge hili, hizo trilioni alizokuwa anasema mkimuachia tu mtaona vitu vyake, nadhani sasa umepewa, lakini kama walivyosema wote ni kwamba kila mtu akifanya kazi yake kwa uhadilifu na kutumia hela hiyo kwa makini kabisa, hayo yote yanawezekana. Kwa hiyo, tunawatakia Wizara na ninyi wenyewe kazi njema katika mwaka huu wa fedha na tunakupongezeni kwa sababu katika kukaa kwangu Bungeni kwa miaka yote hii kama kulikuwa na Wizara timutimu ilikuwa ya Ujenzi. Ikifika tu mtu roho mkononi, lakini miaka ya hivi karibuni kwa sababu ya utendaji mzuri wa Wizara hii imekuwa kama ni mwendo rahisi, nawatakia mafanikio mema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyokubaliana wenzetu wanaenda kufuturu, tunaomba waende wakafuturu vizuri na kwamba sina matangazo mengine zaidi, naahirisha kikao cha leo mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 12. 25 jioni Bunge lilihairishwa mpaka Siku ya Jumatano,*
*Tarehe 3 Agosti, 2011 Saa Tatu Asubuhi)*